# SAA KUBWA

## (MEGA OROLOGION)

**CENTRE DE LA MISSION ORTHODOXE**

**KOLWEZI KONGO**

**2005**

# SALA KATI YA USIKU (MESONIKTIKO)

## Sala ya kwanza asubui mapema

*Kama utalamuka ya kitanda yako, simama na heshima na boka mbele ya Mungu sema:*

Kwa Jina ya Baba na ya Mwana na ya Roho Mutakatifu. Amina.

Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Musiye kufa Mtakatifu, utuhurumie, *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele, Amina.

Utatu Mtakatifu Kamili utuhurumie, Bwana utusamehe zambi zetu, Rabi utuondolee makosa yetu, mtakatifu utukaribie na uponye magonjwa yetu, Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni, utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe ndeni zetu kama sisi vilevile tunawasamehe walio na ndeni zetu, tena usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule mwovu.

*Kisha tunasoma hii wimbo, sauti ya kwanza.*

Tukiamka usingizini, tunasujudu mbele yako na pamoja na Malaika tunasema tena wimbo: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya mbili.

Bwana uliyeniamusha usingizini mwangu, angaza moyo wangu na roho yangu, fungua midomo yangu ili ni kuimbie, ee Utatu Mtakatifu: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ee Mungu wangu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

Sasa na siku zote. Sauti ya tatu.

Mwamzi atakuja kama umeme kufunua matendo ya kila mmoja; na woga tunakuimbia katikati ya usiku: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu utuhurumie.

Bwana hurumia, *(mara kumi na mbili)* na sala hii:

Ninapoamka katika usingizi, ninakushukuru, ee Utatu Mtakatifu; ndivyo, kwa wema wako kubwa na kwa uvumilivu wako, haukunisirikia mimi mzaifu na mkosefu, lakini kwa desturi yako, ulitenda na mapendo, mimi niliyelala katika sikitiko ukaniamusha sababu ya kukesha na kutukuza uwezo wako. Sasa angaza macho ya roho yangu, funfua kinywa changu nitangaze maneno yako na nishike amri zako; nitende mapenzi yako na niseme zaburi kwa ajili yako kwa moyo mumoja na kwa shukrani; nitukuze jina lako takatifu kamili, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, daima sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Sala ingine.*

Utukufu kwako, ee Mfalme na Mungu Mwenyezi. Kwa maongozi yako na unapojaa na mapendo, ulinistahilisha kuamuka katika usingizi mimi mutumishi wako muovu, na kuvuka kizingiti ya makao yako takatifu. Ee Bwana, pokea sauti ya sauti ya maombi yangu kama ile ya majeshi yako takatifu ya kiroho. Unipe wema wako ili niwezi kukutolea kwa moyo safi na kwa roho ya unyenyekevu utukufu wa midomo yangu mchafu. Hapo, nitaweza na mimi pia, kushiriki

pamoja na mabikira wenye akili katika nuru ya roho yangu. Nakutukuza, ee Mungu-Neno Wewe mwenye kutukuzwa katika Baba na Roho Mtakatifu. Amina.

# IBADA YA MESONIKTIKO YA KILA SIKU

*Kama ni padri, anasema:*

Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kama hakuna padri, musomaji atasema hivi:*

Kwa maombezi ya Wapadri Watakatifu wetu, ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe. Amina.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Mfalme wa mbinguni, Wewe Mfariji. Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote, Wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa, hata kuziokoa roho zetu, Mwema We.

Trisagion. Mungu Mutakatifu. . . Kisha:
Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu yeye Mungu Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu yeye Kristu, aliye Mfalme na Mungu wetu.

*Kisha tunasoma Zaburi 50 (51).* Unirehemu, ee Mungu sawa sawa. . .

*Kisha tunasoma Zaburi 118 (119), inayeitwa Amomos. (Angalia ndani ya Ibada ya Wafu (Panihida).*

*Kisha tunasoma Simvolo ya Imani:* Nasadiki Mungu mmoja. . . *Kisha Trisagion:* Mungu Mutakatifu. . . Kwa kuwa. . . *Kisha hii wimbo:*

Tazama Bwana Arusi anakuja katika ya usiku, heri mtumishi atakuta mwenye kuamka; msiyestahili ni yule atamkuta mwenye kulala. Ee roho usilale kusudi usitolewe ku mauti na kuondolewa ku ufalme; lakini amka ulalamike: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sauti ya mnane.

Uwe tayari leo siku ya ajabu, ee roho yangu, kesha ukishika taa yenye kuwaka na mafuta yenyi kuangaa, kwani haujui wakati gani itakufikia sauti itakayokuambia: Tazama Bwana Arusi! Tazama basi, ee roho yangu, usisinzie na usikae inje kwa kupiga hodi kama mabikira tano; Lakini uwe macho sababu ya kwenda kukutana na Kristu ukichukua mafuta mengi, na akuruhusu kuingia katika chumba cha arusi cha utukufu wake.

Sasa na siku zote. . . THEOTOKION..

Ee Bikira Mzazi-Mungu, wewe boma la ushindi tena ngome ya wokovu, tunakuomba, ondoa shauri ya adui, geuza huzuni ya watu wako kuwa furaha, leta nguvu kwa dunia iliyo yako, sabitisha wale wenye kumuogopa Mungu, ombea dunia amani, maana wewe ni matumaini yetu, ee Mzazi-Mungu.

*Kisha tunasema:* Bwana hurumia. *(mara makumi ine) na hii sala:* Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa

Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa, na kutukuzwa wakati wote na katika kila saa mbinguni na duniani, uliye mwadilifu, mrahimu tele, mfazili sana unayependa wenye haki, tena kuwahurumia wenye zambi; unayewaita wote kuona wokovu, ukiwaahidi vitu vema ilvivyokuja; wewe, ee Bwana, hata katika saa hii uyapokee maombi yetu, na kuyashurtisha maisha yetu njiani pa amri, uuzitakase

roho zetu, uyasafishe miili yetu, uyatengeneze mafikira zetu, uzinyoshe nia zetu; ukatuokoe na kila shida, ubaya, na teso, utulindie kwa Malaika wako, ili sisi tukiwa na utunzi na uongozi wao, tufike katika umoja wa imani na kuujulisha utukufu wako usiofikika. Kwa kuwa unahimidiwa milele na milele. Amina.

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku. . . Uliye wadamani. . . Kwa jina la Bwana barikia, ee padri:

Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

*Padri anasoma hii sala:*

Mungu, Rabi, Baba Mwenyezi; Mwokozi, Mwana wa pekee, Yesu Kristu na Roho Mtakatifu, umungu moja, nguvu moja, unihurumie; wakati wa mwisho uniokoe mimi mukoosefu wako, kwani unabarikiwa milele na milele, Amina.

*Kama iko wakati ya kwarezima, mbele ya Paska, tunafanya metania tatu (kupika magoti) na kusema kwa kila metania moja-moja sala ya ile inafwatayo ya Mtakatifu Efremi wa Siria.*

Ee Bwana na Rabi wa uzima wangu, ondoa mbali nami roho ya uvivu, ya utawanyiko, ya kutawala wengine na maneno ya bure.

Unipe roho ya usafi, ya unyenyekevu, ya uvumilivu na ya mapendo, mimi mtumishi wako.

Ndiyo, ee Bwana mfalme, unipe nione zambi zangu tena nisimuhukumu ndugu yangu, kwani umehilidiwa milele na milele, Amina.

*Kisha tunafanya metania kidogo kumi na mbili na kisha musomaji anasoma hii sala:*

Ee Bwana Mwenyezi, Mungu wa majeshi na wa watu wote, wewe unayekaa juu mbinguni na kutazama wanyenyekevu, wewe mwenye kupima mioyo na mapigo na kujua kweli siri za watu; nuru yasipo mwanzo na mwisho ambaye hakuna mabadiliko wala kivuli cha mabadiliko, ee Mfalme wa milele, pokea maombi tunakutolea kwa midomo yetu michafu kwa hii saa ya usiku, tunatumainia rehema yako kubwa. Utuondolea makosa yetu tuliyotenda kwa matendo. kwa maneno na kwa mawazo, kwa kujua ao bila kujua; ututakase kwa kila uovu wa mwili na wa roho, na utufanye sisi kuwa hekalu ya Roho wako Mtakatifu. Utupe tupitishe usiku yote ya hii uzima ya sasa moyo yenye kuwa macho na roho yenye kuamuka, tukingojea kujua kwa siku ya nuru na yenyi kuangaa ya Mwana wako wa pekee Bwana Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristu wakati atakapokuja duniani katika utukufu kama mwamuzi na ulimwengu, kumulipa kila mumoja kadiri ya matendo yake. Anaweza kutukuta, apana wenye kulala, lakini macho wazi na wenye kuamuka, tukishika amuri zake; na tutaweza kuingia pamoja naye katika furaha yake na katika Chumba takatifu cha arusi ya utukufu wake, kule wanaimba daima wale wenye kukutukuza na furaha isiyokadirika ya wale wenyi kutazama uzuri ya kweli ya uso wako. Kwani ni Wewe nuru ya kweli yenye kuangaza na kutakasa ulimwengu, viumbe vyote vinakuimbia milele na milele. Amina.

*Kisha tunasema:* Bwana hurumia. *(mara makumi ine) na hii sala:* Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa. .

Tunakutukuza, ee Mungu aliye-juu Bwana wa rehema, kwa sisi daima ni Muumba wa matendo makubwa yasiyofumbuliwa, matukufu na ya ajabu ambayo hatuwezi kuhesabia. Unatupa sisi usingizi sababu ya kupumzisha uzaifu wetu na kusaidia mwili wetu wenye kuelemewa na mateso. Tunakushukuru, kwani haukutuangamiza sababu ya makosa yetu, lakini unaonyesha daima mapendo yako kwa wanadamu; na ulituamsha toka sikitiko humo tulilala sababu ya kutukuza uwezo wako. Ndiyo maana, tunaomba wema wako kubwa: Angaza macho ya usikilizi wetu, ondoa roho yetu toka usingizi nzito wa uzaifu, fungua kinywa chetu, ukijaze na sifa yako ili tuweze kukuimbia Wewe bila kuregea, ee Mungu mwenye kutukuzwa katika wote na kwa wote. Baba wasiyo mwanzo, pamoja na Mwana wako wa pekee, na Roho yako Mtakatifu kamili, mwema na mletaji uzima, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Kisha: Njooni tumwinamie. . . na zaburi 120 (121)

Nitanyanyua macho yangu kwa milima, kusaidiwa kwangu kunatoka wapi? Kusaidiwa kwangu kunatoka kwa Bwana, aliyefanya mbingu na dunia. Hataacha muguu wako kuhamishwa; mwenye kukulinda hatalala usingizi. Tazama, mwenye kulinda Israeli, hatasinzia wala hatalala usingizi. Bwana ni kivuli chako kwa mukono wako wa kuume. Wala mwezi usiku. Bwana atakuchunga katika mabaya yote; atachunga nafsi yako. Bwana atakuchunga wakati unapotoka na kuingia, toka sasa hata milele.

Tena Zaburi 133(134).

Tazama ninyi munaobariki Bwana, ninyi watumishi wote wa Bwana, munaosimama usiku nyumbani mwa Bwana. Nyanyueni mikono yenu kwa pahali patakatifu, na mubariki Bwana. Bwana akubariki toka Sayuni; hata yeye aliyefanya mbingu na inchi.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Kwa kuwa. . .

*Na hii wimbo.* Sauti ya mnane.

Kumbuka watumishi wako, ee Bwana, wewe uliye mwema, na samehe makosa yaliyotendeka katika hii uzima, kwani hata mumoja asiye na zambi, ila wewe na peke yako unaweza kuwapa marehemu mapumuziko.

Kwa maarifa ya hekima yako, una vyote kadiri ya mapendo yako kwa wanadamu, na unagawanya kwa kila mumoja hii iliyo ya mafaa. Ee peke yako Muumba, pumzisha, ee Bwana, roho za watumishi wako, kwa sababu wamekutumainia wewe Mungu wetu uliyetufanya na kutuumba.

Utukufu kwa Baba. . .

Pamoja na Watakatifu pumuzisha, ee Kristu, roho ya watumishi wako, mu fasi pasipo umivu, bila sikitiko, bila muchoko, lakini uzima wa milele.

Sasa na siku zote. . . THEOTOKION..

Vizazi vyote tunakuita mwenye heri, ee Bikira Mzazi-Mungu, kwani ilimupendeza Kristu Mungu wetu akae tumboni mwako. Wenye heri ni sisi pia tunalindwa kwako; kwa maana mchana na usiku unatuombea, na nguvu ya mamlaka inasabitisshwa kwa maombezi yako. Ndiyo maana, tunakuimbia tukipaza sauti: Salamu, ee Mujaliwa neema. Bwana ni pamoja nawe.

Kisha: Bwana hurumia (*mara kumi na mbili*) na hii sala:

Kumbuka, ee Bwana. Baba zetu na wa ndugu zetu waliolala kwa matumaini ya ufufuo kwa ajili ya uzima wa milele, na wote wale waliomaliza uzima yao kwa imani na kwa ibada. Uwasamehe makosa yao yote ya kutaka na yasiyo kutaka waliotenda kwa maneno, kwa matendo ao kwa mawazo; Uwaweeke katika pahali pa nuru, pa baridi nzuri na pa mapumziko, kule hakuna wala mateso, wala sikitiko, wala kiliyo, lakini uso wako inafurahisha Watakatifu wote tangu milele. Uwaape neema ya ufalme wako, ushariki wa mema isiyokaridika na ya milele, na furaha ya uzima yako ya heri na ya milele, kwani Wewe ni uzima, ufufuo na mapumziko ya watumishi wako waliolala, ee Kristu Mungu wetu, na tunakutolea utukufu pamoja na Baba wasipo mwanzo, na Roho wako Mtakatifu, mwema na mletaji uzima, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Ee Mzazi-Mungu, Mubarikiwa, Bikira daima, Mtukufu kushinda, uipishe sala yetu kwa Mwana wako tena Mungu wetu, na kutuombea aziokoe roho zetu kwa mateteo yako.

Baba ni matumaini yangu, Mwana ni makimbilio yangu, Roho Mtakatifu ni himaya yangu, Utatu Mutakatifu, utukufu kwako.

Matumaini yangu yote ni kwako, ee Mama wa Mungu, unilinde chini ya himaya yako,

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* ee Rabi Mtakatifu barikia:

*Padri anafanya Kuaga:*

Kristu Mungu wetu ukweli, kwa maombezi ya Mama wake Mtakatifu asiye na doa wala si lawama kamili; ya Mitume Watakatifu watukufu, wasifiwa kamili na ya watakatifu wote, atuhurumie na atuokoe, kwani ni Mwema na mupenda-wanadamu.

Tuombe kwa ajili ya amani ya dunia, (Musomaji anasema: Bwana hurumia).
Kwa ajili ya wa Kristiani wa orthodoksi wote.
Kwa ajili ya wakubwa wetu na wale wenye kutuongoza.
Kwa ajili ya Askofu wetu (jina lake) na undungu wetu katika Kristu.
Kwa ajili ya wa padri na ndugu hawapo.
Kwa ajili ya wenye kutusaidia na walitusaidia.
Kwa ajili ya wenye kutuchukia wenye kutupenda.
Kwea ajili ya wale walituomba juu ya kuwaombea, japo uovu wetu.
Kwa ajili ya ukombozi ya wafungwa.
Kwa ajili ya wale weko juu ya bahari.
Kwa ajili ya wagonjwa.
Tuombe tena kwa ajili ya ujazi wa matunda hapa duniani.
Kwa ajili ya wapadri wetu na ndugu wenye kawaida ya dini waliyo kufa mbele yetu; wanaopumzika hapa na dunia nzima.
Kwa ajili ya sisi wenyewe tuseme: Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.
Kwa maombezi ya Wapadri Watakatifu wetu, ee Bwana Yesu kristu. Mungu wetu, utuhurumie.
Amina.

# MESONIKTIKON YA KILA MUPOSHO

PADRI anasema: Abarikiwe Mungu wetu. Mfalme wa mbinguni. . . Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . Bwana hurumia (*mara kumi na mbili).* Njooni tumwinamie. . . Zaburi 50(51) *na kisha hii zaburi:*

ZABURI 64 (65).

Sifa inakungojea, ee Mungu, katika Sayuni; Na kwako naziri itatimizwa. Ee wewe unayesikia maombi, wote wenye miili watakuja kwako, Maovu yananishinda; Na utasafisha makosa yetu. Heri mutu wewe unayemuchagua, na kumukaribisha akae viwanjani mwako; tutashiba kwa wema wa nyumba yako, pahali patakatifu pa hekalu lako, Kwa mambo ya hofu utatujibu kwa haki, ee Mungu wa wokovu wetu; Wewe ni tumaini la miisho yote ya dunia, na kwao walio mbali baharini, anayeweka imara milima kwa nguvu yake, akivalishwa na uwezo; anayetuliza kunguruma kwa bahari, kungururna kwa rnawimbi yake, na makelele ya watu, Nao vilevile wanaokaa mbali kabisa wanaogopa kwa alama zako; unafurahisha matokea ya asubui na ya mangaribi. Umekwenda kutazama dunia, na kuinywesha, umetajirisha kabisa; Muto wa Mungu umejaa maji. Umewapatia nafaka wakati ulipotengeneza inchi hivi. Umenyesha matuta yake kwa kufaa, umeweka vibonde vyake, umeyafanyiza teketeke kwa manyunyo, umebariki kukomea kwake. Umevika mwaka taji ya wema wako, na mapito yako yanatupa mafuta. Yanatupa juu ya malisho ya jangwa, na vilima vimefungiwa furaha. Malisho yamevikwa makundi; mabonde yamefunikwa vilevile na nafaka. Wanapiga makelele kwa furaha, wanaimba vilevile.

Zaburi 65 (66).

Mushangilie Mungu, ee inchi yote; mwimbe utukufu wa jina lake; mutukuze sifa yake.

Mumwambie Mungu: Kazi zako ni za hofu kabisa! Kwa sababu ya ukubwa wa uwezo wako adui zako watajitia chini yako. Inchi yote watakuabudu, na wataimba kwako; wataimba kwa jina lako. Kujeni mutazame kazi za Mungu; Yeye ni wa hofu kwa matendo yake kwa wana wa watu. Akageuza bahari kuwa inchi kavu; wakapita mutoni kwa miguu; pale tulifurahi ndani yake. Kwa uwezo wake anatawala milele; macho yake yanatazama mataifa; waasi wasijitukuze nafsi zao. Barikini Mungu wetu, ee ninyi watu, na sikizeni sauti ya sifa yake; anayechunga nafsi yetu katika uzima, wala haachi miguu yetu kuhamishwa. Kwa maana wewe, ee Mungu, umetupima; umetujaribu kama feza inavyojaribiwa. Umetuingiza ndani ya wavu; Umetia muzigo muzito juu ya viuno vyetu. Umepandisha watu juu ya vichwa vyetu; Tumepita katika moto na katika, maji; lakini wewe ulituleta kwa pahall pa utajiri. Nitaingia nyumbani mwako na sadaka za kuteketezwa; Nitakulipia naziri zangu, midomo yangu ilizotoa, na kinywa changu kilizosema wakati nilipokuwa katika taabu. Nitakutolea sadaka za kuteketezwa za ndama. Pamoja na uvumba wa kondoo ndume; Nitatoa ngombe ndume pamoja na mbuzi. Kujeni musikie, ninyi wote munaoogopa Mungu, na nitatangaza aliyoyafanyia roho yangu. Nililia kwake kwa kinywa changu, na alitukuzwa kwa ulimi wangu. Kama nikichunga maovu moyoni mwangu. Bwana hatanisikia. Lakini hakika Mungu amesikia; akasikiliza sauti ya maombi yangu. Mungu barikiwe, asiyenigeuzia mbali maombi yangu wala rehema yake.

Zaburi 66 (67)

Mungu aturehemu na atubariki, atuangazie uso wake. Njia yako ijulikane duniani. Wokovu wako katika mataifa yote. Watu wakusifu, ee Mungu; Watu wote wakusifu. Mataifa washangilie na waimbe kwa furaha, maana utahukumu watu kwa haki, na kutawala mataifa duniani. Watu wakusifu, ee Mungu; watu wote wakusifu. Inchi imetoa mazao yake; Mungu, hata Mungu wetu, atatubariki. Mungu atatubariki. Miisho yote ya dunia itamwogopa.

Zaburi 67 (68)

Mungu asimame, adui zake zote wasambazwe; wenye kumuchukia wakimbie vilevile mbele yake. Kama moshi inavyopeperushwa. hivi uwapeperushe; kama nta inavyoyeyuka mbele ya moto, hivi waovu wapotee mbele ya Mungu. Lakini wenye haki wafurahi, washangilie mbele ya Mungu ndiyo, washangilie kwa furaha. Imbeni kwa Mungu, imbeni sifa kwa jina lake; fanyieni njia atakayepita kwa farasi jangwani; Jina lake ni JA; na mushangilie mbele yake. Baba ya yatima, mwamuzi wa wajane, ni Mungu katika kao lake takatifu. Mungu anaweka nyumbani walio peke yao, anatoa wafungwa kwa baraka; lakini waasi wanakaa katika inchi ya kukauka. Ee Mungu, wakati ulipotoka mbele ya watu wako, wakati ulipopita jangwani. Inchi ikatetemeka, mbingu vilevile ziliangushwa usoni mwa Mungu; Hata Sayuni kule ukatetemeka usoni mwa Mungu, Mungu wa lsraeli. Wewe, ee Mungu, umetuma mvua ya kufaa; Umetia nguvu uriti wako wakati ulipochoka. Kusanyiko lako lilikaa ndani yake; wewe, ee Mungu, umetengeneza uzuri wako kwa masikini, Bwana anatoa neno, wanawake wanaopasha habari ni jeshi kubwa. Wafalme wa majeshi wanakimbia, wanakimbia; na aliyebaki nyumbani anagawa nyara. Mutalala katikati ya mazizi ya kondoo, kama mabawa ya hua yanayofunikwa kwa feza. Na bawa zake kwa zahabu ya rangi ya zahabu? Wakati Mwenyezi aliposambaza wafalme ndani yake, ilikuwa kama theluji, ilivyoanguka kwa Salmoni. Mulima wa Mungu ni mulima wa Basani; mulima murefu ni mulima wa Basani. Kwa nini munachungulia, ee milima mirefu? Kwa mulima Mungu aliotaka kwa kao lake? Ndiyo. Bwana atakaa ndani yake milele. Magari ya Mungu ni elfu makumi mbili, hata elfu elfu. Bwana ni katikati yao, kama kwa Sayuni katika pahali patakatifu. Umepanda juu, umefunga utumwa wako; umepokea zawadi katikati ya watu. Ndiyo, katikati ya waasi vilevile, hata Bwana Mungu akae pamoja nao. Bwana abarikiwe anayebeba muzigo wetu siku kwa siku, hata Mungu aliye wokovu wetu, Mungu ni kwetu, Mungu wa kuokoa; na kwa Bwana Mungu ni njia za kutoka katika mauti. Lakini Mungu atapasua kichwa cha adui zake. Ngozi ya kichwa pamoja na nyole zake anayeendelea katlka zambl zake. Bwana amesema: Nitaleta tena toka Basani. Nitawaleta tena toka vilindi vya bahari. Upate kuchovya muguu wako kwa damu, na ulimi wa imbwa zako upate sehemu yake toka

adui zako. Wameona miendo yako, ee Mungu, hata miendo ya Mungu wangu. Mufalme wangu, katika pahali patakatifu. Waimbaji walikwenda mbele, wapigaji vinanda walifuata nyuma, katikati ya wasichana wakipiga vingoma. Barikini Mungu katika makusanyiko, hata Bwana, ninyi mulio wa kisima cha Israeli. Yuko Benyamina mudogo mutawala wao. Wakubwa wa Yuda, na diwani lao, wakubwa wa Zebuluni, wakubwa wa Nafutali. Mungu wako ameagiza nguvu yako; tia nguvu, ee Mungu, uliyotutendea. Kwa sababu ya hekalu lako kwa Yerusalema Wafalme watakuletea zawadi. Hamakia nyama za manyasi, wingi wa ngombe ndume, pamoja na ndama za watu, wakikanyaga chini ya miguu vipande vya feza. Amesambaza watu wanaofurahia vita. Wakubwa watatoka kwa Misri; Etiopia itafanya mbio kunyosha mikono yake kwa Mungu. Imbieni Mungu, ninyi falme za dunia; ee, imbeni sifa kwa Bwana; Kwake anayepanda juu ya mbingu za mbingu zilizo za kale. Tazama, anatoa sauti yake, sauti ya uwezo. Hesabia Mungu nguvu; enzi yake ni juu ya Israeli, na nguvu zake mawinguni. Ee Mungu, wewe ni wa kuogopesha toka paha1i pako patakatlfu; Mungu wa Israeli, anawapa watu wake nguvu na uwezo, Mungu abarikiwe.

Zaburi 68 (69).

Uniokoe, ee Mungu; Maana maji yamefika katika nafsi yangu. Ninazama katika matope mengi pahali pasipowezekana kusimama; Nimefika katika maji ya vilindi, pahali maji yanaponlgarlklsha. Ninachoka kwa kulia kwangu; shingo langu limekauka; Macho yangu hayaoni ningali ninangojea Mungu wangu. Wao wanaonichukia pasipo sababu ni wengi kuliko nyole za kichwa changu; wao wanaotaka kunikatia mbali, wakiwa adui zangu pasipo haki ni wenye uwezo; Halafu nilipaswa kurudisha vitu nisivyovichukua. Ee Mungu, anajua upumbafu wangu; na zambi zangu hazifichwi mbele yako. Usiache wao wanaokungojea kupata haya kwa ajili yangu, ee Bwana Mungu wa majeshi; usiache wale wanaokutafuta kuzarauliwa kwa ajili yangu, ee Mungu wa Israeli. Maana kwa ajili yako nimevumilia laumu; Haya imefunika uso wangu. Nimekuwa mugeni kwa ndugu zangu, nisiyepatana na watoto wa mama yangu. Maana wivu wa nyumba yako umenikula; na laumu zao wanaonilaumu zimeniangukia. Wakati nilipotoa machozi na kuazibu roho yangu kwa kufunga, ilikuwa laumu juu yangu. Wakati nilipovaa gunia, nilikuwa mufano kwao. Wao wanaoketi langoni wanasemezana juu yangu; nami ni wimbo wa walevi. Lakini mimi, maombi yangu ni kwako, ee Bwana, kwa wakati unaokubaliwa; ee Mungu, kwa wingi wa rehema yako. Unijibu katika kweli ya wokovu wako. Uniponyeshe kwa kunitoa toka matope, wala usiniache kuzama; Uniokoe nao wanaonichukia. na katika vi1indl vya maji. Usiache maji kunigarikisha. wala kilindi kunimeza; wala shimo lisifunge kinywa chake juu yangu. Unijibu. ee Bwana; maana uzuri wako ni wema; kwa kadiri ya wingi wa rehema zako ugeuke kwangu. Wala usifiche uso wako kwa mutumishi wako; kwa sababu mimi ni katika taabu; unijibu mbio. Ukaribie nafsi yangu. na kuikomboa; Unikomboe kwa sababu ya adui zangu. Wewe unajua laumu yangu. na haya yangu. Na kuzaraullwa kwangu; watesi wangu ni wote mbele yako. Laumu imenivunja moyo; nami ninaugua sana; nikatafuta mwenye kunihurumia. lakini hakuna mutu; na kwa wenye kunifariji, lakini sikupata. Wakanipa nyongo vilevile kuwa chakula changu; na kwa kiu yangu wakanikunywesha siki. Meza yao mbele yao iwe mutego; na wakiwa na salama. iwe shabaki. Macho yao yatiwe giza. wasione; na viuno vyao uvitetemeshe daima. Mwanga gazabu yako juu yao. na ukali wa kasirani yako uwapate. Kao lao liwe ukiwa; pasipo na mutu kukaa hemani mwao. Maana wanatesa mutu wewe uliyemupiga; na wanapasha huzuni yao uliowaumiza. Ongeza uovu juu ya uovu wao; Wala wasiingie katika haki yako. Waondolewe katika kitabu cha uzima. wasiandikwe pamoja na wenye haki. Lakini mimi ni masikini na mwenye huzuni; wokovu wako. ee Mungu. uninyanyue. Nitasifu jina la Mungu kwa wimbo. na kumutukuza na kushukuru. Na itapendeza Bwana kuliko ngombe ndume. Ao ndama mwenye pembe na kwato. Wapole waliona na wanafurahi; ninyi munaotafuta Mungu, moyo wenu uishi; Kwa kuwa Bwana anasikia wenye hitaji, wala hazarau mufungwa wake. Mbingu na inchi zimusifu. Bahari na kila kitu kinachotembea ndam yake. Maana Mungu ataokoa Sayuni na kujenga miji ya Yuda; Nao watakaa pale na kuiriti. Wazao wa watumishi wake watairiti vilevile; nao wanaopenda jina lake watakaa ndani yake.

Zaburi 69 (70). *Kuomba kusaidia kwa Mungu*

Ee Mungu, uniokoe; Unisaidie mbio, ee Bwana. Wapate haya na kufazaishwa wanaotafuta nafsi yangu; Warudishwe nyuma na kuzarauliwa wanaofurahi kwa kuumia kwangu. Warudishwe nyuma kwa ajili ya haya yao wanaosema: Ewe, ewe. Wote wanaokutafuta washangilie na kukufurahia; Nao wanaopenda wokovu wako waseme daima: Mungu atukuzwe. Lakini mimi ni masikini na mwenye hitaji; Unisaidie mbio, ee Mungu; wewe ni musaidia wangu na mwokozi wangu; ee Bwana, usikawie.

Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . .

Nasadiki Mungu mmoja Baba mwenyezi, mwumba wa mbingu na wa dunia, hata vyote vilivyoonekana na visivyoonekana, tena Bwana mmoja Yesu Kristu, Mwana wa pekee wa Mungu, aliyezaliwa na Baba mbele ya wakati wote, Nuru toka Nuru, Mungu kweli toka Mungu kweli, aliyazaliwa, si muumbwa mwenye asili moja (omousion) na Baba, aliye kwake vyote vilifanywa, aliye kwa ajili yetu wanadamu na ya wokovu wetu alishuka mbinguni, akapata mwili kwa Roho Mtakatifu na kwa Bikira Maria, na akawa mtu. Aliye sulibiwa kwa ajili yetu wakati wa Pontio Pilato, Akateswa, akawekwa kaburini. Na aliyefufuka katika siku ya tatu, kama yanavyo Maandiko. Na akapanda mbinguni ndipo anapokaa kuume kwa Baba. Na atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu walio na hai na waliokufa. Ufalme wake utakuwa bila mwisho. Tena Roho Mtakatifu yu Bwana yu Mwumba hai, aliyetoka na Baba, aliyesujudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana, aliyenena kwa midomo ya manabii, kwa Eklezya moja, Takatifu, Katholiki na Apostoliki. Naungama kwa ubatizo moja kwa maondoleo ya zambi. Natumaini ufufuo wa wafu hata uzima wa milele utakapokuja. Amina.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . Na kisha mara moja hii wimbo:

Sisi duniani tunayofananishwa Majeshi ya juu mbinguni. tunakutolea wimbo wa ushindi tukiimba: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee MUngu wetu, kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Hali isiyoumbwa Fundi wa ulimwengu, fungua midomo yetu na kinywa chetu kitatangaza sifa yako pakuimba: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Bwana uliyeniamusha usiingizini mwangu, angaza moyo wangu na roho yangu, fungua midomo yangu ili ni kuimbie, ee Utatu Mtakatifu: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wangu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

*Kisha tunasema:* Bwana hurumia. *(mara makumi ine) na hii sala:*

Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa, na kutukuzwa wakati wote na katika kila saa mbinguni na duniani, uliye mwadilifu, mrahimu tele, mfazili sana unayependa wenye haki, tena kuwahurumia wenye zambi; unayewaita wote kuona wokovu, ukiwaahidi vitu vema vilivyokuja; wewe, ee Bwana, hata katika saa hii uyapokee maombi yetu, na kuyashurtisha maisha yetu njiani pa amri, uzitakase roho zetu, uyasafishe miili yetu, uyatengeneze mafikira zetu, uzinyoshe nia zetu; ukatuokoe na kila shida, ubaya, na teso, utulindie kwa Malaika wako, ili sisi tukiwa na utunzi na uongozi wao, tufike katika umoja wa imani na kuujulisha utukufu wako usiofikika. Kwa kuwa unahimidiwa milele na milele. Amina.

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia. Utukufu kwa Baba. Sasa na siku. Uliye wadamani. Kwa jina la Bwana bariki, ee padri:

Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

*Padri anasoma hii sala:*

Ndiyo, nakutukuza, ee Bwana, kwani ulitazama unyenyekevu wangu, haukunitoa mikononi mwa adui; lakini uliokoa roho yangu toka sikitiko, sasa, ee Rabi, mkono yako inilinde na rehema yako ije juu yangu, maana roho yangu inahangaika na kujazwa na sikitiko ikiwaza kausha hii mwili ya mateso na yenyi kuchafuka, nia mbaya ya adui isisimame juu yake na isiizuie sababu ya zambi mingi ilitenda katika hii uzima, kwa kujua wala bila kujua. Unihurumie, ee Rabi, roho yangu isitazame tendo la giza la pepo mchafu, lakini Malaika wenyi kuangaa na wa nuru waipokee. Tukuza jina lako takatifu, na kwa uwezo wako uniogoze kwa baraza ya hukumu yako takatifu. Wakati wa hukumu yangu, mkono ya mfalme wa hii dunia isinishike sababu ya kunivuta mimi mkosefu kuzimuni ya moto ya milele, lakini uwe karibu nami na uwe kwangu Mwokozi na mulinzi, ee Bwana, hurumia roho yangu yenye kuchafuka kwa tamaa za hii uzima, uipokee yenye kutakaswa kwa toba na maungamo, kwani umetukuzwa hata milele na milele. Amina.

*Kisha:* Njooni tumwinamia. . . *Tutasoma Zaburi 120 (121). 133 (134) na tutaedelea kusoma hii wimbo na hii sala ya yulu mupaka ku mwisho. Padri anafanya kuaga sawa vile inandikwa yulu.*

# MESONIKTIKON YA SIKU YA MUNGU

Kisha Abarikiwe. . . Mfalme wa mbinguni. . . Trisagion. . . Utatu Mutakatifu Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . Bwana *hurumia (kumi na mbili*) Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Njooni tumwinamie. . . Tunasoma Zaburi 50(51).

*Na kisha tunaimba hii wimbo:*

Sauti ya mbili

Inastahili kweli kukuimbia Utatu kamili kimungu uliye bila mwanzo; Baba Muumba wa vyote. Mwana wasipo mwanzo aliyezaliwa bila Baba, toka kwa Baba mbele ya milele, na Roho Mutakatifu aliyetoka kwa Baba mbele ya wakati.

Inastahili kweli kukutukuza, ee Mungu-Neno mwenye kuogopesha na kutetemesha Wakeruvi na kutuzwa na Majeshi ya mbinguni, uliye fufuka kaburini siku ya tatu, Kristu Mletaji-uzima, tunakutukuza na woga.

Sisi wote tunamuimbia kama inavyofaa wimbo takatifu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, utawala wa nyuso tatu, ufalme mmoja na uwezo.

Wakati, ee Bikira bila doa, ulipomuona Mwana wako akifufuka kama inavyofaa katika wafu dunia ilijaa na furaha bila kusema na inamutukuza na kumuheshimu.

Uliye wa thamani kuwashinda Wakeruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi waserafi, uliye ukimzaa Mungu Neno, umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli tunakutukuza wewe.

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . Kisha tunasoma Ipakoi ya sauti ya hii siku (*angalia Kitabu ya Paraklitiki).* Kisha Bwana hurumia (*makumi ine).* Utukufu. . . Sasa. . . Uliye wa thamani. . . Kwa jina la Bwana, bariki, ee Rabi.

PADRI: Mungu atufazili na kutubariki, atuangazie uso wake na kutuhurumia.

Musomaji: Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Rabi Mtakatifu barikia:

*Padri anafanya Kuaga sawa vile inandikwa yulu.*

# IBADA YA ASUBUI (ORTHROS)

Padri: Abarikiwe Mungu wetu daima. . .

*Hii saa padri anatayarisha chetezo na anazunguluka ndani ya kanisa ya kufukiza uvumba na chetezo.*

*Kama ni wakati ya kwarezima tunasoma:* Trisagion. Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . . kisha Bwana hurumia ( *kumi na mbili).* Njooni tumwinamie. . .

*Na hii zaburi ya chini.*

*Kama hakuna wakati ya Kwarezima, tunasoma hivi*: Njooni tumwinamie. . . *na mara moja hii zaburi ya chini:*

Zaburi 19(20)

Bwana akujibu siku ya taabu; Jina la Mungu wa Yakobo likunyanyue; Akutumie kusaidia toka pahali patakatifu na kukupatisha nguvu toka Sayuni; akumbuke za bihu zako zote, na kupokea sadaka yako ya kuteketezwa. Akupe hamu ya moyo wako, na kutimiza mashauri yako yote. Tutashangilia wokovu wako, kwa jina la Mungu wetu tutasimamisha bendera zetu; Bwana atimize maombi yako yote, Sasa ninajua ya kuwa Bwana anaokoa mupakaliwa wake; atamujibu toka mbingu zake takatifu na nguvu ya kuokoa ya mukono wake wa kuume. Wengine wanaamini magari na wengine farasi; lakini sisi tutataja jina la Bwana Mungu wetu. Wameinama na kuanguka; lakini sisi tumenyanyuliwa na tunasimama. Okoa, ee Bwana; Mufalme atujibu wakati tunapoita.

Zaburi 20 (21).

Mufalme atafurahi kwa nguvu yako, ee Bwana; na kwa wokovu wako ataona shangwe nyingi sana! Umemupa hamu ya moyo wake, wala hukuzuiza maombi ya midomo yake. Kwa sababu ulimutangulia na baraka ya vitu vizuri; unaweka taji ya zahabu safi juu ya kichwa chake. Alikuomba uhai, ukamupa; hata siku nyingi kwa milele na milele. Utukufu wake ni mukubwa katika wokovu wako; heshima na enzi unaweka juu yake. Maana umemufanya mubarikiwa zaidi kwa milele; umemufurahisha kwa furaha mbele yako. Kwa kuwa mufalme anaamini Bwana, na kwa sababu ya wema wake aliye juu sana hatatikisika. Mukono wako utapata adui zako zote; mukono wako wa kuume utawapata wanaokuchukia. Utawafanya kuwa kama tanuru ya moto, kwa wakati wa hasira yako. Bwana atawameza katika gazabu yake. na moto utawakula. Utaharibu matunda yao na kuyaondosha katika inchi, na wazao wao katika wana wa watu. Kwa sababu walikusudi mabaya juu yako; Waliwaza hila, wasiyoweza kutimiza. Kwa maana utawafanya kugeuza mugongo wao, utatayarisha na kamba za upinde wako juu ya uso wao. Utukuzwe, ee Bwana kwa nguvu zako; nasi tutaimba na kusifu uwezo wako.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Utatu Mtakatifu kamili utuhurumie, Bwana utusamehe zambi zetu, Rabi utuondolee makosa yetu, Mtakatifu utukaribie na utuponye magonjwa yetu, Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**B**aba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje mapenzi yako ya- timizwe hapa duniani kama kule mbinguni. Utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe ndeni zetu, kama sisi vilevile tunavyosamehe wadeni wetu. Na usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule mwovu.

**K**wa kuwa ufalme, uwezo na utukufu ni wako, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Ee Bwana, okoa taifa yako na bariki urizi wako. Ukiwapa wafalme kushinda juu ya wakafiri, na

kuilinda jamii yako kwa Msalaba wako.

Utukufu kwa Baba. . .

Ewe Kristu Mungu, uliyeinuliwa kusudi msalabani, uipe jamii ile jipya iliyo na jina lako, rehema yako. Uwafurahishe wafalme wetu waaminifu na nguvu yako, ukiwatunza na kushinda juu ya washindanao, wakifurahiwa kwa agano lako jipya, silaha, ya amani, alama isioshindika.

Sasa na siku zote. . . THEOTOKION

Ewe Mzazi-Mungu, Msifiwa pia, Uhifazi kuogopa na kusioshindika, usitupe maombi yetu, Mwema We. Tegemeza zamii ya waorthodoksi, uwaokoe hawa ambao umewamrisha kuwa wafalme, uwape ushindi toka mbinguni, kwa kuwa umemzaa, Mungu u peke yako Mbarikiwa.

PADRI: Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tuakuomba, utusikilize na utuhurumie.
MSOMAJI: Bwana hurumia *(mara tatu).*
PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya wakristu watawa waorthodoksi wote.
MSOMAJI: Bwana hurumia *(mara tatu).*
PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Arkiepiskopo wetu. . *(jina yake)* na kwa ajili ya undugu wetu wote.
MSOMAJI: Bwana hurumia *(mara tatu).*
Kwa kuwa u Mungu mwenye huruma, tena Mpenda-wanadamu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele.
MSOMAJI: Amina. Kwa jina la Bwana himidi, ee Padri,
PADRI: *(Anapaza sauti):*
Kwa Utatu Mtakatifu, Wenye asili moja, Muumba wa uhai, usiotengeka, utukufu uwe daima. Sasa na siku zote, hata milele na milele. MSOMAJI: Amina.

*Msomaji anaanza kusoma EKSAPSALMOS safi na nguvu na woga ya Mungu. Padri anasoma ma Sala I2 kwa siri. Wakati huu watu wanasimama wima kanisani, wenye kuingia watasimama mlangoni mpaka mwisho wa Eksapsalmos.*

MSOMAJI:
Utukufu kwa Mungu juu pia, na nchini amani, urazi kwa wanadamu *(mara tatu).*
Ee Bwana, uifungue midomo yangu, na kinywa changu kitazinena sifa zako (*mara pili*).

ZABURI 3: *Mwenye kutulinda ni Mungu*

Bwana, watesi wangu wamezidi kwangu! Wao ni wengi wanaosimama juu yangu. Wao ni wengi wanaoniambia nafsi yangu, hana wokovu kwa Bwana. Lakini wewe, ee Bwana, ni ngabo yangu pande zote; Utukufu wangu, na mwenye kunyanyua kichwa changu, nimelia kwa Bwana na sauti yangu, naye amenijibu toka mulima wake mutakatifu. Nililala na kupata usingizi; nikaamka; kwa kuwa Bwana amenitegemeza. Sitaogopa elfu kumi za watu waliojipanga juu yangu, pande zote. Simama, ee Bwana; uniokoe, ee Mungu wangu; Maana umepiga kituguta cha adui zangu zote; umevunja meno ya waovu. Wokovu ni wa Bwana; Baraka yako iwe juu ya watu wako.

*Na tena:* Nililala na kupata usingizi; nikaamka; kwa kuwa Bwana amenitegemeza.

ZABURI 37 (38): *Kukiri zambi.*

Ee Bwana, usinihamakie katika gazabu yako; wala usiniazibu kwa ukali wa hasira yako. Kwa sababu mishale yako imenichoma, na mkono wako umenipata. Hakuna uzima katika mwili wangu kwa sababu ya gazabu yako; wala hakuna afya mifupani mwangu kwa sababu ya zambi yangu. Kwa sababu zambi zangu zimenifunikiza kichwa changu; kama muzigo kunishinda.

Vidonda vyangu vinanuka, vimeoza, kwa sababu ya upumbafu wangu. Nimepindika na kuinama sana; muchana kutwa ninakwenda nikiomboleza. Kwa sababu viuno vyangu vinajaa homa; wala hakuna uzima katika mwili wangu. Mimi ni zaifu na nimepondwa sana; nimeugua kwa sababu ya masumbuko ya moyo wangu. Bwana, hamu yangu yote ni mbele yako; na kuugua kwangu hakufichwi mbele yako. Moyo wangu unapigapiga, nguvu zangu zimeniacha; nayo nuru ya macho yangu imeniondokea. Wanaonipenda na rafiki zangu wanasimama mbali na pigo langu; na jamaa zangu wanasimama mbali. Wao vilevile wanaotafuta uzima wangu wananiwekea mitego; nao wanaotafuta kuniumiza wanasema maneno mabaya, na wanawaza hila muchana kutwa. Lakini mimi ni kama kiziwi, sisikii; nami ni kama bubu asiyefungua kinywa chake. Ndiyo, mimi ni kama mutu asiyesikia, asiye na mabishano kinywani mwake. Kwa sababu ndani yako, ee Bwana, ninaweka tumaini langu; wewe utajibu, ee Bwana Mungu wangu. Kwa sababu nilisema: Wasiye wanafurahi juu yangu; wakati muguu wangu unapoteleza wanajikuza juu yangu. Kwa maana mimi ni karibu na kusita, na huzuni yangu ni mbele yangu daima. Kwa maana nitapasha uovu wangu; na kuhuzunika kwa zambi yangu. Lakini adui zangu ni wazima, wenye nguvu; nao wanaonichukia bule wamekuwa wengi. Wao vilivile wanaolipa mabaya kwa mema ni watesi kwangu kwa sababu ninafuata kitu kilicho chema. Usiniache, ee Bwana, Ee Mungu wangu, usiwe mbali nami, Ufanye haraka kunisaidia, ee Bwana wokovu wangu.

*Na tena:* Usiniache, ee Bwana; ee Mungu wangu, usiwe mbali nami, Ufanye haraka kunisaidia, ee Bwana wokovu wangu.

ZABURI 62 (63): *Kiu kwa kutumikia Mungu*

Ee Mungu, wewe ni Mungu wangu; asubui mapema nitakutafuta; nafsi yangu inaona kiu kwako, mwili wangu unakutaka sana, katika inchi ya kukauka na ya kuchoka, isiyo na maji. Hivi nilikutazama katika pahali patakatifu, nione uwezo wako na utukufu wako. Maana wema wako ni muzuri kuliko uzima; midomo yangu itakusifu. Hivi nitakubariki ningali hai; nitanyanyua mikono yangu kwa jina lako. Nafsi yangu itashibishwa kwa mafuta na vinomo; na kinywa changu kitakusifu kwa midomo ya furaha; wakati ninapokumbuka juu ya kitanda changu, na ninawaza juu yako katika makesha ya usiku. Maana wewe umekuwa musaidia wangu, na katika kivuli cha mabawa yako nitafurahi. Nafsi yangu inakufuata sana; mukono wako wa kuume unanitegemeza. Lakini wale wanaotafuta nafsi yangu, ili kuiharibu, watashuka kwa pande za chini za inchi. Watatolewa kwa uwezo wa upanga; watakuwa sehemu za imbwa za mwitu. Lakini mufalme atafurahia Mungu; kila mutu anayeapa kwa yeye atashangalia; kwa maana vinywa vyao vinavyosema uwongo vitafungwa.

*Na tena:* Wakati ninapokukumbuka juu ya kitanda changu, na ninawaza juu yako katika makesha ya usiku. Maneno wewe umekuwa musaidia wangu katika kivuli cha mabawa yako nitafurahi. Nafsi yangu inakufuata sana, mukono wako wa kuume unanitegemeza.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
Alliluia, Alliluia, Alliluia, utukufu kwako, ee Mungu. *( mara tatu na bila usujudu)* Bwana hurumia, Bwana hurumia Bwana, hurumia.

*Ile wakati Padri anatokea mlangoni wa kaskazini na atasimama mbele ya Ikone ya Bwana Yesu; ambako atakapoendelea kusoma sala I2 kwa siri, zile zilizobaki wakati alipokuwa katika pahali patakatifu. Anapoisha sala zote I2, atabusu Ikone ya Bwana Yesu miguuni na nyuma yake ataingilia mlangoni wa kusini. Msomaji anaendelea na Eksapsalmos ama Zaburi Sita.*
Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
ZABURI 87(88): *Kilio cha mugonjwa*

Ee Bwana, Mungu wa wokovu wangu, nimelia muchana na usiku mbele yako: Maombi yangu yaingie mbele yako; utege sikio lako kwa kilio changu, maana nafsi yangu inajaa taabu, na uzima wangu uanakaribi Hadeze. Nimehesabiwa pamoja nao wanaoshuka shimoni; mimi ni kama mutu asiye na munasaidia. Nimetupwa katikati ya wafu, kama waliouawa wanaolala kaburini, usiowakumbuka tena; nao wametengwa mbali na mukono wako. Umenilalisha katika shimo la chini sana, katika pahali pa giza, vilindini. Gazabu yako imenilemea sana, na umenitesa kwa mawimbi yako yote. Wao wanaonijua umewatenga mbali nami; umenifanya kuwa chukizo kwao; nimefungwa, wala siwezi kutoka. Jicho langu linaharibika kwa ajili ya mateso yangu; kila siku nilikuita, ee Bwana, nimenyosha mikono yangu kwako. Utaonyesha maajabu yako kwa wafu? Wao waliokufa watasimama na kukusifu? Wema wako utasimuliwa kaburini? Ao uaminifu wako katika uharibifu? Maajabu yako yatajuulikana gizani, na haki yako katika inchi ya usahaulifu? Lakini nimelia kwako, ee Bwana, na asubui maombi yangu yatakuwa mbele yako, Kwa nini unatupa nafsi yangu, Bwana? Kwa nini unanifichia uso wako? Nimeteswa na hali ya kufa tangu ujana wangu; ningali ninavumilia hofu yako ninafazaishwa. Hasira yako kali imepita juu yangu; maogopesho yako yamenikatilia mbali. Yamenizunguka kama maji muchana kutwa; yamenizunguka pamoja. Mupenzi na rafiki umetenga mbali nami, nao wanaonijua ni giza.

Na tena: Ee Bwana, Mungu wa wokovu wangu, nimelia nuchana na usiku mbele yako: Maombi yangu yaingie mbele yako, utege sikio lako kwa kilio changu.

ZABURI IO2 (IO3): *Bariki Bwana.*

Bariki Bwana, ee nafsi yangu; vyote vilivyo ndani yangu, vibariki jina lake takatifu. Bariki Bwana, ee nafsi yangu, wala usisahau baraka zake zote; anayesamehe maovu yako yote; anayekutia taji ya wema na rehema; anayeshibisha kinywa chako na vitu vizuri; hata ujana wako unafanywa mupya kama tai. Bwana anafanya mambo ya haki, na hukumu kwa wote wanaoteswa. Amejulisha Musa njia zake, wana wa Israeli matendo yake. Bwana anajaa huruma, ni mwenye neema, hakasiri upesi, na anajaa rehema. Hatakemea siku zote; wala hatachunga hasira yake milele. Hakututendea sawasawa na zambi zetu, wala hakutulipa sawasawa na maovu yetu. Maana sawasawa mbingu zilivyo juu sana kupita inchi, kwa kadiri ile rehema yake ni kwao wanaomwogopa. Kama mashariki ilivyo mbali na mangaribi, ndivyo alivyoweka makosa yetu mbali nasi. Kama baba anavyohurumia wana wake, ndivyo Bwana anawahurumia wanaomwogopa. Kwa maana anajua mwili wetu; anakumbuka ya kuwa sisi ni mavumbi, Lakini mutu, siku zake ni kama majani; kama ua la shamba, divyo anavyokua. Maana upepo unapita juu yake, nalo haliko; na pahali pake hapatalijua tena. Lakini wema wa Bwana ni tangu milele hata milele juu yao wanaomwogopa, na haki yake kwa wana wa wana; kwao wanaoshika agano lake, na kwao wanaokumbuka maagizo yake ili kuyafanya. Bwana amesimamisha kiti chake cha ufalme mbinguni; na ufalme wake unatawala vitu vyote. Bariki Bwana, ninyi malaika zake. Ninyi wenye uwezo kwa nguvu, munaotenda neno lake, mukisikiliza sauti ya neno lake. Marikini Bwana, ninyi majeshi yake yote; ninyi watumishi wake, munaofanya mapenzi yake. Barikini Bwana, ninyi matendo yake yote, pahali popote pa utawala wake. Bariki Bwana, ee nafsi yangu.

*Na tena:* Pahali po pote pa utawala wake: bariki Bwana, ee nafsi yangu.

ZABURI I42(I43): *Maombi kwa kusaidia na kuongozwa*

Sikia maombi yangu, ee Bwana, usikilize kusihi kwangu; katika uaminifu wako unijibu, katika haki yako. Usihukumu mutumishi wako; maana machoni mwako hakuna mutu aliye hai atahesabiwa haki. Maana adui amefuata nafsi yangu; amepiga uzima wangu chini hata udongo. Amenikalisha katika pahali pa giza, kama wale waliokufa zamani. Kwa hivi roho yangu imezimia ndani yangu; Moyo wangu ndani yangu ni ukiwa. Ninakumbuka siku za kale; ninafikili matendo yako yote; ninawaza kazi ya mikono yako. Ninakunyoshea mikono yangu; nafsi yangu inaona kiu kwa wewe, kama inchi inayochoka. Fanya mbio kwa kunijibu, ee Bwana; roho yangu inazimia;

usinifichie uso wako; nisiwe kama wao wanaoshuka shimoni. Unifanye kusikia wema wako asubui; kwa maana ninakutumainia wewe; unijulishe njia nitakayoikwenda; kwa maana ninakunyanyulia nafsi yangu. Uniponyeshe, ee Bwana, na adui zangu, ninakukimbilia unifiche. Unifundishe kufanya mapenzi yako; kwa maana wewe ndiwe Mungu wangu; Roho yako ni mwema; uniongoze katika inchi ya haki. Unipatize uzima, ee Bwana, kwa ajili ya jina lako; kwa haki yako utoe nafsi yangu katika taabu. Na kwa wema wako ukatilie mbali adui zangu, na kuwaharibu wote wanaotesa nafsi yangu; kwa maana mimi ni mutumishi wako.

*Na tena*: Ee Bwana, katika uaminifu wako, unijibu, katika haki yako, usihukumu mutumishiwako, *(mara pili*). Roho yako ni mwema; uniongoze katika inchi ya haki.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele, Amina. Alliluia, Alliluia, Alliluia utukufu kwako, ee Mungu*(mara tatu).*Matumaini yetu. ee Bwana, utukufu kwako.

*Wakati Msomaji anaposoma Zaburi sita (ao Eksapsalmos), padri anasoma Sala ya Kumi na pili zifwatazo hapa chini kwa siri mbele ya Meza Takatifu bila kofia. Kisha kwa Sala ya Tatu katika pahali Patakatifu, atatokea ku Mlango wa kaskazini sawa tulivyoandika mbele na vivi hivi.*

SALA 1

Tunakushukuru, Bwana Mungu wetu ulipotuamusha toka kitandani chetu na ulipotuuweka juu ya midomo yetu neno moja la sifa kwa kuliabudu na kuita jina lako takatifu. Tunakuomba kwa huruma ambayo umetupa daima uzima wetu, sasa tena, tuma msaada kwa wale wanaosimama mbele ya utukufu wako takatifu na ambao wakiongojea wingi wa rehema yako. Uwape kwa kusifu kwa wema wako usiyokaridika, wakipokutumikia wakati wowote katika woga wa mapendo. Kwani kwako kunatoka utukufu, heshima na ibada, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 2

Usiku, roho yetu inakesha mbele yako, ee Mungu wetu, kwani amri zako ni mwangaza wa dunia. Utufundishe kutimiza haki na utakatifu katika woga wa jina lako, kwani tunakusifu, wewe Mungu wetu. Tega siki lako, utusikilize, na ukumbuke, kwa majina yao, Bwana, wao wanao hapa na wanaoomba pamoja nasi; uwaokoe kwa nguvu yako, Bariki watu wako na takasa urizi wako, ukiwapa mataifa amani yako, kwa makanisa yako, kwa wapadri wako, kwa wenye kutuongoza na kwa watu wote; kwani jina lako kuu na zuri linabarikiwa na kusifiwa, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 3

Usiku, roho yetu inakesha mbele yako, ee Mungu wetu, kwani amri zako ni mwangaza. Utufundishe, ee Mungu, haki yako, amri zako na hukumu yako; angazia macho yetu na usikilizi wetu, kusudi tusipolala katika zambi zinazotupeleka kifoni. Fukuza giza yoyote rohoni mwetu, utupe jua ya haki na chunga uzima wetu bila magombezi chini ya chapa cha Roho yako Mtakatifu. Ongoza hatua yetu katika njia ya amani. Utupatie kuona, katika furaha, alfajiri na muchana, ili tupate kupandlisha kwako maombi yetu ya asubui. Kwa kuwa Kwako nguvu, ufalme, uwezo na utukufu ni wako Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 4

Ee Rabi, Mungu Mtakatifu hawezaye kushikwa hata na mutu moja, umesema kwa nuru kuangazia gizani, unatupumuzisha katika usingizi wa usiku na unatuamusha kwa kusifu na kurongaronga wema wako; achia kwa rehema yako, utupokee, sasa hapa, tunaposujudu mbele yako, na tunakushukuru, kadiri ya uwezo wetu. Utupatie cho chote tunapokuomba kwa ajili ya wokovu wetu; utufanye kuwa watoto wa nuru na wa muchana, warizi wa mali zako za milele. Utajirini ya

huruma yako, ukumbuke, ee Bwana, watu wako wote, wenye kuwa hapa wakipoomba pamoja nasi, na wandungu wetu wote, chini na baharini ambao po pote panapotandaza ufalme wako, wasihi mapendo yako kwa ajili ya wanadamu. Gawanya kwa wote huruma yako kubwa, ili tukipookolewa, roho na mwili, tuweze sawa milele na kusifu na uhuru wote, jina lako zuri na barikiwa, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 5

Hazina ya chemchem ya uzuri wote isiokauka Baba Mtakatifu, mtenda majabu, Mwenyezi, Rabi wa ulimwengu, wote tunakuabudu na tunakusihi, tukiita rehema na huruma yako kwa kutusaidia na kutukinga ku uzaifu wetu; utukumbuke, ee Bwana, tunakuomba pokea maimbi yetu ya asubui kama uvumba mbele yako, ili hata mmoja kati yetu asikataliwe, lakini utuchunge sisi wote katika huruma yako. Kumbuka, ee Bwana, wale wanaokesha na kuimba sifa yako, na kwa sifa ya Mwana wako wa pekee. Mungu wetu na kwa Roho yako Mtakatifu. Uwe kwao, msaada na mulinzi; upokee malalamiko yao juu ya altare yako ya kimbingu na ya kiroho. Kwani uko Mungu wetu, na tunakutukuza Bwba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

SALA 6

Tunakushukuru, ee Bwana, Mungu wa wokovu wetu, kwa mema yote unatujalia, ambako unajaza uzima wetu bila ukoma, tunangalia kwako. Mwokozi na Mtenda mema wa mioyo zetu. Ulitupumuzisha kipande ya usiku, na ulituamusha toka kitandani chetu, ukitusimamisha mbele yako kwa kuabudu jina lako tukufu. Tena, tunakuomba, ee Bwana, utupe neema nanguvu, kusudi tuwe wastahilivu wa kukuimba pamoja na kieleo, na bila kuregea pamoja na woga na mtetemeko, tukitikiza huvyo wokovu wetu wa pekee kwa ulinzi wa Kristu wako. Kumbuka, ee Bwana, wanaokulilia katika wasiyoonekana na akupingana. Kwani wewe ndiwe mfalme wa amani na Mwokozi wa nioyo zetu na tunakutukuza Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 7

Ee Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristu, umetulamusha kitandani chetu na umetukusanyisha ku saa ya maombi: kubali kufunikiza midomo yetu, pokea shukrani yetu na utufundishe mapenzi yako; kwa sababu hatujuwi ginsi ya kukuomba, isipokuwa kama wewe mwenyewe. Bwana, hautuongozi kwa Roho yako Mtakatifu. Tena, tunakuomba hata na saa hii, hatukutenda zambi, kwa neno, kwa vitendo ao kwa mawazo kwa kusudi ao kwasiyo kusudi, ondoa, rejeza na samehe. Kwani kama unahukumu makosa. Bwana, nani basi ataishi? Lakini karibu nawe kuna wokovu, Wewe peke ndiwe Mtakatifu, wewe msaada wa nguvu na mlinzi wa mioyo zetu, kwako, ee Bwana, kwainuka wimbo wetu wakati wowote ili uwezo wa utawala wako ubarikiwe na utukuzwe Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 8

Ee Bwana Mungu wetu, umefukuza mbali nasi msongonyifu wa usingizi, na ulitualika kwa mwito takatifu ili tuinue mikono wakati wa usiku na kukushukuru kwa uhaki wa hukumu; pokea maombi yetu na haja zetu, nyimbo zetu za utukufu na kazi yetu ya usiku. Utupatie, ee Mungu, ini letu la kitumaini, tumaini sabiti, mapendelezo ya kweli, bariki kuingia na kutoka kwetu, mambo yetu, vitendo vyetu, maneno yetu, tamaa zetu, utupatie kuweza kufika ku mwanzo wa siku hii, kwa kutukuza, kuimba na kwa kubariki wingi wa uzuri wako usiyonewa. Kwani jina lako takatifu kabisa libarikiwe, na utawala wako tukufu utukuzwe, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 9

Ee Rabi, Rafiki wa wanadamu, angazia mioyoni mwetu nuru safi ya ufahamu wa Mungu na fungua macho ya usikilizi wetu ku kieleo ya risala yako ya injili. Weka ndani zetu woga wa amri zako ya haeri, ili zizuwia tamaa yoyote ya uzini, tupate kuendelea katika njia ya kiroho na kuwaza na

kutenda vitu vyote, kadiri ya anasa yako mwema. Kwani wewe ndiwe unayetutakasa na kutangaza, na tunakutukuza, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 1O

Ee Bwana Mungu wetu, uwepatia wanadamu usamehe wa zambi zao kwa toba na umetuonyesha sawasawa mfano wa maarifa na wa ungamo wa zambi kwa ajili ya usamehe, toba ya nabii Daudi, ee Rabi, zambi zetu ni kubwa na nyingi sana ambamo tumeanguka, utuhurumie katika rehema yako kubwa, na katika huruma yako nyingi futa uzalimu wetu kwa sababu tumefanya zambi kwako. Bwana, unajua mafumbo na siri ya Roho za watu, na paka peke yako, una uwezo wa kusamehe zambi, unaumba ndani yetu roho safi, unatusabitisha na roho ya ezi, na unatujalisha furaha ya wokovu wako, usitufukuze mbali ya uso wako, lakini katika fazili yako, rafiki wa wanadamu, utupatie ya kukutolea sadaka ya uhaki hata siku yetu ya lufu, na kuleta zabihu zetu juu ya altare yako takatifu, kwa usamaha, huruma na mapendo kwa watu ya Mwana Wako wa pekee ambaye unabarikiwa naye, kama vile Roho yako Mtakatifu, mwema na mleta uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 11

Ee Bwana Mungu wetu, wewe unayetiisha ku mapenzi yako uwezo wa kieleo na wa roho, tunakuomba na tunakusihi, pokea utukufu wa sifa tunaokutolea, na viumbe vyote kadiri ya uwezo wetu, na utupatie kwa marudio, ipaji vingi vya wema wako kwani kila goti lipigwe mbele yako, la vitu vya mbinguni, na vya duniani na chini ya dunia; na chochote kinachovuta pumzi, kiumbe chochote, kiumbe sifa yako na kukiri ya kuwa Yesu Kristu ni Bwana kweli na mtajiri katika rehema. Kwani uwezo wote wa mbinguni unakutukuza, na tunakutukuza, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA 12

Tunakukuza, tunakuimba, tunakubariki, tunakushukuru, ee Mungu wa mababu zetu kwani umetenga mivuli ya usiku na umetuonyesha tena mwangaza wa muchana; lakini tunasihi wema wako, utupe usamehe wa zambi, na katika huruma yako kubwa, upokee maombi yetu; kwani tunajua kweli ya yhaki wako; angazia usikilizi wetu na ulinde tamaa zetu za mwili; ili tupate kutembea wastahilivu kwa kufurahi katika nuru tupate halafu kufika ku uzima wa milele, kwa sababu karibu nawe kuna chemchem ya uzima. Kwani, wewe ndiwe Mungu wetu, na tunakutukuza Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha kuzimaliza Zaburi hizi sita ao Eksapsalmos. Padri atasema na kupaza sauti kubwa hivi (Irinika):*

PADRI: Kwa amani, tumwombe, Bwana. *Msomaji atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.
PADRI: Kwa ajili ya amani kutoka juu, na ya wokovu wa roho zetu, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya amani ya dunia yote, ya kusimama kuzuri kwa Ekklezia Takatifu ya Mungu na ya umoja wa wote, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya nyumba hii Takatifu, na ya wanaoingiamo kwa imani, kwa hesima na kwa kumcha Mungu, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya Arkiepiskopo wetu. . . *(jina lake)*, ya Upresbiteri uheshimiwa, ya Ushemasi katika Kristu, ya Wateule wote na ya Watu wote, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya mji huu na inchi hii, kila mji na inchi, na ya waaminifu wanaoishi humo, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya kutupewa na hema tamu, na manenevu ya arzi, na nyakati za amani, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya sawafiri hewani, baharini na nchini, ya wagonjwa, ya wachoshwa, ya mateka, na kwa ajili ya wokovu wao, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya kutuokoa na kila sikitiko, gazabu, hatari na uhitaji, tumwombw Bwana.

PADRI: Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utufazilie, ee Mungu kwa neema yako.
PADRI: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, Asiye na doa, Mbarikiwa kushinda, Bibi wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenywe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekeye mikononi mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI: Kwako, ee Bwana.
PADRI: Kwa kuwa utukufu wote, na heshima na usujudu ni haki yako, ya Baba, na ya Mwana na ya Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha tunaimba:* Bwana ndiwe Mungu. . . (*mara Ine*). na mashairi (Zaburi 118, 29, 10, 23) yake kwa sauti ya Tropari ya JumaBwana. Kisha tunaimba: Utukufu kwa Baba. . . Tropari ya Mtakatifu ya hii siku na kisha: Sasa na siku zote. . . Theotokion ya Mzazi Mungu.

Bwana ndiwe Mungu, naye amefunuliwa kwetu, abarikiwe yeye ajaye kwa jina la Bwana.

Shairi 1: Mushukuruni Bwana kwa kuwa ni Mwema, kwa maana huruma yake ni ya milele.
Bwana ndiwe Mungu. . .

Shairi 2: Mataifa yote walinizunguka, kwa jina la Bwana naliwakatilia mbali,
Bwana ndiwe Mungu. . .

Shairi 3: Mutendo huu mutendo wa Bwana, nao ni ajabu machoni mwetu.
Bwana ndiwe Mungu. . .

*Msomaji anaimba Apolitikion ya Ufufuo ya Sauti ya ile Juma-Bwana. Kila Juma-Bwana ina sauti yake. Sauti inaanza siku ya Posho katika Esperinos (Sala ya Mangaribi) na itaisha mu Posho ingine yafwatayo mbele ya Esperinos(Sala ya Saa Tisa). Kila Sauti ina Apolitikion na Ufufuo yake.*

*Kila mwaka Kanisa Yetu Orthodokse ikona wakati ya Kwarezima mkubwa mbele ya siku Kuu ya Paska. Ile wakati ya ma siku 40 kila siku yote ya Juma, bila mu Posho na Siku ya Bwana tunaimba kisha Eksapsalmos mwimbo ingine. Nikusema pahali ya kuimba:* "Bwana ndiwe Mungu. . . . *"ile wakati ya Kwarezima tunaimba "Alliluia, Alliluia, Alliluia" mara Ine na ma shahiri katikati yao. Kisha hatuimbe Apolitikia ya Watakatifu, lakini tunaimba Wwimbo za Utatu Mutakafu katika sauti ya ile Juma. (Tafuta ndani ya Saa Ukubwa).*

*Tazama ma shahiri ya wakati ya Kwarezima:*
MSOMAJI:
Vituo: 1)Ee Bwana. tangu usiku roho yangu kwa sala inaongojea alfajiri Yako. maana amri zako ni nuru duniani.
MWIMBAJI: Alliluia *(mara tatu).*

Vituo: 2) Jifunzeni haki. ninyi wote wakaaji wa dunia.
MWIMBAJI: Alliluia *(mara tatu).*

Vituo: 3) Wivu utangukia watu wapotevu. sasa moto itawateketeza maadui zako.
MWIMBAJI: Alliluia *(mara tatu).*

Vituo: 4) Mwaajibu. ee Bwana. uwazibu vikali kwa mateso Wenye sifa wote wa dunia.
MWIMBAJI: Alliluia *(mara tatu).*

*Kisha Tropari yote na Theotokion Padri anasema:*
Tena na tena, kwa amani, tumwombe Bwana.

MSOMAJI: Bwana, hurumia.
PADRI: Utulinde, utuokoe, utuhurumie, ee Mungu kwa neema yako.
MSOMAJI: Bwana, hurumia.
PADRI: Tumukumbuke Maria Mtakatifu Kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, Bibi wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mumoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia tujiwekee mikononi mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI: Kwako, ee Bwana.
PADRI: Kwa kuwa nguvu ni yako, na ufalme, na uwezo, na utukufu na wako, wa Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha Waimbaji wataimba katika kitabu ya Paraklitiki ao katika kitabu ya Pentekostari, kama ni wakati yake. Pentekostari maana yake: Mwanzo wa Paska mpaka masiku makumi tano(50). Kathisma mbili ya Ufufuo na Theotokion. Kama hakuna siku ya makumbusho wa Mtakatifu, wataimba Kathisma moja ya Mtakatifu na Theotokion yake. Kila Juma ya Bwana kwa mwaka muzima wanaimba Evlogitaria ya Ufufuo.*

## MAHIMIDI YA UFUFUO (EVLOGITARIA)

*Kila Juma ya Bwana ku Mwaka Muzima.*
*Sauti ya Tano. Mbele ya kila Tropari tunasema:*

Ee Bwana, umehimidiwa U, unifundishe zilizo haki zako.
Makusanyo ya Malaika yalistaajabu ukikuona umehesabiwa mfu, tena kuiharibu nguvu ya kifo, ee Mwokozi, na kumfufua Adamu pamoja nawe, hata kuwapa uhuru kwa mateka wote wa kuzimu.

Ee Bwana, umehimidiwa U, unifundishe zilizo haki zako.
Enyi Binti wanafunzi kwa nini munayachanganya machozi na manukato kwa huzuni? Malaika aliyemeta Kamurini, aliwanenea wanawake walioleta manukato: Tazameni kaburi na kufahamu, maana Mwokozi amefufuka shimoni.

Ee Bwana, umehimidiwa U, unifundishe zilizo haki zako.
Alfajiri mapema wanawake walioleta manukato, walijiharikisha kwenda kaburini pako, ee Bwana, wakiomboleza. Walakini walimuona malaika mbele yao, aliyewaambia: Wakati wa maombolezo umekwisha kuisha; musilinieni na kuwahubiri mitume neno la ufufuo.

Ee Bwana, umehimidiwa U, unifundishe zilizo haki yako.
Wanawake walioleta manukato wakija nayo kaburini pako, ee Mwokozi, walimusikiliza Malaika, ambaye kwa sauti kubwa aliwanenea; munamuzania ndiye aliye hai kuwa katika wafu? Maana kwa kuwa Mungu amefufuka shimoni.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.
Tumsujudu Baba, tena Mwana, na Roho Mutakatifu, Utatu Mutakatifu, hali ya asili moja, tunapaliza sauti pamoja na Waserafi, tukisema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, wewe, ee Bwana.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
Ewe Bikira, ukimzaa Mpaji wa uhai, umemkomboa Adamu na zambi, tena umempa Eva furaha kisha huzuni, na hawa wanaoanguka na uzima, wamerudishwa na yeye, aliyepata mwili nawe, Yu Mungu binadamu.
Alliluia, Alliluia, Alliluia, tukufu kwako. ee Mungu *(mara tatu).*

*Kisha Padri atasoma kwambatisha fupi hivi:*
PADRI:  Tena na tena, kwa amani tumwombe Bwana.
MSOMAJI:  Bwana, hurumia.
PADRI:  Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utufazilie, ee Mungu, kwa neema yako.
MSOMAJI:  Bwana, hurumia.
PADRI:   Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, Mbarikiwa  kushinda, Bibi wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu  wote, ili sisi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu  pia, tujiwekeye mikononi mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI:  Kwako, ee Bwana.
PADRI:   Kwa kuwa jina lako limehimidiwa, ufalme wako umetukuzwa, wa  Baba na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele  na milele. Amina.

*Kisha Msomaji atasoma Hypakoi ya sauti;  tena waimbaji wataimba  Anabathmi ya Sauti yaJuma-Bwana na Prokimenon ya Ufufuo mu Kitabu  ya Paraklitiki.*

## KANUNI

*Kisha Prokimenon Msomaji ataimba Kanuni ya Paraklitiki na Mineo. Kama ni wakati ya Triodi ao wa Pentekosti, ataimba:  Kanuni ya Ufufuo, anuni ya Triodi ao Pentekostari na Kanuni ya Mineo. Mbele ya Tropari ya Kanuni ya Ufufuo, wataimba hii:*
**" Utukufu ku Ufufuo wako Takatifu, ee Bwana".**
*Mbele ya Tropari ya Kanuni za Mzazi-Mungu, wataimba:*
**"Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe".**
*Mbele ya Tropari ya Kanuni za Watakatifu, wataimba:  "*
**Mutakatifu (kama iko mingi Watakatifu) wa Mungu, utuombee (ao mutuombee)".**
*Mbele ya Tropari ya Kanuni za Triode ao za Siku Kuu ya Rabi, wataimba:  "*
Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako".
*Kisha Shairi ya tatu ya Kanuni hizi, Padri atatuma kwambatisha  fupi hivi:*

PADRI:   Tena na tena, kwa amani, tumwombe Bwana.
MSOMAJI:   Bwana, hurumia.
PADRI:   Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utufazilie, ee Mungu kwa neema yako.
MSOMAJI:   Bwana, hurumia.
PADRI:   Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, Bibi  wetu Mutukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili  sisi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia tujiwekeye  mikononi mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI:   Kwako, ee Bwana.
PADRI:   Kwa kuwa u Mungu wetu, na kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siklu zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha wataimba Kathisma na Theotokion  toka Mineon ao Triode ao Pentikostari. Kisha wataendelea  Kanuni. Msomaji akimaliza mashairi ya ine, na sita. Padri atasoma tena kwambatisha fupi hivi:*
PADRI:   Tena na tena kwa amani, tumwombe, Bwana.
MSOMAJI:   Bwana, hurumia.
PADRI:   Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utufazilie, ee Mungu kwa neema yako.
MSOMAJI:   Bwana, hurumia.
PADRI:   Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, Mbarikiwa kushinda, Bibi  wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili  sasi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia tujiwekeye  mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI:   Kwako, ee Bwana.

PADRI: Kwa kuwa wewe u Mfalme wa amani tena Mwokozi wa roho zetu, na kwako tunautoautukufu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha, atasoma Kondakion na Ikos. Wakati huu atasoma maneno ya mwisho ya Kondakion ao ya Ikos, ataimba pia pole pole kwa mara ya pili maneno haya mwishoni. Kisha Ikos atasoma Sinaksari ya Watakatifu wa ile siku. Kisha waimbaji wataimba ao watasoma ma Kanuni ingine: (7. 8. 9. )*

*Kanuni zikimalizika, waimbaji wataimba Katavasia (maana yake Kushuka). Wakati huu watu wanashuka vitini mwao vinavyowekwa kandokando ya ukuta wa Kanisa mpaka ku shairi ya mwimbo mnane. Kila wakati una Katavasia yake.*

## EVANGELIO YA ASUBUI

*Kila Juma-Bwana, hapa kisha KATAVASIA. wanasoma Evangelio ya Asubui ya Juma-Bwana kwa taratibu hii:*
*TANGAZO: Padri anasoma Evangelio katika pahali Patakatifu, kuume kwa Altare (Meza Takatifu), kusini kwake na kutazama upande wa kushoto "Kaskasini" alipo mutu wa taa, Karibu kuumaliza usomi anakwenda mlangoni Bora na kuwabariki watu kwa kitabu cha Evangelio. Wa Evangelio wote ya asubui iko 11. Angalia hapa:*

1. Matayo: 28. 16-2 2.
2. Marko: 16. 1-8 3.
3. Marko: 16. 9-20.
4. Luka: 24. 1-12.
5. Luka: 24. 12-35.
6. Luka: 24. 36-53.
7. Yoane 20. 1-10.
8. Yoane 20. 11-18.
9. Yoane 20. 19-31 10.
10. Yoane 21. 1-14 11.
11. Yoane 21. 15-25

PADRI: Tumwombe Bwana.
MSOMAJI: Bwana hurumia.
PADRI: Kwa kuwa U Mtakatifu, ee Mungu wetu, na kuwakalia watakatifu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Tunaimba mara tatu Shairi hii:*
Kila mwenye pumuzi, na amsifu Bwana. Kila mwenye pumuzi, ma amsifu Bwana. Na amsifu Bwana, kila mwenye pumuzi.

PADRI: Na tumusihi pumuzi Mungu wetu atustahilize, kusikiliza Evangelio Takatifu. .
MSOMAJI: Bwana, hurumia, Bwana, hurumia, Bwana hurumia.
PADRI: Hekima; inukeni tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote. *(anabariki watu).*
MSOMAJI: Na kwa roho yako.
PADRI: Somo ya Evangelio Takatifu ilioandikwa na. . . *(Jina la Mwevangelizaji).* Tusikilize.
MSOMAJI: Utukufu kwako. ee Bwana, utukufu kwako.

*Anasoma na sauti nzuri hii sala ya chini.*
MSOMAJI: Tukiona ufufuo wa Kristu, tumsujudu Yesu Bwana Mtakatifu aliye peke yake bila zambi. Tunausujudu msalaba wako, ee Kristu, tena tunausifu na kuutukuza ufufuo wako

takatifu. Kwa kuwa wewe Mungu wetu, la wewe peke yako hatumjui mwengine, jina lako tunaliita. Njoni enyi waaminifu wote, tuusujudu ufufuo takatifu wa Kristu. Kwa kuwa. je! Kwa ajili ya msalaba umefika furaha katika dunia mzima. Tukimhimidi Bwana daima, tunasifu ufufuo wako; kwa sababu akiuvumilia masalaba kwa ajili yetu, aliangamiza kifo kwa kifo chake.

ZABURI 50 (51)

*Wakati wanapoimba "Unirehemu. . . "Padri anatoka Mlangoni Bora akisimama kati ya Kanisa na kuwabususha watu Evangelio Takatifu na mkono wake wa kuume.*

Unirehemu, ee Mungu, sawasawa na wema wako; sawasawa na wingi wa rehema zako uzime makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, na kunisafisha na zambi yangu. Maana ninajua makosa yangu, na zambi yangu ni mbele yangu daima. Nimekukosea wewe peke yako, na kufanya yaliyo mabaya machoni mwako; ili ujulikane kuwa mwenye haki wakati unaposema, na kuwa safi wakati unapotea hukumu. Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu; na katika makosa mama yangu alinichukua mimba. Tazama, wewe unataka kweli moyoni, na kwa siri utanijuulisha hekina. Unisafishe kwa hisopo na nitakuwa safi; unioshe, na nitakuwa mweupe kupita theluji. Unifanye kusikia furaha na shangwe; ili mifupa uliyovunja ifurahi. Ufiche uso wako usitazame zambi zangu; na uzima maovu yangu yote. Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye eupya roho nzuri ndani yangu. Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako Mtakatifu. Unirudishie furaha ya wokovu wako; unitegemeze kwa roho ya tayari. Halafu nitafundisha wenye makosa njia zako; na wenye zambi watarudi kwako. Uniponyeshe na damu ya watu, ee Mungu, wewe Mungu wa wokovu wangu; ulimi wangu utaimba na sauti haki yako. Ee Bwana, ufungue midomo yangu, na kinywa changu kitaonyesha sifa zako. Maana hupendezwi na zabihu, ao ningeitoa, huvunjika, moyo uliovunjika na wa toba hutauzarau, ee Mungu. Utendee Sayuni mema kwa mapenzi yako, ujenge kuta za Yerusalema. Halafu utafurahi kwa zabihu za haki, kwa sadaka ya kuteketezwa, na sadaka nzima ya kuteketezwa; halafu watatoa ngombe ndume juu ya masabahu yako.

*Kisha Zaburi 50 (51) katika Juma-Bwana tunaimba Tropari zake hii:*

Sauti ya pili.
Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Kwa ajili ya maombezi ya Mitume, ee Mrahimu, uufute wingi wa zambi zangu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Kwa ajili ya maombezi ya Mzazi-Mungu, ee Mrahimu, uufute wingi wa zambi zangu.

Mrahimu, unihurumie, ee Mungu, sawasawa na huruma yako kubwa, kiasi cha wingi wa rehema zako, uyafute makosa yangu. Yesu akifufuka kamurini vivi hivi alivyosema, ametupa uzima wa milele, na huruma kubwa.

*Kisha Padri ataingia ku Mlango Bora; akisimama mbele ya Meza Takatifu, atasema kwa sauti nzuri sala hii: Kama ni Shemasi Kanisani atasimama inje ya Mlango Bora na atasema hii sala.*

PADRI. Ee Mungu uwaokoe watu wako ukaubarikie urizi wako. Agua dunia yako kwa huruma na rehema; paza pempe ya wakristu waorthodoksi, ukakunjua juu yetu mafazili yako tele; kwa ajili ya maombezi ya Maria Bibi yetu msiye na doa. Mzazi-Mungu na Bikira daima. Kwa nguvu ya Msalaba mheshimiwa na tukufu. Kwa matunzo ya majeshi yaheshimiwa ya mbinguni yaliyo bila mwili. Kwa maombi ya Yoane Mtangulizi, Mbatizaji, Nabii, Mtukufu na Muheshimiwa, Ya Mitume Watakatifu Watukufu na Wasifiwa, ya Wapadri wetu ambao katika Watakatifu na Waaskofu na Walimu Wakubwa, Bazile Mkubwa, Grigori Mutheologo, Yoane Krisostomo, Athanasie na Kirilli, Yoane Mrahimu, wapatriarka wa Aleksandria, Nikola wa Mira, Spirido Askofu Trimithunta wa muujiza, ya

Mashahidi Watakatifu watukufu na washindaji wazuri; ya wapadri Watawa na Wabebaji-Mungu; ya Mashahidi Watakatifu watukufu wakubwa, ya Yeorghi Mumebaji ya ushindi (Mtropeoforo), Dimitri mwenye kutosha manukato (Mirovliti), Theodoro Mukubwa wa askari na Theodoro Jemadari (Mstratilati); ya Mababu-Mungu Watakatifu na wenye haki Yoakimu na Anna; ya Mtakatifu *(anataja jina na majina ya kujulisha mtakatifu wa siku ile*) aliye tunakumbuka (tunamukumbuka) leo hata na Watakatifu wako wote pamoja, Tunakusihi, ee Bwana, uliye peke yako na huruma kubwa, usikie sisi watu wenye zambi tukikuomba na ukatuhurumie.

MSOMAJI: Bwana, hurumia *(mara 12).*
PADRI: Kwa kurehemu, na huruma, na upendo-wanadamu wa Mwana wako wa pekee, pamoja naye Uhimidiwa, pamoja na Roho wako Mtakatifu kamili, Mwema, Mpaji-uhai, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
PADRI: Mzazi Mungu na Mama wa Nuru, tukimheshimu kwa nyimbo, na kumtukuza.

## WIMBO WA MARIA MZAZI-MUNGU (Luka 1, (46-55).

MSOMAJI: Inamutukuza Bwana nafsi yangu na roho yangu imeshangilia katika Mungu Mwokozi wangu.
*Kisha ya kila shairi tunaimba hii mwimbo ya Mzazi-Mungu:*
Uliye wa thamani kuwashinda Wakeruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi Waserafi, uliye ukimzaa Mungu Neno, umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli tunakutukuza wewe.

MSOMAJI: Kwa kuwa umeaangalia unyenyekevu wa mjakazi wako, maana sasa vizazi vyote wataniita mbarikiwa.
Uliye wa thamani. . .

MSOMAJI: Kwa kuwa Mweza yeye amenitendea makuu, na jina lake ni takatifu; tena huruma yake hudumu vizazi hata vizazi kwa wao wanaomwacha.
Uliye wa thamani. . .

MSOMAJI: Amefanya nguvu kwa mkono wake; amewatanya walio na kiburi katika mawazo ya mioyo yao.
Uliye wa thamani. . .

MSOMAJI: Amewaangusha waweza na viti vyao vya ezi, tena amewapaza wanyenyekevu; wenye njaa amewashibisha mema, na wenye mali amewaondoa mikono mitupu.
Uliye wa thamani. . .

MSOMAJI: Amesaidia Israele mtumishi wake, ili kukumbuka huruma, kama alivyowaambia Baba zetu, Ibrahimu na uzao wake hata milele.
Uliye wa thamani. . .

*TANGAZO: Tropari: " Uliye wa thamani. . . "inaimbwa kila mara kwa sauti ya Katavasia vilevile. Mwishoni tunaimba Katavasia ya Tisa.*

PADRI: Tena na tena, kwa amani tumwombe Bwana.
MSOMAJI: Bwana, hurumia.
PADRI: Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utuhifazie, ee Mungu kwa neema yako.
MSOMAJI: Bwana, hurumia.

PADRI: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili Asiye na doa, mbarikiwa kushinda. Bibi wetu Mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yatu pia, ujiwekeye mikononi mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI: Kwako, ee Bwana.
PADRI: Kwa kuwa yanakusifu majeshi yote ya mbuinguni, na kuuleta utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kunafwata Shairi za ufufuo zifwatazo:*
WAIMBAJI A: Bwana Mungu wetu ndiye Mtakatifu.
WAIMBAJI B: Bwana Mungu wetu ndiye Mtakatifu.
WAIMBAJI A: Mpazeni Bwana Mungu wetu; sujuduni penye kiti cha miguu yake.
WAIMBAJI B: Kwa kuwa ndiye Mtakatifu.

*Eksapostilari ya Ufufuo na Nyimbo ya Mzazi-Mungu (Theotokion). Utawapata mu Kitabu ya Paraklitiki ku mwisho yake. Kisha tunaimba Eksapostilari ya Mtakatifu ya hii siku na Theotokion ya Mineon.*

## MASIFU.

WAIMBAJI *wa kwanza.*
Kila mwenye pumuzi na amsifu Bwana. Musifu Bwana katika mbinguni, musifu Bwana katika pahali palipo juu. Sifa inafaa kwako, ee Mungu.
WAIMBAJI *wa pili.*
Mumusifu ninyi Malaika zake zote. Mumusifu nguvu yake yote. Sifa inafaa kwako, ee Mungu.

*Waimbaji wa kwanza wataanza kuimba Tropari ya Masifu ya Paraklitiki. Mbele ya kila mwimbo wataimba moya shairi ya Zaburi yafwatayo:*

1. Kuwafanya hukumu iliyoandikwa; huo utukufu wa watawa wake wote.
2. Musifuni Mungu katika patakatifu pake; musifuni katika anga la uwezo wake.
3. Musifuni kwa matendo yake makuu, usifuni kwa kadiri ya wingi wa ukuu wake.
4. Musifuni kwa mvumo wa trumpeta, musifuni kwa kinanda na kinubi.
5. Musifuni kwa ngoma na michezo, musifuni kwa nzenze na filimbi.
6. Musifuni kwa matoazi yavumayo tamu; musifuni kwa matoazi yavumayo sana, Kwa mwenye pumuzi na amsifu Bwana.
7. Amuka, ee Mungu, Bwana wangu, uinue mkono wako, usisahau wamasikini wako mwisho.
8. Nitakushukuru, ee Bwana, kwa moyo wangu wote, nitayasimulia matendo yako ya ajabu.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.
*Sasa wanaimba mwimbo Eothinon. Iko ku mwisho ya Paraklitiki. Kisha Eothinon wanaimba hii:*

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
Mbarikiwa Ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, Laana imekufa, Eva amekombolewa, Mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa U Kristu Mungu wetu, liyependezwa hivi. Utukufu kwako.

*Kisha Masifu wataimba Doksologia Mkubwa, maana yake ni mwimbo kubwa kwa kumusifu na kumushukuru Mungu.*

# DOKSOLOGIA MKUBWA

Utukufu kwako uliyeonyesha mwangaza, utukufu kwa Mungu juu pia; amani katika inchi mapendo kwa wanadamu.
Tukusifu, tukuhimidi, tukusujudu, tukutukuza, tukushukuru, maana utukufu wako ni mukubwa.
Ee Bwana Mufalme Mungu wa yulu na mbinguni, Baba mwenyezi; Ee Bwana Mwana wa pekee Yesu Kristu, na wewe Roho Mutakatifu.
Ee Bwana Mungu we, Mwana Kondoo wa Mungu, Mwana wa Baba, unayezibeba zambi za dunia, utuhurumie, unayezibeba zambi za dunia.
Upokee ombi letu, Unayeketi kuume kwa Baba na kutuhurumia.
Kwa kuwa Mtakatifu wa pekee, Bwana wa pekee Yesu Krtistu, katika utukufu wa Mungu Baba. Amina.
Kila siku nitakuhimidi, nitasifu jina 1ako la milele, hata milele na milele.
Ee Bwana, utujalie siku hii kutujilinda na zambi.
Umehimidiwa u, ee Bwana Mungu wa Baba zetu, jina lako Iimesifiwa na limetukuzwa milele. Amina.
Ee Bwana, huruma yako iwe nasi, sawa tunakutumainia wewe.
Ee Bwana, umehimidiwa u, unifundishe zilizo haki zako, *(mara tatu ).*
Ee Bwana wewe U kimbilio letu kizazi baada ya kizazi. Mimi nilisema: ee Bwana unihurumie. uiponye roho yangu, maana nimekutendea zambi.
Kwa sababu kwako iko chemchem ya uzima, katika mwangaza yako tutaona rnwangaza. Onyesha huruma yako kwa wao wakujuwa.
Mungu Mutakatifu, Mweza Mutakatifu, Musiye kufa Mutakatifu, utuhurumie. *(mara tatu).*
Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mutakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
Musiye kufa Mutakatifu, hutuhurumie.

Mungu Mutakatifu, Mweza Mutakatifu, Musiye kufa Mutakatifu, utuhurumie.

Leo wokovu ulifanyika duniani, tumwimbie mwenye kufufuka toka kaburi na mukubwa wa uzima wetu. Kwa sababu kwa lufu alibomoa mauti na alitupatia ushindi na rehema kubwa.

*Wakati inaimbwa Doksologia. Padri anasoma kwa siri moyoni mwake na Shemasi (ao peke yake) mbele ya Meza Takatifu kwambatisha kubwa, kumaliza na mwago (kuacha).*

## KWAMBATISHA KUBWA

SHEMASI ao PADRI:

Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba, utusikie na utuhurumie.

Tena tunakuomba kwa ajili ya Askofu wetu. . . *(jina yake).* na kwa ajili ya wandugu wote.

Tena tunakuomba kwa ajili ya wakristu watawa waorthodoksi wote.

Tena tunakuomba kwa ajili zetu wapresviteri, washemasi, Watawa na ndugu zetu wote katika Kristu.

Tena tunakuomba kwa ajili ya watumishi wa Mungu wakristu waorthodoksi wanaokaa ao kupita mji na inchi hii, waparishyoni, wasimamizi, wasaidizi, wanaoweka sadaka katika nyumba hii takatifu, ili wapewe huruma, uzima, amani, afya, wokovu, kuzuru, masameo na maondoleo ya zambi.

Tena tunakuomba kwa ajili ya warehemu wajengazi wa nyumba hii Takatifu na heshimiwa kamili, wakichoka, wakiimba, na ya watu wote wanaosimama hapa, na kuingojea wapewe huruma yako kubwa na kitajiri.

PADRI: Kwa kuwa U Mungu Mrahimu na Mpenda-Wanadamu, na kwako tunakutolea utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

## KUMALIZA

SHEMASI ao Padri:
Tumalize ombi letu la asubui kwa Bwana.
Utulindie, utuokoe, utuhurumie, utufazile, ee Mungu kwa neema yako.
Siku hii kubwa kamila, takatifu, tulivu, bila zambi tuombe kwa Bwana.
Malaika wa amani, mwongozi mutumainifu, mulinzi wa roho na mwili yetu, tuombe . .
Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na ya makosa yetu pia, tuombe. . .
Vilivyo vyema na vifanyo kwa roho zetu kwa amani na toba ya dunia yote, tuombe. . .
Kuimarisha maisha yetu inabaki katika amani na toba, tuombe kwa Bwana.
Tuombe ili mwisho wetu uwe kikristu, kwa amani, bila maumivu, bila aibu, tena kutuona teto njema mbele ya kiti cha hukumu cha Kristu.
Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda, Bibi wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote; ili sisi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekeye mikononi mwa Kristu Mungu.
PADRI: Kwa kuwa U Mungui wa huruma, wa rehema na kuwapenda wanadamu, kwako tunautoa utukufu, kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

MSOMAJI: Amina.
PADRI: Amani kwa wote.
WAIMBAJI: Na kwa roho yako.
SHEMASI: Tuinamishe vichwa vyetu mbele ya Bwana.

WAIMBAJI: Kwako, ee Bwana.

*Padri kwa siri anasoma hii sala:*

Ee Bwana, uliye ukikea, juuni, unavisimamisha vilivyo chini, tena kwa jicho lako lilio kuviona vyote unauangalia ulimwengu wote, tumekuinamia shingo la roho na la mwili, tunakyomba ewe Mtakatifu wa Watakatifu, Uunyoshe mkono wako juu ya sisi kuuona kutoka katika makao yako matakatifu, ukatubariki sisi wote, ukatusamehe kila kosa tuliikosa kwa kutaka wala si kwa kutaka, utupe sisi vyema vyako vilivyo hapa duniani na huku uliimwenguni wa kuja.

*Padri anapaza sauti na anasema:*

Kwa kuwa kutuhurumia na kutuokoa ni kwako, ee Mungu wetu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Waimbaji sasa wanaimba wimbo ya Apostikha toka kitabu Paraklitiki ao ya kitabu ya Mineon; Kisha Apostikha padri atasema hii sala:*

Ni vema kumuungama Bwana, kuimbia jina lako ewe uliye juu kutangaza alfajiri rehema yako, na ukweli wako usiku kucha.

*Kisha Trisagion:* Mungu Mutakatifu. . . Utatu Mutakatifu. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

*Waimbaji wanaimba Apolitkion ya Watakatifu wa leo na Theotokion ya sauti ya Apolitikion. Kisha Padri atasema Ektenia:*

Tuseme sisi wote...Ee Bwana Mwenyezi...Utuhurumie sisi, ee Mungu kadiri ya wingi wa rehema yako..Kwa kuwa Wewe Mpenda wanadamu Mungu...Amina.

SHEMASI ao PADRIi: Hekima.
*Padri mkubwa ao waimbaji:* Bwana Mungu aiimarishe imani takatifu isiyo na lawama ya wakristu watawa waorthodoksi, katika Kanisa Takatifu milele na milele.

PADRI: Utukufu kwako, ee Mungu, Matumaini yetu, utukufu kwako.
WAIMBAJI: Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia, Rabi Mutakatifu barikia.

PADRI: Uliye umefufuka katika wafu, (hivi: *paka siku ya Mungu asubuyi*) Kristu Mungu wetu wa kweli, kwa maombi ya Mama Mtakatifu asiye na doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa msalaba uheshimiwa na uhuishaji, kwa matunzo ya Majeshi maheshimiwa ya mbinguni juu yasiyo na mwili; kwa maombezi ya Yoanno Nabii, Mtangulizi, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu, ya Mitume Watakatifu, Watukufu, Wasifiwa kamili, ya Mashahidi Watakatifu, Watukufu,Washindaji wazuri, ya Wapateri Watawa na wabebaji-Mungu (*ya Mutakatifu musimamizi wa Kanisa*), ya Yoakim na Anna Mababu-Mungu, watakatifu na wenye haki, (*ya mutakatifu wa ile siku*) makumbusho yake ya leo, hata ya watakatifu wote, atuhurumie, akatuokoe, ya Mungu Mwema, Mrahimu na Mpenda-wanadamu.

Kwa maombezi ya Wapadri Watakatifu wetu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

Waimbaji*:* Amina.

Elezo*: Kama ni nyakati ya Kwarezima mbele ya Pasaka, kisha Trisagion, hatuimbe Apolitikia ya Watakatifu, lakini padri ao Mukubwa padri ya Kanisa anasema hii sala:*

Ee Mzazi-Mungu, mlango wa mbingu, tunaposimama hekaluni kwa utukufu wako, tunazani ya kama tunasimama mbele ya mbingu, basi, utufungulie mlango ya huruma yako.

Msomaji*:* Bwana hurumia *(Mara makumi ine).* Uliye wa thamani. . . Kwa jina la Bwana bariki, ee Rabi.

Padri*:* Ahimidiwe Kristu Mungu wetu, daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

*Padri ao Mukubwa ya Kanisa anasoma hii sala:*

Ewe Mfalme wa mbingu, chunga waaminifu, wafalme, wetu; sabitisha imani; leta amani kwa inchi zote; ukimya duniani; linda vema Kanisa yetu Takatifu (Mission ao Monasteri); wale walioondoka toka hii dunia*:* Mapadri na ndugu zetu uwaweke pahali pa wenye haki; na sisi utupokee katika toba na ungamo kama Mwema na Mpenda-wanadamu.

**ELEZO:** *Kisha tunafanya Metania (kupika magoti) tatu na kusema kwa kila metania moja-moja sala ya ile inafwatayo ya Mtakatifu Efremi wa Siria*

Ee Bwana na Rabi wa uzima wangu, ondoa mbali nami roho ya uvivu, ya utawanyiko, ya kutawala wengine na maneno ya bure.

Unipe roho ya usafi, ya unyenyekevu, ya uvumilivu na ya mapendo, mimi mtumishi wako.

Ndiyo, ee Bwana mfalme, unipe nione zambi zangu tena nisimuhukumu ndugu yangu, kwani umehimidiwa milele na milele. Amina.

*Kisha tunafanya Metania kidogo Kumi na mbili na kisha moya Metania mukubwa na kusema:*
Ndiyo, ee Bwana mfalme, unipe nione zambi. .
*Padri anafanya Kuaga, sawa juu pia. ( Apolisis).*

**MAFASIRIO**

*Wakati wanapoimba wimbo hii, kisha Doksologia.* "Leo wokovu umefika duniani. . . *"Shemasi atachukua Orario kwa vidole Tatu vya mkono ya kuume atainamisha kichwa kwa Padri akisema:*
SHEMASI: Huo ndio wakati wa kutenda kwa ajili ya Bwana; Bariki, ee Rabi Mutakatifu.

*Padri atamuweka mukono ya kuume kichwani pake akisema:*
Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
SHEMASI: Uniombee, ee Padri Mutakatifu.
PADRI: Bwana aongeze hatua zako katika matendo mema.
SHEMASI: Unikumbuke, ee Rabi Mutakatifu.
PADRI: Bwana Mungu akukumbuke katika ufalme wake, wakati wowote, sasa na siku zote, hata milele na milele.
SHEMASI: Amina.
*Shemasi atatoka na atasimama pa fasi yake ya desturi. Padri atasimama mbele ya Meza Takatifu. kichwa bila kofia, atasujudia mara tatu na kusema kwa sauti chini:*

Mfalme wa mbingu, wewe mfariji, Roho wa kweli, uliye pahali popote na kuvijaza vitu vyote, wewe hazina ya mambo mema, tena mpaji wa uhai, kuja kukaa nasi na kutusafisha na kila doa, hata kuziokoa roho zetu, wewe mwema.
Utukufu kwa Mungu juu pia, chini amani, urazi kati ya wanadamu *(mara tatu)* (Luka 2. 14). Bwana uifunguwe midomo yangu ni kinywa changukitaonyesha sifa zako (Zaburi 51. 15).

*Sasa itaanza Liturgia Takatifu; lakini ndani ya Monasteri yetu Watawa wanasoma Saa ya kwanza na kisha Liturgia.*

# SALA YA SAA

## SAA YA KWANZA

*Hii Sala tunaisoma kiisha Orthros:*

Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu ya Mungu na Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu yeye Kristu aliye Mfalme na Mungu wetu.

ZABURI 5.
Sikiliza maneno yangu, ee Bwana, uangalie mafikili yanguuuuu. Usikie sauti ya kilio changu. Mfalme wangu, na Mungu wangu: Kwa maana ninaomba kwako. Ee Bwana, asubui utasikia sauti yangu; Asubui nitatengeneza maombi yangu kwako, na kuangalia sana. Kwa maana wewe si Mungu anayependezwa na uovu. Utaharibu wale wanaosema uwongo; Bwana anachukia mwuaji na mwenye hila. Lakini mimi, kwa wingi wa wema wako nitaingia nyumbani mwako; Katika kukuogopa wewe nitaabudu kwa upande wa hekalu lako takatifu. Uniongoze, ee Bwana. kwa haki yako kwa sababu ya adui zangu; Unifanyie njia yako wazi mbele ya uso wangu. Kwa maana hapana uaminifu kinywani mwako; Mutima wao ni shimo tupu; Koo lao ni kaburi waziii; Wanabembeleza na ulimi wao. Uwahesabie zambi zao, ee Mungu; Waanguke kwa mashauri yao wenyewe; Uwatoe inje katika wingi wa makosa yao, kwa maana wamekuasi wewe. Lakini wote wanaokuwekea tumaini lao wafurahi, wapige kele daima kwa furaha kwa sababu unawasimamia; Wao vilevile wanaopenda

jina lako wafurahi ndani yako. Kwa maana utabariki mwenye haki; Ee Bwana, utamuzungusha na mapendeleo kama ngabo.

ZABURI 89 (90)

Bwana wewe umekuwa makao yetu, kizazi kwa kizazi. Mbele ya kuzaliwa kwa milima, wala hujaumba bado inchi na ulimwengu, tangu milele hata milele wewe ni Mungu. Unarudisha mutu kwa mavumbi; Na unasema: Rudieni, ninyi wana wa watu. Maana miaka elfu moja machoni mwako ni kama jana iliopita, na kama kesha la usiku. Unawachukulia kama na garika; Nayo ni kama usingizi; Asubui wao ni kama majani yanayoota. Asubui yanaota vizuri, na yanakua; Mangaribi yanakatwa chini na kukauka. Maana tunaharibiwa kwa kasirani yako, na tunafazaishwa na hasira yako. Umeweka maovu yetu mbele yako, zambi zetu za maficho kwa nuru ya uso wako. Kwa maana siku zote zimepita kwa hasira yako; Tunamaliza miaka yetu ni makumi saba, ao labda kwa sababu ya nguvu makumi nane; hata hivi kiburi chao ni kazi na taabu tu kwa maana umepita upesi nasi tumekwenda zetu. Kwa anayejua uwezo wa kasirani yako, na hasira yako kwa woga unaopaswa kupokea? Utufundishe tuhesabu siku zetu, tujipatie moyo wa akili, Rudi, ee Bwana; hata wakati gani? Uhurumie watumishi wako. Utushibishe asubui na rehema yako; Tupate kushangilia na kufurahi siku zetu zote. Utufurahishe kwa kadiri ya siku ulizotutesa na miaka tulipoona mabaya. Kazi yako ionekane kwa watumishi wako, na utukufu wako juu ya watoto wao. Uzuri wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu; na wewe usimamishe kazi ya mikono yetu juu yetu; ndiyo, kazi ya mikono yetu uisimamishe.

ZABURI 101

Nitaimba juu ya rehema na hukumu: Wewe, ee Bwana, nitakuimbia sifa. Nitajiangalia katika njia kamilifu: Utakuja kwangu wakati gani? Nitatembea ndani ya nyumba yangu kwa haki ya moyo. Sitaweka mbele ya macho yangu neno la uovu: Ninachukia kazi yao wanaogeuka kando; haitafungana nami. Moyo wa ukaidi utaondoka kwangu: Sijui kitu cha uovu. Mutu yo yote anayesingizia jirani yake, nitamuharibu, mwenye macho ya kiburi na moyo wa majivuno sitamuvumilia. Macho yangu yatakuwa juu ya waaminifu wa inchi, ili wakae pamoja nami: Yeye anayekwenda katika njia kamilifu atanitumikia. Mwenye kutenda hila hatakaa ndani ya nyumba yangu: Mwenye kusema uwongo hatasimamishwa mbele ya macho yangu. Kila asubui nitaharibu wabaya wote wa inchi; nitenge wote wanaotenda ouvu na muji wa Bwana.

Utukufu kwa Baba. . .
Apolitikion ya Mutakatifu ya siku.
Sasa na siku zote. . . THEOTOKION.:

Namuna gani tutakuita ewe Mujaliwa neema? Mbingu? Kwa sababu ulileta duniani jua ya haki. Paradiso? Kwa sababu uliotesha ua isiyo harabika. Kwa sababu ulibaki Bikira bila uharibifu. Mama kamili? Kwa sababu ulichukua katika kifua chako takatifu Mtoto, aliye Mungu wawote, Umuombe yeye aokoe mioyo yetu. .

*Elezeo: Wakati ya kwarezima mbele ya Paska hatusomake vyote, lakini tunaimba hii:*
Sauti ya sita
Sikia sauti yangu asubui ee Mfalme na Mungu wangu *(mara tatu).*

Shairi 1: Sikia maneno yangu, ee Bwana, na sikiliza kusihi kwangu.
Shairi 2: Kwa kuwa nitaomba kwako Bwana asubui hii sikia sauti yangu.

*Kama hakuna wakati ya Kwarezima tunasoma hii*: Utukufu. . . Sasa. . . Namuna gani tutakuita ewe. . .
*Na kisha tutaimba hii Wimbo pole-pole:*

Sauti ya sita.
Ongoza mwendo wangu katika neno lako: wala uovu wowote usinitawale *(mara 2).*
Unikomboe na mateso ya mutu: Hivi nitachunga mafundisho yako yote *(mara 2).*
Uangazie Mtumishi wako na uso wako; na unifundishe amri yako *(mara 2).*
Kinywa changu kinajazwa na sifa yako Bwana, kama ninavyotukuza siku zote uzuri wako *(mara tatu).*

ELEZO: *Kisha juma ya kusujudu Msalaba: Siku ya kwanza. Siku ya tatu na siku ya tano ya juma ya ine ya kwarezima hahatuseme*: Ongoza mwendo. . . lakini tunaimba: Tunasujudu Msalaba wako, ee Bwana, na tunatukuza Ufufuo wako Takatifu.

Kisha: Mungu Mutakatifu. . . Utukufu. . . Sasa. . . Utatu Mutakatifu. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu. . . Sasa. . . Baba yetu. . . Kwa kuwa. . .

*Kama ni siku Kuu kubwa ya Mtakatifu fulani ao siku ya Mama Maria ao ya Bwana Yesu Kristu hatutaseme " Aliluia". Lakini tunasema Kontakion ya Mtakatifu ao ya ile Siku Kuu.*

ELEZO: *Kama hana siku ya Mutakatifu ao ya Mama Maria ao ya Bwana Yesu Kristu tunasema siku ya kwanza, siku ya pili na siku ya ine hii wimbo wa Mama Maria:*

Tumwimbie Mama Mtakatifu wa Mungu na Mtakatifu kamili bila kuchoka kwa roho na kwa kinywa, tukiimba huyu ni Mzazi-Mungu, kwani alizala kweli Mungu katika mwili na anaomba bila kuchoka kwa ajili ya mioyo yetu.

*Elezo: Siku ya ine na siku ya tano tunaimba wimbo hii:*

Kristu Mungu wetu utusaidie mbio mbele ya kufungua na madui zetu, waliyo kuzarau nakututendea mabaya; uliwasambaza kwa Msalaba wako wale wanaotukombanisha. Wajue ya kamaimani ya Orthodoxe ni nguvu kwa maombi ya Mzazi-Mungu, ewe Mpenda wanadamu.

*Elezo: Siku ya sita tunaimba hivi:*

Kwako, ee Bwana. Muumba wa ulimwengu dunia inatolea mashahidi wa Mungu kama sadaka kwa maombi yao na ya Mzazi-Mungu chunga Kanisa yako kwa imani nguvu, ewe nwenye rehema.

*Elezo: Siku ya Mungu tunasema Hypakoi ya sauti ya juma.*

ELEZO: *Juma ya ine ya kwarezima, tunasema Kontakion ya Juma ya usujudu ya Msalaba.*

Mupanga wa moto hauchunge tena mulango wa Paradiso. Kwani mti wa Msalaba ilizima moto wa mupanga kwa ajabu. Kwa lufu yake Kristu alikanyaga nguvu na ushindi ya gehena. Ulishuka kuzimuni Mwokozi wangu ukisema ingieni tena katika Paradiso.

*Elezo: Katika Juma Mkubwa tunasema hivi:*

Siku ya kwanza Mkubwa. Sauti ya mnane.

Yakobo aliliya kupotea kwa Mwana wake Yosefu, na yeye alikaa pa kiti chake cha ufalme. Kwa sababu zamani hakutenda zambi, alitukuzwa kwa huyu mwenye kutezama mioyo ya watu, na mwenye kuleta taji isioharabika.

Siku ya Pili Mkubwa. Sauti ya pili.

Roho yangu, wakati inafika mwisho yako na unaogopa kutatwa na mukuyu tumika na mapendo, neema hii uliyopewa kesho na kuita tusibaki inje ya nyumba ya arusi.

Siku ya Tatu Mkubwa. Sauti ya ine.

Nilitenda zambi mingi kuliko mwanamuke kahaba, ee Bwana. Murehemu, lakini sikulia mingi nakutosha machozi basi naanguka mbele yako na kuomba kimia nakukumbatia na mapendo miguu yako takatifu, juu unihurumie zambi yangu, ee Rabi. Mwokozi, nikisema. Uniokoe toka wingi ya zambi.

Kisha: Bwana hurumia *(makumi ine).*

Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa, na kutukuzwa wakati wote na katika kila saa mbinguni na duniani, uliye mwadilifu, mrahimu tele, mfazili sana unayependa wenye haki, tena kuwahurumia wenye zambi; unayewaita wote kuona wokovu, ukiwaahidi vitu vema vilivyokuja; wewe, ee Bwana, hata katika saa hii uyapokee maombi yetu, na kuyashurtisha maisha yetu njiani pa amri, uuzitakase roho zetu, uyasafishe miili yetu, uyatengeneze mafikira zetu, uzinyoshe nia zetu; ukatuokoe na kila shida, ubaya, na teso, utulindie kwa Malaika wako, ili sisi tukiwa na utunzi na uongozi wao, tufike katika umoja wa imani na kuujulisha utukufu wako usiofikika. Kwa kuwa unahimidiwa milele na milele. Amina.

Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu. . . Sasa. . . Uliye wa tamani. . . Kwa jina ya Bwana, barikia, ee Padri.
PADRI: Mungu atuhurumie na atubariki, atuangazie na uso wake na atuhurumie.
*Padri atasoma hii Sala ya Kristu.*
PADRI: Kristu, nuru ya kweli, aliyeangaza na kutakasa kila mutu, anayekuja duniani, na imeonekana kwetu nuru ya uso wako, ulituonyesha nuru ya uso wako isio zimika na ongoza mwendo wetu katika kazi ya amri yako. Kwa maombi ya Mama wako Mtakatifu na ya Watakatifu wote. Amina.

*Elezo: Kama hakuna Liturgia, kisha hii sala, tunasoma Apostolo (Matendo ya Mitume) na Evangelio ya hii siku.*
*Kisha Padri atasema Ektenia:* Tuseme sisi wote. . . Ee Bwana Mwenyezi. . . Utuhurumie sisi, ee Mungu kadiri ya wingi wa rehema yako. . . Kwa kuwa Wewe Mpenda wanadamu Mungu. . . Amin.
PADRI: Hekima.
*(Na atafanya mwisho ya hii sala).*

# SAA YA TATU

PADRI: Ahimidiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
PADRI: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.
Mfalme wa mbinguni, wewe Mfariji, Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote. Wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa kuziokoa roho zetu, Mwema We.
MSOMAJI: Amina.

Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Musiye kufa Mtakatifu, utuhurumie. *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...

Utatu Mtakatifu Kamili utuhurumie...Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... Baba yetu uliye mbinguni...

PADRI: Kwa kuwa ufalme...

MSOMAJI: Bwana hurumia *(kumi na pili).*

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.

Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu ya Mungu na Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme na Mungu wetu.

Zaburi 16 (17).

Usikie haki, usikilize kilio changu; utege masikio kwa maombi yangu yasiyotoka ka tika midomo ya hila. Hukumu yangu itoke kwako; Macho yako yatazame haki. Ume jaribu moyo wangu; umenifikia usiku; Umenipima wala hakuti kitu, nimekusudi kinywa changu kisikose. Kwa maneno ya kazi za watu, kwa neno Ia midomo yako, nimejichunga kwa njia za wenyi jeuri. Nyayo zangu zimeshikamana na njia zako, miguu yangu haikuon doshwa. Nimekuita, kwa sababu utanijibu, ee Mungu; Utege sikio lako kwangu na sikia neno langu. Onyesha wema wako wa ajabu, ee wewe unayeokoa wale wanaokuwekea tu maini lao, kwa wale wanaosimama juu yao, kwa mukono wako wa kuume. Unilinde kama mboni ya jisho, unifïchc chini ya kivuli cha rnabawa yako, kwa waovu wanaoniteka, adui zangu hata kufa wanaonizunguka. Wamefunga mioyo yao; Wanatoa majivuno kwa kinywa chao. Wametuzunguka sasa hatua zetu; Wamekaza macho yao watuangushe chini. Yeye ni kama simba mwenye choyo kwa kupata mawindo yake, na kama mwana-simba anayeji fïcha pahali pa kuficha. Simama, ee Bwana, umupiganishe, umutupe chini; kwa upanga wako uokoe nafsi yangu kwa mwovu; Ee Bwana kwa mukono wako uniokoe na watu, toka watu wa dunia, fungu lao ni katika maisha haya, na unajaza tumbo lao na hazina yako; wanashiba wa wana, na wanaacha baki la mali lao kwa watoto wao wachanga. Lakini mimi, nitaona uso wako katika haki; nitashibishwa wakati ninapoamka kwa sura yako.

Zaburi 24 (25).

Inchi na kujaa kwake ni mali ya Bwana; Dunia, nao wanaokaa ndani yake. Kwa maana ameweka misingi yake juu ya bahari, na kuisimamishajuu ya garika. Nani atakayepanda mulimani mwa Bwana? Na nani atakayesimama katika pahali pake patakatifu? Mtu aliye na mikono safi, na moyo mweupe; asiyenyanyua nafsi yake kwa uwongo, wala hakuapa kwa hila. Yeye atapokea baraka kwa Bwana, na haki kwa Mungu wa wokovu wake. Hiki ni kizazi chao wanaomutafuta, wanaotafuta uso wako, ee Mungu wa Yakobo. Nyanyueni vichwa vyetu, ee ninyi malango; na munyanyuliwe, ninyi milango ya milele; na mfalme wa utukufu ataingia. Nani aliye mfalme wa utukufu? Bwana mwenye nguvu na uwezo. Bwana mwenye uwezo vitani. Nanyueni vichwa yenu, ec ninyi malango, ndiyo, muvinyanyue, ninyi milango ya milele, na mfalme wa utukufu ataingia, Ni nani huyu mfalme wa utukufu? Bwana wa majeshi, yeye ni Mfalme wa utukufu.

Zaburi 50 (51).

Unirehemu, ee Mungu, sawasawa na wema wako; sawasawa na wingi wa rehema zako uzime makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, na kunisafisha na zambi yangu. Maana ninajua makosa yangu, na zambi yangu ni mbele yangu daima. Nimekukosea wewe peke yako, na kufanya yaliyo mabaya machoni mwako; ili ujulikane kuwa mwenye haki wakati unaposema, na kuwa safi wakati unapotea hukumu. Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu; na katika makosa mama yangu alinichukua mimba. Tazama, wewe unataka kweli moyoni, na kwa siri utanijuulisha hekina. Unisafishe kwa hisopo na nitakuwa safi; unioshe, na nitakuwa mweupe kupita theluji. Unifanye kusikia furaha na shangwe; ili mifupa uliyovunja ifurahi. Ufiche uso wako usitazame zambi zangu; na uzima maovu yangu yote, Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye eupya roho nzuri ndani yangu. Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu, Unirudishie furaha ya wokovu wako; unitegemeze kwa roho ya tayari, Halafu nitafundisha wenye makosa njia zako; na wenye zambi watarudi kwako. Uniponyeshe na damu ya watu, ee Mungu, wewe Mungu wa wokovu wangu; ulimi wangu utaimba na sauti haki yako. Ee Bwana. ufungue midomo yangu, na kinywa changu kitaonyesha sifa zako. Maana hupendezwi na zabihu, ao ningeitoa, huvunjika, moyo uliovunjika na wa toba hutauzarau, ee Mungu. Utendee Sayuni mema kwa mapenzi yako, ujenge kuta za Yerusalema. Halafu utafurahi kwa zabihu za haki, kwa sadaka ya

kuteketezwa, na sadaka nzima ya kuteketezwa; halafu watatoa ngombe ndume juu ya masabahu yako.

Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . . Alliluia. Alliluia. Alliluia, utukufu kwako, ee Mungu *(mara tatu).* Bwana hurumia *(mara tatu).*

Apolitikion *(Siku ya Mungu ya hii siku Kuu).*
Utukufu kwa Baba. . . Apolitikion ya Mtakatifu ya siku ya leo.

*Wakati ya Kwarezima na kama desturi vituo vya Zaburi 50 (51) na mwimbo ifwatayo, yenye kusemwa kisha kila kituo.*

Sauti ya Sita.
Bwana, wewe uliyetuma Roho Mtakatifu pa saa tatu kwa Mitume Wako, usituondoleeyo, ewe Mwema sana, lakini tunakuomba ufanye tendo lako mpya yetu.

Kituo: Ee Mungu, umba moya safi ndani yangu, ufanye upya roho nzuri ndani yangu.
Kituo: Usinitenge mbali na uso wako, wala usiniondolee Roho yako Mtakafu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . THEOTOKION.. Sauti ya sita.
Ee Mzazi-Mungu, ndiwe mzabibu wa kweli wenyi kuzidisha tunda la uzima. Tunakuomba: Utuombee, ee Malkia, pamoja na Mitume na Watakatifu wote, ili roho zetu zipate rehema. Ahimidiwe Bwana Mungu wetu, ahimidiwe Bwana siku kwa siku. Mungu huyu anatuletea wokovu. Mungu wetu ni Mungu mwenye kuokoa.

Trisagion: Mungu Mtakatifu. . .
PADRI: Kwa kuwa. . . MSOMAJI: Amina.
Kontakion ya siku.
*Siku ya Mungu kama ilivyo desturi ua Kigreki tunasoma Ipakoi. Wakati ya Kwarezima na siku za Desturi, tunaimba Wimbo zifwatayo:*

Sauti ya mnane.
Uhimidiwe, ee Kristu Mungu wetu, wewe uliyewashushia Mitume wako Roho Mtakatifu, ukiwageuza kwa hekima yako wavuvi kuwa wavuvi wa watu ambao nyavu yata vua dunia yote. Bwana mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . .

Uwape watumishi wako, ee Yesu, faraja ya wepesi na imara katika sikitiko humo muna patikana mioyo yetu. Usiache roho zetu katIka huzuru, usijitenge mbali na mawazo yetu katika majaribu, lakini bila pumziko utuaribu. Uwe karibu nasi, uwe karibu, wewe uliye pahali pote. Kama ulivyokuwa kila wakati na Mitume wako, ukae mwenyi kuungana na wale wenye kukupenda, ewe mwenye rehema. Hivi, tukiwa moja pamoja nawe, tutaweza kusifu na kutukuza Roho wako Mtakatifu kamili.

Sasa na siku zote. . . THEOTOKION..

Matumaini, ulinzi na kimbilio la wakristu, ngome yao isiyoweza kushindwa, bandari ya amani ya wenye kusumbuka, ni wewe Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili; kama unavyookoa ulimwengu na ombi lako, utukumbuke sisi pia, ee Bikira mstahili kamili wa sifa.

MSOMAJI: Bwana hurumia *(makumi ine).*
Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa, na kutukuzwa wakati wote na katika kila saa mbinguni na duniani, uliye mwadilifu, mrahimu tele, mfazili sana unayependa wenye haki, tena kuwahurumia wenye zambi; unayewaita wote kuona wokovu, ukiwaahidi vitu vema vilivyokuja; wewe, ee Bwana, hata katika saa hii uyapokee maombi yetu, na kuyashurtisha maisha yetu njiani pa amri, uuzitakase

roho zetu, uyasafishe miili yetu, uyatengeneze mafikira zetu, uzinyoshe nia zetu; ukatuokoe na kila shida, ubaya, na teso, utulindie kwa Malaika wako, ili sisi tukiwa na utunzi na uongozi wao, tufike katika umoja wa imani na kuujulisha utukufu wako usiofikika, Kwa kuwa unahimidiwa milele na milele. Amina.

Bwana hurumia*(mara tatu).* Utukufu. . . Sasa. . . Uliye watamani. . . Kwa jina ya Bwana, bariki, ee Padri.
PADRI: Mungu atuhurumie na atubariki, atuangazie na uso wake na atuhurumie

*Wakati ya Kwarezima tunasoma kisha sala ya Mtakatifu Efremi wa Siria:*
*Kisha tunafanya Metania (kupika magoti) tatu na kusema kwa kila metania moja-moja sala ya ile inafwatayo ya Mtakatifu Efremi wa Siria.*

Ee Bwana na Rabi wa uzima wangu, ondoa mbali nami roho ya uvivu, ya utawanyiko, ya kutawala wengine na maneno ya bure.

Unipe roho ya usafi, ya unyenyekevu, ya uvumilivu na ya mapendo, mimi mtumishi wako.

Ndiyo, ee Bwana mfalme, unipe nione zambi zangu tena nisimuhukumu ndugu yangu, kwani umehimidiwa milele na milele. Amina.

*Kisha tunafanya Metania kidogo Kumi na mbili na kisha moya Metania mukubwa na kusema:*
Ndiyo, ee Bwana mfalme, unipe nione zambi. . .

Trisagion: Mungu Mutakatifu. . . PADRI: Kwa kuwa. . MSOMAJI: Amina. Bwana hurumia *(kumi na pili).*

*Kisha Padri ao Mkubwa ya kanisa atasoma sala ya Mtakatifu Mardarios.*
Ee Mungu Rabi wetu. Baba mwenyezi. Bwana wa pekee Yesu Kristu, pamoja na Roho Mtakatifu, umungu moja, uwezo moja, unihurumie mimi mwenye zambi na kwa hukumu unazojuwa, uniokoe mimi mtumishi wako msiyestahili, kwani umetukuzwa milele hata milele. Amina.

PADRI: Utukufu kwako, ee Kristu Mungu, kitumaini wetu, utukufu kwako.
MSOMAJI: Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Ee padri mtakatifu, bariki.
PADRI: Kristu Mungu wetu kweli aliyefufuka katika wafu, kwa maombi ya Mama yake Mtakatifu asiye na doa wala si lawama kamili; ya Mitume Watakatifu Watukufu. Wasifiwa kamili na ya Watakatifu wote, atuhurumie na atuokoe, kwani Yeye ni Mwema na Mpenda-wanadamu.
MSOMAJI. Amina.

# SAA YA SITA

Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu ya Mungu na Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme na Mungu wetu.

Zaburi 53 (54).
Uniokoe, ee Mungu kwa jina lako, na unihukumu kwa uwezo wako. Sikia maombi yangu, ee Mungu, usikilize maneno ya kinywa changu. Kwa maana wageni wamesi mama juu yangu, na watu wakali wametafuta nafsi yangu, hawakuweka Mungu mbele yao. Tazama. Mungu ni musaidia wangu; Bwana ni kati yao wanaotegemeza nafsi yangu. Atarudishia adui zangu ubaya wao,

uwaharibu kwa kweli yako. Nitakutolea sadaka ya moyo, nitashukuru jiina lako, ee Bwana, maana ni jema. Kwa kuwa ameniokoa toka taabu zotc, na jicho langu limeona mapenzi yangu juu ya adui zangu.

Zaburi 54 (55).

Usikilize maombi yangu, ee Mungu, wala usijifiche kwa kusihi kwangu, unisikilize na kunijibu, sina pumziko katika mashitaki yangu, na ninaugua, kwa sababu ya sauti ya adui, kwa sababu ya mateso ya waovu; kwa kuwa wananitupia uovu, na wananitesa kwa gazaba yao. Moyo wangu unaumia sana ndani yangu, na hofu za mauti zimeniangukia. Woga na kutetemeka kumekuja juu yangu, na hofu kubwa imenishinda. Na nilisema: Kama ningekuwa na mabawa kama hua! Ningeruka mbali na kustarehe. Ningekwenda zangu mbali na kustarehe. Ningekwenda zangu bali, ningepanga jangwani. Ningefanya haraka kukimbilia pahali pa salama, mbali na zoruba na tufani. Haribu, ee Bwana, na tenga ulimi wao; maana nimeona ukali na fitina mujini. Muchana na usiku wanauzungukajuu ya kuta zake; uovu vilevile na taabu ni katikati yake. Mabaya ni katikati yake; mateso na hila haziondoki katika njia zake. Kwa maana hakuna adui aliyenilaumu; kama ndivyo, kama ningevumilia. Wala hakuna yeye aliyenichukia aliyejitukuza juu yangu, kama ndivyo, kama ningejificha kwake. Lakini alikuwa wewe, mutu mwenzangu, mwezi wangu, rafïki yangu niliyejuana naye sana. Tulifanya shauri tamu pamoja, tulikwenda nyumbani mwa Mungu pamoja na makutano. Mauti iwapate kwa gafula, washuke kwa Hadeze wangali hai; kwa kuwa uovu ni katika kao lao, katikati yao. Lakini mimi, nitaita Mungu; na Bwana ataniokoa. Mangaribi, asubui na azuhuri nitashitaki na kuugua; naye atasikia sauti yangu.

Amekomboa nafsi yangu na salama toka vita ilivyokuwa juu yangu, maana walikuwa wengi walioshindana nami. Mungu atasikia na kuwajibu, hata yeye anayekaa tangu milele.Watu wasiogeuka, wala wasioogopa Mungu. Amenyosha mikono yake juu yaowaliopatana naye; amefanya bule agano lake. Kinywa moyo wake ulikuwa vita; masemo yake yalikuwa teketeke kama mafuta, hata hivi yalikuwa panga zilizofutwa. Utupie Bwana muzigo wako, naye atakutegemeza; hataacha mwenye haki kutikisika. Lakini wewe, ee Bwana, utawashusha hata shimo la uharibu; watu wa damu na hila hawataishi nusu ya siku zao; lakini mimi nitakutumainia wewe.

Zaburi 90 (91).

Yeye anayekaa kwa pahali pa maficho yake aliye juu atakaa chini ya kivuli cha Mwenyezi. Nitasema juu ya Bwana, yeye ni pahali pangu pa kukimbilia na boma la nguvu langu. Mungu wangu ninayemwamini. Kwa maana atakuokoa toka mutego wa muwindají ndege, na kwa tauni ya uharibifu. Na manyonya yake atakufunika, na chini ya mabaya yakc utakimbilia; kweli yake ni ngabo na kígabo. Hutaogopa kwa woga wa usiku, wala kwa mushale unaoruka muchana; kwa tauni inayotembea katika giza, wala kwa kuharíbu kunakoharibu azuhuri. Elfu moja wataanguka kando yako, na elfu kumi kwa mukono wako wa kuume; lakini hakutafika karibu nawe. Na macho yako tu utatazama, na kuona zawabu ya waovu. Maana wewe, ee Bwana, ni pahali pangu pa kukimbilia! Umefanya aliye juu kao lako; mabaya hayatakupata wewe wala tauni haitafíka na hema yako. Maana ataagiza malaika yake juu yako, wakuchunge katika njia zako zote. Watakuchukua juu mikononi mwao, usivunje muguu wako kwa jiwe. Utakanyaga simba na nyoka mudogo mwenye sumu, utakanyaga mwana-simba na joka. Kwa sababu ametia mapendo yake juu yangu, kwa hivi nitamuponyesha, nitamuweka juu kwa sababu amejua jina langu. Ataniita na nitamujibu; nitakuwa pamoja naye katika taabu; nitamuponyesha na kumuheshimu. Kwa maisha ndefu nitamushibisha, na kumwonyesha wokovu wangu.

**U**tukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Alliluia. Alliluia. Alliluia, utukufu kwako, ee Mungu. *(mara tatu).*

Utukufu kwa Baba. . . Apolitikion ya Mtakatifu wa siku. Sasa na siku zote. .THEOTOKION.

**K**wani hatuna matumaini hata moja sababu ya zambi zetu nyingi, umwombe huyu aliyezaliwa kwako, ee Bikira Mzazi-Mungu. Maana ni la nguvu, ombi la Mama kwa kupata neema ya Rabi.

Usizarau maombi ya wenye zambi, ewe Mtukufu kamili, kwa kuwa yeye ni mwenye rehema na Mweza kwa kuokoa, huyu aliyekubali kuteswa mwilini kwa ajili yetu.

*Wakati ya Kwarezima, kisha Apolitkion tunaimba hii Wimbo:*
Sauti ya pili. .
Siku ya sita, pa saa ya sita, uliipigilia msalabani ile zambi aliyotenda Adamu Paradizoni, zima pia, ile barua ya deni zetu, ee Kristu Mungu wetu, na utuokoe.

Kituo: Ee Mungu sala usikie sala yangu usikatae maombi yangu.
Kituo: Lakini mimi namlilia Mungu, naye Bwana ataniokoa.
Siku ya sita, pa saa ya sita, uliipigilia msalabani. . .
**U** tukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . THEOTOKION.

*(Angalia kidogo yulu):* Kwani hatuna matumaini. . .
*Kisha Theotokion tunasoma hii sala tena:*
**U**lifanya katika inchi matendo ya wokovu, ec Kristu Mungu wetu. Ulipanua mikono yako mitakatifu msalabani, ukakusanya mataifa yote yenye kukupazia sauti: Bwana, utukufu kwako.

**U**tukufu kwa Baba. . .
Tunatukuza Ikone Yako isiyo na doa, ee Mwema kamili, tukiomba maondoleo ya zambi zetu, ee Kristu Mungu wetu; kwani ilikupendeza, kwa kutaka kwako, kupanda msalabani katika mwili kwa ajili ya kuokoa ku utumwa wa adui wale uliyoumba. Tena, katika ushukuru, tunakulalamikia: Ee Mwokozi wetu, ulijaza ulimwengu wa furaha wakati ulikuja kuokoa ulimwengu.

Sasa na siku zote. . .
Chemchem, ya rehema, ewe Mzazi-Mungu, utustahilishe ku huruma yako, tazama watu wenye zambi; onyesha, kama siku zote, uwezo wako, kwani tunatumainia kwako na tunakulalamikía: Salamu, kama Gabrieli zamani. Jemadari wa majeshi ya Malaika.

*Kama ni siku ya kazi tatu na kazi tano tunasoma hii:* **STAYROTHEOTOKION**

> Umejazwa na utukufu, ee Bikira Mzazi-Mungu, tunakuimbia, kwani Gehena imevunjwa Una lufu imeondolewa kwa Msalaba wa Mwana wako; tukikufa na tunafufuka; tulipopapa haki ya kuwa wastahili wa uzima, tulipokea paradizo, furaha yetu ya zamani. Tena, katika ushukuru tunatoa utukufu kwa Kristu Mungu wetu, mwenyezi na peke yake mtajiri wa rehema.

MSOMAJI: Bwana hurumia *(kumi na pili).*

Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa, na kutukuzwa wakati wowote na katika kila saa mbinguni na duniani, uliye mwadilifu, mrahimu teie, mfazili sana unayependa wenye haki, tena kuwahurumia wenye zambi; unayewaita wote kuona wakovu, ukiwaahidi vitu vema vilivyokuja; wewe, ee Bwana, hata katika saa hii uyapokee maombi yetu, na kuyasurutisha maisha yetu njiani pa amri yako, uuzitakase roho zetu, uyasafishe miili zetu, uyatengeneze mafikira zetu, usinyoshe nia zetu; ukatuokoe na kila shida, ubaya, na teso, utulindie kwa Malaika wako, ili sisi tukiwa na utunzi na uongozi wao, tufike katika umoja wa imani na kuujulisha utukufu wako usiokufika. Kwa kuwa unahimidiwa milele na milele. Amina.
MSOMAJI: Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu. . . Sasa. . . Uliye wathamani. . . Kwa jina ya Bwana, bariki, ee Padri.

PADRI: Mungu atuhurumie na atubariki, atuangazie na uso wake na atuhurumie.

*Wakati ya Kwarezima tunasoma kisha sala ya Mtakatifu Efremi wa Siria:*

*Kisha tunafanya Metania (kupika magoti) tatu na kusema kwa kila metania moja-moja sala ya ile inafwatayo ya Mtakatifu Efremi wa Siria.*
PADRI: Bwana na Rabi wa uzima wangu. . . *(Angalia yulu ndani ya Saa ya tatu)*
MSOMAJI: Trisagion. Mungu Mutakatifu. . .
PADRI: Kwa kuwa. . .
MSOMAJI: Amina.

*Padri atasoma kisha Sala ya Mtakatifu Basile Mkubwa.*

Ee Mungu na Bwana wa majeshi, fundi wa kiumbe yote, kwa mapendo ya rehema yako isiyoweza kufananishwa, ulimtuma Mwana wako wa pekee. Bwana wetu Yesu Kristu, kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Ulizima ile barua ya deni zetu, kwa msalaba wake tukufu na ulishinda, katika hii, ufalme na nguvu za giza. Wewe mwenyewe, ee Rabi mpenda-wanadamu, utupokee sisi wenye zambi; pokea shukrani zetu na maombi yetu. Utuopoe ku kosa yote yenye kuzuru na ya giza na kwa wale wotc wcnyi kutafuta kutuzuru, maadui wenye kuonekana na wasioonekana. Toboa mwili wetu na woga wako, usiinamishe mioyo yetu ku maneno wala ku mawazo mabaya, lakini umiza mioyo yetu ku mapendo yako ili wakati wote macho yenye kukaza kwako, na tukiongozwa na nuru yako, tutaweza kukutazama, ewe nuru isiyokaribika na ya milele, na kukutolea, ewe nuru isiyokaribika na ya milele, na kukutolea utukufu na shukrani. Baba wasipo mwanzo, pamoja na Mwana wako wa pekee na Roho wako Mtakatifu kamili, mwema na mletaji uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Kuaga (Apolisis).
PADRI: Utukufu kwako, ewe Kristu Mungu, matumaini wetu, utukufu kwako.
MSOMAJI: Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. Bwana hurumia *(mara tatu).* Ee Rabi Mtakatifu bariki.
PADRI: **K**ristu Mungu wetu kweli alìyefufuka katika wafu kwa maombezi ya Mama yake Mtakatifu asiye na doa wala si lawama kamili; ya Mitume Watakatifu, watukufu, wasifiwa kamili na ya Watakatifu wote, atuhurumie na atuokoe, kwani yeye ni Mwema na mpenda-wanadamu.
MSOMAJI: Amina.

# SAA YA TISA.

PADRI: Ahimidiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.
MSOMAJI: Amina.
PADRI: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.
Mfalme wa mbinguni, wewe Mfariji. Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote. Wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa kuziopkoa roho zetu. Mwema We.
MSOMAJI: Amina. Mungu Mtakatifu.*(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. Sasa na siku zote...
Utatu Mtakatifu Kamili... Bwana hurumia. Bwana hurumia. Bwana hurumia.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni, utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe ndeni zetu kama sisi vilevile tunawasamehe walio na ndeni zetu, tena usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule mwovu.

PADRI: Kwa kuwa ufalme, uwezo na utukufu ni wako, wa Baba na wa Mwana na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

MSOMAJI: Bwana hurumia *(kumi na pili).*

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu ya Mungu na Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme na Mungu wetu.

Zaburi 83 (84).

Makao yako yapendeza sana, ee Bwana wa ulimwengu! Ninazitamani wanja za Bwana kwa roho yangu yote. Moyo wangu na mwili wangu vinamlilia Mungu aliye mzima. Hata ndege amekuta nyumba, na mbayuwayu amepata kiota cha kuweka makinda yake, kwenye altare zako, ee Bwana wa ulimwengu. Mfalme wangu na Mungu wangu. Heri wale wanaokaa nyumbani mwako, wanakusifu daima! Heri mtu anayepata nguvu kwako, anayetamani kupanda hekaluni kwako. Wakipita katika bonde kavu wanalifanya kuwa pahali pa chemchem, nayo mvua ya kwanza inalivika baraka. Wanapoendelea nguvu inazidi: Watamwona Mungu wa miungu kule Siyoni. Ee Bwana. Mungu wa ulimwengu, usikie sala yangu; utege sikio lako, ee Mungu wa Yakobo. Ee Mungu uliye ngao yetu, uangalie, utazame uso wa mpakwa wako. Kweli, siku moja katika wanja zako ni bora kuliko nyingi elfu. Napenda zaidi kusimama kizingitini pa nyumba ya Mungu wangu, kuliko kukaa he mani mwa wenye zambi. Maana Bwana ni boma na ngao; Mungu anatoa neema na utukufu; Bwana hawanyimi kitu chema wale waendao katika ukamilifu. Ee Bwana wa ulimwengu, heri mtu anayekuamini !

Zaburi 84 (85).

Umebarikia inchi yako, ee Bwana, umerudisha vema hali ya Yakobo. Umeondoa uovu wa watu wako, umefunika zambi zao zote. Umezuia chuki yako yote, umeacha ukali wa hasira yako. Utuponye tena, ee Mungu. Mwokozi wetu, uondoe chuki uliyo nayo juu yetu! Je! Utatukasirikia milele? Utaeneza hasira yako kizazi kwa kizazi? Je! Hutatu rudishia uzima, taifa lako lifurahiwe na Wewe? Utuonyeshe wema wako, ee Bwana, utuletee wokovu wako! Ninasikia anayosema Bwana Mungu: Hakika, anasema maneno ya amani na watu wake na waamini wake; nao wasirudie tena upumbavu wao. Wokovu wake ni karibu nao wenye kumheshimu, utukufu wake utakaa katika inchi yetu. Wema na uaminifu zitakutana, haki na amani zitabusana. Katika inchi uaminifu utaota, na haki itainama toka mbinguni. Naye Bwana atatoa yaliyo mema, na inchi yetu itatoa mazao. Haki itatangulia mbele yake, wokovu utafuata nyayo zake.

Zaburi 85 (86).

**U**tege sikio lako, ee Bwana, unisikilize: maana mimi ni munyonge na maskini. Ulinde uzima wangu, maana mimi ni mwamini, umwokoe mtumishi wako anayekutumaini. Unihurumie, ee Bwana, kwa maana ninakulilia mchana kutwa. Ufurahishe roho ya mtumishi wako, kwani, ee Bwana, ninakuinulia roho yangu. Kwa sababu wewe, ee Bwana, ni mwema na mpole umejaa huruma kwa wote wanaokuomba. Usikie, ee Bwana, sala yangu, uelekee sauti ya maombi yangu! Siku ya taabu yangu ninakulilia, kwa maana wewe utanisikiliza. Katika miungu, hakuna aliye sawa nawe, ee Bwana; wala hakuna anayefanya matendo sawa na matendo yako. Mataifa yote uliyofanya watakuja, ee Bwana, watakuabudu wewe, watatukuza lina lako. Kwani wewe ni mkubwa tena na mfanya miujiza, wewe, ndiwe Mungu peke yako! Unifundishe, ee Bwana, njia ya kuheshimu jina lako. Nitakusifu, ee Mungu wangu, kwa moyo wote, nitatangaza jina lako hata milele, Maana wema wako ulionitolea ni mkubwa, umeopoa roho yangu katika mashimo ya kuzimuni. Ee Mungu, watu wenye kiburi wameniondokea na kundi la wakorofi wanatafuta uzima wangu mwenye huruma na mpole, mvumilivu, mwenye wema na uaminifu mwingi. Unielekezee
macho, unihurumie, umpe mtumishi wako nguvu yako, umwokoe mwana wa mjakazi wako. Unipe alama ya fazili, ili waione wanaonichukia, waone haya. Kwa kuwa Wewe, ee Bwana, umenisaidia, ukanituliza moyo.

**U**tukufu kwa Baba. , sasa na siku zote. , Alliluia. Alliluia. Alliluia, utukufu kwako, ee Mungu, *(mara tatu).* Bwana hurumia *(mara tatu).*

WAIMBAJI: Sauti ya mnane.
**K**u saa Tisa kwa ajili yetu, ulionja lufu ku mwili wako, regeza mawazo yetu ya mwili, ee Kristu Mungu, na utuokoe.

Shairi 1**:** **E**e Bwana, sala yangu ifike mbele yako, ku sauti yako unisikilize.
Ku Saa tisa kwa ajili yetu. . .

Shairi 2: Ee Bwana, maombi yangu ifike mbele yako, uniopoe kwa neno lako.
**K**u Saa Tisa kwa ajili yetu. . .
*Kama hii siku ni makumbusho ya Mtakatifu Mkubwa tunasema:*

Utukufu kwa Baba. . Apolitikion yake. Na kisha:
Sasa na siku zote. . . THEOTOKION.

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyanganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioubwa kwa mukono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu, murehemu; pokea Mzazi-Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

*Na mara moja tunasoma hii ifwatayo:*

**U**situache mpaka mwisho, sababu ya jina lako tatatifu, usiharibu agano lako, na usitenge kwa sisi rehema yako, sababu ya Abrahamu mpendwa wako, na Isaaka mtumishi wako, na Israeli mtakatifu wako.

*Mu Juma Mkubwa hatutaimbe hii mwimbo: «Ku Saa Tisa kwa ajili yetu. . . », lakini tutasoma hii mwimbo ifwatayo:* Tazama. Bwana anafika katika ya usiku. . . (*Angalia mu Kazi Moja Mkubwa ya Kitabu Juma Takatifu).*

MSOMAJI: Trisagion: Mungu Mutakatifu. . .
PADRI: Kwa kuwa. . . Amina.
*Kontakion ya Mtakatifu ya hii siku. Lakini mu Juma Mkubwa tutasoma hii Kontakion:*

Yakobo alilia ukosefu wa Yosefu, na msharibu mwenye kupanda juu ya gari yake, aliheshimiwa sawa mfalme mshindaji, alikataa mawazo mbaya ya mwanamuke wa mu Msiri. Alitukuzwa kwa yule anayejua mioyo ya watu na anayeleta taji isiyoweza kupevushwa.

*Mu Kazi Pili ya Juma Mkubwa tunasoma hii Kontakion:*

**K**umbuka, ee roho yangu, saa ya kufa na tetemeka ku wazo la mti uliokauka, hii talanta uliopewa izae matunda, roho yangu maskini, uwe macho na paza sauti: Tusibaki inje ya chumba cha arusi cha Kristu.

*Mu Kazi tatu Mkubwa.*

**K**uliko mtenda zambi, ee Mungu mwema, nilikosa. Sikutoe machozi sawa wimbi ya mvua; Lakini napiga magoti, na ninasali kwa ukimya kwa mapendo makubwa ninabusu. Miguu yako safi, sawa Rabi, unisamehe deni zangu, mimi ninayelia, ee Mwokozi uniokoe ku matope ya makosa yangu.

*Kama hakuna Siku Kuu kubwa, tunasoma hii Kontakion.*

**A**lipomwona Mkubwa wa uzima ametundikwa Msalabani, munyanganyi akasema: Kamahakukuwe Mungu katika Mwili, huyu anayesulubiwa pamoja nasi, jua halikuweza

kufichamwangaza wakc, na dunia yenye kutikisika haikuweza kutetemeka. Lakini wewe unayevumilia yote, unikumbuke, ee Bwana, katika Ufalme wako.

**U**tukufu kwa Baba. . .

**M**salaba wako ulisimama sawa mizani ya haki kati ya wanyanganyi wawili; mumoja alishuka chini ya Hadeze juu ya uzito wa matusi; mwengine alipunguza makosa yake, na alipata akili ya Mungu. Kristu Mungu, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. . .

**M**zazi wakati aliona Mwana-Kondoo na Mchungaji na Mwokozi wa dunia, yulu ya Musalaba, akaombolezwa na akasema: Dunia inafurahi, kwani inapokea wokovu, lakini moye wangu unaungua, pakuona usulubisho wako, unayevumilia kwa ajili yetu. Mwana wangu na Mungu wangu.

MSOMAJI: Bwana hurumia *(kumi na pili).* Utukufu. . . Sasa. . . Uliye wathamani. . . Kwa jina ya Bwana, bariki, ee Padri.
PADRI: Kwa maombezi wa Wapadri wetu watakatifu, ee Bwana yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe. Amina.

Elezo: *Sasa tunasema hii 5a!a ya Mtakatifu Efremi wa Siria). (Angalia ma Saa ingine).*

*Na mara moja tunaanza kuimba Heri. . . na kisha kila Heri. . . tunaimba hii mwimbo:*
Utukumbuke, ee Bwana, wakati, utakapokuja katika Ufalme wako.

## HERI

**K**atika ufalme wako, utukumbuke, ee Bwana, wakati utakapokuja katika ufalme wako.
**H**eri walio maskini moyoni, kwani ufalme wa mbingu ni wao. Utukumbuke ee Bwana. . . .
**H**eri wenye uchungu, kwani wao watatulizwa. Utukumbuke ee Bwana. . . . . .
**H**eri walio wapole, kwani wao watariti inchi. Utukumbuke. ee Bwana. . .
**H**eri wenye njaa na kiu ya haki, kwani watashibishwa. Utukumbuke, ee Bwana. . . .
**H**eri wenye huruma, kwani wao watahurumiwa. Utukumbuke, ee Bwana. . . .
**H**eri wenye moyo safi, kwani wao watamwona Mungu. Utukumbuke, ee Bwana. . .
**H**eri wenye kuleta amani, kwani wao wataitwa waana wa Mungu. Utukumbuke, ee Bwana. . . .
**H**eri walioteswa kwa sababu ya haki, kwani ufalme wa mbingu ni wao. Utukumbuke, ee Bwana. .
**U**tukumbuke, ee Bwana, wakati utakapokuja katika ufalme wako *(moja Metania ukubwa).*
Utukumbuke, ee Rabi, wakati utakapokuja katika ufalme wako *(metania ukumbwa).*
Utukumbuke. Mtakatifu, wakati utakapokouja katika ufalme wako (*metania ukubwa).*

*Kisha tunasoma:*
Kundi la waimbaji wa mbinguni wanakuimbia, na wanasema: Mtakatifu. Mtakatifu. Mtakatifu. Bwana Savaothi, mbingu na dunia zimejaa na utukufu wako.

Shairi: Jongeeni kwake, na mutaangaziwa, na uso wenu usipate haya.
**K**undi la waimbaji wa mbinguni wanakuimbia, na wanasema: Mtakatifu. Mtakatifu. Bwana Savaothi, mbingu na dunia zimejaa na utukufu wako.

**U**tukufu kwa Baba. . .
Kundi la Malaika na Malaika Wakuu, pamoja na ma, jeshi ya mbinguni, wanakuimbia na wanasema: Mtakatifu. Mtakatifu. Mtakatifu. Bwana Savaothi, mbingu na dunia zime jaa na utukufu wako.
Sasa na siku zote. . .

## SlMVOLO Y A IMANI

**N**asadiki Mungu mmoja Baba mwenyezi, mwumba wa mbingu na wa dunia, hata vyote vilivyoonekana na visivyoonekana, tena Bwana mmoja Yesu Kristu. Mwana wa pekee wa Mungu, aliyezaliwa na Baba mbele ya wakati wowote. Nuru toka Nuru. Mungu ukweli toka Mungu kweli, aliyezaliwa, si umbwa mwenye asili moja (omousion) na Baba, aliye kwake vyote vilifanywa, aliye kwa ajili yetu wanadamu na ya wokovu wetu alishuka mbinguni, akapata mwili kwa Roho Mtakatifu na kwa Bikira Maria, na akawa mtu. Aliye sulibiwa kwa ajili yetu wakati wa Pontio Pilato. Akateswa, akawekwa kaburini, Na aliyefufuka katika siku ya tatu, kama ya navyo maandiko. Na akapanda mbinguni ndipo anapokaa kuume kwa Baba. Na atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu walio na hai na waliokufa. Ufalme wake utakuwa bila mwisho. Tena Roho Mtakatifu yu Bwana yu Mwumba hai, aliyetoka na Baba, aliyesujudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana, aliyenena kwa midomo ya manabii, kwa Ekklezia moja Takatifu. Katholiki na Apostoliki. Naungama kwa ubatizo moja kwa maondoleo ya zambi. Natumaini ufufuo wa wafu hata uzima wa milele utakapokuja. Amina.

*Kisha tunasoma:*

Zima, ashilia, hurumia, ee Mungu, makosa yetu, ya kutaka na yisiyokutaka, iliyofanyika kwa matendo na maneno, ya kujuwa na ya kutokujuwa ya usiku ao ya mchana, ndani ya akili na ya ufahamu; yote utuhurumie, sawa mwema na mpenda wanadamu.

*Kisha*: Baba yetu uliye mbinguni. . .
PADRI: Kwa kuwa. . .
*Kama ni Siku Kuu ya Mtakatifu fulani, tunasoma Kontakion yake, Juma ya Ine ya Kwarezima tunasoma Kontakion ya Kusujudu Msalaba ya Kristu, (Angalia Kontakion yulu)=* Sasa upanga wa moto hauchunge tena mlango wa Edeni. . .

*Mu Kazi Moja ya Juma Mkubwa tuinasoma hii:* Yakobo alilia ukosefu wa Yosefu. . . (*Angalia yulu).*
*Mu kazi Pili ya Juma Mkubwa tunasoma hii*: Kumbuka, ee roho yangu, saa ya kufa. . .
*Kama ni mu Kazi Tatu tunasoma hii:* Kuliko mtenda zambi, ee Mungu Mwema. . .

*Ma Juma ingine tunasoma Kontakion ya Mageuzo ya Kristu.*
Mlimani ulijigeuza, na kama inavyowezekana wanafunzi wako waliona, ewe Kristu Mungu, utukufu wako; ile wakati walikuona Msalabani, na walisikia mateso yako kwa mapenzi yako na watahubiri duniani, ya kama ndiwe uko kweli Mtukufu wa Baba.

*Kisha tutasoma Kontakion ya Mtakatifu ya Kanisa na mwisho tutasoma Kontakion ya hii siku sawa ifwatayo hapa chini.*

KONTAKION ya Mtakatifu Mtangulizi

Ee Nabii wa Mungu, na Mtangulizi wa neema, tulipata kichwa chako ku udongo, sawa ua mwekunda takatifu, na tunapata mu wakati wote maponyesho; na kwani mara ingine zamani, unashauria dunia ku toba.

*Siku ya Tatu na ya Tano tunasoma hii:*

KONTAKION ya Msalaba.

Ulipopandishwa msalabani kwa kutaka, ee Kristu Mungu, leta huruma yako, ku taifa lipya linaloitwa kwa jina lako; furahisha kwa uwezo wako wafalme wetu waaminifu, ukiwapa ushindi juu ya adui; ili wapate katika agano lako, silaha ya amani, ushindi usiyosubutishwa.

*Siku ya Ine tunasoma hii:*

KONTAKION ya Mitume Watakatifu.

Wafundishaji wa usawa na wenye kuongozwa na Mungu, cha ya mitume wako. Bwana, uliwapokea katika furaha ya mema yako na ya mapumziko yako; ulipokea mateso na lufu yao, kuliko sadaka yote ya kuteketeza kwani peke yako unajua ndani ya mloyo.

KONTAKION ya Mtakatifu Nikola.

Ku Mira, ewe Mtakatifu, ulionekana kuhani; kwani ulitimiza siku hii Evangelio ya Kristu, ulitoa uzima wako kwa ajili ya taifa lako, na uliokoa ku Iufu wasiyo na mabaya; ndiyo maana umetakaswa, sawa fundi wa neema ya Mungu.

KONTAKION ya Mtakatifu ya Kanisa na Martirikon (Mwimbo ya Mashahidi) ya Wimbo wa Saba.

Utukufu kwa Baba. . .

Pamoja na Watakatifu, pumzisha, ee Kristu, roho ya watumishi wako, mu fasi pasipo kuuma, pasipo sikitiko, pasipo malalamiko, lakini uzima wa milele.

Sasa na siku zote. . .

**E**e Mulinzi usiyepatìsha wakristu haya, na mupatanishi wa Muumba usiyeweza kubadilika, usizarau sauti ya kusihi Ya wenye zambi. Lakini fika kama Mwema, kwa kutusaidia sisi, turlaokuita na imani: Ujiharikishe kwa upatanisho, na ukimbie kwa usìfu, ewe Mzazi-Mungu unayelinda, wanaokuheshimu daima.

Masomaji: Bwana hurumia *(makumi ine).*

Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa, na kutukuzwa wakati wowote na katika kila saa mbinguni na duniani, uliye mwadilifu, mrahimu teie, mfazili sana unayependa wenye haki, tena kuwahurumia wenye zambi; unayewaita wote kuona wakovu, ukiwaahidi vitu vema vilivyokuja; wewe, ee Bwana, hata katika saa hii uyapokee maombi yetu, na kuyasurutisha maisha yetu njiani pa amri yako, uuzitakase roho zetu, uyasafishe miili zetu, uyatengeneze mafikira zetu, usinyoshe nia zetu; ukatuokoe na kila shida, ubaya, na teso, utulindie kwa Malaika wako, ili sisi tukiwa na utunzi na uongozi wao, tufike katika umoja wa imani na kuujulisha utukufu wako usiokufika. Kwa kuwa unahimidiwa milele na milele. Amina.

MSOMAJI: Bwana hurumia*(mara tatu).* Utukufu. . . Sasa. . . Uliye wathamani. . . Kwa jina ya Bwana, bariki, ee Padri.

PADRI: Mungu atuhurumie na atubariki, atuangazie na uso wake na atuhurumie.

*Wakati ya Kwarezima tunasoma kisha sala ya Mtakatifu Efremi wa Siria:*
*Kisha tunafanya Metania (kupika magoti) tatu na kusema kwa kila metania moja-moja sala ya ile inafwatayo ya Mtakatifu Efremi wa Siria, (Angalia ndani ya Saa ya Sita)*

PADRI: Bwana na Rabi wa uzima wangu. . . *(Angalia yulu ndani ya Saa ya tatu).*
MSOMAJI: Trisagion. Mungu Mutakatifu. . .
PADRI: Kwa kuwa. . . MSOMAJI: Amina.
*Padri kisha atasoma hii sala:*

Utatu Mtakatifu kamili, nguvu ya umoja, ufalme usiyogawanyika, kisa ya mema yote leta wema wako kwa miml mtenda zambi, sabitisha, na fundisha moyo wangu, uniopoe ku aibu yote, angaza akili yangu; ili wakati wote nitukuze utukufu naimba, naabudu na nasema: Mtakatifu ni Moja. Bwana ni Moja. Yesu Kristu, ku utukufu wa Mungu Baba. Amina.

PADRI: Utukufu kwako, ee Mungu, matumaini yetu, utukufu kwako.
MSOMAJI: Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu).*

Ee Rabi, mtakatifu bariki.

PADRI: Kristu Mungu wetu ukweli, kwa maombezi ya Mama wako Mtakatifu asiye na doa wala
na lawama kamili. Kwa maombezi ya Yoane Nabii, Mtangulizi, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu, ya Mitume Watakatifu, watukufu, washindaji wazuri, ya Wapadri wetu Watawa na wabebaji-Mungu, ya Yoakimu na Anna Mababu-Mungu. Watakatifu, na wenye haki, hata ya Watakatifu wote, utuhurumie, ukatuokoe sawa Mungu Mwema, marahimu na mpenda-wanadamu. Kwa maombezi ya wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

MSOMAJI: Amina.

# SALA YA MANGARIBI (ESPERINOS)

PADRI: Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

MSOMAJI: Amina.

*Wakati Msomaji anasoma zaburi ya mwanzo (IO4), padri anasimama wima kichwa wazi mbele ya Altare, anasoma kwa siri sala za Mangaribi saba zifwatazo:*

SALA I

Ee Bwana mwenyi huruma, aendaye polepole kwa hasira na mwenye tele na huruma, usikie ombi letu, sikiliza sauti ya maombi yetu. Utufanyizie kuwa alama ya wema; utuongoze katika njia zako, ili tutembee katika wema wako; Furahisha moyo wetu katika woga wa jina lako takatifu, kwani u Mkuu na unafanya maajabu; u Mungu wa pekee, hakuna afananaye nawe miongoni mwa wakuwako kimungu. Ee Bwana, mwenyezi katika rehema na mwema katika uwezo kwa kusaidia kufariji na kuokoa wao ambao wanatumainia katika jina lako takatifu. Kwa kuwa kwako tunautoa utukufu wote, heshima na uabudu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA II

Ee Bwana, usituajibu katika hasira yako nyingi, usitutwalii tena katika ukali wako; lakini ututendee kadiri ya wema wako, ewe mganga na mponya wa roho zetu; utuongoze bandarini ya mapenzi yako, angaza macho ya moyo wetu ili tupate kujua ukweli wako; utupe kuisha masalio ya siku hii na ya uzima wetu, katika amani na bila zambi; kwa maombezi ya mtakatifu Mzazi Mungu, na ya watakatifu wote. Kwani kwako tunakutoa nguvu, utawala, uwezo, na utukufu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA III

Ee Bwana Mungu wetu, utukumbuke sisi watumishi wako, watenda zambi na batilifu; tukipokumbuka jina lako takatifu, usituchanganya katika ungojezi wetu wa rehema yako; lakini utupatie, ee Bwana, wema wote tunaokuomba kwa ajili ya wokovu wetu; uturudishe kuwa wastahilivu wa kukupenda na roho yetu yote, wa kukuogopa na wa kutenda katika vyo vyote mapenzi yako. Kwani u Mungu mwema na mpenda wanadamu, na tunakutukuza. Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA IV

Ee Wewe unaye tukuziwa kwa nyimbo bila kuachilia na nyimbo ya utukuzo wa mfululizo, ya uwezo takatifu, ikipojazwa kinywa chetu na sifa zako, ili tuweze kutukuza jina lako takatifu, utupe sisi fungu na uriti pamoja na wao wote wanaokuogopa katika ukweli, a wanaochunga amri zako; kwa maombezi ya mtakatifu Mzazi-Mungu, na ya watakatifu wote. Kwani kwako tunautoa utukufu

wote, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA V

Ee Bwana, unayeshika ulimwengu mikononi mwako bila doa; u mvumilivu kwetu, na unajitesa kwa vitendo vyetu vibaya; ukumbuke huruma yako na rehema, utuangalie katika wema wako; utupe, kwa neema yako, kwa kukimbia pia, kwa wakati wa masalio ya siku hii, kwa fitina mbalimbali ya mwovu; zuia uzima wetu ku makimbilio ya mitego yoyote kwa neema ya roho yako mtakatifu unapobarikiwa naye, kama vile roho yako mtakatifu kamili. Kwa rehema na upendo kwa ajili ya wanadamu wa mwana wako wa pekee, unapobarikiwa naye, kama vile roho yako mtakatifu kamili, mwema na muletauhai, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA VI

Ee Mungu, mkuu na mwenye maajabu, unatawala na unaongoza ulimwengu na wema usiyoweza kusema na tuzo kubwa; umetupa mali ya ulimwengu huu, na ulipotuongoza kwa mali uliyotupa, unatupa rahani ya ufalme uliyotuhaidia majira ya siku hii mkosama uliyotupa, umetuepusha ubaya wo wote; utupe sisi kwa kuishi bila magombezi, katika ukuwapo wa utukufu wako takatifu, na kwa kukuimba, ewe Mungu wa pekee, mwema kamili na mpenda wanadamu. Kwani u Mungu wetu na tunakutukuza Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SALA VII

Ee Mungu mkuu na uliye juu, u peke uliye umilele, a unayekaa nuru kutokaribika; na hekima ukafanya kiumbe cho chote, ukatenganisha nuru na giza ukiweka jua kutawala mchana, mwezi na nyota kutawala usiku, isipokuwa zambi zetu, ukatuhukumu wastahilivu, na kusimama, wakati huu, mbele ya uso wako, wa kutangaza jina lako na kukutolea sifa ya mangaribi; ee Bwana rafiki wa watu, peleka wewe mwenyewe sala yetu kama uvumba mbele yako, na uyapokee sawa sawa manukato ya arufu nzuri. Utupe mangaribi na usiku tulivu, utuvike silaha za mwangaza; utuokoe kwa woga kubwa wa usiku na kwa werevu wo wote unaotupeleka gizani; utupe usingizi ambao ulitupatia kama pumziko kwa uregevu wetu, ukipofukuza mbali nao sura yo yote ya kishetani. Ndiyo, ee Rabi, mgawanyi wa wema yo yote, fanya, ili katika usiku huu, ukipenywa na juto la zambi kitandani mwetu, tukumbuke jina lako takatifu na tukiangaziwa kwa usimamizi wa amri zako, tukisimama, roho ikipojazwa tele na furaha, kwa kutukuza wema wako, na kutolea ku huruma yako maombi na sala zetu kwa ajili ya zambi zetu na kwa ajili ya yale ya watu wako; katika rehema yako, utulinde kwa maombezi ya mtakatifu Mzazi-Mungu, Kwani u Mungu mwema na mpenda wanadamu, na tunakutukuza. Baba. Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**ELEZO:** *Wakati Padri anaposoma Sala saba. Msomaji yeye anasoma zaburi ya mwanzo (IO4) nguvu na kwa sauti tamu kama hivi:*
Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu na Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu na Mungu Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu aliye Mfalme na Mungu wetu.

ZABURI IO4: *Uwezo wa Bwana katika viumbe.*

Bariki Bwana, ee nafsi yangu, ee Bwana Mungu, wewe ni mkubwa sana; umevikwa heshima na ukubwa. Unayejifunika na nuru kama vazi; unayetandika mbingu kama pazia; anayeweka boriti za nyumba yake ndani ya maji; anayefanya mawingu magari yake, anayetembea juu ya mawingu ya upepo; anayefanya pepo zake wajumbe wake, watumishi wake moto wa kuwaka: Aliyeweka misingi ya inchi, isitikisike milele. Umeifunika kwa vilindi kama vazi; maji yalisimama juu ya milima. Kwa kukemea kwako yalikimbia; kwa sauti ya radi yako yalikwenda zao mbio. (Yakapanda milima,

yakashuka mabondeni), mupaka pahali ulipoyatengenezea. Umeweka mupaka yasiupite; yasirudi kufunika inchi. Anatuma chemchem katika mabonde; zinapita mbio kati ya milima. Zinakunywesha kihewa wana kao lao, wanaimba kati ya matawi. Ananyesha milima toka vyumba vyake; inchi inashiba kwa tunda la kazi zako. Anafanya majani kuota kwa ajili ya ngombe, na mboga kwa utumishi wa mutu; ili apate kutoa chakula toka inchi: na mvinyo inayofurahisha moyo wa mutu, na mafuta kwa kuangaza uso wake, na chakula kinachopatiza nguvu moyo wa mutu. Miti ya Bwana inashiba; mierezi ya Lebanoni aliyoipanda; pahali ndege wanapofanya vitundu vyao: Lakini korongo, misunobari ni nyumba yake. Milima iliyo juu ni kwa mbuzi za mwitu; miamba ni kimbilio kwa wibari. Ameweka mwezi kwa ajili ya nyakati: jua linajua kushuka kwake. Umefanya giza, nalo ni usiku; wakati nyama zote za mwitu wanatambaa. Wana-simba wanaguruma wakitaka mawindo, na wanatafuta chakula chao kwa Mungu. Jua linapanda, wao wanakwenda zao, na kulala mapangoni mwao. Mutu anatoka kwenda kwa kazi yake, na kwa utumishi wake hata mangaribi. Ee Bwana, kazi zako ni nyingi sana! Kwa akili ulizifanya zote: inchi inajaa mali zako. Bahari ni kule, kubwa na pana, ndani yake ni vitu vya kutambaa visivyoweza kuhesabiwa, nyama wadogo na wakubwa. Pale zinapita merikebu; pale ni lewiatani uliemwumba acheze ndani yake. Hawa wote wanakungojea wewe, ili uwape chakula chao kwa wakati wake. Kitu unachowapa wanakiokokota; unafunguwa mukono wako, wanashibishwa na mema. Unaficha uso wako, wanafazaishwa; unaondoa pumuzi wao, wanakufa, wanarudia mavumbi yao. Unatuma roho yako, wanaumbwa; na unafanya uso wa udongo. Utukufu wa Bwana udumu milele; Na Bwana afurahi katika kazi zake: anayetazama inchi nayo inatetemeka; Anagusa milima nayo inatoa moshi. Nitaimbia Bwana hata mwisho wa uzima wangu sifa ningali nikiwa hai. Mawazo yangu yawe matamu kwake: nitafurahia Bwana. Wenye zambi waharibie katika inchi, wala waovu wasiwe tena. Bariki Bwana, ee nafsi yangu. Musifu Bwana.

*Na tena:* Jua linajua kushuka kwake, umefania giza, nalo ni usiku; ee Bwana kazi zako ni nyingi sana, kwa akili ulizifanya zote.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...Alliluia-Alliluia-Alliluia, utukufu kwako, ee Mungu, *(mara tatu).* Kitumaini yetu, ee Bwana, utukufu kwako.

*Elezo: Msomaji akipomaliza kusoma Zaburi hiyo IO4. Padri anatumaka kwambatisha kubwa (Irinika) hivi:*
PADRI: Kwa amani, tumuombe, Bwana.
*Msomaji atasema kisha kila ombi*: Bwana, hurumia.
PADRI: Kwa ajili ya amani kutoka juu, na ya wokovu wa roho zetu, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya amani ya dunia yote, ya kusimama kuzuri kwa Eklezia Takatifu ya Mungu na ya umoja wa wote, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya waKristu watawa wa Orthodoksi wote, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya Arkiepiskopu wetu. . . *(jina lake),* ya upresbyteri uheshimiwa, ushemasi katika Kristu, ya wateule wote na ya watu wote, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya mji hii na inchi hii, kila mji na inchi, na ya waaminifu ya wanaoishimo, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya kutupewa na hewa tamu, na manenevuya arzi, na nyakati za amani, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya wasafiri hewani, baharini na nchini, ya wagonjwa, ya wateswa, ya mateka, na kwa ajili ya wokovu wao, tumwombe Bwana.
PADRI: Kwa ajili ya kutuokolewa na kila sikitiko, gazabu, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.

PADRI: Utulinde, utuokoe, utuhurumie, utuhifazie, ee Mungu kwa neema yako.

PADRI: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda. Despina wetu mtukufu. Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekee mikononi mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI: Kwako, ee Bwana.
PADRI: Kwa kuwa utukufu wote ni wako, heshima na uabudu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.
MSOMAJI: Amina.

**ELEZO:** *Mu siku ya Posho Mangaribi wanatayarisha msomo wa kathisma ya kofia ya wafalme wazamani wenye kuwa na fungu za mashairi tatu: Zaburi 1-3; 4-6;*
*7-8. Kila fungu linaisha na sala ndogo ambayo ekfonezi inabadilika katika utimizo, usomi wa kofia unachiliwa zaidi ao unaondoshwa kwa vituo moja maja Zaburi tatu na wimbo: Alliluia.*

PADRI: Tena na tena kwa amani, tumwombe Bwana.
MSOMAJI: Bwana, hurumia.
PADRI: Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuchunge, ee Mungu kwa neema yako.
MSOMAJI: Bwana, hurumia.
PADRI: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda. Despina wetu mtakatifu. Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili nasi kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiwekee mikononi mwa Kristu Mungu.
MSOMAJI: Kwako, ee Bwana.
PADRI: Kwa kuwa kwako ni nguvu, utawala, uwezo na utukufu, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.
MSOMAJI: Amina.

*Elezo: Msomaji akipofika pa: "Sala yangu mbele yako" ya Zaburi I4I. Padri anabariki uvumba akisema:*
PADRI: Tunakutolea uvumba huu, ee Kristu Mungu wetu, kama manukato ya kiroho; ukiyapokea mezani yako mbinguni, ututumie, kwa marudio, neema ya Roho yako Mtakatifu kamili. Anafukiza Meza Takatifu na Nafasi Matakatifu, kiisha Kanisa yote kama kwa zoezo.

MSOMAJI: Zaburi I4I: *Kuomba Mungu atulinde.*

Bwana, nimekuita, unisikilize, Unisikilize, ee Bwana. Bwana nimekuita, unisikilize; usikie sauti ya kusihi kwangu. Wakati ninapokuita, unisikilize, ee Bwana.

Maombi yangu ya elekezwe, kama uvumba mbele yako. Kunyanyua kwa mikono yangu, kama zabihu ya mangaribi, unisikilize, ee Bwana.
Uniweke mulinzi, ee Bwana, mbele ya kinywa changu uchunge mulango wa midomo yangu.
Usisukume moyo wangu kwa kitu kibaya, nifanye matendo ya uovu.
Pamoja na watu wanaotenda uovu, wala nisile vyakula vyao vitamu.
Mwenye haki anipige, itakuwa vema; naye anihamakie, itakuwa kama mafuta kichwani.
Kichwa changu kisikatae: maana siachi maombi yangu katika uovu wao.
Waamuzi wao wanaangushwa kando ya mwamba; nao watasikia maneno yangu; maana ni matamu.
Kama wakati mutu anapolima na kupasua udongo, mifupa yetu inasambalishwa kwa kinywa cha kaburi.
Macho yangu ni kwako. Mungu Bwana; ninakutumainia wewe; Usiache nafsi yangu.
Unilinde na mutego walioniwekea, na matanzi ya watenda uovu.
Waovu waanguke katika nyavu zao wenyewe, wakati mimi ninapopona na salama.

Zaburi I42: *Kilio cha mwenye kusongwa.*
Kwa sauti yangu ninalilia Bwana; kwa sauti yangu ninasihi Bwana.

Ninamwanga mashitaki yangu mbele yake; ninamwonyesha taabu yangu.
Wakati nilipozima roho, umejua njia yangu.
Katika njia ninapokwenda wamenifichia mutego.
Utazama kwa mukono wa kuume, uone, kwa maana hakuna mutu anayenijua:
Makimbilio yamenipotea; hakuna mutu anayekumbuka nafsi yangu.
Nikalia kwako, ee Bwana; Ninasema: wewe ni kimbilio langu, sehemu yangu katika inchi yao waliohai.
Usikilize kilio changu; kwa maana nimeshushwa chini sana:
Uniponyeshe nao wanaonifuata; kwa maana wao wana nguvu kuliko mimi

*Kibeti (couplet) ya Tropari Kumi (IO)*
Toa nafsi yangu katika kifungo. ili nishukuru jina lako:
Wenye haki watanizunguka; kwa kuwa wewe utanitendea kwa ukarimu.

Kibeti (Couplet)ya Tropari Nane (8) Zaburi I3O: *Kuomba Usamehe*
Toka vilindini nimekulilia, ee Bwana. Bwana, sikia sauti yangu.
Masikio yako yasikilize sauti ya kusihi kwangu.

Kibeti (Coupler) ya Tropari sita (6)
Kama wewe Bwana, ukihesabu maovu, ee Bwana, nani atayesimama? Lakini usameni pamoja nawe, ili uogopwe.
Ninangojea Bwana, nafsi yangu inangoja, na ninatarajia neno lake.

Kibeti (Coupler) ya Tropari Ine (4)
Nafsi yangu inangoja Bwana, kuliko walinzi wanaongoja asubuhi; ndiyo, walinzi wanaongoja asubuhi. Ee Israeli, utarajie Bwana.
Maana pamoja na Bwana ni rehema, na pamoja naye ukooombozi mwingi. Naye atakomboa Israeli na maovu yake yote.

Zaburi 117. *Wote watukuze Mungu*.
Musifu Bwana, ninyi mataifa yote; mumutolee, ninyi watu wote.
Maana rehema yake kwetu ni kubwa; na kweli ya Bwana inakaa milele. Musifu Bwana.

*Sasa tunaimba Wimbo ya siku Kuu ya Mtakatifu.*
Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

*Elezo: Waimbaji wanaimba Doksastikon na Theotokion.*

## Mwandamano wa kwingia

*Elezo: Kisha Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. . . Shemasi anakamata chetezo atakachopeleka mbele ya Padri na atasema:*

SHEMASI: Bariki, ee Rabi, ubani.
PADRI: Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

*Kisha kwa Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatafu. Wote wawili wikipofika mbele ya Meza Takatifu, wanainama kwa ajili ya Sala ya kwingia wanayosema kwa sauti ya chini:*
SHEMASI: Tumwombe Bwana.
PADRI: Mangaribi, asubui na azuhuri tunakusifu, tunakubariki, tunakushukuru na tunakukililia, ee Rabi wa ulimwengu. Bwana mpenda wanadamu. Pokea sala yetu kama uvumba mbele yako, usiinamishe roho yetu kwa sauti ao kwa mawazo mabaya lakini utuokoe kwa wale wanasakaroho

yetu. Kwako, ee Bwana, kunanyanyuka macho yetu; katika wewe tunatumaini, ee Mungu wetu, fanya kusudi tusichanganywi. Kwa kuwa kwako tunautoa utukufu wote, heshima na kuabudu. Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
SHEMASI: Bariki, ee Rabi, kuingia huku takatifu.
PADRI: Kubarikiwe kuingia kwa watakatifu wako, wakati wowote, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
*Shemasi anafukiza na kusema kwa kupaza sauti:*
SHEMASI: Hekima. Tusimameni.
WAIMBAJI: Mwangaza ilaron ya sifa mtakatifu, ya Baba Musiye kufa wa mbinguni, mtakatifu na heri, ee Yesu Kristu, kufika kuingia kwa jua, kuangalia mwangaza wa mangaribi; tunasifu Baba. Mwana na Roho Mtakatifu Mungu mmoja, uko kweli wakati wote. Kukuimbia kwa ma sauti nzuri, ee Mwana wa Mungu, chemchem ya uzima, ulimwengu utaita sifa yako.

SHEMASI: Esperas (Mangaribi) Prokimenon.
*Waimbaji wanaimba:*
Siku ya Mungu: Tazama ninyi munaobariki Bwana, ninyi watumishi wote wa Bwana *(mara tatu).*
Shairi: Munaosimama usiku nyumbani mwa Bwana *(mara moja).*

Mukazi moya: Bwana atasikia wakati ninapomuita *(mara tatu).*
Shairi: Unijibu wakati ninapoita, ee Mungu wa haki yangu *(mara moja).*

Mukazi mbili: Hakika wema na rehema zitanifuata siku zote za maisha yangu *(mara tatu).*
Shairi: Bwana ni muchungaji wangu; sitapungukiwa na kitu *(mara moja).*

Mukazi Tatu: Uniokoe, ee Mungu, kwa jina lako na unihukumu kwa uwezo wako *(mara tatu).*
Shairi: Ee Mungu, sikia maombi yangu. *(mara moja).*

Mukazi ine: Kusaidiwa kwangu kunatoka kwa Bwana aliyefanya mbingu na dunia *(mara tatu).*
Shairi: Nitanyanyua macho yangu kwa milima, kusaidiwa kwangu kunatoka wapi. *(mara moja).*

Mukazi tano: Mungu ni ngoma yangu wa rehema yangu atanitangulia *(mara tatu).*
Shairi: Uniponyeshe na adui zangu, ee Mungu wangu. *(mara moja).*

Mu Posho: Bwana anatawala, amevikwa utukufu *(mara tatu).*
Shairi: Bwana amevikwa, amejifungia nguvu.
Shairi: Ulimwengu umesimamishwa usiweze kuhamiswa.

*Kama kuna somo la Manabii. Padri atasema:* Tusikilize. Hekima. Tusikilize.
*Elezo: Siku za Siku Kuu, kunafuata usomi tatu wa Biblia. Ambamo Shemasi anasema:*
SHEMASI: Hekima. Simameni.
*Kwa Barua za Mitume anasema:* Tusikilize. Hekima.
*Kisha usomi. Shemasi anasimama mbele ya Milango Takatifu na sauti kubwa anasema maombi yafwatayo:*
SHEMASI: Tuseme sisi wote, kwa moyo wetu na kwa roho yetu, tuseme.
MSOMAJI *atasema kisha kila ombi:* Bwana, hurumia.
SHEMASI ao Padri: Bwana mwenyezi. Mungu wa mababu, tunakuomba, utusikie na ukatuhurumie.
PADRI: Utuhurumie, ee Mungu, katika huruma yako kubwa, tunakuomba utusikie na ukatuhurumie.
PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya wa madini na wakristu waorthodoksi wote.
PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiepiskopo wetu. . . . *(jina lake)*

PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya ndugu zetu, mapadri, washemasi, watawa na wandugu wote katika Kristu.
PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya kupata rehema, uzima, amani, afya, wokovu, ulinzi, usamehe na maondoleo ya zambi za watumishi wa Mungu, wadini wote na wakristu waorthodoksi ambao wanakaamo na wanakutana katika muji huu (ao nyumba wa watawa), wa parokia, na walakini na wapotani wa hekalu hii takatifu.
PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya watulivu na wenye heri, wajengaji wa hekalu hii takatifu, kwa ajili ya Baba na ndugu zetu wanaofariki ambao wanaolala kwa madini na kwa ajili ya waorthodoksi wanaolala hapa na popote.
PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya wafazili wa hekalu hii takatifu na heshima kwa ajili ya wapaji, kwa ajili ya wote wanaotumikamo na wanaoimbamo na kwa ajili ya watu wote walipo hapa ambao wanakujongea kwa rehema kubwa na nyingi.
PADRI: Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu wa huruma na mpenda wanadamu na tunakutukuza. Baba. Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.
WAIMBAJI: Amina.
MSOMAJI ao Padri mkubwa:

Ee Bwana, utujalie mangaribi hii kutulinda na zambi, umehimidiwa u, ee Mwana na Mungu wa Baba zetu, jina lako limehimidiwa na limetukuzwa milele. Amina. Ee Bwana, huruma yako iwe nasi tunavyokutumaini wewe, Ee Bwana umehimidiwa u, unifundishe zilizo haki zako. Ee Mtakatifu, umehimidiwa u, uniangaze kwa zilizo haki zako. Ee Bwana, huruma yako ni ya milele usitutoangalie sisi, viumbe vya mikono yako. Sifa zakulaiki kukuimbia ni kwako, utukuufu ni wako, wa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

SHEMASI: Tuumalize ombi wetu wa mangaribi kwa Bwana.
WAIMBAJI: Bwana, hurumia.
SHEMASI: Utulindie, utuokoe, utuhurumie, utuchunge, ee Mungu kwa neema yako.
WAIMBAJI: Bwana hurumia.
SHEMASI: Mangaribi hii kamili iwe timilifu, takatifu, tulivu, yasio zambi, tuombe kwa Bwana.

*Waimbaji wataimba kisha kila ombi:* Utupe, ee Bwana.
SHEMASI: Malaika wa amani, mlinzi wa roho na miili yetu, tuombe kwa Bwana.
SHEMASI: Usamehe na maondoleo ya zambi zetu na ya makosa yetu pia, tuombe kwa Bwana.
SHEMASI: Vilivyovyema na vifaavyo kwa roho zetu, tena kuwe amani katika dunia, tuombe kwa Bwana.
SHEMASI: Kuyamaliza maisha yetu inabaki, katika amani na toba, tuombe kwa Bwana. .
SHEMASI: Tuombe ili mwisho wa maisha yetu uwe kiKristu, kwa amani, bila aibu, tena tuone mufano mzuri mbele ya kiti cha hukumu cha Kristu.
SHEMASI: Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa kushinda Malkia wetu mtukufu. Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, ili sisi kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristu Mungu.
WAIMBAJI: Kwako, ee Bwana.
PADRI: Kwa kuwa u Mungu mwema na mpenda wanadamu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
PADRI: Amani kwa wote.
WAIMBAJI: Na kwa roho yako.
PADRI: Tuinamishe vichwa vyetu kwa Bwana.
WAIMBAJI: Kwako, ee Bwana.
*Sala ya kuinamisha nayo kichwa kwa sauti ya chini:*

PADRI: Ee Bwana Mungu wetu uliyeinamisha mbingu na ukashuka kwa ajili ya wokovu wa binadamu, uwatazamie watumishi wako na uriti wako kwa sababu wewe u Kuhani Mshindaji na rafiki wa watu. Usiyeongoja masaidio ya watu, kwa kuwa wao wamewazia huruma yako na

kutumaini ukombozi wako, uwachunge mangaribi na usiku huu hata na wakati wowote kwa maadui, na kwa vitendo vidogo vya Shetani asiye na mafaa ya akili na mwenye mawazo mabaya.

*Padri anapaza sauti.*

PADRI: Kwa kuwa uwezo wa ufalme wako uhimidiwe na utukuzwe Baba. Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

## APOSTIKHA WIMBO (TROPARI).

*Kila siku Mangaribi tunaimba Wimbo ya Apostikha toka Paraklitiki na sauti ya hii Juma, kwa sababu kila Juma tunaimba na sauti ingine. Kisha mwimbo ya kwanza tunasoma hii shairi inafwata.*

Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala mbinguni, tazama macho ya watumishi yanaangalia kwa mkono wa Bwana kama macho ya kijakazi kwa mkono wa bibi yake, hivyo macho yetu yanavyoangalia kwa Bwana Mungu wetu hata akatuhurumia.

Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na kuzarauliwa. Nafsi yetu inayala na kuzarauliwa kwa wenye kuikala na salama tena na kuzarau kwa wenye kiburi.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

PADRI: Sasa Bwana umuache mtumishi wako aende na amani, vile ulivyosema kwa maana macho yangu yameona wokovu wako uliyoutayarisha mbele ya makabila yote, mwanga wa kwangazia mataifa na sifa ya kundi lako Israeli.

MSOMAJI: Amina. Mungu Mtakatifu. Mweza Mtakatifu. Msiye kufa Mtakatifu, utuhurumie, *(mara tatu).* Utukufu Kwa Baba. , . Sasa na siku. . . Utatu Mtakatifu kamili utuhurumie. Bwana utusamehe zambi zetu. Rabi utuondolee makosa yetu. Mtakatifu utukaribie ukatuponye magonjwa yetu. Bwana hurumia, Bwana hurumua, Bwana hurumia.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . . Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni, utupe leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe makosa yetu kama sisi vilevile nasi tunawasamehe waliotukosea, tena tusishindwe na vishawishi, lakini utuokoe na yule mwovu.

PADRI: Kwa kuwa ufalme na uwezo, na utukufu ni wako, wa Baba, na wa Mwana na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

*Apolitikion ya ule Mutakatifu Kanisa yetu anashangilia ile siku.*
Utukufu. . . Sasa. . . . Theotokion ya ile sauti ya hii juma na siku fulani.

PADRI: Hekima.
WAIMBAJI: Himidi.
PADRI: Aliye ahimidiwe. Kristu Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.
MSOMAJI: Amina. Bwana Mungu aimarishe imani takatifu, isiyo na lawama ya waKristu watawa waorthodoksi katika mji na inchi hii milele na milele. Amina.
PADRI: Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.
MSOMAJI: Uliye wa thamani kuwashinda wakheruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi Waserafi, uliye ukimzaa Mungu Neno umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli, tunakutukuza we.
PADRI: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.
MSOMAJI: Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. Bwana hurumia*(mara tatu).* Ee Rabi Mtakatifu bariki.

PADRI: Kristu Mungu wetu ukweli, kwa maombezi ya Mama wake asiye na doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa msalaba uheshimiwa na uhuitaji, kwa matunzo ya majeshi yaheshimiwe ya mbinguni yaliyo bila mwili, kwa maombezi ya Yoanno Nabii, Mtakatifu, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu; ya Mitume Watakatifu, watukufu, wasifiwe kamili. . . *(kutaja jina la Mtakatifu, wa Kanisa ile),* ya wapateri Watakatifu wetu na Waekumeniki Wakubwa, walimu na Waierarka, ya Washahidi. Watakatifu, Watukufu, Washindaji Wazuri, ya Wapateri Wabebaji-Mungu, ya Mpateri Mtakatifu wetu Yoanno Krisostomo, Mwarkiepiskopo wa Konstantinopoli, ya Yoakim na Anna, Mababu Mungu Watakatifu na wenye haki *(Mtakatifu wa ile siku),* makumbusho yake leo, hata ya Watakatifu wote atuhurumie, akatuokoe, yu Mungu mwema, Mrahimu na Mpenda wanadamu.

PADRI: Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

MSOMAJI: Amina.

*Wakati ya Paska Padri anasema ivi:*

Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti; kwa wale walikuwa ndani ya kaburi aliwapatia uzima.

WAIMBAJI: Kweli alifufuka Bwana.

# APODIPNO KIDOGO

## (Sala ya usiku mbele ya Kulala)

PADRI: Ahimidiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

MSOMAJI: Amina.

*Elezo: Kama hakuna Padri mwaminifu moja anaweza kusoma hii sala mpaka ku mwanzo kusema hivi:*

Kwa Jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina. Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Mfalme wa mbinguni, wewe mfariji. Roho wa ukweli, uliye mahali popote na kuvijaza vitu vyote, hazina ya mema, tena Mupaji wa uzima, uje ukae kwetu, na kutusafisha kwa kila aibu, okoa roho zetu, wewe mwema. Amina.

MSOMAJI: Mungu Mutakatifu, Mweza Mtakatifu, Msiye kufa Mtakatifu, utuhurumie. *(mara tatu).*

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Utatu Mtakatifu kamili utuhurumie. Bwana utusamehe zambi zetu; Rabi utuondolee makosa yetu. Mtakatifu utukaribie na uponye magonjwa yetu. Bwana hurumia. Bwana hurumia. Bwana hurumia.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni, utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe deni zetu kama sisi vilevile tunawasamehe walio na deni zetu, tena usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule mwovu.

PADRI: Kwa kuwa ufalme, na uwezo, na utukufu ni Kwako. Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

MSOMAJI: Bwana hurumia. *(mara 12).*

Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu Mfalme wetu.

Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu yeye Mungu Mfalme wetu.

Njooni tumwinamie na tumsujudu yeye Kristu, aliye Mfalme na Mungu wetu.

**ZABURI 50 (51)**

Unirehemu, ee Mungu, sawasawa na wema wako; sawasawa na wingi wa rehema zako uzime makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, na kunisafisha na zambi yangu. Maana ninajua makosa yangu, na zambi yangu ni mbele yangu daima. Nimekukosea wewe peke yako, na kufanya yaliyo mabaya machoni mwako; ili ujulikane kuwa mwenye haki wakati unaposema, na kuwa safi wakati unapotoa hukumu. Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu; na katika makosa mama yangu alinichukua mimba. Tazama, wewe unataka kweli moyoni, na kwa siri utanijulisha hekina. Unisafishe kwa hisopo na nitakuwa safi; unioshe, na nitakuwa mweupe kupita theluji. Unifanye kusikia furaha na shangwe; ili mifupa uliyovunja ifurahi. Ufiche uso wako usitazame zambi zangu; na uzima maovu yangu yote. Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu. Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu. Unirudishie furaha ya wokovu wako; unitegemeze kwa roho ya tayari. Halafu nitafundisha wenye makosa njia zako; na wenye zambi watarudi kwako. Uniponyeshe na damu ya watu, ee Mungu, wewe Mungu wa wokovu wangu; ulimi wangu utaimba na sauti haki yako. Ee Bwana, ufungue midomo yangu, na kinywa changu kitaonyesha sifa zako. Maana hupendezwi na zabihu, ao ningeitoa, hufurahi kwa sadaka ya kuteketezwa. Zabihu za Mungu ni roho ya kuvunjika, moyo uliovunjika na wa toba hutauzarau, ee Mungu. Utendee Sayuni mema kwa mapenzi yako, ujenge kuta za Yerusalema. Halafu utafurahi kwa zabihu za haki, kwa sadaka ya kuteketezwa, na sadaka nzima ya kuteketezwa; halafu watatoa ngombe ndume juu ya masabahu yako.

**ZABURI** 69 (70)

Ee Mungu, uniokoe; unisaidie mbio, ee Bwana. Wapate haya na kufazaishwa wanaotafuta nafsi yangu; warudishwe nyuma na kuzarauliwa wanaofurahi kwa kuumia kwangu. Warudishwe nyuma kwa ajili ya haya yao wanaosema: Ewe, ewe, wote wanaokutafuta washangilie na kukufurahia; nao wanaopenda wokovu wako waseme daima: Mungu atukuzwe. Lakini mimi ni masikini na mwenye hitaji unisaidie mbio, ee Mungu; wewe ni musaidia wangu na mwokozi wangu; ee Bwana, usikawie.

**ZABURI 142 (143)**

Sikia maombi yangu, ee Bwana; usikilize kusihi kwangu; katika uaminifu wako unijibu, katika haki yako. Usihukumu mtumishi wako; maana machoni mwako hakuna mtu aliye hai atahesabiwa haki. Maana adui amefuata nafsi yangu; amepiga uzima wangu chini hata udongo: Amenikalisha katika pahali pa giza, kama wale waliokufa zamani. Kwa hivi roho yangu imezimia ndani yangu; moyo wangu ndani yangu ni ukiwa. Ninakumbuka siku za kale; Ninafikili matendo yako yote: Ninawaza kazi ya mikono yako. Ninakunyoshea mikono yangu; nafsi yangu inaona kiu kwa wewe, kama inchi inayochoka. Fanya mbio kwa kuni jibu, ee Bwana; roho yangu inazimia: Usinifichie uso wako; nisiwe kama wao wanaoshuka shimoni: Unifanye kusikia wema wako asubui; kwa maana ninakutumainia wewe: Unijulishe njia nitakayoikwenda; kwa maana ninakunyanyulia nafsi yangu. Uniponyeshe, ee Bwana, na adui zangu: Ninakukimbilia unifiche. Unifundishe kufanya mapenzi yako; kwa maana wewe ndiwe Mungu wangu: Roho yako ni mwema; uniongoze katika inchi ya haki. Unipatize uzima, kwa ajili ya jina lako: Kwa haki yako utoe nafsi yangu katika taabu. Na kwa wema wako ukatilie mbali adui zangu, na kuwaharibu wote wanaotesa nafsi yangu; kwa maana mimi ni mtumishi wako.

**DOKSOLOGIA KIDOGO**

Utukufu kwa Mungu juu pia, nchini amani urazi kwa wanadamu. Tukusifu, tukuhimidi, tukusujudu, tukutukuza, tukushukuru, maana utukufu wako ni mkuu. Ee Bwana mfalme, Mungu wa juu mbinguni, Baba mwenyezi, ee Bwana Mwana wa pekee Yesu Kristu na wewe Roho Mtakatifu. Ee Bwana, Mungu we, Mwana Kondoo wa Mungu, Mwana wa Baba, unazibeba zambi za dunia utuhurumie, unazibeba zambi za dunia. Upokee ombi letu, uliyeketi kuume kwa Baba na utuhurumie. Kwa kuwa Mtakatifu wa pekee, Bwana wa pekee, Yesu Kristu katika utukufu wa Mungu Baba. Amina. Kila Mangaribi nitakuhimidi, nitalisifu jina lako la milele, hata milele na milele. Ee Bwana

wewe ni kimbilio letu, kizazi baada ya kizazi. Mimi nilisema: Ee Bwana, unihurumie, uiponye roho yangu, maana nimekutendea zambi. Ee Bwana, nimekimbilia kwako, unifundishe kutenda mapenzi yako, maana ndiwe Mungu wangu. Maana kwako wewe iko chemchem ya uzima; katika mwangaza wako tutaona mwangaza. Onyesha huruma yako kwao wakujue. Ee Bwana, utujalie usiku huu, kutulinda na zambi. Umehimidiwa, ee Bwana Mungu wa Baba zetu jina lako limesifiwa, na limetukuzwa milele. Amina. Ee Bwana, huruma yako iwe nasi, tumevyokutumainia wewe. Ee Bwana, umehimidiwa, unifundishe zilizo haki zako. Ee Rabi, umehimidiwa, unifahamishe zilizo haki zako. Ee Mtakatifu, umehimidiwa, uniangaze kwa zilizo haki zako. Ee Bwana huruma yako ni ya milele; usiache kutuangalia sisi viumbe vya mikono yako. Sifa zakulaiki, kukuimbia ni kwako, utukufu ni wako, wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

## SIMVOLO YA IMANI

Nasadiki Mungu mmoja Baba mwenyezi, mwumba wa mbingu na wa dunia, hata vyote vilivyo onekana na visivyoonekana, tena Bwana mmoja Yesu Kristu. Mwana wa pekee wa Mungu, aliyezaliwa na Baba mbele ya wakati wote. Nuru toka Nuru, Mungu kweli toka Mungu kweli, aliyezaliwa, si Muumbwa mwenye asili moja (omousion) na Baba, aliye kwake vyote vilifanywa, aliye kwa ajili yetu wanadamu na ya wokovu wetu alishuka mbinguni, akapata mwili kwa Roho Mtakatifu na kwa Bikira Maria, na akawa mtu. Aliye sulibiwa kwa ajili yetu wakati wa Pontio Pilato. Akateswa, akawekwa kaburini. Na aliyefufuka katika siku ya tatu, kama yanavyo Maandiko. Na akapanda mbinguni ndipo anapokaa kuume kwa Baba. Na atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu walio na hai na waliokufa. Ufalme wake utakuwa bila mwisho. Tena Roho Mtakatifu yu Bwana yu Mwumba hai, aliyetoka na Baba, aliyesujudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana, aliyenena kwa midomo ya manabii, kwa Eklezya moja, Takatifu, Katholiki na Apostoliki. Naungama kwa ubatizo moja kwa maondoleo ya zambi. Natumaini ufufuo wa wafu hata uzima wa milele utakaokuja. Amina

Niwajibu kweli, kukuita, ee Mzazi Mungu, mwenye heri daima na usiye na doa tena Mama wa Mungu wetu. Uliye wa thamani kuwashinda wa Keruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi wa Serafi. Uliye ukimzaa Mungu Neno umebaki bila kukuharibu. Uliye Mzazi-Mungu kweli, tunakutukuza wewe.

Mungu Mutakatifu. . . *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . Utatu Mtakatifu kamili. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Baba yetu uliye mbinguni. . .

PADRI: Kwa kuwa ufalme na uwezo, na utukufu ni wako, Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Kisha tutasoma Kontakion ya wale watakatifu wa ile siku. Kama hakuna tutasoma hii:*

Mungu wa mababu zetu, kwa mapendo yako umetusaidia tangu zamani mpaka sasa usituondolee huruma yako lakini kwa maombi ya mababu zetu, uiongoze amani ya uzima wetu.

Kanisa yako inapamba sawa nguo nyekundu nzuri kabisa, damu ya mashahidi wako wa dunia nzima, na inapaza sauti ya ile damu ya mashahidi. Kristu tuma rehema yako ku mataifa yote, amani kwa watu wote sawa kipawa na ku roho huruma yetu.

Utukufu kwa Baba. . .

Kristu, pumuzisha, karibu na Mtakatifu, roho za watumishi wako kule kusio kuuma, kusio sikitiko, kusio kutoa pumuzi lakini kuliye uzima wa milele.

Sasa na siku zote. . .

Ee Bwana, kwa maombezi, ya Mzazi Mungu, na ya Watakatifu wote, utume amani yako na utuhurumie, kwa sababu wewe ni mwenye huruma.

Bwana hurumia *(ma kumi ine).*

Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa, na kutukuzwa wakati wote na katika kila saa mbinguni na duniani, uliye mwadilifu, mrahimu tele, mfazili sana unayependa wenye haki, tena kuwahurumia wenye zambi; unayewaita wote kuona wokovu, ukiwaahidi vitu vema vilivyokuja; wewe, ee Bwana, hata katika saa hii uyapokee maombi yetu, na kuyashurtisha maisha yetu njiani pa amri, uuzitakase roho zetu, uyasafishe miili yetu, uyatengeneze mafikira zetu, uzinyoshe nia zetu; ukatuokoe na kila shida, ubaya, na teso, utulindie kwa Malaika wako, ili sisi tukiwa na utunzi na uongozi wao, tufike katika umoja wa imani na kuujulisha utukufu wako usiofikika, Kwa kuwa unahimidiwa milele na milele. Amina.

MSOMAJI: Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Uliye wa thamani kuwashinda. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Kwa jina la Bwana, ee Rabi, bariki.

PADRI: Mungu atufazili, na kutubariki, atuangazie uso wake, na kutuhurumia.

MSOMAJI: Bwana hurumia *(kumi na pili),* Mutakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu utuokoe.

**SALA KWA BIKIRA MARIA MZAZI MUNGU MTAKATIFU KAMILI**

Ewe Bibi Malkia; uliye bila doa, bila waa, bila uchafu, safi kamili Bikira Bibi Mungu, uliyemwunganisha Mungu Mwana, na wanadamu kwa uzazi wako wa ajabu, na kuuchanganisha uumba wetu, uliokuwa ondoshwa, nao walio mbinguni, uliye peke yako matumaini ya wakufa moyo, na msaada wa washawishwa, uliye tayari kuwalinda wote wanakukimbilia wewe; wewe makimbilio ya Wakristu wote, usinikiri mimi mtu mwenye zambi, mtu wa waa; niliofanya kufaa hata si kitu kwa mafikiri, na maneno, na matendo yangu ya aibu, tena kuwa mtumwa hiari wa anasa kihebu ya maisha kwa uzembe wangu, Lakini kwa kuwa wewe ni Mama wa Mungu Mpenda Wanadamu, unirehemu kwa upendo wanadamu wako mimi mtu mukosaji, na mpotevu, na kuipokea ombi langu linalokutolewa na midomo michafu yangu, na mtoto wako, na Rabi wetu, Na kwa ujasiri wako kama Mama wako unipatanishe, ili kuniikunjua rehema yako ya kupenda wanadamu ya wema wake, na akiyasamehe makosa yangu yasiyohesabiwa, anirudishe katika utubu na kunionyesha mshika mstahiliwa, wa amri yako, uwe daima karibu nami, ewe Mama mrahimu, mwenye upole, na mpenda uwema, katika maisha haya mhifazi na msaidizi wa moto, kuyazuia marukio ya madui, na kuniongoza njiani ya wokovu. Tena katika saa ile ya kufariki duniani, kuitunza roho yangu ya kizilini na kuzifukuza mbali yake zile nyuso za giza za mashetani maovu. Hata katika siku ile ya hukumu iliyokuongofya, kuniokoa na azabu ile ya milele, na kunijalia ku uriti utukufu usiokuelewa wa Mwana wako, na Mungu wetu. Uwe kuniufike, ewe Mzazi Mungu. Mtakatifu kushinda Bibi Malkia wangu, kwa utetezi na hifazi wako, nikiwa na neema, na upenda wanadamu wa Mwana wako wa pekee yeye Bwana, na Mungu, na Mwokozi wetu anaye na haki, utukufu wote, heshima na usujudu, pamoja na Baba yake asiye na mwanzo, pamoja na Roho Mtakatifu Kamili, Mwema, Mwumba hai, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SALA KWA BWANA WETU YESU KRISTU**

Na utupe, ee Rabi, saa hii tukienda kulala, mapumziko ya mwili, na ya roho tena utulindie na ule usingizi wa giza ya zambi, na ya kila ubaya ungine wa giza, na wa usiku. Zuia mashawishi kuturukia, zimisha mishale ya yule mwovu, yaliyo na moto, yanatupwa kwetu kwa hila. Punguza vitu vibaya vya mwili wetu, ukiangaza kila nia yetu ya nchini na kidunia. Tena kizi yetu, ee Mungu akili ya kukesha, mafikira sawa moyo wangalifu, usingizi wa kisahala, safi na bila mwogofyo wa kishetani. Hata kutuamusha wakati wa kusali tuwe wahodari mu amri zako, na kuyakamata makumbusho ya hukumu yako. Tena utujalie usiku kucha tuwe na sifa yako, ili tulisifu, tulihimidi, tulitukuze jina lako linaloheshimiwa kamili, na kulipaza sana, jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Ee Mzazi Mungu, Mbarikiwa, Bikira daima, Mtukufu kushinda, uipishe sala yetu kwa Mwana wako tena Mungu wetu, na kutuombea aziokoe roho zetu kwa mateteo yako.

Baba ni Matumaini yangu, Mwana ni makimbilio yangu, Roho Mtakatifu ni himaya yangu. Utatu Mtakatifu, utukufu kwako.

Matumaini yangu yote ni kwako, ee Mama wa Mungu, unilinde chini ya himaya yako.

Ewe, Mjaliwa na neema kabisa, dunia yote inafurahi, mifano yote ya wamalaika na makabila yote ya wanadamu, na nyumba ya Mungu Takatifu, na paradizo ya akili. Bikira mrahimu, kwa hii Mungu alichukua mwili na akajifanya mtoto, na tangu milele, alikuwako Mungu wetu. Kwa sababu utumbu wako umefanya kiti cha ufalme na utumbo wako tena umefanya mkuu kupita mbingu. Ewe, mjaliwa na neema kabisa, duniani yote inafurahi.

**SALA KWA MALAIKA MLINZI**

Malaika Mtakatifu, musimamizi wa kuchunga moyo wangu maskini na uzima wangu wa tamaa, usiniache mimi mukosefu na usinitenge kwa sababu ya ulaji wangu. Usiniachilie na shetani mwovu kwa kunikamata na kwazibisha mwili wa mauti. Sabitisha mukono wangu mwembamba na mregevu, uniongoze katika njia ya wokovu. Ndiyo, ee Malaika Mtakatifu wa Mungu, mulinzi wa moyo wangu na wa mwili maskini, unisamehe zambi zangu zote kwani nilikutukana siku zote za uzima wangu na zambi zangu za hizi siku, unifunike usiku ya leo na unichunge ku vishawishi vya shetani ili nisivute tena hasira ya Mungu na kutenda zambi ingine. Uniombee kwa Bwana ili asinisabitishe katika oga wake na anifanye mtumishi mstahilivu wa rehema yake. Amina.

Kwako, jemadari kunilinda nina deni
kukushukuru kwa wokovu na kushinda kwangu;
Mimi mji wako, ee Mzazi Mungu.
Tena kwa mamlaka yako si kushindwa.
na hatari kila namna niepuke kukuimba.
Kwa kelele kuu: Salamu. Bibi-arusi, usiyeolewa.

Salamu Mujaliwa Mzazi-Mungu Bikira Maria. Bwana ni pamoja nawe. Unahimidiwa Wewe katika wanawake na muhimidiwa ni tunda la tumbo lako, kwani ulizaa Mwokozi wa roho zetu, *(mara tatu).*

PADRI: Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

MSOMAJI: Utukufu kwa Baba. Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Ee Padri Mtakatifu, bariki.

PADRI: Kristu Mungu wetu ukweli, kwa maombezi ya Mama wake asiye na doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa msalaba uheshimiwa na uhuitaji, kwa matunzo ya majeshi yaheshimiwe ya mbinguni yaliyo bila mwili, kwa maombezi ya Yoane Nabii, Mtakatifu, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu; ya Mitume Watakatifu, watukufu, wasifiwe kamili. . . *(kutaja jina la Mtakatifu, wa Kanisa ile),* ya wapateri Watakatifu wetu na Waekumeniki Wakubwa, walimu na Waierarka, ya Washahidi, Watakatifu, Watukufu, Washindaji Wazuri, ya Wapateri Wabebaji-Mungu, ya Mpateri Mtakatifu wetu Yoanno Krisostomo, Mwarkiepiskopo wa Konstantinopoli, ya Yoakim na Anna, Mababu Mungu, Watakatifu na wenye haki *(Mtakatifu wa ile siku),* makumbusho yake leo, hata ya watakatifu wote atuhurumie, akatuokoe, yu Mungu mwema, Mrahimu na Mpenda wanadamu.

PADRI: Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe. Amina.

*Elezo: Kama hakuna Padri mwaminifu ataisha hii sala hivi:*

Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

*Sala mbele ya kulala ya kila mwaminifu Orthodokse*

Bwana hurumia wale wanatuchukia na walitutukana; fanya mema kwa wafazili (wenyi mema). Upokee maombi ya ndugu na jirani zetu kwa ajili ya wokovu na uzima wa milele. Angalia wagonjwa, uwape tunzo; ongoza wale weko juu ya bahari, sindikiza wasafiri; uchunge mukubwa wetu mu vita. Kwa wale wanatusaidia na wanatuonyesha mapendo yao, uwape maondoleo ya zambi, Hurumia, kwa ajili ya rehema yako, wale walituomba kuwaombea japo uovu wetu. Ukumbuke. Bwana, wapadri na ndugu waliolala mbele yetu, uwape mapumuziko, kule kunangara nuru ya uso wako, Kumbuka, ee Bwana, ndugu zetu wafungwa, uwafungue mu mateso yao, Kumbuka. Bwana wale wanaoleta sadaka, na wale wanaotumika mu ma Eklezya zako Takatifu; Uwapatie rehema ya maombi yao wanakuomba kwa ajili ya uokovu na uzima wa milele, Bwana, kumbuka tena sisi, watumishi wako wanyenyekevu na wakosefu, kwa uovu, utuangazie roho zetu kwa nuru ya maarifa yako, utuongoze njiani za kanuni zako, kwa maombezi ya mama yako Bikira, Mama wa Mungu, Maria, Bikira siku zote, na ya Watakatifu wote, sababu umebarikiwa hata milele na milele. Amina.

# NYIMBO ZA UTATU MTAKATIFU NA WIMBO WA MWANGAZA (FOTAGOGIKA)

*Ya kuimba wakati wa kwarezima mkubwa ya sauti ya wakati Kwa mwimbo ya kwanza (Ya Utatu)ku mwisho yake na ku mwisho ya Fotagogikon tunaimba ivi:*
*Kila mu kazi moya:* kwa ulinzi wa Malaika utuhurumie.
*Mukazi pili:* Kwa maombi ya Mtakatifu Mubatizaji Yoanno, utuhurumie.
*Mukazi Tatu:* Kwa nguvu ya Musalaba wako na utuokoe.
*Mukazi Ine:* Kwa maombi ya Wamitume wako, utuhurumie.
*Mukazi Tano:* Kwa nguvu ya Musalaba wako na utuokoe.

*Mu Posho: Hatuimbie Nyimbo za Utatu Mtakatifu na Fotagogika. Tunaimba kisha Eksapsalmos Bwana ndiwe Mungu. . . pamoja na Shairi ha Ine wa Zaburi na kisha wimbo ya Wafu. Iko ndani kwa kitabu Triodion.*

## SAUTI YA KWANZA

Ya Utatu

Kwa umbo ya Majeshi ya Wabila-mwili tumefika ku hali isiyo mwili na ya kiroho, na kwa wimbo wa Trisayion tulipokea nuru ya umungu katika watu tatu; tuimbe pamoja na Wakeruvi kwa ajili ya Bwana wetu peke Yake: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu Wetu, kwa ulinzi wa Malaika utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Pamoja na Majeshi ya mbinguni, kama Wakeruvi tumuimbie Aliye-Juu, tukiimba sifa ya Trisayion: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu Wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Tukiamka usingizini, tunasujudu mbele Yako na pamoja na Malaika tunasema tena wimbo: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

**FOTAGOGIKON:**

Ee Kristu unayeonekanisha nuru, takasa roho yangu ku zambi yo yote kwa ulinzi wa Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

## SAUTI YA PILI

Ya Utatu

Sisi duniani tunayofananishwa Majesi ya Juu mbinguni, tunakotolea wimbo wa ushindi tukiimba: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Hali isiyoumbwa Fundi wa ulimwengu, mungua midomo yetu na kinywa chetu kitatangaza sifa yako pakuimba: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Bwana uliyeniamusha usingizini mwangu, angaza moyo wangu na roho yangu, fungua midomo yangu ili ni kuimbie, ee Utatu Mtakatifu: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wangu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

### FOTAGOGIKON

Tuma nuru yako ya milele, ee Kristu Mungu wetu, angaza macho yangu na moyo wangu kwa ulinzi wa Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

## SAUTI YA TATU

Ya Utatu

Utatu wa asili moja na usiyogawanyika. Umoja katika watu tatu wa milele, pamoja na Malaika tunakuimba, ee Bwana: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Baba wa milele. Bwana wa milele pia. Roho Mtakatifu anayegawanya umilele wa Mungu mmoja, pamoja na Wakeruvi tunasubutu kukutukuza tukisema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Mwamzi atakuja kama umeme kufumia matendo ya kila mmoja; na woga tunakuimbia katikati ya usiku: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu utuhurumie.

### FOTAGOGIKON.

Tuma nuru yako, ee Kristu MUngu wetu, angaza moyo wangu kwa maombi ya Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

## SAUTI YA INE

Ya Utatu. . .

Pamoja na watumishi wako wa mbinguni, sisi wenye mauti tunasubutu kukuimbia: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Kama jeshi la Malaika mbinguni, na woga duniani tunakutolea wimbo huu wa ushindi, ee Bwana: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Pamoja na Baba yako wa milele na Roho Mtakatifu Kamili, ee Kristu Mungu, tunasubutu kukutukuza kama Wakeruvi tukisema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

### FOTAGOGIKON.

Wewe unayeleta nuru duniani, angaza roho yangu ukiitakasa ku zambi yo yote kwa ulinzi wa Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

## SAUTI YA TANO

Ya Utatu. . .

Ni Malaika wa kuimba na kuomba, bila kwacha tumulalamikie Bwana: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Tunaposubutu kuwafananisha Majeshi ya mbinguni japo masauti yetu uasiostahili tunakuimbia, ee Utatu wa milele: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Ee Kristu uliyekaa tumboni mwa Bikira bila kutengana na kifua cha Baba, pokea sauti yetu pamoja na ile ya Malaika: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

### FOTAGOGIKON

Bwana, Chemchem ya nuru, tuma mwangaza wako, angaza wangu kwa ulinzi wa Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

## SAUTI YA SITA

Ya Utatu. . .

Wakeruvi na woga, Waserafi na kutetemeka, wanaimba bila kwacha wimbo mara tatu: Mtakatifu; na sisi wenye zambi tunapaza sauti pamoja nao: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Wakeruvi na vinywa vyao vya mwili. Waserafi na doksologia yasipo kwacha, wanakuimbia wimbo mara tatu Mtakatifu, ee Mungu wetu, na sisi duniani na midomo yetu isiyostahili kuimba tunakutolea sifa yetu tukiswema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Tutukuzeni watu watatu wa umungu moja, wenyi kuungana bila fujo, na tunaimba tena wimbo wa Malaika tukisema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Myngu, utuhurumie.

### FOTAGOGIKON

Bwana, tuma rohoni mwangu nuru yako ya milele kwa ulinzi wa Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

## SAUTI YA SABA

Ya Utatu

Bwana. Wakeruvi wanaimba juu ya utukufu wako wa juu na Malaika wanaabudu ukuu wako kimungu, pokea ku midomo yetu ya zambi wimbo wetu: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Tutolee sifa tatu za Waserafi ku Umungu usiyokaribika, ku Utatu moja na tuimbe na woga na mtetemeko: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

Sasa na siku zote...

Ee nafsi yangu fukuza kama musigishi uvivu yako na onyesha kwa Muhukumu mapendo ya toba yako na katika boka paza sauti kusema hivi: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, iwe Wewe Mungu.

**FOTAGOGIKON**

Bwana, angaza moyo wangu ili ukuimbe, unifundishe kufanya mapenzi yako kwa ulinzi wa Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

## SAUTI YA MNANE

Ya Utatu. . .

Tunapoinua mioyo yetu mbinguni, tufananishe Majeshi ya mbingu, tujydusu na woga mbele ya Bwana, tukimwimbia wimbo wa ushinda tukisema: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa ulinzi wa Malaika, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . .

Wakeruvi bila kusubutu kunyanyua macho yao Kwako wanaimba na furaha maneno kimyngu ya Trisayion; na sisi wenye zambi pia, tunapaza sauti pamoja nao: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Sasa na siku zote. . .

Tunapoelemewa na uzito wa zambi zetu na tunaposubutu kuinua macho ku mbingu yako roho na mwili zenye kuinamishwa, tunaimba pamoja na Malaika: Mtakatifu. Mtakatifu. Mtakatifu ndiwe, ee Mungu wetu, kwa maombi ya Mzazi-Mungu, utuhurumie.

**FOTAGOGIKON**

Ee Kristu, nuru ya milele, uniangaze mimi wote kwa ulinzi wa Malaika na uniokoe. *(mara tatu).*

# KANUNI AKATHISTE YA MZAZI-MUNGU

**WIMBO 1. Sauti ya Ine.**

Kinywa changu kitafunguka, na kitajaa na Roho Mtakatifu: Natolea Shairi yangu kwa Mama wa Mfalme; na wataniona, katika hii siku kuu kubwa, nikiimba na furaha maajabu yake yote.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi Mungu, utuokoe.

Malaika mkuu Gabrieli akakutambua kama Kitabu cha hai cha Kristu chenye kutiliwa muhuri ya Roho Mtakatifu, na akakulalamikia, ee Bikira Safi: Salamu, chombo cha furaha humo munapotea laana ya Mama ya wenye hai.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi Mungu, utuokoe.

Salamu. Bibi Bikira wa Mungu, matumaini ya Adamu na ya ukombozi wake, woga wa Hadeze uliyoua, makao takatifu ya Mfalme wetu, Salamu, kiti cha moto cha Bwana Mwenyezi.

Utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Salamu peke yako ulitoa ua halitafifia kamwe; Salamu, wewe uliyezaa tunda nzuri na manukato ya Mfalome wetu, Salamu. Bibi-Arusi usiolewa mwenye kuleta wokovu duniani.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Salamu, hazina ya usafi yenye kutuamusha humo tuliangukia; Salamu, ua mweupe ya ufalme ambayo manukato yanapakwa waaminifu, ubani wa harufi nzuri na manukato ya Samani kamili.

**WIMBO 3**

Chunga kwa ulinzi wako, ee Mzazi-Mungu na Chemchem isiyokauka, waimbaji wote wenye kukutukuza kwa nyimbo zao, na katika utukufu wako kimungu uwape taji la washindaji.

Ulioteshe ngano ya mbinguni mu udongo wasipo kulima; Salamu, meza ya fumbo iliyochukua mkate wa uzima, Salamu, Bikira Malkia, Chemchem isiyokauka ya wimbi lenye kuleta uzima.

Salamu, maana ulizaa kwa ajili ya waaminifu sadaka yasipo kilema; Salamu, Mama wa Mwana kondoo anayeondoa zambi ya dunia yote; Salamu, majaliwa ya heri.

Salamu, alfajiri ya kwangaa ambaye peke yako ulichukua Kristu Jua letu. Salamu, hema ya Nuru iliyofukuza giza za mauti na kuondoa giza ya Hadeze.

Salamu, Mlango wa peke ambamo mulipita Neno peke yake. Bikira uliyevunja katika uzazi wako milango na makomeo ya Hadeze; Salamu, mlango kimungu wa taifa lililokombolewa. Bikira mstahili kamili wa nyimbo zetu.

**WIMBO 4**

Huyu mwenye kukaa na utukufu pa kiti cha umungu alikuja pa wimgu nyepesi: Ni Yesu. Mwokozi wetu kimungu; na kwa mkono wake safi Kamili aliokoa wale wenye kumwimbia: Ee Kristu Mungu wetu, utukufu ku uwezo wako,

Kwa myimbo zetu na kwa masauti yetu tunakupazia sauti na ibada. Bikira mstahili wa nuimbo zetu: Salamu, mlima wa ustawi wenye kunyanyuliwa na Roho Mtakatifu. Salamu, kinara cha zahabu na chombo ambamo maua inalindwa, uzuri wa waaminifu.

Mjaliwa ya ulimwengu, Salamu, Malkia usiye na doa, Salamu, mungazi wenye kutuongoza toka dunia mpaka ku wokovu. Salamu, Kilalo chenye kufufua waaminifu wote wenye kukutukuza na nyimbo zao.

Nguzo refu zaidi kuliko mbingu, Salamu, ee Bikira Safi, uliyechukua bila uchungu msingi wa ulimwengu tumboni mwako; Salamu, Shinikizo uliyetosha kwa damu yako nyekundu kimungu ya Mfalme Mwenyezi.

Ulizaa Mpana-Sheria wetu, Salamu, Malkia kweli, kwani anazima bure uhalifu wetu, Salamu, bahari isiyoweza kupimwa, ncha isiyokadirika. Bibi-Arusi usiyeolewa ambaye katika wewe tunakuwa miungu.

Kwa ajili ya ulimwengu ulisuka taji isiyofanyika na mkono wa mwanadamu; tunakuimbia na tunakulalamikia: Bikira Mtakatifu. Salamu, mlinzi wa ulimwengu, boma imara, ngome na kimbilio takatifu.

**WIMBO 5**

Ulimwengu umechukuliwa kwa utukufu wako kimungu, ee Bikira usiyeolewa, kwani ulichukua Mungu Mkuu tumboni mwako na ulizaa Mwana asiye wa wakati mwenye kuleta wokovu kwa wale wenye kuimba sifa yako.

Wewe uliyezaa njia ya uzima; Salamu, usiye na doa, kwani uliokoa ulimwengu ku garika na ku zambi, Salamu, mchumba takatifu uliyepokea Neno ya Mungu na woga, Salamu, makao ya Muumba na ya Bwana.

Salamu, siye na doa, ngome na boma la wanadamu, makao ya utukufu na woga wa Hadeze, nuru ya mabikira, furaha ya Malaika mbinguni, mlinzi wa waaminifu wenye kukuomba.

Gari la moto la neno Mtakatifu, Salamu, Malkia, Paradizo ya fumbo ambamo katikati Bwana anakuwa mti mpya wa uzima ambao utamu unakaa pahali pa uchungu wa mauti kwa ajili ya waaminifu wenye kuonja tunda lake lenye kuleta uzima.

Tunaposabitishwa kwa uwezo wako, tunakupazia Sauti na ibada: Salamu, mji wa Mfalme Mkuu; mwenye kusema juu yako anakutukuza na ustahilivu, Salamu, zimu isiyoweza kupimwa na mlima haramu.

Hema kubwa ya Neno la Mungu, Salamu, usiye na doa, kwani uliumba johari kimungu, Salamu, ajabu isiyosawanishwa; pamoja na Mungu unapatanisha wale wenye kukutangaza mwenye heri, ee Mzazi-Mungu.

**WIMBO 6**

Tunapotukuza hii siku Kuu kimungu na takatifu ya Mzazi-Mungu, njooni, enye waaminifu, tupigeni mikono, tukimutukuza Mungu aliyezaa.

Chumba cha arusi takatifu kamili cha Neno la Mungu, kisa ya umungu wetu, Salamu, ee Bikira Safi, utukufu wa Manabii waliokutukuza, pampo la Mitume, Salamu.

Ulikomesha umande uliyozimisha moto ya miungu ya uongo; tena tunakupazia sauti: Salamu, manyonya ya fumbo yenye kufunikwa na umanda ambayo Gideoni alitangulia kufikiri.

Kwa sisi wenye kukuimbia: Salamu, uwe bandari ya amani katikati ya mawimbi, kimbilio katika bahari ya mateso, makimbilio juu ya werevu wa Adui.

Kisa ya furaha yote, utupe hekima ya kukuimbia: Salamu, kichaka cha moto bila kuteketezwa, Salamu, wingi la nuru lenye kufuwanika waaminifu na kivuli chake cha milele.

KONTAKION Sauti ya mnane.

Masauti yetu ya ushindi yavume kwa ajili ya heshima yako, ewe Malkia msiyeweza kushindwa, wewe mwenye kutuokoa ku hatari ya vita, Mzazi-Mungu, Bikira Mkuu. Sifa zetu na nyimbo zetu za shukrani zinapanda kwako. Simika pembveni yetu moja ya maboma imara na mkono wako wa uwezo, utuokoe ku hatari yote ujiharikishe kuwasaidia waaminifu wanaokuimbia: Salamu, Bibi-Arusi usiyeolewa.

**WIMBO 7**

Hawakuabudu kiumbe pahali pa Muumba, waaminifu wa Mungu Aliye-Juu, lakini wakapambana kwa furaha na moto uliyowatisha; na wakaimba katika tanuru ya moto: Utukuzwe, ee Bwana mwenye kustahili Sifa. Mungu wa Baba zetu.

Tunakuimbia na tunakupazia sauti: Salamu, gari la Jua la roho, ndiwe, kweli mzabibu uliyotoa zabibu tamu ambayo divai inafurahisha waaminifu wenye kukutukuza.

Ulizaa huyu mwenye kuponyesha kidonda yote. Salamu, mchumba wa Mungu, tawi la fumbo uliyechanukisha umilele; Salamu, ee Malkia mwenye kutujaza na furaha na mwenye kutufanya wariti wa uzima.

Ulimi wa wasemaji unahangaishwa kwa kukutukuza, ewe Mzazi-Mungu; uliinuka juu zaidi kuwapita waserafi ulipomza Kristu Mfalme wetu; umuombe ili awaokoe ku hatari yote waaminifu wenye kusujadu mbele yako.

Mipaka ya dunia inakutangaza mwenye heri na inaimba na mapendo: Salamu, Kitabu takatifu humo kidole cha Baba iliandika Neno ambaye tunakuomba umusihi ili awaandike watumishi wako ku kitabu cha uzima.

Sisi watumishi wako tunakusihi na tunainamisha mioyo yetu mbeele yako: Inamisha sikio lako kwa sisi na utuokoe ku zimu ya vishawishi; kinga taifa lako ku mishale ya Adui, ewe Mtakatifu Mzazi-Mungu.

**WIMBO 8**

Vijana walikombolewa ku tanuru ya moto na huyu aliyezaliwa kwa Mzazi-Mungu; hii zamani ilikuwa ni mfano sasa inakuwa kweli, kwani anakusanya ulimwengu wote wenye kwendelea kuimba: Enye wote, viumbe vya Bwana, tukuzeni Bwana, kwake utukufu mkuu na sifa mbele.

Ulimupokea Neno tumboni mwako, ulichukua huyu anayachukua dunia mkononi mwake, ulilisha na maziwa Yako huyu mwenye kulisha na alama moja ulimwengu wote; tena tutaimba kwa ajili yake: Enyi wote, viumbe vya Bwana, tukuzeni Bwana, kwake utukufu mkuu na sifa milele.

Musa alitambua katika kichaka cha moto fumbo kubwa ya uzazi wako; Vijana walitangulia kuuona wazi kabisa wakati waliposimama katikati ya moto bila kuteketezwa; Bikira Mtakatifu na usiye na do, tunaimba sifa yako ya milele.

Zamani tulipotwaliwa kwa werevu wa nyoka, tulipata vazi la umilele katika uzazi wako, sisi ambao zamani tulikaa katika giza ya zambi tuliona Nuru ikikaa tumboni mwako; ee Bikira, hema ya nuru, tutaimba sifa yako milele.

Kwa ajili ya ulimwengu ulizaa Mwokozi mwenye kutuchukua toka dunia mpaka mbinguni; Salamu, ewe Mbarikiwa kamili, nguvu na ulinzi, ngome na boma ya wale wenye kuimba pamoja nawe: Enyi wote, viumbe vya Bwana, tukuzeni Bwana, kwake utukufu mkuu na sifa milele.

**WIMBO 9**

Kila mwana wa dunia afurahiwe rohoni, achukuwe taa yake yenye kuwaka, Malaika mbinguni washangilie na furaha Siku kuu Takatifu ya Mzazi-Mungu na wamuimbie: Salamu, ee mwenye heri na Bikira daima. Mtakatifu Mzazi-Mungu.

Ili tukuimbie: Salamu, sisi waaminifu tunaokuwa washariki wa furaha yako, utuokoe ku majaribu yasipo mwisho, ku minyororo ya Adui na ku mateso mengine yote yenyi kututisha sababu ya wingi wa zambi zetu.

Ndiwe matumaini yetu na nuru yetu, tena tunakulalamikia: Salamu, nyota yasipo mwisho uliyeingiza Jua letu ulimwenguni; Salamu, Bikira usiye na doa, kwani umetufungulia Edeni iliyofungwa mpaka ku inchi yao ya mbinguni.

Tusimame na woga katika nyumba ya Mungu na tuseme: Salamu, Malkia wa ulimwengu, salamu, Maria, Bibi wa mioyo zetu, Salamu, ewe mzuri kamili na usiye doa kamili hombo cha manemane uliyepokea mpako usiyokwisha uliyomwangwa pa wewe. Njiwa Bikira daima. Salamu, uliyezaa Mungu wa wema. Salamu, utukufu wa Wakakatifu wote na taji ya Mashahidi, pambo la wenye haki na wokovu wa roho zetu sisi wote.

Bwana, samehe uriti wako, ukifunga macho pa zambi zetu zote, pokea vema ombi la huyu aliyekuchukua duniani, ee Kristu, wakati katika mapendo yako kubwa ulikubali kuvaa hali ya wanadamu.

**KONDAKION Sauti ya Mnane**

Masauti yetu ya ushindi yavume kwa ajili ya heshima yako, ewe Malkia msiyeweza kushindwa, wewe mwenye kutuokoa ku hatari ya vita, Mzazi-Mungu, Bikira mkuu, Sifa zetu na nyimbo zetu za shukrani zinapanda kwako. Simika pembeni yetu moja ya maboma imara na mkono wako wa uwezo, utuokoe ku hatari yote, ujiharikishe kuwasaidia waaminifu wanaokuimbia: Salamu, Bibi-Arusi usiyeolewa.

# MAFUNGU YA WIMBO AKATHISTE

*Wimbo Akathiste wa Mzazi-Mungu ao Salamu ya Maria Mtakatifu kamili, haiko paka Ibada ya wakati wa Kwarezima.*

*Tunaweza kuisoma tena kila siku pamoja na Apodipnon Kidogo.*

*Ni hivi wanafanya Matawa Waorthodoksi ku Monasteri yetu, na zwezo ni yenyi kubarikiwa na waaminifu wengi duniani wanaifuata.*

*Kama tunasoma Apodipnon Kidogo. Salamu ya Mzazi-Mungu tutaisoma kisha Symvolo ya Imani.*

**KONTAKION**. Sauti ya Mnane.

Kwako, jemadari kunilinda nina deni
kukushukuru kwa wokovu na kushinda wangu.
Mimi muji wako, ee Mzazi Mungu.
Tena kwa mamlaka yako si kushindwa,
na hatari kila namna niepuwe kukuimba,
kwa kelele kuu: Salamu, Bibi-Arusi, usiyeolewa.

## FUNGU 1

### I K O S 1

Alitumwa toka mbinguni Malaika Mkuu kumwambia Mzazi-Mungu: Salamu. Yeye alipokuona wewe, ee Bwana, ukipata mwili mara ileile kwa sauti yake ya bila-mwili, alistaajabu, akasimama na akasema na sauti kubwa.

Salamu, kwa kuwa unaangaza wokovu wetu.
Salamu, kwa kuwa katika wewe uovu uliondolewa.
Salamu, uliyemusimamisha tena Adamu aliyeanguka.
Salamu, uliyemwoka Eva halii tena.
Salamu, ndiwe mlima kutofikika kwa mawazo ya wanadamu;
Salamu, ndiwe bahari isiyoweza kufumbuliwa hata kwa macho ya Malaika.
Salamu, kwa kuwa wewe ni kiti cha ezi na makao ya Mfalme.
Salamu, kwa kuwa unamubeba Muumba wako.
Salamu, ndiwe nyota iliyoonyesha Jua, Salamu, ndiwe tumbo Mungu alimojifanya mtu.
Salamu, kwani katika wewe kiumbe kinapata upya;

Salamu, kwani kwako Muumba anakuwa mtoto.

Salamu, Bibi-Arusi usiyeolewa.

**I K O S 2**

Bikira Mtakatifu alipojua hali ya ubikira wake akamujibu Malaika Gabrieli na uhodari: Neno lako ni la ajabu rohoni mwangu, namna gani unasema nitachukua mimba, maana sijui mume?

Alliluia.

**I K O S 3**

Kwa kufahamu fumbo isiyo julikana. Bikira akamuelekea Mtumishi na akauliza namna gani anaweza kuzaliwa Mwana tumboni mwake. Malaika mwenye kujaa na heshima akamuambia na furaha: Salamu, maana umefumbuliwa shauri iliyo siri. Salamu, mlinzi wa fumbo yenye kufichwa. Salamu, ewe utangulizi takatifu wa miujiza ya Kristu. Salamu, ewe jumla ya Kanuni zake kimungu.

Salamu, ewe mungazi ya mbinguni huko Mungu alishuka;

Salamu, ewe kilalo chenye kutuongoza toka dunia mpaka mbinguni.

Salamu, ewe mastaajabu ya Malaika Watakatifu yasiyokwisha.

Salamu, kisa ya maombolezo ya Hadeze na ya mashetani.

Salamu, ewe uliyezaa nuru kwa njia isiyoelezwa;

Salamu, ewe usiyemufumbulia namna gani mtu hata mmoja;

Salamu, ewe unayepita maarifa ya wenye hekima;

Salamu, unayeiangazia akili ya waaminifu

Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

**I K O S 4**

Uwezo wa aliye-Juu ukamufunika na kivuli chake Bikira msiyeolewa kwa kupata mimba, na tumbo lake likawa Shamba tamu kwa wote watakao kuvuna wokovu kwa kuimba:

Alliluia.

**I K O S 5**

Alipochukua Bwana Mungu tumboni mwake. Bikira akaenda kuonana na Elisabeti: Mwana wake akatambua wokovu wa ajabu na akaruka tumboni mwa Mama yake akaimba kwa ajili ya Mzazi-Mungu: Salamu chipukizi la ua la milele;

Salamu, shamba la tunda tamu kabisa, bustani ya Bwana rafiki yetu.

Salamu, shamba munamoota uzima wetu.

Salamu, udongo wa kutoa wingi wa ukombozi.

Salamu, meza Takatifu na musamaha wa zambi;

Salamu, kwani unaotesha kwa ajili yetu shamba nzuri;

Salamu, kwani unatengenezea roho zetu bandari ya amani:

Salamu, uvumba wa harufu nzuri;

Salamu, ufidio wa ulimwengu wote;

Salamu, urazi wa Mungu kwa ajili ya wenye kufa;

Salamu, mwombezi wa wanadamu kwa Mungu.

Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

**I K O S 6**

Roho ilipopata mashaka. Yosefu mtu wa haki akasikitika, kwani alijua ubikira wako, akizani wewe umejua mume kwa siri, ewe Mama usiye na doa, lakini mara alipata habari ya kuwa umepata mimba kwa tendo la Roho Mtakatifu akasema:

Alliluia

## FUNGU 2

**I K O S 7**

Wachungaji waliposikia Malaika wakiimba umwilisho wa Kristu, wakamwendea Mchungaji wao ili wamutazame Mwana-Kondoo, mzaliwa mpya aliyelishwa tumboni mwa Maria, wakaimba wakasema:

Salamu, Mama wa Mwana-Kondoo na Mchungaji Mwema;
Salamu, zizi la Kondoo kwa akili;
Salamu, ulinzi juu ya maadui wasiyoonekana;
Salamu, funguo ya milango ya Paradizo.
Salamu, kwani mbingu inafurahi pamoja na dunia;
Salamu, maana wanadamu wanashangilia pamoja na Malaika;
Salamu, kinywa cha Mitume kisichonyamaza;
Salamu, uhodari wa Mashahidi washindaji usioshindwa.
Salamu, tegemeo sabiti ya imani.
Salamu, alama ya neema ya Mungu;
Salamu, kwani kwa ajili yako Gehena imenyanganywa mateka yake;
Salamu, kwa ajili yako tumevaa utukufu.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

**I K O S 8**

Majusi walipoiona ile nyota ya njia-Kimungu, wakafuata mwangaza wake, wakaikamata kama taa kwa kumutafuta nayo mfalme Mwenyezi. Walipomufikia Msiyekaribika wakafurahi na wakasema:

Alliluia.

**I K O S 9**

Majusi wa Kaldea walipomuona Muumba wao mikononi mwa Bikira, wakamwabudu Bwana wao mu hali yake ya utumwa na wakamtolea zawadi zao, wakamsema na furaha mbarikiwa kamili:

Salamu, Mama wa Nuru ya milele.
Salamu, pambazuko ya siku iliyo Siri;
Salamu, uliyezimisha moto ya Gehena;
Salamu, taa yenye kutuonyesha Utatu.
Salamu, kwani ulimufuka mzalimu ku utawala wake;
Salamu, uliyemuonyesha Kristu Bwana mpenda-wanadamu;
Salamu, kwani ulituopoa ku ibada za upagani;
Salamu, kwani ulituondoa ku matendo yetu mabaya.
Salamu, uliyeizuia ibada ya moto;
Salamu, kwani ulizima moto ya tamaa;
Salamu, kwani unatuongoza ku hekima ya Mungu;
Salamu, ewe Shangilio ya vizazi vyote.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

**I K O S 10**

Walipokuwa wanadi wabebaji-Mungu. Majusi wakarudi ku Babyloni wakitimiza unabii wako na kukuhubiri mbele ya wote kama Kristu, wakamwacha Herodi sawasawa mpumbafu asiyejua kuimba:

Alliluia.

**I K O S 11**

Ku Misri, ee Bwana, alipoangazwa na ukweli wako, ukafukuza giza ya uongo; maana sanamu zao zilishindwa na nuru yako, tena watu waliookolewa wakamwimbia Bikira:

Salamu, ewe matumaini ya wanadamu na ukombozi wao;
Salamu, ewe mregeo na anguko la mashetani;
Salamu, ewe uliyekanyanga hila ya nyoka.
Salamu, ewe uliyeangusha uongo ya sanamu.
Salamu, ewe bahari uliyemzamisha Farao;
Salamu, Mwamba unayowapa kinywaji wale wenye kiu ya uzima;
Salamu, Mwongozi na nguzo ya moto yenye kuwaongoza walio gizani;
Salamu, ewe boma la ulimwengu, pana zaidi kuliko mbingu.

Salamu, kikombe munamolindwa manna mkate wa mbinguni;
Salamu, mtumishi unayetayarisha furaha takatifu;
Salamu, Paradizo ya siri ya inchi ya ahadi;
Salamu, inchi yenye kubarikiwa vinayotaa asili na maziwa.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

**I K O S 12**

Simeoni alipokuwa karibu kuondoka katika dunia hii ya udanganyifu, ukapewa kwake kama kitoto; Lakini akatambua katika wewe kuwa Mungu kamili, na alipostaajabia hekima yako, akapaza sauti na kusema:

Alliluia.

# FUNGU 3

**I K O S 13**

Mungu alifanya mpya kazi yake wakati alizaliwa mbele ya sisi viumbe vyake, akajifuma: Bila mbegu akachipuka tumboni takatifu, akailinda bila kuiharibu, ili sisi tukiona mwujiza huo, tuisifu tukisema kwa sauti kuu:

Salamu, ua lisiloharibika milele;
Salamu, taji ya utakatifu;
Salamu, nuru ya mfano wa ufufuo;
Salamu, peke yako mshindani wa Malaika na wa hali yao.
Salamu, mumea wa matunda bora, wenye kulisha waaminifu;
Salamu, mti wa kivuli na wa ubaridi, wa majani ya ulinzi;
Salamu, kwani ulizaa Mwongozi wa wenye kupotea;
Salamu, kwani kwa wafungwa unawapa Mwokozi.
Salamu, ewe Mwombezi wetu kwa Mwamzi wa haki na mwema;
Salamu, ewe mupatanishi wa wakosefu wengi;
Salamu, mavazi ya Wauchi;
Salamu, ewe moyo wa kushinda kila tamaa.
Salamu, Bibi-Arusi usiyeolewa.

**I K O S 14**

Tukiona kuzaliwa kwa namna kigeni, tujifanye wageni katika dunia hii, na kuweka mioyo yetu na akili zetu mbinguni, Ni kwa ajili yetu Mungu aliye-Juu akajionyesha duniani kama mtu munyenyekevu kamili, kwani alitaka kuvuta juu wale wote wanaomwimbia:

Alliluia.

**I K O S 15**

Aliyeko mbinguni, bila mageuzo ya fasi, wote hapa chini. Neno msiyeteseka, kwa sababu ya upendeleo wa Mungu, anakua Mwana wa Bikira tunayeshangilia hivi:

Salamu, ewe kiti cha Mungu kisichoweza kukaliwa;
Salamu, ewe mlango wa siri;
Salamu, ewe habari isiyosikika kwa waaminifu;
Salamu, tukufu bila shaka wa waaminifu.
Salamu, gari ya huyu anayekaa juu ya Wakheruvi.
Salamu, makao ya Mungu anayeketi juu ya Waserafi;
Salamu, kwani unavifanya vitu vyote kuwa vya mafaa;
Salamu maana katika wewe bikira amezaa.
Salamu, ewe mwenye kutuopoa ku mauti na kaburini;
Salamu, katika wewe Paradizo imefunguliwa tena;
Salamu, ewe funguo ya ufalme wa Kristu na ya mlango wa mbinguni;
Salamu, rala ya matumaini ya mema ya milele.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

**I K O S 16**

Rabi. Malaika wote mbinguni walistaajabu kwa umwilisho wako, maana walimwona Mungu msiyekaribika karibu ya wanadamu, akizungumuza na watu na kupokea shangwe yao:

Alliluia.

**I K O S 17**

Wasemaji wa maneno mengi wamenyamaza bila sauti kama samaki sababu yako, ewe Mzazi-Mungu, hawajui kueleza namna ulipata mimba katika ubikira, lakini tunastaajabu fumbo yako na tunapaza sauti:

Salamu, ewe chombo cha hekima ya ajabu ya Mungu;
Salamu, ewe sanduku ya maongozi ya mbinguni;
Salamu, mbele yako wenye akili hawana maarifa hata moja;
Salamu, kwani wenye hekima hawana uwezo.
Salamu, kwani wanenaji wakubwa wamekuwa wapumbafu;
Salamu, kwani watungaji wa hadizi wanayumbayumba.
Salamu, kwani ulifumua matanzi ya Waathina;
Salamu, uliyejaza wavu wa Wavuvi wa watu.
Salamu, unayetukokota inje ya zimu ya ujinga.
Salamu, unayetupatia nuru ya hekima ya kweli;
Salamu, mashua yenye kutuokoa baharini kali;
Salamu, bandari ya amani ya wasafiri baharini wa hii uzima.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

**I K O S 18**

Alipotaka kuokoa dunia Muumba wa ulimwengu alikuja kwa kutaka kwake; Mchungaji wetu alijifanya mtu kati yetu na kwa ajili ya wokovu wetu akaonekana kwetu kama Mwana-Kondoo wa Mungu; anaita kiumbe chake ku mfano wake na anatusikiliza tunajibu ku mwito wake:

Alliluia.

# FUNGU 4

**I K O S 19**

Bikira Mzazi-Mungu, boma ya mabikira, ulinzi wa wote wenye kukimbilia Kwako Mungu Muumba amekutengeneza sababu ya kukaa tumboni Mwako, na tunaimba kwa ajili yako:

Salamu, nguzo ya moyo safi na ya ubikira;
Salamu, mlango ya wokovu na ya ukombozi.
Salamu, mwanzo ya uumba wetu upya;
Salamu, mtume wa wema kimungu.
Salamu, unayewapa wenye zambi kuzaliwa kupya;
Salamu, mletaji nuru ku akili zetu;
Salamu, ewe uliyekanyanga nyoka muharibifu;
Salamu, ewe uliyezaa Mwana-Kondoo mpandaji wa usafi.
Salamu, Chumba-arusi bila mwungano;
Salamu, unayewaunganisha waaminifu na Mwana;
Salamu, mtunzaji mwema wa mabikira na wa vijana;
Salamu, mpambaji wa mioyo ku arusi ya Mwana-Kondoo.
Salamu, Bibi-Arusi Usiyeolewa.

**I K O S 20**

Bwana, wimbo wote ni zaifu wakati inajikaza kujisawanisha na wingi wa rehema zako; tutaweza kukuletea nyimbo nyingi kama mchanga wa bahari bila kuufikia ukamilisho wenye kustahili zawadi uliotufanyia pakuturuhusu kukuimbia:

Alliluia

**I K O S 21**

Kama taa yenye kwangaa katika giza. Bikira Mtakatifu anawakisha nuru ya kiroho sababu ya kutuongoza wote ku maarifa ya mbinguni; tutukuze mwangaza wake wenye kustahili zaidi nyimbo zetu:

Salamu, mwangaza wa Jua la wakristu;
Salamu, mwana wa Nuru ya milele;
Salamu, umeme wenye kuangaza mioyo yetu;
Salamu, mungurumo wenye kumuogopesha Adui.
Salamu, Mtume-mbebaji taa takatifu;
Salamu, pwani kunakoingia mto wa maji mengi;
Salamu, mfano takatifu na wa hai wa kisima cha maji ya ubatizo;
Salamu, kwani unaondoa alama ya zambi mioyoni mwetu.
Salamu, Bikira munamosafishwa zamiri yenyewe;
Salamu, kikombe chenye kutapanya furaha na uzima; ;
Salamu, manukato ya harufu nzuri ya kiroho; ;
Salamu, nuru ya hai ya Karamu ya mbinguni.
Salamu. Bibi-Arusi Usiyeolewa.

**I K O S 22**

Alipotaka kuwasamehe wenye deni wake wa zamani, huyu mwenye kuhurumia deni za wanadamu alikuja kwa kutaka kwake kuwaletea neema wale waliojitenga mbali; alipopasua hati ya deni zetu, akasikia watu wote wakimuimbia:

Alliluia.

**I K O S 23**

Tunaposifu uzazi wako, tunakutukuza ewe Mtakatifu Mzazi-Mungu, hekalu la hai alimokaa Bwana wa milele, na alipokutakasa na kukutukuza, akatufundisha wote tuimbe:

Salamu, hema takatifu ya Mungu-Neno;
Salamu, pahali takatifu kuu zaidi kuliko Patakatifu;
Salamu, sanduku iliopambwa kwa zahabu na Roho Mtakatifu;
Salamu, hazina ya uzima isiyomalizika.
Salamu, ewe taji heshimiwa ya Wafalme Wakristu;
Salamu, sifa ya kiroho ya Mapadri Watakatifu;
Salamu, ewe njia pana ya Eklezia isiyotikisika;
Salamu, ewe boma la Wakristu lisiloweza kuharibika.
Salamu, utukufu wa ushindi wetu;
Salamu, kwani katika wewe adui ameshindwa;
Salamu, ewe maponyesho ya mwili wangu;
Salamu, ewe wokovu wa roho yangu.
Salamu. Bibi-Arusi usiyeolewa.

**I K O S 24**

Ee Mama mstahili kamili wa nyimbo zetu, uliyezaa Neno Takatifu kuwapita watakatifu wote, pokea sasa heshima tunayokutolea, utuopoe ku mateso yo yote na linda ku azabu ijayo hawa wanaokuimbia na moyo mmoja:

Alliluia.

*Na tena tunasoma Kontakion ya Akathiste.*

*Elezo: Hii Ma Fungu ya Mzazi-Mungu tunasoma Wakati ya kwarezima. Kisha Juma ya kufunga chakula (Tirofagi) kanisa yetu Orthodokse inashangilia na hii wimbo inayeitwa Akathiste ya Mzazi-Mungu Maria. Kila Kazi Tano mangaribi tunafanya hii sala pamoja na Apodipnon Kidogo. Kisha Simvolo ya Imani tunaanza kuimba ya kwanza Kanuni ya Mzazi-Mungu na kisha kila Juma (mu Kazi tano) padri anasoma na moja Fungu.*

# K A T A V A S I E S

## KATAVASIA YA PASKA.

Wimbo ya kwanza.
Ufufuo ni leo, ataifa tuangazwe, Paska ya Bwana, Paska. Kwani toka mauti kwa uzima, na toka inchi kwa mbingu. Kristu Mungu ulitupitisha, sisi tuliyoimba wimbo wa ushindi.

Wimbo ya Tatu.
Kujeni tunywe kinywaji kipya, kienye kufanyika kwa ajabu si toka mwamba isiyopandwa, lakini toka kaburi, pahali Kristu alitosha chemchem ya uzima usiyoharibika, na juu yake tunasimamishwa.

Wimbo ya Ine.
Katika zamu kimungu, Habakuki aliyesema neno ya kimungu, asimame pamoja nasi na aoneshe malaika muletaji wa nuru na mwenyekupaza sauti kubwa: Leo wokovu umekuja duniani, ya kama Kristu alifufuka, kwa kuwa Yeye ni Mwenyezi.

Wimbo ya Tano.
Asubui mapema tukutafute Rabi, na tukutolee sifa pahali ya manukato, na tutaona Kristu, jua la haki, linayoleta uzima kwa wote.

Wimbo ya Sita.
Ulishuka katika vilindi ya inchi, na ulivunja mapingo ya milele iliyochunga wafungwa, ee Kristu, na katika siku tatu, kama Yona alikuza toka samaki, wewe ulifufuka toka kaburi.

Wimbo ya saba.
Huyu aliyeponyesha watoto toka tanuru ya moto, akijifanya mutu, anateswa kama mwenye kuweza kufa, na kwa mateso anavika mwili ya kufa kwa uzuri na uzima usiyoharibika. Huyu ni peke yako Mungu wamababu mubarikiwa na mutukuzwa kamili.

Wimbo ya Mnane.
Tunamusifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.
Hii siku inaitwa takatifu, siku ya kwanza ya juma, siku ya ufalme na ya utawala, karamu ya makaramu, na siku Kuu ya Siku Kuu, na katika hii siku tunabarikia Kristu milele.

Wimbi ya Tisa.
Mustari: Malaika aliita Maria aliyepewa neema: Bikira safi, alamu na tena nitasema salamu, wana wako alifufuka katika siku tatu toka kaburi.

Ungae, ungae, Yerusalema pupya, kwa sababu utukufu wa Bwana umepambazuka juu yako. Cheza sasa na shangilia, ee Sayuni. Na wewe, ee Muzazi-Mungu Safi, furahi, katika ufufuo wa Mwana wako.

# KATAVASIA YA KUZALIWA KWA KRISTU.

Wimbo ya Kwanza.
Kristu anazaliwa, mumutukuze, Kristu toka mbinguni, mumupokelee, Kristu duniani, mupandwe. Mwimbie Bwana, ninyi inchi, na kw3a furaha mumusifu, mataifa, kwani Yeye ameshinda kwa utukufu.

Wimbo ya Tatu.
Mwana alizaliwa bila geuzo toka Baba tangu milele, na alitwaa mwili bila mbegu toka Bikira wakati wa mwisho. Tumupazie Yeye Kristu Mungu sauti: Ewe uliyetukuza pembe yetu. Mutakatifu wiko, Bwana.

Wimbo ya Ine.
Kitawi toka shina la Yeye, na ua toka Kitawi, ee Kristu, ulimea kwa Bikira, wewe unayestahili kuimbiwa, toka mulima wa kivuli na muhuru, ulikuja kwa mwili toka kwa musiyeolewa. Mungu wasipo kiwiliwili. Utukufu kwa uwezo wako, ee Bwana.

Wimbo ya Tano.
Ukikuwa Mungu wa amani, Baba wa rehema, ulituma kwetu Malaika wa shauri kubwa, mwenye-kuleta amani. Kwa hivi, sisi tuliiyongozwa kwa nuru ya ufahamu wa Mungu, tunakutafuta asubui mapema, na tunakutukuza, ee Mupenda-Wanadamu.

Wimbo ya Sita.
Toka utumbo Yona, alitapikwa kama tungama kwa samaki kubwa wa bahari, aliyemupokea. Na Neno, wakati alikaa kwa Bikira na alitwaa mwili, alipita kwa kumuchunga bila uharibifu, Kwani Kristu toka yeye hakupata ugeuzo, na alichunga muzazi wake bila doa.

Wimbo ya Saba.
Watoto, waliokomea kwa heshima, walizarau amri isiyo na heshima, hawakuongope wakamio ya moto, lakini katikati ya ulimiya moto, walisimama na kuimba: Mungu wa mababu, ni mubarikiwa.

Wimbo ya Mnane.
Tunamusifu, tunamuhimidi, na tunamusujudu Bwana.
Tanuru ya moto iliyotosha umande ilionesha mbele mufano wa ajabu isiyofikili. Kwani haikuteketeze vijana walipoingia ndani yake, kama moto ya umungu haikuteketeze tumbo la Bikira, alipoingia ndani yake. Kwa hii tuimbe na tusifu: Viumbe vyote vibarikie Bwana, na vimutukuze katika milele yote.

Wimbo ya Tisa.
Tukuza, ee nafsi yangu, aliye wa damani na utukufu kushinda majeshi ya juu.
Minaona siri isiyofahamiwa na ya ajabu, Pango ilifanyika mbingu. Bikira alifanyika kiti cha ufalme ya heruvim. Sanduku ya kulisha nyama ilifanyika pahali penye alilala Kristu Mungu asiyeweza kufungwa, tunayesifu na tunayetukuza.

# KATAVASIA YA MZAZI-MUNGU.

1) Tokea Septemba 22 mpaka Novemba 20.
2)Tokea Februari 10 mpaka mwanzo wa Triodi.
3) Juma-Bwana ya Kwarezima ya 2, 4, na ya 5.

4)Tarehe 25 ya Mwezi wa Mei
5) Juma-Bwana ya Watakatifu wote mpaka Tarehe 26 Julai.
6)Tarehe 14 Augusto.

Wimbo ya kwanza.
Nitafungua kinywa changu, na kitajazwa Roho, nikatoa maneno kwa Malkia Mama, nikaonyesha, kushangilia na furaha, nikayaimbia miujiza yake na furaha.

Wimbo ya tatu.
Ee Mzazi-Mungu, uliye chemchem ya uhai na kujaa tele, usifu wao waliochanganya kwa mchango wa Roho, uwape mkazo; tena kuwastahilisha kuona taji tukufu kwa utukufu wako wa kimungu.

Wimbo ya ine.
Mapenzi yako ya kimungu, yalio si kuchungwa, ili kupata mwili na Bikira, ewe uliye juu pia, akimwangazia yule nabii Abakuki, alipaza sauti na kusema: utukufu kwa uwezo wako, ee Bwana.

Wimbo ya tano.
Ulimwengu ulistaajabu na utukufu wako wa kimungu; kwa kuwa wewe, ee Bikira usiyolewa, ulimshika mimba yeye, aliye Mungu wa wote, tena ulimzaa aliye Mwana bila mwanzo, ili kuwapa wasifu wako wote, kipaji cha wokovu.

Wimbo ya sita.
Sisi tunaofikiri kimungu, ikiwa tunaazimisha siku Kuu hii ya Mama-Mungu, iliyo kimungu na ya samani kamili, njoni tuyapigie mikono tukimtukuza Mungu aliyezaliwa naye.

Wimbo ya saba.
Waliofikiri kimungu hawakuabudu umbo, ila Muumba, bali waliukanyanga, hodari ogofyo ya moto, wakishangilia waliimba: Ewe Mungu na Bwana wa mababu zetu, uliye msifiwa bila kiasi, uhimidiwe U.

Wimbo ya mnane.
Tunamsifu, tunamuhimidi, tunamusujudu Bwana.
Vijana wa tabia njema tanuruni, mzao wa Mzazi-Mungu aliwaokoa, mfananishwapo, tena sasa mtimilizwapo, anakusanya ulimwengu wote ukiimba: Enyi viumbe msifuni Bwana, na kumtukuza milele na milele.

Wimbo ya tisa.
Mwana wowote wa dunia furahi rohoni, akishikataa yake, yenyi kuwaka Malaika mbinguni. Watukuze wa furahi siku Kuu Takatifu ya Mzazi-Mungu na wamuimbie salamu, ee mwenye heri na Bikira daima Mtakatifu Mzazi-Mungu.

## KATAVASIA YA EPIFANIA YA JESU KRISTU.

*Kwa siku ya kwanza na ya Sita ya mwezi ya Kwanza tunaimba hii KATAVASIA, yote wa Pili. Kutoka siku ya pili mupaka siku ya tano ya hii mwezi tunaimba KATAVASIA, mwenye ya kwanza. Kutoka ya siku saba mupaka siku ya kumi na ine ya hii mwezi tunaimba KATAVASIA, mwenye ya Pili.*

Wimbo ya Kwanza. Sauti ya pili
Kilindi ya Bahari kilifunuliwa na Bwana, mwenye-uwezo katika vita, na anakokota watu wake juu ya inchi kavu, na anafunika kilindini adui. Kwa maana ameshinda kwa utukufu.

Israeli akaingia pa mawimbi ya bahari iliyoonekana kwake pa inchi kavu; lakini mawimbi ya giza kama kaburi ya majimaji, ikawafunika maakicha wote wa Msri kwa nguvu ya mkono wa Bwana.

Wimbo ya Tatu.
Bwana anamupa mufalme wetu nguvu, na anatukuza pombe ya wapakaliwa wake, anazaliwa toka Bikira, na anaenda kwa ubatizo. Kwa hii sisi waaminifu tupaze sauti: Hakuna mumoja mutakatifu kama Bwana, hakuna mwenye-haki ila wewe, Bwana.

Sisi wote tuliyo huru ku mitego ya zamani kwani meno ya nyama kali yamevunjwa, tufungue kinywa kwa ajili ya nyimbo za furaha, tukisuka myororo wa nyimbo, zetu kwa kumutukuza Neno mwenye kupanda kutujaza na vipaji vyake.

Wimbo ya Ine.
Yoanne aliyeitwa kwa wewe, ee Bwana, sauti ya mutu akilia jangwani, alisikia sauti yako, wakati ulipiza radi juu ya maji mengi, ukishuhudia Mwana yako. Wakati alijazwa na Roho aliyekuwapo, akilia: Wewe ni Kristu, Akili na Nguvu ya Mungu.

Alipotakaswa na moto ya wangalivu kimungu. Nabii akaimba upya wa mwenyi kufa wote, kwa Sauti yake Roho Mtakatifu aliyosikiilizisha akahubiri umwilisho usiyokadirika wa Neno aliyevunja nguvu ya wenye nguvu.

Wimbo ya Tano.
Yesu. Mukubwa wa uzima, alifika kwa kufungua hukumu ya ajabu, ya Adamu muumbwa wa kwanza. Kwani Yeye ni Mungu, hakuhitaji hata kusafishwa, lakini anasafisha mwenye-kuanguka katika Yordani. Ndani yake akiuua wa adui, litolea amani inayopita akili zote.

Tunapooshwa kwa utakaso wa roho ku sumu ya adui mwenye kujaa matope na mwenyi giza, tujongee bila udanganifu ku njia mpya yenye kuongoza ku furaha isiyokadirika ambako kunakaribia paka wale Mungu alipatanisha.

Wimbo ya Sita.
Sauti ya Neno, bakuli ya Nuru, nyota ya asubui, Mutangulizi la jua, analia katika jangwani kwa mataifa yote: Tubuni, na satisheni mbele. Kwani tazama! Kristu ni hapa, wa kukomboa duniani toka uharibifu.

Baba anatangaza na sauti yake ya heri " Mpenzi" huyu anayenena kifuani mwake: Huyu anavyosema, ndiye Mwana wangu wa asili moja, na nuru amezaliwa na kwa upendeleo ni wa mauti.

Wimbo ya Saba.
Vijana waheshimiwa, walipoingia katika tanuru ya moto, walibaki bila hasara kwa sababu ya upepo ya umande iliyopuliza, na ya kushuka kwa malaika wa Mungu. Kwa hii walipozwa katika moto, na walisifu kwa kupendeza: Ewe Musifiwa kamili. Bwana wa mababu na Mungu, ni mubarikiwa.

Katika moto akateketeza vichwa vya nyama, huyu aliyetuliza moto kuubwa wa tanuru mulimopatikana vijana; na uweusi wa zambi usiyofutwa anautakasa kwa umande wa Roho Mtakatifu.

Wimbo ya Mnane.
Tunamusifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.
Siri ya ajabu ilionekana katika tanuru ya moto ya Babyloni, iliyokuwa chemchem ya umande.
Kwani Yordane afazali kupokea moto bila kiwiliwili. Ndani ya maji yake, na kufunika muumba

aliyebarikiwa na kutukuzwa katika mwili, aliyebarikiwa na kutukuzwa kwa mataifa katika milele yote.

Kiumbe kinapata uhuru: Wenye giza wanakuwa waana wa nuru; mfalme wa giza peke yake analalamika; urisi wa mataifa unamutukuza sasa uumba wake mbali ya mateso.

Wimbo ya Tisa
Tukuza, ee nafsi yangu, aliye wa damani kushinda majeshi ya juu.
Kila luga haiwezi kukutukuza, ee Muzazi-Mungu, kama inavyostahili. Na tena kila akili ya ulimwengu na ya mbingu inapata kizunguzungu kwa kukusifu. Lakini uko mwema, na kwa hii pokea imani yetu. Hakika unajua hamu yetu kubwa katika Mungu, kwani wewe ni Mukinga wa wakristiani, na tunatukuza wewe.

Uzazi wako ni ajabu yenye kupita wazoo lote. Ewe Bibi asiye na doa; katika wewe. Mama mbarikiwa, tulipopata wokovu, tunakutolea wimbo wa shukrani wenye kukustahili na tunakushangilia kama Mwema.

## KATAVASIA YA KUTUKUZA MUSALABA MWESHIMIWA.

Wimbo ya kwanza. Sauti ya Mnane.
Musalaba ilichorwa na Musa, wakati aligawanya Bahari Nyekundu kwa ajili ya Israeli, akiipiga kwa bakora kiwimawima. Na wakati alipoipiga kwa upana, aliunganisha maji juu ya magari ya Farao. Hivi silaha isiyoshindwa ilichorwa juu ya bahariyenye kupanika. Kwa hii tuimbe kwa Kristu, Mungu wetu, kwa maana ameshinda kwa utukufu.

Wimbo ya Tatu.
Bakora ilibebwa ili ifananishe hii siri. Kwani kwa kuchipuka ilichagua kuhani. Na sasa katika Kanisa iliyokuwa zamani tasa, muti ya musalaba ilichipuka, kusudi Kanisa ipate nguvu na kusimamishwa.

Wimbo ya Ine.
Nilisikia, ee Bwana, siri ya shuruli yako, nilifahamu kazi zako, na nilitukuza umungu wako.

Wimbo ya Tano.
Ah! Heri muti za heri mingi! Juu ya hii Kristu, Mufalme na Bwana, alisulubiwa. Kwa njia ya hii yule aliyedanganya kwa muti, alianguka, wakati alikokotwa nawe. Mungu uliyepigiliwa kwa mwili, na kuleta amani kwa nafsi yetu.

Wimbo ya Sita.
Katika matumbo la samaki. Yona alinyanyua mikono yake kwa alama ya Musalaba, na kufananisha zamani wazi mateso ya Mwokozi. Tena, wakati alitoka toka samaki katika siku tatu, alionesha mufano ya ufufuo kamili wa Kristu Mungu, aliyesulubiwa kwa mwili na kuangaza duniani kwa ufufuo wake katika siku tatu.

Wimbo ya Saba.
Amri ya ujinga ya Muzulumu asiyeheshimiwa, ilitikiza mataifa, iliyopumuzika makamio na kukufuru, Mungu aliyochukia. Lakini wala hasira kali, wala moto iliyonguruma haikuogopesha watoto tatu. Lakini wakati upepo ulipuliza uliyotosha umande, hawa waliimba katika moto: Mungu musifiwa kamili wa mababu na wetu, uko mubarikiwa.
Wimbo ya Mnane.
Tunasifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.

Watoto tatu, sawa Utatu Mutakatifu, mubarikie Muumba, Baba Mungu, Musifu Neno aliyeshuka na kugeuza moto kwa umande. Na mutukuze Roho Mtakatifu kamili, iliyoleta uzima kwa wote, milele.

Wimbo ya Tisa.
Paradizo ya siri ni wewe, Muzazi-Mungu. Bila mbegu uliotesha Kristu, na Yeye alipanda duniani muti ya Musalaba iletayo-uzima. Sasa hii inatukuzwa, na sisi, tukimusifu Kristu, tunakutukuza.

Lufu iliyokuja kwa kizazi chetu kwa sababu ya kula tunda, leo iliharibiwa kwa Musalaba. Kwani mafingo ya Mama Eva iliyofunga kizazi kiote ilifungula kwa tunda ya Muzazi-Mungu safi, na wakuu wa mbinguni wanamutukuza.

## KATAVASIA YA KULALA MUZAZI-MUNGU.

Wimbo ya kwanza. Sauti ya Kwanza.
Mapambo ya utukufu kimungu ni makubusho yako, takatifu na ya utukufu, ee Bikira, iliyokusanya waaminifu wote kwa kufurahiwa. Miriamu ni mukubwa wa matoazi na muchezo na wakiimbia Mwana wako wa pekee, kwa kuwa ameshinda kwa utukufu.

Wimbo ya Tatu.
Ee Kristu, Akili na Nguvu ya Mungu, uliyeumba na kuchunga ulimwengu, simamisha Kanisa yako isitikizike na isifazaike. Kwani wewe peke yako ni Mutakatifu, uliyekaa juu ya watakatifu.

Wimbo ya Ine.
Maneno na mifano ya manabii zilionyesha kutwaa mwili yako toka Bikira, ee Kristu nuru ya umeme yako iliyokuja kuangaza dunia. Na kilindi kilikupazia sauti kwa shangwe: Utukufu kwa uwezo wako, ee Mupenda-Wanadamu.

Wimbo ya Tano.
Nitajulisha uzuri ya wema wako kimungu na isiyosemwa, ee Kristu. Kwani toka utukufu ya milele ya Baba uliangaa kama mwangaza kwa uso wa milele, na ulitwaa mwili toka tumbo la Bikira, na ulipanda kama jua uliangazia waliokaa katika giza ya kivuli.

Wimbo ya Sita.
Moto ya Bahari iliyozaliwa katika tumbo la samaki, ilikuwa mufano mbele ya ajabu ya maziko yako katika siku tatu, na Yona aliifananisha na mwenyewe. Kwani aliokolewa na alibaki bila taka, sawa mbele ya lumezwa, na alilia: Mitatoa zabihu kwako, ee Bwana, kwa sauti ya kushukuru.

Wimbo ya Saba.
Mapendo kimungu ya watoto tatu ilishindana na gazabu mingi na moto. Hii ilipoza moto, na ilichekelea gazabu, na ilibisha kwa matari ya pumuzi kimungu na hekima, kwa nzenze tatu ya watoto watakatifu, juu ya viombo vya muziki katika moto, kwa kusema: Mungu mutukuzwa wa Mababu na wetu, uko mubarikiwa.

Wimbo ya Mnane.
Tunasifu, tunabarikia na tunasujudu Bwana.
Malaika mwenyezi aliyeshuka pamoja na watoto tatu, aligeuza moto kwa umande juu ya watoto watakatifu, na alilungusha wasioheshimia Mungu. Sawasawa Malaika alifanya Muzazi-Mungu kuwa chemchem ya uzima, inayotosha uharibifu ya mauti na uzima kwao wanaoimba: Sisi tuliokombolewa, tunasifu Muumba mumoja, na tunamutukuza katika milele yote.
Wimbo ya Tisa.

Vizazi vyote tunakuita heri, ee Mzazi-Mungu. Sheria ya hali ya watu ilishindwa katika wewe, ee Bikira bila doa. Kwani kuzala kwako ilikuwa ya ubikira, na lufu yako inajulisha mbele uzima. Ewe Muzazi-Mungu. Bikira kisha kuzaa, na muzima kisha lufu, ikikupendeza uokoe daima uriti yako.

# KATAVASIA YA KUPOKELEA KWA KRISTU.

Wimbo ya kwanza. Sauti ya Tatu.
Uwanja bila kulimwa iliyozaa kilinfi wakati moja ilionekana mbele ya jua. Kwani maji ilisimamishwa kama ukuta kwa ngambo mbili, kwa ajili ya taifa akitembea katika bahari, na kuimba kwa mapenzi ya Mungu: Tutaimbia Bwana, kwa maana ameshinda kwa utukufu.

Wimbo ya Tatu.
Usimamisho ya wenye-kukuamini, ni wewe, Bwana, na usimamisha Kanisa yako, uliyopata kwa damu yako yeshimiwa.

Wimbo ya Ine.
Wema wako, ee Kristu, ulifunika mbingu. Kwani ulikuja toka sanduku takatifu, maana lake toka Mama asiye na uharibifu, na ulioonekana katika Hekalu ya utukufu yako kama mutoto akiletwa kifuani, na dunia yote inajaa na sifa yako.

Wimbo ya Tano.
Wakati Isaya alipoona kwa mufano Mungu juu ya kiti cha ufalme kenye kunyanyuliwa juu, na kufuatana na malaika la utukufu, akalia: Ole wangu! Kwani niliona mbele, Mungu kwa mwili, mwenye-kutawala katika nuru isiyomwisho na amani.

Wimbo ya Sita.
Wakati muzee alipokuona kwa macho yake, wewe wokovu, uliyeonekana kwa mataifa, alikulilia:
Ee Kristu, uko Mungu wangu toka Mungu.

Wimbo ya Saba.
Wewe. Mungu Neno, ulipoza katika moto watoto waliokushuhudia, na ulikaa katika Bikira bila doa. Tunakusifu na kukuimbia kwa heshima: Mubarikiwa ni Mungu wa Mababu zetu.

Wimbo ya Mnane.
Tunasifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.
Vijana waliokuwa kwanza na heshima, wakiungana kwa moto isiyofungwa, hawakuuteketezwa kwa moto, lakini waliimba wimbo kimungu: Kazi zote mubarikie Bwana, na mumutukuze, katika milele yote.

Wimbo ya Tisa.
Muzazi-Mungu, tumaini wa wote wakristiani, funika, chunga, linda wanaokutumainia wewe.

Katika sheria, kivuli na maandiko, sisi waaminifu tuone mufano: Kila mume aliyefungwa tumbo ataitwa mutakatifu kwa Bwana. Kwa hii Neno Muzaliwa wa kwanza. Mwana wa Baba bila Mwanzo, alizaliwa wa kwanza toka Mama asiyejua Bwana, na tunamutukuza yeye.

# KATAVASIA YA KUPANDA YESU KRISTU MBINGUNI NA YA PENTEKOSTE.

Wimbo ya Kwanza. Sauti ya Saba.
Akamzika Farao na magari yake katika bahari Nyekundu huyu mwenye kuvunja vita kwa nguvu ya mkono wake: Tumwimbie, kwani amevaa Utukufu.

Sauti ya Ine.
Wingu wa kimungu ulifunika Musa mwenye-ulimi muzito, na Yeye alihubiri sheria iliyoandikwa na Mungu. Kwani akiondosha uchafu toka macho ya roho aliona Mungu Aliye, na aliingiza katika mafikili ya Roho, akimwimbia kwa wimbo kimungu.

Wimbo ya Tatu. Sauti ya saba.
Uliwaambia Mitume: Musitoke Yerusalema lakini mungoje mpaka siku mutakayoviiikwa nguvu ya Juu mbinguni, nami nitawatumia Mfariji mwengine, Roho ya Baba na yangu, naye atawasabitisha ninyi.

Sauti ya ine.
Minyororo la tumbo ya tasa ilikatika, na tena laumu isiyovumiliwa ya Muzazi, paka kwa maombi ya Hana nabii wakate, mwenye-kuwa moyo uliovunjika mbele ya Mufalme wa uwezo, na Mungu wa kujua yote.

Wimbo ya Ine. Sauti ya saba.
Alipofikiri pa majilio yako ya mwisho, ee Kristu. Nabii akapaza sauti: Niliona uwezo wako.
Bwana, maana ulikuja kuokoa wale waliotolewa Kwako.

Sauti ya ine.
Mufalme wa wafalme. Mwana wa pekee na Neno, uliyezaliwa na Baba peke yake asiye mwanzo, ulituma Roho kweli sawa na wewe kwa mitume, kwa sababu wewe ni mwema, na wao waliimba: Utukufu kwa uwezo wako, ee Bwana.

Wimbo ya Tano. Sauti ya saba.
Bwana, Roho ya wokovu yako zamani Manabii walipokea na woga anafanya moyo safi ndani ya Mitume na anabadilisha katika mioyo yetu akili ya haki, kwani amri zake, ee Bwana, zinatuletea nuru na amani.
Sauti ya ine.
Mupokee usafisho unaozimisha zambi, mupokee upepo wa Roho ya umande na ya moto, enyi watoto wa Kanisa kwa uso ya nuru. Kwa maana sasa katika sayuni sheria ilitoka, neema ya Roho ilionekana ndini kama za moto.

Wimbo ya Sita. Sauti ya saba.
Ninaposafiri baharini mwenye kunyanyuliwa kwa Shurali za dunia, ninapoangamizwa katikati ya zambi zangu, na kutupwa kwa nyama mwenyi kurarua roho, kama Yona, ee Kristu, nakulalamikia: uniopoe kuzimuni kwa mauti.

Sauti ya ine.
Kristu Rabi, uko usamehe na wokovu, ukianga toka Bikira, ili utoshe toka uharibifu Adamu mwenye kuanguka na wote, kama ulitosha toka matumbo ya samaki nabii Yona.
Wimbo ya Saba. Sauti ya saba.

Katika tanuru ya moto Vijana wakageuza moto uliyowazunguuuka kuwa umande kwani walimuuuutukuza Bwana wakiimba: Ee Mungu wa Baba zetu, umetuuukuzwa.

Sauti ya ine.
Upatanisho wa viombo vya musiki ilinguruma, kusudi mataifa waabudu sanamu isiyo na nafsi iliyofanywa kwa zahabu. Lakini neema ya Mufariji ilitayonuru iliwapatia moyo ya ukimya kwa waaminifu wapaze sauti: Utatu wa usawa pasipo mwanzo, uko peke yako mubarikiwa.

Wimbo ya Mnane. Sauti ya saba.
Tunasifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.
Kichaka cha Sinai chenye kuwaka moto bila kuteketezwa kiliiifunua Mungu kwa Musa, kilipoeleeekea kwa huyu wasipo usemi wepesi; na katika moto Vijana watatu washujaa katika bidii yao kwa Mungu wakaimba wimbo wa Sifa: Mwimbieni Bwana, enyi wote viumbe vyake, mtukuzeni milele.

Sauti ya ine.
Mufano wa nuru tatu ya Umungu unafungula minyororo na unapoza moto. Watoto wanaimba na viumbe vyote vilivyoumbwa na Mungu, Mwokozi na Muumba peke yake, vinamubarikia, kwaq kuwa Yeye ni Mwema.

Wimbo ya Tisa. Sauti ya saba.
Wewe uliyepata mimba katika usafi wote na kwako Neno muumba wa ulimwengu akajifanya mtu, ewe Mama usiyeolewa. Mzazi Bikira wa Mungu, Makao ya huyu mtu hata mmoja hawezi, kusonga, nyumba ya Wamilele, Muumba wako, tunakutukuza.

Sauti ya ine.
Salamu, Malkia, utukufu kwa wazazi na wabikira. Katika kila kinywa kisemaji wepesi, wakati kinasema, hakitaweza kukusifu kwa kustahili. Tena kila akili kinapata kizunguzungu bila kuweza kusikia kulala kwako. Kwa hii sisi wote tunakusifu kwa sauti moja.

## KATAVASIA JUMA YA MTOZA KODI NA MFARISAYO. JUMA YA JIVINI NA MPOSHO MBELE YA PENTECOSTI.

Wimbo ya kwanza. Sauti ya sita.
Wakati Waisraeli waliposafiri kilindini kama pa inchi kavu, na walipoomuona Farao mzalimu ameangamizwa katika mawimbi, hapo wakapaza sauti: Tuimbeni wimbo wa ushindi kwa utukufu wa Mungu wetu.

Wimbo ya tatu.
Hakuna hata mmoja aliye Mtakatifu kama Wewe Bwana Mungu wangu; ulitukuza nguuuuvu ya Waaminifu katika wema wako, na ulitutia msingi pa mwamba imara wa maungamo ya jina Lako.

Wimbo ya ine.
Kristu ni nguvu yangu, Bwana wangu na Mungu wangu: huu ni wimbo kimungu Eklezia Takatifu inatangaza, na moyo wenye kutakasa inamuheshimu Bwana.

Wimbo ya tano.
Ewe Mungu mwema mno, nakuomba, angaza na nuru yako ya umungu roho za wapendwa wako wenye kukesha mbele yako ili wakujue, ewe Neno la Mungu, Wewe Mungu wa kweli mwenye kututosha ku giza ya zambi.

Wimbo ya sita.
Wakati ninapoona bahari ya hii uzima inanyanyuliwa kwa tufani ya vishawishi, nakimbilia ku bandari yako ya amani na napaza sauti, ee Mungu wa Wema: Komboa uzima wangu ku shimo.

Wimbo ya saba.
Katika tanuru ya moto Malaika akawamwangia Vijana washarifu umande, lakini moto ukawateketeza wakaldea kwa amri ya Mungu, na mzalima akalazimishwa kuimba: Umetukuzwa. Bwana Mungu wa Baba zetu.

Wimbo ya mnane.
Tunamsifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.
Toka moto ukachirikiza umande kwa ajili ya Watakatifu Wako na kwa maji ukawakisha sadaka ya mwenyi haki, kwani ulitimiza vitu vyote paka kwa mapenzi yako: Ee Kristu, tunakutukuza milele.

Wimbo ya tisa.
Kwa wanadamu haiwezekane kumuona Mungu ambaye hata Malaika hawasubutu kutazama, lakini Neno aliyejifanya mtu kwako alionekana kwa wenye kufa, ewe Safi kamili, na wakati tunamutukuza pamoja na majeshi ya mbinguni tunakutangaza mwenye heri.

## KATAVASIA JUMA YA MWANA MPOTEVU.

Wimbo ya kwanza. Sauti ya pili.
Imba, ee roho yangu, wimbo wa Musa: Bwana ni msaada wangu na mlinzi wangu, ni yeye aliyeniokoa, ndiye Mungu wangu, na nataka kumutukuza.

Wimbo ya tatu.
Ee Bwana, jangwa kavu ya roho yangu uifanye iwe yenyi kutoa na yenyi neema. Wewe mwenye kukesha ku ustawi wa mema yote katika wema wako wa umungu.

Wimbo ya ine.
Nabii alipoona Bikira amekuzaa akatangaza, akasema: Bwana, nilisikia sauti yako na nimejaa na woga, maana umetoka ku Themani, ee Kristu, ku mlima takatifu wa kivuli.

Wimbo ya tano.
Usiku umepita, na sasa hivi jua limeonekana litakaloangaza ulimwengu kwa nuru yake, ndiyo maana kundi la Malaika wote wanaimba wimbo wao kwa kutukuza, ee Kristu Mungu wetu.
Wimbo ya sita.
Mungu Mwokozi, nazama katika shimo ya zambi, nazama katika bahari ya hii uzima, lakini Yona alivyotoka tumboni mwa Samaki, uniiondoshe ku shimo ya tamaa na uniokoe, ee Bwana.

Wimbo ya saba.
Katika tanuru ya moto Vijana wakawaza wakeruvi wakati walipoimba: Utukuzwe, ee Mungu wetu, ulileta hukumu ya haki, ni kwa makosa yetu unatutendea hivi, utukufu na Sifa ya milele ni Kwako.

Wimbo ya mnane.
Tunamusifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.
Kwa huyu ambaye katika kichaka mlimani wa Sinai mbele ya Musa akatagulia kuonyeesha fumbo ya ajabu ya Bikira, imbeni wimbo wa utukufu: Utukufu kwake milele.

Wimbo ya tisa.
Nani mwenyi mauti alisikia hii? Na nani amekuisha kuona Bikira kupata mimba na kuzaa mutoto bila uchungu? Lakini hii ni fumbo yako ya ajabu, Mtakatifu Mzazi-Mungu, tunakutukuza.

## KATAVASIA JUMA YA APOKREO.

Wimbo ya kwanza. Sauti ya Sita.
Bwana ni msaada wangu, ulinzi wangu, ni yeye aliyeniokoa, ndiye Mungu wangu na nataka kumutukuza, Mungu wa Baba yangu, na nitamutukuza, kwani amevaa utukufu.

Wimbo ya tatu.
Bwana, sabitisha moyo wangu pa mwamba wa amri zako ili isiyumbeyumbe, kwani peke yako ndiwe Mtakatifu na Bwana.

Wimbo ya ine.
Bwana, Nabii aliposikia kuja kwako akashangaa, kwani ulitaka kuzaliwa kwa Bikira na kuonekana kati ya wanadamu, na akasema: Nimesikia sauti yako na nimejaa na woga; Bwana, utukufu ku uwezo Wako.

Wimbo ya tano.
Usiku ninakesha mbele yako, ee Bwana Mpenda-Wanadamu, nakuomba uniangaze uniongeze njiani mwa amri zako na unifundishe, Mungu-Mwokozi, kufanya mapenzi yako.

Wimbo ya sita.
Nimelalamika na moyo wangu wote kwa Mungu wa mapendo, anasikiliza mwito wangu toka chini ya Hadeze na ku shimo anakomboa uzima wangu.

Wimbo ya saba.
Tulitenda zambi, uovu na uzulumu mbele yako, hatukuchunga wala kushika amri zako, usitutupe mpaka mwisho, ee Bwana, Mungu wa Baba zetu.

Wimbo ya mnane.
Tunamsifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.
Huyu Malaika wote wanatukuza, mbele yake wakeruvi na Waserafi wanatetemeka, kila kiumbe na kila mwenye pumzi amuimbe, amutukuze na kumusifu milele.

Wimbo ya tisa.
Ulipata mimba, bila mbengu, uzazi wako ni usiyokadirika, ee Mama usiyeolewa: Mungu anajifanya mtu kwa Bikira na anabadirisha amri za ubinadamu; na kadiri ya imani ya kweli, ee Bikira Mzazi-Mungu, tunakutukuza kizazi hata kizazi.

## KATAVASIA JUMA YA UORTHODOKSI.

Wimbo ya kwanza. Sauti ya Ine.
Wakati walipovuka katikati ya bahari nyekundu kwa inchi kavu, waisraeli wa zamani wakakimbiza jangwani jeshi la Amaleki kwa nguvu ya mikono Musa aliyopanua mu alama ya msalaba.

Wimbo ya tatu.
Eklezia yako, ee Kristu, inafurahiwa katika Wewe na inakulalamikia: Bwana, ndiwe nguvu yangu, kimbilio langu na msaada wangu.

Wimbo ya ine.
Ilipokuona umetundikwa msalabani, Wewe Jua ya Haki, Eklezia tangu pa fasi yake ikalalamika kweli: Utukufu kwa uwezo wako, Bwana.

Wimbo ya tano.
Bwana, ulikuja kama nuru duniani, nuru takatifu yenye kuondoa ku ujinga wa giza hawa wenye kukuimba na imani.

Wimbo ya sita.
Eklezia yako inakulalamikia na sauti kubwa: " Nitakutolea Sadaka ya sifa. Bwana, katika rehema yako ulitakasa ku damu ya mashetani kwa damu yenye kutoka ku ubavu wako.

Wimbo ya saba.
Katika tanuru ya Persi waana wa Abrahamu, japo mwako wa moto uliyowaka kwa ibada yao, wakalalamika: Umetukuzwa, ee Bwana, katika hekalu la Utukufu.

Wimbo ya mnane.
Tunamusifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.
Daniele alipopanua mikono katika shimo akafunga kinywa cha Simba; Vijana, wenye kuja na bidiii ya imani yao, wenye kuvaa fazila, wakazima nguvu ya moto wakatipo walipolalamika: Tukuzeni Bwana, enyi wote viumbe vya Bwana.

Wimbo ya tisa.
Kristu, jiwe la pembe ambelo mkono hata mmoja haukuchonga lakini likachongwa nawe, ee Bikira, mlima haramu; ni aliyeunganisha hali zenye kutengana: Tena tunapojazwa na furaha, ee Mzazi-Mungu, tunakutukuza.

## KATAVASIA SIKU YA MUNGU YA TATU YA KWAREZIMA KWA KUBUSU MSALABA YA BWANA YESU KRISTU.

Wimbo ya kwanza. Sauti ya Kwanza.
Ee Kristu Mungu wetu, zamani Musa alitangulia kuonyesha mfano wa Msalaba wako wa zamani na Takatifu wakati alipofungwa bahari Nyekundu na fimbo yake na akapitisha Waisraeli wakiimba ushindi wa Bwana.
Wimbo ya tatu.
Ee Kristu Bwana, unisabitisha pa mwamba wa imani kwa nguvu ya Msalaba wako ili roho yangu isiyumbeyumbe ku mshale wa Adui, kwani peke yako ndiwe Mtakatifu na Bwana.

Wimbo ya ine.
Ee Mungu Mwenyezi, wakati Jua lilipokuona umeteswa Msalabani, likaogopa na likazuia nuru ya miangaza yake, lakini kiumbe yote ikaimba na woga uvumilivu wako na dunia ikajaa na Sifa yako. Bwana.

Wimbo ya tano.
Tutangulie alfajiri. Bwana wa ulimwengu, tunakuimba kwani Msalaba Wako ulitupatia amani; katika hii ulifanya ubinadamu kuwa upya ambao uliyoongoza ku nuru ya milele.

Wimbo ya sita.
Yona alipopanua mikono tomboni mwa samaki akatangulia kuonyesha mfano wa Msalaba wako Takatifu, na alipotoka tumboni mwa samaki akaokoka, ee Neno, kwa uwezo wako mkuu.

Wimbo ya saba.
Huyu aliyeokoa Vijana ku tanuru ya moto alichukua mwili na alishuka duniani; alipoitika kusulibiwa Msalabani, akatupatia wokovu; ndiye Mungu wa Baba zetu, baraka na Utukufu ni Kwake peke yake.

Wimbo ya mnane.
Tunamusufu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.
Alipotupwa katika shimo la Simba. Nabii Danieli akapanua mikono mu alama ya msalaba na hakuwa mateka ya meno yao.

Wimbo ya tisa.
Bikira Mzazi-Mungu ambaye kweli ulizaa Kristu Mungu wetu bila mbegu, huyu aliyeinuliwa msalabani, sisi waaminifu, wote pamoja kama yeye sasa tunakutukuza.

## KATAVASIA SIKU YA MUNGU YA WATAWI.

Wimbo ya kwanza. Sauti ya Ine.
Chemchem za kuzimuni zilizuia wimbi lao, pofu ya bahari haifiiiche misingi yake; kwa alama moja ulirudisha nyuma sababu ya kuokoa taifa lako teule lenyi kukuimbia, ee Bwana, wimbo wa ushindi.

Wimbo ya tatu.
Waisraeli walikunywa maji ku mwamba gumu kabisa ambao kwa amri yako ukageuka kuwa chemchem; na Wewe mwenyewe, ee Kristu, ndiwe mwamba wa uzima wetu; na juu ya mwamba huo palijengwa Eklezia yenye kukulamikia: Hosana, Bwana unayekuja, umetukuzwa.

Wimbo ya ine.
Kristu anayekuja na mwenye kufunuliwa kama Mungu wetu atafika bila kukawia: alipozaliwa kwa Bikira asiyeolewa ametokaa ku mlima wa kivuli kama alivyosema Nabii zamani, na tunaunganisha masauti yetu sababu ya kuimba: Utukufu ku uwezo wako, ee Bwana.

Wimbo ya tano.
Kuja utangaze mlimani wa Sayuni habari njema ya Yerusalema, paza sauti kwa kutangaza utukufu unaokuja ku mji wa Mungu: Amani kwa Israeli na wokovu ku mataifa.

Wimbo ya sita.
Moya wa wenye haki unafurahiwa: Kwa ulimwengu inanza angano Jupya: Agano inabadirika kwa damu ya Mungu.

Wimbo ya saba.
Ku tanuru ya moto ukawaokoa waana wa Abrahamu, ukama wakaldea kwa moto waliyotayarisha wenyewe. Bwana mstahili kamili wa nyimbo zetu, Mungu wa Baba zetu, umetukuzwa.

Wimbo ya mnane.
Tunamusifu, tunamuhimidi na tunamusujudu Bwana.
FurahiwaYerusalema, shangilieni, ninyi munaopenda Sayuni: Huyu anayetawala milele Bwana wa majeshi, amekuja, ulimwengu uiname mbele yake, dunia iimbe mbele yake: Viumbe vyote vya Bwana, tukuzeni Bwana.
Wimbo ya tisa.
Bwana ni Mungu, ameonekana kwetu, shangilieni hii Siku Kuu, na katika furaha nujeni, tutukuzeni Kristu na mitende na matawi: tumulalamikie na furaha: Mbarikiwa anayekuja kwa Jina la Bwana Mwokozi wetu.

# KATAVASIA YA KUTOKA 27 MWEZI YA SABA MUPAKA 31 MWEZI YA SABA.

Wimbo ya Kwanza. Sauti ya Ine.
Walipopita pakavu katika bahari Nuekundu zimuni ya maji na walipoona waaskari wa Farao Wapandaji frasi wameangamizwa kwa mawimbi, makundi ya waisraeli wakaimba nyimbo na furaha: Tumwimbie Mungu wetu, kwani amevaa utukufu.

Wimbo ya Tatu.
Upinde wa wenyi nguvu umeregea, wazaifu wanapata nguvu; na tazama ndiyo maana moyo wangu umesabitishwa katika Bwana.

Wimbo ya Ine.
Bwana nimeona taswira ya wokovu wako, kwani umezaliwa kwa Bikira, ee Kristu Mungu wetu, sababu ya kuokoa wale wenye kulalamika: Utukufu kwa uwezo wako, ee Bwana.

Wimbo ya Tano.
Wewe uliyeonekanisha nuru katika usiku wa nyakati za kwanza ili katika mchana viumbe vyako, ee Kristu, vitukuze katika wewe Muumba wao, ongoza hatua zetu katika nuru yako.

Wimbo ya Sita.
Katika taabu ya moyo wangu nikamulilia Bwana na Mungu wa wokovu wangu akajiharikisha kunisikiliza.

Wimbo ya Saba.
Zamani ku Babyloni waana wa Abrahamu wakakanyanga tanuru ya moto, kwa nyimbo zao wakalalamika na furaha: Umetukuza, ee Mungu wa Baba zetu.

Wimbo ya Mnane.
Ku Babyloni Vijana walipowashwa na bidii ya Mungu, wakazarau na ushujaa amri ya Mzalimu na utisho wa moto: Katikati ya moto walipofunikwa na umande, wakaanza kuimba: Enyi viumbe vyote vya Bwana, tukuzeni Bwana.
Wimbo ya Tisa.
Wa milele alifunuliwa ni huyu uliyezaa na Mungu Mwenyewe alitaka kutoka tumboni Mwako, alipovaa mwili wetu, akaonekana duniani sababu ya kuzungumuza na wanadamu, ee Mzazi-Mungu, tunakutukuza na moyo mmoja.

# KATAVASIA SIKU YA INE YA KUPAA.

*Tunaimba Juma Sita mpaka mukazi mbili ya Juma ya Kipofu.*
Wimbo ya Kwanza. Sauti ya Tano.
Mungu Mwokozi aliyeongoza wana wa Israeli pakavu baharini Nyekundu, akizamisha Farao na jeshi lake lote, tumwimbe kama peke yake ni mstahili wa nyimbo zetu, kwani amevaa utukufu.

Wimbo ya Tatu.
Ee Kristu, kwa uwezo wa Msalaba wako sabitisha nia zetu, sababu ya kuturuhusu kuimba na kutukuza kupaa kwako kwenyi kuleta wokovu.
Wimbo ya Ine.

Bwana, nilisikia sauti yako, niliungama nguvu ya Msalaba wako, maana kwa hii Paradizo ilifunguliwa na nilisema: Utukufu ku uwezo wako, ewe Bwana.

Wimbo ya Tano.
Bwana kwa hii zamu na kwa matumaini ya asubui, tunakulalamikia: Hurumia na utuokoe, kwani ndiwe kweli Mungu wetu, hatujui mwengine ila Wewe.

Wimbo ya Sita.
Shimo ilinizunguka pande zote, nyama alinikamata kama kaburiri; Mpenda-Wanadamu, nililalamika kwako na kume kwako, ee Bwana, kuliniokoa.

Wimbo ya Saba.
Mwokozi uliyekinga katika tanuru ya moto Vijana waliokuimba, umetukuzwa. Bwana. Mungu wa Baba zetu.

Wimbo ya Mnane.
Mwana wa Mungu, aliyezaliwa kwa Baba mbele ya nyakati, akajifanya mtu Bikira Mzazi-Mungu: Ninyi makohani, mutukuzeni, enyi mataifa yote, makuzeni milele.

Wimbo ya Tisa.
Ewe Mzazi-Mungu, uliposhinda akili yetu na usikilizi wetu, ukamzaa mu wakati Bwana wa milele; kwa sauti moja na kwa moyo moja, sisi waaminifu, tunakusifu.

# SALA YA CHAKULA

## Chakula cha asubui

### 1. Mbele ya chakula

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote hata milele na milele. Amina. Bwana hurumia *(mara tatu).* Rabi mtakatifu barikia:

Ee Bwana Yesu Kristu, bariki chakula na kinywaji cha watumishi wako, kwani wewe peke yako ni Mtakatifu daima, sasa na siku zote hata milele. Amina.

*Kama hakuna padri tunasema paka sala ya padri bila kubariki.*

*Kisha chakula cha asubui tunasema ivi:*

Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu. . .

## Chakula cha katikati ya muchana (midi)

## Mbele ya chakula

Baba yetu. . . Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Ee Rabi mtakatifu barikia.

PADRI: Ee Bwana Yesu Kristu, bariki chakula na kinywaji. . .

*Kisha hii chakula tunasema:*

Ee Kristu Mungu wetu, tunakushukuru kwa maana ulitushibisha na vitu nyako vya inchi; usikatae kutupatia na ufalme wako wa mbinguni, lakini kama ulivyokuwa katikati ya wafwasi wako kwa kuwapa amani, vile, ee Mwokozi, kuja pia na kwa sisi na utuokoe. Amina.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Ee Rabi mtakatifu barikia:

PADRI: Ee Kristu Mungu wetu, bariki mabaki ya hii chakula iliyo mezani, uiongeze kwa hii nyumba na kwa dunia yote, wewe ni Mungu Mwema. Mrahimu na Mpenda Wanadamu. Kwa maombezi ya Wapadri wetu. . . .

*Kama hakuna padri, kisha **B**wana hurumia (mara tatu). tunasema:*
Kwa maombezi. . .

### Chakula cha mangaribi
### Mbele ya chakula

Maskini watakula na kushiba, wenye kumutafuta Bwana watamusifu na mioyo yao iishi kwa milele. Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia
*(mara tatu).* Ee Rabi mtakatifu barikia:

PADRI: Ee Bwana Yesu Kristu, bariki chakula na kinywaji. . .

*Kama hakuna Padri, tunasema hii sala ya Pardi bila kubariki.*

### Kisha chakula cha mangaribi

Umetufurahisha, ee Bwana, kwa matendo yako na tulishangilia kazi ya mikono yako, Utunyanyulie nuru ya uso wako, ee Bwana, ulitupatia furaha moyoni mwetu, kwani katika matunda ya ngano, na vinyo na mafuta yako tulizibishwa. Hivi katika amani tutapumuzika na kupata usingizi, kwa maana Wewe Bwana wa peke na kitumaini unaikaa ndani yetu. Amina.

Utukufu. . . Sasa. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Kwa maombezi ya wa Padri wetu. . .

# APOLITIKIA NA THEOTOKIA ZA UFUFUO WA BWANA YESU KRISTU

## Sauti ya kwanza

### APOLITIKION

Wakati jiwe lilitiliwa muhuri na wayuda, na wakati Waaskari walichunga mwili wako usiyo doa, ulifufuka siku ya tatu ee Mwokozi, uliupatia ulimwengu uzima. Kwa hii ezi mbingu ilipaza sauti kwa wewe mpaji wa uzima; utukufu kwa ufufuo wako, ee Kristu. utukufu kwa ufalme wako, utukufu kwa shuruli yako ya ulimwengu, wewe peke Mpenda-Wanadamu.

### THEOTOKION

Wakati Gabrieli alisema kwako Bikira, Salamu, kwa sauti; Rabi wa wote alichukua mwili, ndani yako safina takatifu, sawa mwenye haki Daudi alivyosema. Ulionekana kuwa munene sana kuliko mbingu, kwa sababu ulichukuwa Muumba wako. Utukufu kwa yule alikaa ndani yako; utukufu kwa huyu alitoka kwako; utukufu kwa huyu alitupatia uhuru juu ya uzazi wako.

### IPAKOI

Toba ya Munyanganyi ikashurtisha Paradizo, maombolezo ya Wabebaji manukato ya kutangaza furaha: Ee Kristu Mungu wetu, ulifufuka kwa kuleta ku dunia neema kubwa.

## Sauti ya pili

### APOLITIKION

Wakati ulishuka ku mauti, uzima usiyo kufa, hapo uliregeza kuzimu, kwa unara wa umungu wako; na wakati ulifufua wafu waliyolala kuzimuni, ezi zote za mbinguni zilipaza sauti; Mpaji wa uzima Kristu, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

### THEOTOKION

Siri zako zote, zinapita wazo lolote na zote ni utukufu sana, ee Mzazi-Mungu, wewe uliyewekwa alama ya safi, uliyelindwa kwa ubikira, ulijulikana kuwa Mama msema kweli, ulizaa Mungu kweli; umwombe aokoe roho zetu.

### IPAKOI

Ee Kristu Mungu Wanawake wakaenda kaburini kisha mateso Yako kwa kuupakaa mwili wako manukato. Wakaona Malaika ndani ya kaburi na wakashikwa na woga, kwani wakasema: Bwana amefufuka kwa ajili ya kuleta duniani neema kubwa.

## Sauti ya tatu

### APOLITIKION

Mbingu zifurahiwe, na inchi ishangilie, kwa sababu Bwana ametenda nguvu, kwa mukono wake; na kwa lufu alishinda mauti; na akawa muzaliwa wa kwanza katika wafu; akatuondosha katika tumbo la kuzimu, na akaleta ku dunia huruma kubwa.

### THEOTOKION

Bikira Mzazi-Mungu tunakuimbia, wewe mupatanishi wa wokovu juu ya ukoo wetu; katika mwili alipata Kwako, Mwana wako na Mungu wetu, alitaka kuteswa msalabani, juu ya kutukomboa ku lufu, sawa Mpenda-wanadamu.

### IPAKOI

Wa ajabu ku sura yake, Malaika mwenye kuangaa, kwa maneno yake akamwanga umande, akawaambia wabebaji-manukato: Kwa nini munamutafuta katika wafu huyu aliye hai? Alipotosha vyote kaburini, amefufuka! Na kwa mabadiliko yenye kufanyika kaburini mutambue huyu hawezi kugeuka na mumuambieni: Matendo yako ni ya ajabu. Bwana! Kwani uliokoa ubinadamu ku lufu.

## Sauti ya ine

### APOLITIKION

Wakati wanawake-wanafunzi wa Bwana, walipofundisha na Malaika kuhubiri habari ya furaha ya ufufuo, na walipotupa hukumu kwa mababu zetu, wakasema kwa Mitume kwa kujisifu: Mauti imenyanganywa, Kristu Mungu alisimama, kwa kuleta duniani rehema kubwa.

### THEOTOKION

Siri ya kificho tangu milele iliyokuwa isijulikane na Malaika, imeonekana duniani katika wewe, ee Mzazi-Mungu; maana Mungu alitwaa mwili kwa ushirika, bila muchanganyo, na alikubali msalaba kwa kutaka kwake kwa ajili yetu; juu ya hii akifufua Muumbwa wa kwanza, akaokoa toka lufu nafsi yetu.

### IPAKOI

Ee Kristu. Wabebaji manukato, watangazaji wa kwanza wa ufufuo wako, wa ajabu, wakaenda mbio kwa Mitume wakasema: Kristu amefufuka kama Mungu, analeta duniani neema kubwa.

## Sauti ya tano.

### APOLITIKION

Neno lasipo mwanzo pamoja na Baba na Roho, huyu alizaliwa kwa Bikira kwa ajili ya wokovu wetu; basi, waaminifu, tumwimbie na tumwabudu; kwani mapenzi yake katika mwili, alipanda juu ya msalaba, akavumilia lufu, na alifufua wafu, katika ufufuo wake muheshimiwa.

### THEOTOKION

Salamu, mulango wa Bwana usioweza kupitwa; Salamu, ukuta na kivuli cha wale waliokimbilia kwako; salamu, kivuko bila kutikisika, na musiyeolewa, uliyezaa katika mwili Muumba na Mungu wako; usiache kupatanisha kwa ajili ya wale walikuimbia, na walioabudu Mwana wako.

### IPAKOI

Walipoogopeshwa kwa mwangaza wa malaika, walipoangazwa kwa nuru ya ufufuo, Mirofori wakaenda mbio kwa Mitume wakasema: Tangazieni mataifa yote habari njema ya Ufufuo wa Bwana wenye kutenda hapa chini maajabu ya nuru na kutupatia neema kubwa.

## Sauti ya sita.

### APOLITIKION

Majeshi ya Malaika pa kaburi yako, na walinzi walikuwa kama wafu; Maria alisimama kaburini, akitafuta mwili wako usiye na doa. Ulinyanganya Hadeze bila kujaribiwa kwake. Ulikuta Bikira, ukileta uzima. Ewe Bwana uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako.

### THEOTOKION

Ewe uliyeita Mama yako mubarikiwa, ulikuja kwa mateso kama ulivyotaka; uliangaa kwa musalaba, kwani ulitaka kutafuta Adamu; ukasema kwa Malaika: Mufurahi pamoja nami, kwa kuwa ilipatikana feza iliyopotea. Ewe uliyefanya yote na akili, utukufu kwako.

### IPAKOI

Ee Kristu, kwa lufu yako ya kutaka na yenye kuleta uzima, ulivunja milango ya Hadeze; ee Mungu, unatufungulia Paradizo ya zamani; ulipofufuka katika wafu, unanyanganya uzima wetu kuzimuni.

## Sauti ya saba.

### APOLITIKION

Uliharibu mauti kwa musalaba wako; ulifungua Paradizo kwa munyanganyi; ulibadilisha maombolezo ya wanawake wabebaji manukato, na uliamuru Mitume wako kuhubiri, kwamba ulifufuka, ee Kristu Mungu, ukileta duniani rehema kubwa.

### THEOTOKION

Ewe Mwimbiwa kamili kama hazina ya ufufuo wetu, ututoshe sisi wenye kukuamini, toka shimo na vilindi vya makosa yetu; kwani wewe uliokoa wenye daraka ya zambi; ku uzao wa wokovu. Wewe ni Bikira mbele ya kuzaa, na Bikira katika kuzaa, na tena Bikira kisha kuzaa.

### IPAKOI

Ulichukua hali yetu, uliteswa mwilini mwako msalabani; uniokoe, ee Kristu Mungu kwa ufufuo wako, ewe Mpenda-Wanadamu.

## Sauti ya mnane.

### APOLITIKION

Toka juu ulishuka, ee Mwema, na ulikubali maziko ya siku tatu, kusudi utuopoe toka tamaa. Uzima na Ufufuo wetu. Bwana, utukufu kwako.

### THEOTOKION

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyanganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioumbwa kwa mukono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu. Murehemu; pokea Mzazi Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

### IPAKOI

Mirofori walipokuja kaburini ya chemchem ya uzima wakatafuta katika wafu Rabi msiyekufa; lakini walipopokea kwa Malaika habari ya furaha, wakawaambia Mitume ya kama Bwana alifufuka kuleta duniani neema kubwa.

# APOLITIKIA YA WATAKATIFU

*Kila siku Kanisa yetu inashangilia Mtakatifu moja ao wengi. Hawa ni Maaskofu, Watawa. Mashahindi, Manabii, Mitume na weingine. Kila Kundi yao hapa chini iko na na Apolitikion yake. Basi, kwa sala ya Mangaribi kisha Sala:* «Sasa Bwana umuache mtumishi wako. . . » *na kisha Trisagion tunaweza kusoma ao kuimba Apolitikion ya ule Mtakatifu ya hii siku ya leo. Kisha tunaimba* Utukufu. . . Sasa. . . *Theotokion ya Mzazi-Mungu. Hivi tunaweza kusoma ao kuimba na asubui kisha Eksapsalmos na kisha ma shairi.*

## APOLITIKION YA ASKOFU

**Sauti ya Ine (Kanona pisteos)**

Haki ya matendo yako ilikufanya wewe kuwa kanuni ya imani ya kundi lako la kondoo, mfano wa upole, rabi wa kiasi; ndiyo maana katika unyenyekevu wako ulipata utukufu na katika umasikini wako ulipata utajiri. Baba Mtakatifu. . . *(jina lake).* . . umuombe Kristu Mungu wetu aokoe roho zetu.

## APOLITIKION YA SHAHIDI

**Sauti ya Ine (O martis su Kirie)**

Shahidi wako, . . . *(jina lake)* , ee Bwana, kwa mashindano aliyoshindana alipokea kwako. Mungu wetu, taji ya milele; aliposukumwa na nguvu yako, uliangusha wazalimu na kuondoa nguvu ya mashetani; kwa maombezi yake okoa roho zetu, ee Kristu Mungu wetu.

## APOLITIKION YA MASHAHIDI WENGI

**Sauti ya Ine (I Martires su Kirie)**

Mashahidi wako, ee Bwana, kwa ajili ya mashindano walioshindana walipokea kwako. Mungu wetu, taji ya milele, waliposukumwa na nguvu yako waliangusha wazalimu na kuondoa nguvu ya mashetani; kwa maombezi yao okoa roho zetu, ee Kristu Mungu wetu.

## APOLITIKION YA PADRI NA SHAHIDI (Ieromartis)

**Sauti ya Ine (Ke tropon metohos)**

Ulipokuwa na hali ya uzima wa Mitume na ulipokuwa halifa wa kiti yao, ulipata katika zoezi ya fazila njia yenye kwenda ku mawazo ya umungu; ndio maana, ulipoeneza na ibada neno la ukweli, ulishindana mpaka ku damu sababu ya ulinzi wa imani. . . *(jina lake).* . . Shahidi Mutakatifu umwombe Kristu Mungu wetu aokoe roho zetu.

## APOLITIKION YA MUTAKATIFU MUTAWA

**Sauti ya kwanza (Tis erimu politis)**

Jangwa ilikuwa mji wako, katika mwili ulikuwa Malaika, miujiza yako yamekushuhudia. Baba yetu. . . *(jina lake),* Mubebaji-Mungu. Kwa kufunga, kukesha na sala ulipokea vipaji vya mbinguni sababu ya kuponya wagonjwa na roho za waaminifu wenye kukimbilia kwako. Utukufu kwa huyu aliyekupa hii uwezo, utukufu kwa huyu aliyekutukuza, utukufu kwa huyu anayetenda matunzo kwa wote katika maombezi yako.

**Ingine:**

**Sauti ya Mnane (Tes ton dakrion su roes)**

Kwa mawimbi ya machozi yako ulistawisha jangwa kavu, kwa maombolezo yako ya ndani ulitoa ku mateso yako matunda mara mia moja na kupita, kwa miujiza yako ya ajabu umekuwa taa yenye kuangaza ulimwengu wote: Mutawa Baba yetu. . . *(jina lake),* umuombe Kristu Mungu wetu aokoe roho zetu.

## Ingine:
## Sauti ya Mnane (En si pater akrivos)

Katika wewe. Baba, sura ya umungu ilionekana kabisa, kwa kufanana nayo ulichukuwa msalaba wako na ulimufwata Kristu; na kwa uzima wako ulifundisha kuzarau mwili kwa sababu ni ya kupotea, kwa kushurulika na roho isiyokufa hata milele. Ni hivi roho yako inafurahiwa, ewe Mtawa. . . *(jina lake),* pamoja na malaika.

## APOLITIKION YA MUTAKATIFU MWANAMUKE MUTAWA
## Sauti ya Mnane (En si Miter akribos)

Katika wewe Mama, sura ya umungu ilionekana kabisa, kwa kafanana nayo ulichukua msalaba wako na ulimufwata Kristu; na kwa uzima wako ulifundisha kuzarau mwili, kwa sababu ni ya kupotea, kwa kushurulika na roho isiyokufa hata milele; ni hivi roho yako inafurahiwa, ewe Mutawa. . . *(jina lake),* pamoja na Malaika.

## APOLITIKION YA MWANAMUKE SHAHIDI
## Sauti ya Ine (I Amnas su Yesu)

Kondoo wako, ee Yesu analia nguvu na sauti yake; Ni wewe napenda Bwana arusi wangu, ni wewe natafuta ninaposindana, nimesulubiwa na nimezikwa kwa ubatizo wako, na nateswa kwa ajili yako, ili niishi pia ndani yako; lakini pokea sawa sadaka yasipo kosa huyu mwenye kujitoa kwa kutaka kwake kwa ajili yako kwa maombezi yake, ee Mungu wa huruma okoa roho zetu.

## APOLITIKION YA MT. MTHEOLOGO.
## Sauti ya Mnane (Orthodoksias odige)

Mwogozi wa Orthodoksi, mwalimu wa imani na mupole, taa ya Kanisa, pambo kimungu ya watawa, mwenye hekima. . . *(jina lake),* uliangaza wote kwa mafundisho yako kwa sababu ulikuwa kiumbe cha Roho Mtakatifu. Umwombe Kristu Mungu wetu ili aokoe roho zetu.

## APOLITIKION YA MUTUME MOJA
## Sauti ya Tatu (Apostole agie)

Mutakatifu Mutume. . . *(jina lake),* umuombe Mungu wa huruma, ili alete ku roho zetu maondoleo ya zambi zetu.

*Maelezo: Kama Mutume eko tena Mwevangelisti, tanaimba ivi:*
Ee Mutakatifu Mutume na Mwevangelizaji. . . *(jina lake),* umuombe Mungu wa huruma. .
*Kama Mitume weko mengi tunaimba ivi:*
Enyi Watakatifu Mitume, mumwombee Mungu wa huruma. . .

## APOLITIKION YA NABII
## Sauti ya Pili (Tu Profitu su. . )

Ee Bwana, tunashangilia leo makumbusho ya Nabii wako. . . *(jina lake)* na tunakuomba katika huyu aokoe roho zetu.

# APOLITIKIA NA KONTAKIA ZA SIKU KUU ZA BWANA WETU YESU KRISTU

## SIKU KUU YA KUZALIWA KWA YESU KRISTU

### Apolitikion. Sauti ya Ine.

Katika kuzaliwa kwako, ee Kristu Mungu wetu, ilionekana duniani nuru ya maarifa: kwa mwangaza wake waabudu wenye akili ya nyota walifunza kwa nyota kukuabudu, jua la Haki, nakukutambua kama mashariki aliyetoka juu; Bwana, utukufu kwako.

### Kontakion. Sauti ya Tatu.

Leo Bikira amezaa Mungu Mkuu na dunia pango inapokea msiye karibika. Malaika na wachungaji-Kondoo wanatukuza. Majusi pamoja na nyota wanatembea. Kwani kwa ajili yetu alizaliwa, Mtoto Mchanga, Mungu wa mbele ya nyakati.

## SIKU KUU YA TOHARA YA BWANA WETU YESU KRISTU

### Apolitikion. Sauti ya Kwanza.

Ulichukuwa mwili wa ubinadamu bila ugeuzi, wewe uliye Mungu kwa hali yako. Bwana mwenyi huruma; kwa kutimiza kanuni ya sheria, ulitaka kutahiriwa mwilini sababu ya kuondoa giza na pazia kunakofichama tamaa zetu. Utukufu kwa wema wako kubwa, utukufu ku rehema yako, ee Neno la Mungu, utukufu ku mapendo isiyokaridika iliyokushusha mpaka kwa sisi.

## SIKU KUU YA EPIFANI YA BWANA WETU YESU KRISTU

### Apolitikion, Sauti ya Kwanza.

Bwana, wakati ulipobatizwa katika Yordani. Utatu Mtakatifu ulifunuliwa ku ulimwengu; sauti ya Baba ikasikilika kwa ajili yako ikikutaja kama Mwana wake mpendwa; na Roho kama jiwa akashuhudia, Kristu Mungu wetu ulijifunua, mwanga wa ulimwengu, utukufu kwako.

### KONTAKION, Sauti ya Ine.

Leo siku ya Epifania ulimwengu umeona mwangaza wako, kwani, ee Bwana, ulijifunua na nuru yako inatuangaza; ndio maana na ufahamu wetu tunakuimbia: Ulikuja na ulijifunua, Nuru isiyokaribika.

## SIKU KUU YA KUPOKELEWA KWA BWANA YESU KRISTU MIKONONI MWA MWENYI HAKI SIMEONI

### Apolitikion. Sauti ya Kwanza.

Salamu, Mjaliwa neema, Bikira Mzazi-Mungu, kwani kwako kulitoka jua la haki, Kristu Mungu wetu, anayewangaza wale waliokuwa gizani. Salamu pia, mwenye haki Mzee Simeoni, kwani ulibeba mikononi mwako Mkombozi wa roho zetu mwenye kujitoa kwa Ufufuo wake.

### Kontakion, Sauti ya Kwanza.

Katika kuzaliwa kwako ulitakasa tumbo la Bikira, katika kutolewa kwako ulibariki mikono ya Simeoni, sawa ilivyofaa, ulikuja sasa na ulituokoa ee Kristu Mungu wetu. Leta mu wakati wetu amani ku uzima wetu, na sabitisha wafalme wetu, wale uliyopenda, wewe peke Mpenda-wanadamu.

## SIKU KUU YA MUNGU YA MATAWI NA UFUFUO WA LAZARO

### Apolitikion, Sauti ya Kwanza.

Ewe Kristu Mungu, mbele ya mateso yako ulimufufua Lazaro katika wafu na unatuonyesha ufufuo wa watu wote. Alafu na sisi kama watoto tunakamata alama ya ushindi na tunapaza sauti kwako Mshahidi wa lufu: Hosana juu mbinguni. Mbarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana.

**Apolitikion ingine. Sauti ya Ine.**

Ewe Kristu Mungu wetu, tulipozikwa pamoja nawe katika ubatizo, tulistahili uzima wa milele katika Ufufuo wako, na tunapaza sauti katika wimbo: Hosana juu mbinguni, Mbarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana.

**Kondakion. Sauti ya Sita.**

Ewe Kristu Mungu wetu, unashuka toka kiti cha mbinguni na unatembea katika inchi juu ya punda, unapokea wimbo wa Malaika na wale watoto wa wayuda, wote wanakupazia sauti: Ndiwe Mbarikiwa anayekuja kumurudisha Adamu.

## SIKU KUU YA PASKA

### Apolitikion. Sauti ya Kwanza.

Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya kaburi aliwapatia uzima.

**Kondakion. Sauti ya Mnane.**

Ewe Msiyekufa, ulishuka kaburini na uliharibu nguvu ya Hadeze, Kristu Mungu wetu, ulifufuka kama Mshindi ukawaambia wanawake Wabebaji-manukato: Furahini! Uliwapa Mitume wako amani, na wale walioanguka uliwafufua.

## SIKU KUU YA KUPANDA MBINGUNI

### Apolitikion. Sauti ya Ine.

Unapanda katika utukufu, ee Kristu Mungu wetu, ukiwajaza wafwasi wako na furaha kwa ahadi ya Roho Mtakatifu, ukawapa nguvu na kuwabariki na mikono yako, kwani ndiwe Mwana wa Mungu, Mkombozi wa dunia.

**Kondakion. Sauti ya Sita.**

Ulipotimiza kwa ajili yetu tendo lako la wokovu, kisha kuunganisha mbingu na dunia, watu na Mungu, katika utukufu, ee Kristu Mungu wetu, ukapanda mbinguni bila kutwacha, lakini umekaa siku zote katikati yetu na ukawaambia wale wanaochunga mapendo yako: Mimi ni pamoja nanyi siku zote na mutu hata mumoja hawezi kufanya chochote juu yenu.

## SIKU KUU YA PENTEKOSTI

### Apolitikion. Sauti ya Mnane.

Uhimidiwe, ee Kristu Mungu wetu, wewe uliyewashushia Mitume wako Roho Mtakatifu, ukawageuza kwa hekima yako wavuvi kuwa wavuvi wa watu ambao nyavu yatavua dunia yote. Bwana Mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

**Kondakion. Sauti ya Mnane.**

Alipochanganya lugha za ulimwengu, Bwana wa juu mbinguni akasambaza mataifa; lakini alipogawanya ndimi za moto, anawalika watu wote ku umoja na wote pamoja tunamutukuza Roho Mtakatifu kamili.

## SIKU KUU YA MAGEUZO SURA YA YESU KRISTU MWOKOZI WETU

### Apolitikion. Sauti ya Saba.

Uligeuza sura mlimani, ee Kristu Mungu wetu, uliwaonyesha wanafunzi wako utukufu wako kama walivyoweza: Utuangazie pia sisi wenye zambi na mwangaza yako ya milele kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, ewe muletaji wa Nuru, utukufu kwako.

**Kondakion. Sauti ya Saba.**

Mlimani ulijigeuza, na kama inavyowezekana wanafunzi wako waliona, ewe Kristu Mungu, utukufu wako; wakati walikuona Msalabani, na walisikia mateso yako kwa mapenzi yako na, watahubiri duniani, ya kama ndiwe kweli Mtukufu wa Baba.

# APOLITIKIA NA KONDAKIA ZA SIKU KUU ZA MZAZI-MUNGU

## SIKU KUU YA KUZALIWA KWA MAMA MZAZI-MUNGU

**Apolitikion. Sauti ya Ine.**

Katika kujaliwa kwako, ewe Mzazi-Mungu, furaha ilifunuliwa ulimwenguni yote, kwani kwako kulitokea Jua la haki, Kristu Mungu wetu ambaye, alipotukomboa ku laana, akatuletea baraka, na aliposhinda mauti, akatupatia uzima wa milele.

**Kondakion. Sauti ya Ine**

Yoakimu na Anna ku utasa wa haya, Adamu na Eva ku mauti ya uharibifu waliombolezwa Bikira Safi, kwa ajili ya kuzaliwa kwako; hivi mataifa yake wanakushangilia, kwa maana walikombolewa ku utumwa wa zambi na wanaimbia tasa aliyezaa Mzazi-Mungu na mlinzi wa uzima wetu.

## SIKU KUU YA KUINGIA KWAKE MZAZI-MUNGU HEKALUNI

**Apolitikion. Sauti ya Ine.**

Leo ni mwanzo wa wema wa Mungu wa kuwatangazia wanadamu wokovu. Bikira ameonekana Hekaluni mwa Mungu na anawaonyesha watu wote kuja kwake Kristu. Sisi pamoja naye tunapaza sauti tukisema: Salamu, matimizo ya mapendo ya Muumba.

**Kondakion. Sauti ya Ine.**

Leo ameingia nyumbani mwa Bwana Hekalu safi ya Mwokozi, chumba tukufu na Bikira, zahabu takatifu ya utukufu wa Mungu na neema ya Roho Mtakatifu pamoja naye huyu, mwenye kuimbiwa na Malaika wa Mungu, kwani yeye ni hema ya mbingu.

## SIKU KUU YA HABARI NJEMA YA BIKIRA MARIA MZAZI-MUNGU

**Apolitikion. Sauti ya Ine.**

Leo ni asili ya wokovu wetu na ufufuo wa fumbo ya milele; kwani Mwana wa Mungu amejifanya kuwa Mwana wa Bikira na Gabrieli anamutangazia Bikira neema kwa hii sisi pamoja na huyu tunamwimbia Mzazi-Mungu: Salamu, Mjaliwa neema, Bwana ni nawe.

**Kondakion. Sauti ya Ine.**

Masauti yetu ya ushindi yavume kwa ajili ya heshima yako, ewe Malkia msiyeweza kushindwa, wewe mwenye kutuokoa ku hatari ya vita, Mzazi-Mungu. Bikira Mkuu. Sifa zetu na nyimbo zetu za shukrani zinapanda kwako. Simika pembeni yetu moja ya maboma imara na mkono wako wa uwezo, utuokoe ku hatari yote ujiharikishe kuwasaidia waaminifu wanaokuimbia: Salamu, Bibi-arusi usiyeolewa.

## SIKU KUU YA KULALA KWAKE MZAZI-MUNGU

**Apolitikion. Sauti ya Kwanza.**

Katika uzazi wako ulichunga ubikira, katika lufu yako haukwache dunia, ee Mzazi-Mungu: Ulipanda ku uzima, kwa kuwa ulikuwa wewe Mama wa uzima, na kwa maombi yako unaokoa roho zetu ku lufu.

**Kondakion. Sauti ya mbili.**

Ee Mzazi-Mungu usiyechoka kutuombea kamwa kwa ulinzi wako hauwezi kuacha kuwa matumaini yetu, uwakamate kaburi na lufu kwani ndiwe Mama wa Uzima aliyeikaa tumboni mwa bikira daima na kukupandisha.

*Kila siku ya Juma iko na walinzi wake. Nikusema mu kazi moja ni ya Malaika Watakatifu. Mu kazi mbili ni ya Mtakatifu Yoane Mutangulizi. Mu kazi tatu na mu kazi tano ni ya Msalaba wa Kristu. Mu kazi ine ni ya Mitume Watakatifu na Mtakatifu, Nikola. Muposho ni ya Watakatifu wote na ya ndugu zetu wotee waliofariki. Sisi tunapaswa kumuomba kwa Mungu apumzishe roho zao.*

*Siku ya Juma, ni siku ya Ufufuo wa Bwana wetu Yesu Kristu. Hapa tunaandika Apolitikia na Kontakia za kila siku za wale Watakatifu.*

# APOLITIKIA NA KONTAKIA YA JUMA.

## MUKAZI MOJA

## Apolitikion ya wabila-mwili (Malaika).
## Sauti ya ine

Ee Wakubwa wa majeshi wa mbingu sisi mwenye bila stahili tunamiomba juu katika maombi wenu mutufunike, katika ufuniko ya mabawa ya utukufu wenu na kutuchunga sisi wenye tunapika magoti kwenu na tunapaza sauti; mutuokoe toka ma hatari, ee ninyi Wakubwa wa Nguvu juu pia.

**Kontakion. Sauti ya pili**

Enyi Wakubwa wa majeshi ya Mungu, watumishi wa utukufu wa kimungu, waongozi wa watu, na wakubwa wa wabila-mwili, mwombe kwa ajili yetu ile iliyo ya mafaa, na rehema kubwa, ee ninyi wakubwa wa wabila-mwili.

## MUKAZI MBILI

### Apolitikion ya Mtakatifu Yoane Mtangulizi na Mbatizaji .
### Sauti ya mbili.

Ewe Mtangulizi, unastahili makumbusho ya mwenye haki katika utukufu, juu ya ushuhunda wako kwa Bwana; kwani ulionekana kweli mheshimiwa kamili wa Manabii, sababu ulistahili Mkubatiza katika maji mwenye kuhubiriwa. Basi, kwani ulichunga ukweli katika furaha uliwahubiri na wote walikuwa ku Gehena ya kama Mungu ameonekana katika mwili, huyu aliondoa zambi ya dunia na alitupatia rehema kubwa.

**Kontakion Sauti ya mbili**

Ee Nabii wa Mungu, na Mtangulizi wa neema, tulipata kichwa chako ku udongo, sawa ua takatifu nyekundu, na tunaponyeshwa wakati wote, kwani zamani, ulishauria dunia kwa kutubu.

## MUKAZI TATU NA MUKAZI TANO

**Apolitikion ya Musalaba ya Kristu.**
**Sauti ya kwanza**

Ee Bwana okoa taifa lako na bariki urizi wako. Ukiwapa wafalme kushinda juu ya wakafiri, na kuilinda jamii yako kwa Msalaba wako.

**Kontakion ya Musalaba Sauti ya ine**

Ulipopandishwa msalabani kwa kutaka kwako, ee Kristu Mungu, leta huruma yako, ku taifa lipya linaloitwa kwa jina Lako; furahisha kwa uwezo wako wafalme wetu waaminifu, ukiwapa ushindi juu ya adui; ili wapate katika agano Lako, silaha ya amani, ushindi usiyosubutishwa.

## MUKAZI INE

### Apolitikion ya Watakatifu Mitume.

### Sauti ya tatu.

Enyi Mitume Watakatifu, mumwombee Mungu wa huruma, ili alete ku roho zetu maondoleo ya zambi zetu.

### Apolitikion ya Mtakatifu Nikolaos.

### Sauti ya ine. (Kanona Pisteos)

Haki ya matendo yako ilikufanya wewe kuwa kanuni ya imani ya kundi lako la kondoo, mfano wa upole, ee rabi kwa kiasi; ndiyo maana katika unyenyekevu wako ulipata utukufu na katika umasikini wako ulipata utajiri. Baba Mtakatifu. . . umuombe Kristu Mungu wetu aokoe roho zetu.

### Kontakion ya Mitume Watakatifu.

### Sauti ya mbili.

Wafundishaji wa usawa na wenye kuongozwa na Mungu, cha ya Mitume wako; Bwana, uliwapokea katika furaha ya mema Yako na ya mapumziko yako; ulipokea mateso na lufu yao, kuliko sadaka yote ya kuteketeza, kwani peke yako unajua ndani ya mioyo.

### Kontakion ya Mtakatifu Nikolaos.

### Sauti ya tatu

Ku Mira, ewe Mtakatifu, ulionekana kuwa kuhani; kwani ulitimiza hii siku Evangelio ya Kristu, ulitoa uzima wako kwa ajili ya taifa lako, na uliokoa ku lufu wasiyo na mabaya; ndio maana umetakaswa, sawa fundi wa neema ya Mungu.

## MUPOSHO NI MAKUMBUSHO YA WATAKATIFU WOTE.

### Apolitikion Sauti ya mbili.

Enyi Mitume, Mashahindi na Manabii, Maaskofu, Watawa na Wenye Haki, ninyi mumemaliza mashindano nzuri na mumelinda imani, kwani kuwa uwezo kwa Mwokozi Mwema, mutuombee aokoe roho zetu.

### Apolitikion ya Wafu.

### Sauti ya mnane.

Ee Bwana Mwema uwakumbuke Watumishi wako na wote wale walikosa katika uzima wao, uwasamehe; kwani hakuna mutu asiye na zambi, paka Wewe peke yako, na kwa wale waliokufa uwapatia mapumziko.

### Kontakion ya Mashahindi

### Sauti ya Mnane

Ee Bwana, ulimwengu inakutoa, kama mwanzo ya inchi, kwa Muumba ya dunia, Washahindi Wabebaji-Mungu; basi, ewe Mwenye huruma kamili, katika maombi wao, chunga Kanisa wako katika amani mingi kwa maombezi ya Mzazi-Mungu.

### Kontakion ya Wafu.

### Sauti ya Mnane

Pamoja na watakatifu, pumzisha, ee Kristu, roho za watumishi wako, pahali pasipo umivu, bila sikitiko, bila muchoko, lakini uzima wa milele.

# SALA YA KOMONYO TAKATIFU

*Kama umejitayarisha kwa kukomunika, mangaribi yenyi kutangulia siku ya kupokea Komonyo Takatifu, kisha ya sala ya usiku (Apodipno), tokea ukurasa wa kwanza mpaka ukurasa wa tano, na kisha simvolo ya imani, anza sasa, kwa sikitiko ya zambi zako, kusoma sala ya Komonyo Takatifu.*

**SHAIRI 1 WIMBO 1**

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Mwili wako Takatifu uwe kwangu mkate wa uzima wa milele, ee Bwana mwenye huruma, na damu yako ya bei uponya wa maovu yangu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Nimechafuka na vitendo vibaya, mimi mukosefu, sistahili kukomunika mwili na damu yako ya bei, Ee Bwana Kristu unistahilishe kwa kuyapokea mwili na damu Takatifu.

Mutakatifu Kamili, ee Mzazi Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**

Mbarikiwa Bibi-Arusi wa Mungu, udongo ambamo mumekomea suke bila mlimo, wokovu wa dunia, unistahilishe kwa niikule ili nipate kuokolewa.

**WIMBO 3**

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Kristu. Rabi wa dunia, unipe kulia machozi yazimayo maovu ya moyo wangu, ili zamiri ikitakaswa, niikaribie kwa imani na woga komonyo Takatifu iliyo vyako kimungu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Mwili wako bila doa na damu yako yenye bei iwe kwangu maondoleo ya zambi zangu, ushirika wa Roho Mtakatifu na uzima wa milele, ee Mpenda wa binadamu, na iwe mbali nami maumivu na usumbufu.

Mutakatifu Kamili, ee Mzazi Mungu utuokoe. **THEOTOKION**

Ee Bibi-Arusi, meza ya mkate wa uzima ulioshuka toka mbingu ulileta duniani kwa rehema yake, uzima mpya, unistahilishe sasa, mimi nisiyestahili, kuionja na oga na kwa kuyaishi vema hata milele.

**WIMBO 4**

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Yesu Kristu mwenye huruma, kwa mapendo yako ulijifanya mtu kwa ajili yetu, na umejitolea kwa sadaka sawa kondoo sababu ya zambi ya binadamu, Basi ninakuomba unisafishe zambi zangu.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ponyesha vidonda vya moyo wangu. Bwana, na unitakase kamili. Unifanye mstahilivu, ee Rabi, nikomunike, mimi mukosefu.

Mutakatifu kamili, ee Mzazi Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**

Ee Mama wetu, uniombee kwa yeye aliyetoka kwa tumboni mwako, na unichunge kuwa mtumishi wako bila doa na bila magombezi, ili, kiisha kupata ushanga wa roho, nipate kutakaswa.

**WIMBO 5**

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Sawa ulivyoagua, ifanyike hivi kwa mtumishi wako maskini. Kaa ndani yangu kama ulivyoahidi kwa sababu nakula mwili wako na nakunywa damu yako heshimiwa.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Mwana wa Mungu, na Mungu, makaa ya moto yaliyo mwili wako iwe mwangaza wangu mimi niliye katika giza yaambi zangu na damu yako iwe utakaso wa moyo wangu mchafu.

Mutakatifu kamili, ee Mzazi Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**

Ee Maria. Mama wa Mungu, chombo tukufu cha manukato, kwa maombezi yako unifanye kuwa chombo cha uchaguzi ili nipate kushiriki ku utakaso wa Mwana wako.

**WIMBO 6**

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Bwana, utakase akili yangu, moyo wangu na roho yangu na mwili wangu pia, na unifanye mstahilivu. Bwana, kwa kukaribia bila hukumu ku mafumbo yako.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Niwe mugeni ku tamaa, ee Kristu, nipate maongezo ya rehema na usabitisho katika uzima wangu kwa muungano Fumbo zako Takatifu.

Mutakatifu kamili, ee Mzazi Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**

Mungu Mtakatifu. Mwana wa Mungu, unitakase kamili wakati ninapokaribia Fumbo zako kimungu. kwa maombezi ya Mama yako Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

## KONTAKION Sauti ya pili

Ee Kristu usinizarau kwa kuwa ninapokea mkate unapokuwa mwili wako na damu yako kimungu. Ee Rabi, mapokezi Fumbo hiyo, na ya woga isinihukumu mimi kaskini, lakini iwe kwangu furaha ya uzima wa milele.

**WIMBO 7**

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee. Kristu, hii Komonyo ya Fumbo ya uzima wa meilele iwe sasa kwangu Chemchem ya uzuri, mwangaza na uzima na upole na idumu ndani yangu kwa kwendelea katika fazila ya kimungu kusudi nikutukuze wewe mwema.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee, Mpenda wa binadamu, ninapokaribia sasa na oga, mapendo na ibada yako ku mafumbo yako ya uzima wa milele, uniokoe ku mateso ya adui, uhitaji na huzuni yote ili nikuimbie wewe mbarikiwa, Bwana Mungu wa Baba zetu.

Mutakatifu kamili, ee Mzazi Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**

Ewe, Mjaliwa na rehema kimungu kupita akili, umezaa Kristu Mwokozi, wewe uliye safi, mimi mtumishi wako mwovu nataka kukaribia sasa ku mafumbo Takatifu, unisafishe niwe safi kamili toka uchafu wa mwili na wa roho.

**WIMBO 8**

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee, Kristu, unistahilishe sasa mimi niliyepoteza tumaini lako, nisharikie mafumbo yako kimungu ya woga na Takatifu na kwa karamu yako ya mwisho.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ninakimbilia ku rehema yako, wewe mwema, ninakuita na oga: Uwe ndani yangu nami ndani yako kama ulivyoahidi. Kwani, tazama, mwamini katika rehema yako, ninakula mwili wako na ninakunya damu yako.

Mutakatifu kamili, ee Mzazi Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**

Nikipokea moto, natetemeka kwa kuungua kama mshumaa na nyasi: Ee Fumbo yenye kuogopesha: Ee Mungu wa huruma, namna gani nitaweza kupokea mwili wako na damu yako, mimi udongo na kuwa na uzima wa milele.

**WIMBO 9**

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Mwema tele ni Bwana: Onja na utasikia. Zamani alikuja jwetu na alijitoa mara moja mwenyewe katika zabibu kwa Baba, haishi kujitoa sababu ya kutakasa waale wenye kukomunika.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Ee Rabi wangu mjaliwa na huruma, nitakaswe kwa moyo na kwa mwili, ee Bwana, niangae, niokoke, niwe makayo yako kwa muungano wa Fumbo zako Takatifu, wakati ninapokupokea ndani yangu na Baba wa Roho.

Utukufu kwako, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

Mwili wako na damu yako heshimiwa iwe kwangu moto na mwangaza wengi kuchoma ulimwengu wa maovu na kuteketeza miiba ya tamaa zangu zenyi kuwaka ndani yangu ili nipate kwabudu umungu wako.

Mutakatifu kamili, ee Mzazi Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**

Ee, Bibi-Arusi wetu Mungu alichukuwa mwili kwa damu yako Takatifu. Kwa hii vizazi vinakuimba; na watu mengi wenye kusikia maana wanakusifu sababu wameona waziwazi ya kama huyu alichukua mwili kwako ni Bwana wa vitu vyote.

Mungu Mtakatifu. . . Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Utatu Mtakatifu. . . Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote Bwana hurumia *(mara tatu).* Baba yetu uliye mbinguni. . .

**ASUBUI SIKU YA KOMONYO TAKATIFU**

*Asubui mapema sema hii sala:*

Mungu Mutakatifu, mweza Mutakatifu, msiye kufa Mutakatifu, utuhurumie *(mara tatu).*

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Utatu Mutakatifu. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Baba yetu uliye mbinguni. . . Bwana hurumie (kumi na pili).
Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Njooni tumwinamie na tumsujudu Mungu Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Kristu Yeye Mungu Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumsujudu Yeye Kristu, aliye Mfalme na Mungu wetu.

**ZABURI 23**

Bwana ni mchungaji wangu; sitapungukiwa na kitu. Ananilalisha katika malisho ya majani mabichi; ananiongoza kando ya maji matulivu. Anarudisha nafsi yangu; ananiongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. Ndiyo, hata nikipita kati ya bonde la kivuli cha mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe ni pamoja nami; Gongo lako na fimbo yako zinanifariji. Unanitengenezea meza mbele ya adui zangu; Umenipakalia mafuta kichwani; kikombe changu kinafurika. Hakika wema na rehema zitanifuata siku zote za maisha yangu; na nitakaa nyumbani mwa Bwana milele.

**ZABURI 24**

Inchi na kujaa kwake ni mali ya Bwana; Dunia, nao wanaokaa ndani yake. Kwa maana ameweka misingi yake juu ya bahari, na kuisimamisha juu ya garika. Nani atakayepanda mulimani mwa Bwana? Na nani atakayesimama katika pahali pake patakatifu? Mtu aliye na mikono safi, na moyo mweupe; asiyenyanyua nafsi yake kwa uwongo, wala hakuapa kwa hila. Yeye atapokea baraka kwa Bwana, na haki kwa Mungu wa wokovu wake. Hiki ni kizazi chao wanaomutafuta, wanaotafuta uso wako, ee Mungu wa Yakobo. Nyanyueni vichwa vyetu, ee ninyi malango; na munyanyuliwe, ninyi milango ya milele; na mfalme wa utukufu ataingia. Nani aliye mfalme wa utukufu? Bwana mwenye nguvu na uwezo. Bwana mwenye uwezo vitani. Nyanyulisheni vichwa vyenu, ee ninyi malango, ndiyo, muvinyanyue, ninyi milango ya milele, na mfalme wa utukufu ataingia, Ni nani huyu mfalme wa utukufu? Bwana ya majeshi, yeye ni Mfalme wa utukufu. Sela.

**ZABURI 116. 10-19**

Ninaamini, kwa maana nitasema: Niliteswa sana: Nikasema katika haraka yangu: Watu wote ni wawongo. Nitamupa Bwana nini kwa ukarimu wake wote alionitendea? Nitapokea kikombe cha wokovu, na kuitia jina la Bwana. Nitalipa Bwana naziri zangu, ndiyo, mbele ya watu wake wote. Ni ya damani machoni mwa Bwana mauti ya watakatifu wake. Ee Bwana, kweli mimi ni mtumishi wako: Mimi ni mtumishi wako, mwana wa kijakazi chako; umefungua vifungo vyangu. Nitakutolea zabihu ya kushukuru, na kuita jina la Bwana. Nitalipa naziri zangu kwa Bwana, ndiyo, mbele ya watu wake wote; katika viwanja vya nyumba ya Bwana, katikati yako, ee Yerusalema. Musifu Bwana.

Utukufu. . . Sasa. . . Alliluia *(mara tatu).* Utukufu kwako, ee Mungu. Bwana hurumia *(mara tatu).*

*Kiisha anza kusoma nyimbo zifuatavyo: Sauti ya sita*

Zarau wovu wangu, ee Mungu wewe uliyezaliwa kwa Bikira, takasa roho yangu, ulifanye hekalu ya mwili na damu yako kuwa takatifu, kwa hasira yako usinitupe mbali ya uso wako, wewe mwenyi huruma usiyokadirikana kisilani mbele ya uso wako, wewe uliyekuwa na huruma yasiyo kipimo.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Nitasubutu je, mimi mwovu, kujongea mafumbo yako Takatifu? Nikijaribu kujongea pamoja na wenye kustahili nguo yangu itanitoa maana haiko ya arusi. Na nitavuta mbegu ya hukumu kwa moyoni mwangu mtenda zambi nyingi. Ee Bwana, takasa roho yangu yenyi kuchafuka na uniponye kwani wewe ni mwema na Mpenda wanadamu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. **THEOTOKION**

Ee Mama wa Mungu, zambi zangu zinapita wingiu; ninakimbilia kwako Mtakatifu kwa kutafuta wokovu. Angalia moyo wangu wenye kushikwa na ugonjwa na uniombee kwa mwana wako. Mungu wetu, anisamehe mabaya yote niliofanya kwako, ewe Mbarikiwa.

*Paka siku kubwa ya kazi Ine Takatifu wanaongeza kusoma: Sauti ya Mnane.*

Mitume watukufu waliangazwa, wakati walioshwa miguu ku karamu ya mwisho, kwa ile wakati Yudasi kafiri, kwa tamaa yake mbaya, akaingia gizani na akakutoa wewe mwamuzi wa kweli, kwa mwamuzi waovu. Ee mnyanganyi, tazama ni kwa sababu ya hii amejitundika: Epuka tamaa iliyomuongoza kutendee Rabo wake maovu ya hii namna. Ee Bwana mwema wa wote, utukufu kwako.

Bwana hurumia (Mara 40)

**NAMNA YA KUKARIBIA KOMUNYO TAKATIFU.**

**SIMEONI MFASIRI**

Ee Wewe menyi lujitayarisha kuwa kuonja mwili wa Bwana, karibia na woga kusudi usiungue: Ni moto. Kwa kunywa Damu ya ushirika, mbele ya upatano vema na wao walikukosea, kisha jongeo uonje chakula cha fumbo.

**INGINE VILEVILE**

Mbele ya kukomunika sadaka ya woga, mwili wa Rabi, wenye kuleta uzima, sala hivi namna yafuatayo na matetemeko:

**SALA 1 YA MTAKATIFU BAZILE MKUBWA**

Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, chemchem ya uzima na ya uzima usiyo kufa. Muumba wa ulimwengu unaoonekana na usiyoonekana. Mwana wa milele pamoja na Baba bila mwanzo na Wewe Mwenyewe usiye mwanzo: Wewe ambao katika ziada ya wema, ulikamata mwili, wewe ulisulubiwa na kuwekwa kaburini kwa ajili yetu sisi wasio shukrani na wapotevu ambao kwa ajili ya damu yako ulitupatanisha na hali yetu ya zambi, wewe mwenyewe. Mfalme wa milele, ulikubali majuto yangu, mimi mukosefu; inamisha sikio lako kwangu na usikie chochote ninapotaka kusema. Nilikosea mbingu na Wewe Mwenyewe na sistahili tena kunyanyua macho yangu juu kulio sifa yako, kwani nilikasirikisha wema wako nilipovunja amri zako na kukataa kutii amri zako. Lakini, ee Rabi, uko mvumilivu na mwenye huruma; tena wakati unapogonja ubadilisho wangu, haukuniacha kupotea na zambi zangu. Wewe, ee rafiki wa binadamu, uliyesema mwenyewe kwa kinywa cha manabii wako: Hakuna hata kamwe ginsi yangu mimi kuachilia mukosefu, lakini ninataka abadilike na awe hai, hautaki, ee Rabi, kupoteza kazi ya mikono yako na haukupenda uharibifu wa wanadamu, lakini unataka kama wote waokolewe na wafike kwa kujuwa ukweli. Tena mimi ninapokuwa mwovu, wa mbingu, wa dunia na wa maisha ya kidunia, mimi ninayetii kamili ku zambi na kuwa mtumwa wa tamaa zangu, mimi nilichafusha sura yako, nikuwapo lakini jambo la mkono wako na muumbwa wako, sikukati tumaini ya wokovu wangu, mimi maskini mzima, kwani mimi niko mtumaini katika rehema yako yasiyo mpaka na ninakukaribia. Unipokee basi, ee Kristu, rafiki wa wanadamu, sawa bibi mkosefu, mwivi, mtenda zambi na mtoto mpotevu na uniokoe ku zambi zangu zote. Wewe unaondoa zambi za dunia na kuponya magonjwa ya wanadamu, wewe unaoita na kutuliza wao wanaoteswa na wanaolemewa, wewe ulikuja kuwaita ku majuto, hapana wenye haki, lakini wakosefu, unitakase uchafu wa mwili na wa roho. Unifundishe kutenda vitendo vitakatifu katika oga yako. Ninapokua na ushahidi mwema wa zamiri, na ninapokea upaji wako takatifu, nitaungana na mwili na damu, utakuwa ndani yangu mkaaji na Baba na Roho Mtakatifu, ndiyo, ee Bwana Yesu Mungu wangu, ushiriki huo ku mistiri zako takatifu na zileta uhai zisiwe nami upatilivu wala hukumu na nisiwe munyonge wa moyo na wa mwili kwa kuyashariki bila ustahilivu. Lakini unipatie kuyapokea daima mpaka mwisho wa pumzi yangu vipaji vyako vitakatifu, bila kupatikana na upatilivu; uwe nami upasho wa Roho Mtakatifu, ukaristia wa mwisho ku uzima wa milele, uhakikisho unaokubaliwa mbele ya hukumu yako ya hofu, kusudi pamoja na wateule wako wote, niwe nami mshariki wa mali isiyo wovu uliotengenezea wao wanaokupenda. Bwana, uhimidiwe katikati yao milele na milele. Amina.

**SALA 2 YA MTAKATIFU BAZILE MKUBWA**

Ninajua, Bwana, ya kuwa ninakomunika nisio mstahilivu mwili wako Takatifu na Damu yako yenye bei, niko mukosefu ninakula na ninakunywa uhukumu yangu, ninapokosa kutambua Mwili na Damu yako, lakini ninapoamini ukarimu wako ninakujongea wewe uliyesema: Ye yote anayekula mwili na damu anakaa ndani yangu nami ndani yake. Unirehemu Bwana, usiniaibishe, mimi mukosefu, lakini unitendee kadiri ya rehema yako: Aina hiyo takatifu iwe nami matunzo, utakaso na mwangaza, ulinzi na wokovu, utakaso wa moyo na wa mwili wangu, ifukuze mbali nami sanamu na vitendo vyote vya shetani zinapojizoeza na roho yangu mpaka na maungu yangu yote; uniongezee kitumaini na mapendo kwangu, ilinde na kutengeneza uzima wangu, iniendeleshe mbele katika njia ya fazila na ukamilifu; nipate kutimiza amri zako na kushariki Roho yako Takatifu, iwe nami chakula changu cha uzima nitapoingia nacho katika uzima wa milele; iwe nami katazo mbele ya hukumu yako; isiwe nami maamzi ao hukumu. Amina.

**SALA 3 YA MTAKATIFU YOANNE KRISOSTOMO**

Ee Rabi Mungu wangu, ninajua ya kama sistahili uingie rohoni mwangu kwa sababu niko mtupu na mharibifu na ndani yangu hauna fasi nzuri wewe kustarehe kichwa chako. Lakini vile kwa sababu ya ajili yetu sisi ulishuka mbinguni na shuka sasa karibu na udogo wangu. Tena ulitaka kuwekwa katika pango na katika sanduku ya kulisha nyama bila sababu, uliingia ndani ya sanduku yakulisha nyama ya roho yangu mupiswa na ya mwili wangu mchafu. Ulipenda kuingia na kula pamoja na wakosefu ndani ya nyumba ya Simoni mukoma kubali kuingia ndani ya nyumba ya moyo wangu mimi mkoma na mkosefu. Haukutupa hata moja anafanana nami, mimi mkosefu, wakati alikujongee na kukugusa wala haukuchukia kinywa chake mchafu na laanifu wakati alikubusu, usichukie vilevile kinywa changu kichafu na laanifu sawasawa chake hata midomo yangu michafu na mikufuru na hata ulimi wangu mchafu pia. Lakini makala ya moto yaliyo katika Mwili wako Takatifu na Damu yenye bei yiwe nami utakaso, mwangaza na afya ya moyo na ya mwili wangu ili itulize makosa mengi mno na kunikinga kwa shetani; ifukuze zoezo zangu mbaya, izuie na kuharibu tamaa, kutimiza amri zako, kuzizidisha na neema yako ya kimungu na kuzikaribisha katika ufalme wako wa milele kwani, ee Mungu, nisikaribie karibu nawe na boka. Lakini na kitumaini katika wema wako nisikose nawe ushirikisho na nishikwe na mnyanganyi mbwa wa mwitu. Ninakuomba kwani uko Mtakatifu mmoja. Bwana, na utakase moyo, roho na mwili wangu, mafigo na matumbo yangu unifanye mpya kamili, tia oga wako katika maungu yangu na utakaso wako ukae ndani yangu. Uwe msaada na mkingaji wangu, kiongozi wa uzima na salama yangu, unifanye mstahilivu wa kuwa mkono wako wa kuume pamoja na Watakatifu wako kwa usimamizi na maombezi ya Mama wako bila doa na nguvu yasiyo mwili Takatifu inaokutumikia na kwa Watakatifu wote walikupendeza tangu mwanzo wa milele na milele. Amina.

**SALA 4 YALEYALE YA MTAKATIFU YOANNE KRISOSTOMO**

Ee Rabi na Bwana, sistahili uingie rohoni mwangu, kwa sababu unataka, sawa rafiki ya wanadamu, kukaa ndani yangu mimi ninapokukaribia na uhodari. Uamuru nifunguwe milango iliyo paka wewe peke uliumba kwa kuingia na mapendo yako imara. Utaingia na kwangaza mawazo yangu mabaya, ninasadiki kweli haukufukuza muke mtenda zambi aliyekuja kwako na machozi mbele yako, haukusukuma nyuma mkosefu anaotubu, wala haukumkatalia mwivi wakati walipotambua ufalme wako; ama haukumzarau aliyekuja kutubu haukumwacha, lakini wote waliyekuja kwako kutubu, uliwaweka fasi ya warafiki wako, wewe mbarikiwa pekee wakati wowote, sasa na milele bila mwisho. Amina.

**SALA 5 YALEYALE YA MTAKATIFU YOANNE KRISOSTOMO**

Bwana Yesu Kristu, unisafishe mimi mkosefu na mtumishi mwovu. Sahau na unisamehe makosa na zambi niliyokutukana nayo tangu utoto wangu mpaka siku ya leo na saa hii: Isipokuwa kwa akili ao kwa upiswa, kwa sauti kwa vitendo ao kwa mawazo, kwa zoezo ao maana yangu yote. Kwa maombezi ya yule aliyekuzaa bila mbegu. Bikira Maria Mama yako, yeye peke kitumaini chetu

kisichochanganyikwa, msaada na wokovu wangu; unirudishe mstahilivu nikomunike bila hukumu ku maisha yasiyo mwisho, yenye uzima na maumbo ya maondoleo ya zambi zangu, na uzima wa milele kwa utakaso, mwangaza, utunzo na afya ya moyo na mwili wangu kwa maondoleo na maangamizi ya mawazo yangu mabaya, ya kusudi na kwa mawazo yangu ya ngiza ililetwa na roho za ngiza na kali. Kwa kuwa kwako ni utawala, uwezo na sifa; Utukufu na ibada kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

**SALA 6 YA MTAKATIFU YOANNE DAMASCENI.**

Ee Rabi, Bwana wetu Yesu Kristu, Mungu wetu, wewe peke una uwezo wa kuondoa zambi, wewe rafiki wa wanadamu, unisamehe zambi zangu zote ninazofahamu na nisizofahamu, nistahili bila kuhukumiwa, niungane na mafumbo yako Matakatifu ya bumungu yenye kuleta uzima. Bila kuvuta azabu, masumbuko na kuongeza zambi zangu, nitakaswe na niwe rahani ya uzima wa ufalme utakayokuja, ukingo na msaada zitawanye wadui zangu na ziondoe zambi zangu nyingi. Kwa sababu uko Mungu Mwema, wa huruma na wa mapendo ya wanadamu na tunakushukuru na Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SALA 7 YA SIMEONI MUTHEOLOGO MUPYA**

Kwa midomo iliochafuka, kwa roho mubaya, kwa ulimi ulioambukizwa, kwa moyo muchafu, kamata sala, ee Kristu wangu, usinifukuze mbali nawe, kwa vitendo na mifano yangu mibaya, hata kwa ukosefu wangu wa haya, unisaidie niseme kwa uhodari, ee Kristu wangu, yote yaliyo ndani ya roho yangu, lakini ni vizuri zaidi unifundishe, yaliyo ya kutenda na yaliyo yakunena. Nilifanya zambi kuliko zile za mzinifu, ambaye aliposikia wapi unapoikala, alinunua manukato, alipofika akapakaa kwa uhodari, miguu yako. Kristu wangu, ya Rabi na ya Mungu wangu.

Kama vile haukumufukuze yule, aliyejikaribia kwa haraka kwa haraka. Pamoja nami mwana, usinifukuze mbali nawe, unipe miguu yako nitakayogusa na kuyabusu, na kwa mitoni mingi ya machozi, kama manukato ya bei mingi, nitakuja kwa uhodari kukupakaa. Kwa machozi yangu unisafishe mwana, unitakase, ee Bwana. Uniachilie ukosefu wangu; unipe rehema yako. Unapojua idadi ya zambi zangu, unajua madonda yangu; na unajua maumivu yangu; lakini unapojua imani yangu, unajua haraka yangu, na unasikia kite langu, bila kufichwa. Mungu wangu. Muumba wangu. Mwokozi wangu hata tone ya machozi, hata sehemu ya tone.

Kwa jambo la ugumu wangu, macho yako yaliona; kitabuni chako, hata zambi zangu zote nitakazo fanya, zinandikizwa. Angalia unyenyekevu wangu, unaona mchoko wangu, ee Bwana Mungu, uniachilie ukosefu wangu; ili roho yangu isafishwe, kwa hofu ya akili, na moyo nyenyekevu, nikamate kwa bila doa, siri zako takatifu, ambako atekukamata uzima na atekugeuzwa Mungu, yeyote atakayekula na atakaye kunywa, na roho ya ukweli. Kwani, ee Rabi wangu, ndivyo ulivyo sema, Yeye mwenye kula mwili wangu, na kunywa damu yangu, nami ndani yake, neno la Rabi Mungu wangu ni kweli japo lolote. Akamataye vipaji Takatifu na neema ya vitu kimbingu, habaki pekee lakini pamoja nawe, ee Kristu wangu, nuru ya Utatu Mtakatifu, yaletayo mwangaza duniani.

Basi ili nisibaki peke. Mbali nawe mwenye kutoa uzima, pumzi yangu, uzima wangu, furaha yangu, wokovu wa dunia, kwa hiyo ninakukaribia kama unanipoona na machozi na moyo wenye sikitiko ninakuomba unipe fidia ya makosa yangu, yaleta uzima na mistiri safi, kuyashariki bila kulaumu ili ibaki sawasawa ulivyosema, karibu nami mukosefu; ili nisipate pasipo neema yako yenye kudanganyika, kusudi nikamate mwenye udanganyi abembelezaye kwa kunikamata neno lako kimungu. Kwa hiyo ninakusujudia, na kwa uvuguto ninakulilia; sawasawa uliyemupokea mupotevu na kahaba aliyekukaribia, pamoja unipokee nami kahaba na mupotevu, ewe mwenye huruma, na moyo wenye sikitiko, ninapokukaribia hapa sasa.

Mwengine alifanya kosa kuliko mimi, na kufanya yaliyo mabaya, sawasawa niliotenda mimi. Lakini kwa hiyo ninajuwa mara ingine kuomba hakuna unene wa kosa, na idadi ya zambi kupita kwa Mungu wangu, wingi wa uvumilivu na mapendo ya wanadamu yasiyo na mwisho; lakini kwa mafuta ya pendeleo, ya watu wanaotubu kwa uvuguto unawasafisha na kuwaangarisha, na kuwasharikisha mwangaza yako, wenzi ya umungu wako. Unawaleteya neema yako mingi mno; na jambo hilo la

ajabu na la malaika, na akili ya binadamu. Unaposumulia na wale mara nyingi, sawa marafiki zako za kweli na mambo haya yote yananipatia uhodari. Na mambo haya yote yananipa mabaya Kristu, na ninapata uhodari wa neema ya utajiri wako, ya furaha na kutetemeka pamoja, ninakomunika moto yako, ninapokuwa majani na muujiza ya ajabu! Ninashikwa na baridi jinsi isiyoweza kusema sawasawa kijiti cha zamani kiliwaka lakini hakikuteketei. Basi, uniwe razi ya wazo langu, uniwe razi ya roho yangu, uniwie razi ya vipindi vya mwili wangu, ya roho na ya mwili wangu, ninakubusu kwa mazidisho, na ninakukuza wee Mungu wangu, sawa mhimidiwa kweli sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

**SALA 8 YA SIMEONI MFASIRI**

Ee Bwana, wewe peke mtakatifu na bila doa, uliye na rehema na mapendo kwa wanadamu, uliyechukua hali yetu nzima na damu yako takatifu na ya ubikira wa yule alikuzaa kwa usimamizi wa Roho Mtakatifu na kwa ukubali wa Baba wa milele. Kristu Yesu akili ya Mungu, amani yake na nguvu yake aliyependa kuongeza kujifanya mtu, mateso yako yenye uzima na ya ukombozi, msalaba, musumari, mukuki, kifo, ziharibu, tamaa mbaya inaouwa roho yangu. Wewe uliyetwalia ufalme wa shetani kwa maongezi yako mema na kukuza roho zangu chafu. Wewe, kwa ufufuko wako siku ya tatu, uliinua jiwe letu lililoanguka; nilianguka katika zambi, unishimamishe unipatie majuto, wakati uliopanda mbinguni, uliwapatia wanadamu maisha kuchukuliwa kwako juu na kuituza kwa makao yako mkono wa kuume wa Baba. Nistahili ku komonyo na kupata fazi mkono wa kuume kati ya wenye kuokoka. Kwa ukoo wa Roho Mtakatifu. Mfariji, ulishukuru mitume wako kwa chombo cha heshima, unifanye niwe makao mastahilivu ya kuja kwako. Wewe utakaokuja tena kuhukumu ulimwengu na uhaki wote, uniruhusu nami kuja mbele yako mwamzi na mwumba wangu. Kwa Baba yako na kwa Roho Mtakatifu. Mwema na Mpaji wa roho na uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SALA 9 YA YOANNE DAMASCENI**

Ninasimama mbele ya milango ya hekalu yako na mawazo mabaya yanaokataa kunitoka. Lakini wewe Kristu Mungu ulihakikisha mtoza ushuru aliyemhurumia mkanana moja aliyemfungulia mwivi milango ya mbinguni, unifungulie basi nami matunbo ya mapendo ya binadamu na unipokee nami ninakukaribia na kukugusa sawa yule mwanamke kahaba na mbawasiri, mmoja alipogusa kanzu yako: Na alipata sasa hivi kupona, na mwengine aliposhika miguu yako takatifu, aliondolewa zambi zake zote. Na vilevile nami mkosefu, wakati ninaposubutu kupokeya mwili wako kamili nisiteketezwe. Lakini unipokee sawa wale wawili na angazia makosa ya moyo wangu unaonguza uinamizi wa zambi kwa maombezi ya yule bila doa alikuzaa kwa nguvu ya mbinguni, kwa sababu uko mbarikiwa milele na milele.

**SALA 10 YA MTAKATIFU YOANNE KRISOSTOMO**

Nasadiki, ee Bwana, na naungama ya kama wewe kweli Kristu, Mwana wa Mungu mzima, ulikuja duniani kwa ajili ya kuokoa wenye zambi, ambao mimi ni wa kwanza. Nasadiki tena ya kama huu ni Mwili wako safi na hiyi ni Damu yako ya samani. Minakuomba: Unihurumie na unisamehe makosa yangu yakupenda na yasiyokupenda niliotenda kwa maneno, kwa matendo, kwa kujua ao bila kujua, tena niwe mstahilivu wakusharikia, bila hukumu, kubeba Mwili na Damu zako safi, juu ya maondoleo ya zambi zangu na sababu ya uzima wa milele. Amina.

*Wakati wa kukomunika ukipofika, wanasoma sala zifuatayo za Simeoni Mfasiri.*

**SALA 11 YA SIMEONI MFASIRI**

Angalia sasa najongea karibu ya Komonyo yako Takatifu, ee Mwumba wangu, usiniunguze ku ushariki huo. Sababu Wewe ni moto unaounguza wasiyostahili. Lakini unitakase ku aibu hiyi.

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku Karamu yako ya mwisho: Kwani sitafumbua siri zako kwa adui zako; sitakubusu sawa Yudasi, lakini sawa Munyanganyi, nakuungamia: Ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

Akionapo Damu Kimungu, atetemeke, ee Mwanadamu, kwa sababu ni makala ya moto ilunguzayo wasiostahilivu. Mwili Kimungu unageuzwa kimungu na unalisha, unatakasa na unalisha mawazo namna isiosikilizwa

Ee Kristu, kwa mapendo yako ulinipeleka ku furaha na kwa ulinzi wako ulinigeuza kuwa mtu mwengine: Choma zambi zangu kwa moto usiyo vyombo na kubali kunijaza na furaha zako, sababu nikiwa tele na furaha, nitasifu majio zako mawili, ee Wewe mjaliwa na wema.

Nitaingia je, mimi msiye stahili, katika ukuu wa watakatifu wako? Nikisubutu kwingia katika nyumba ya arusi, nguo langu litanitoa, maana hayuko ya arusi na nikifwatane, malaika watanifukuza. Bwana, safisha basi mataka ya moyo wangu na uniokoe, wewe mpenda wanadamu.

*Na pia Sala hii:*

Rabi, rafiki ya wanadamu, Bwana Yesu Kristu, Mungu wangu, vipaji vyako vitakatifu visiwe nami hukumu sababu ya maovu yangu: Lakini utakaso wa moyo na wa mwili na rahani ya uzima na ya ufalme wa milele. Ni vizuri kwangu kwa kumshika Mungu na kuweka tumaini la wokovu wangu katika Bwana.

*Na tena tunasoma hii:*

Ee Mwana wa Mungu, unipokee mimi leo ku Karamu yako. . . .

*Kila mara Bwana wetu Yesu Kristu anatustahiliha kupewa Mwili na Damu Yake, sisi tunapaswa kumushukuru.*

*Ttunasoma Ibada ya Shukrani kwa Mungu.*

*Somo la hii Ibada inafanyika mu Kanisa, ku mwisho wa Liturgia Takatifu, ao nyumbani mwetu, wakati tunarudi.*

## SHUKRANI YA NEEMA BAADA YA KOMONYO KIMUNGU

**SALA 1**

Unapokamata vizuri komonyo, siri hizi zinaleta uzima. Unisifu na unishukuru. Mkuu, na sema kwa rafla rohoni mwako na uvuguto Kimungu, (utukufu kwako, ee Mungu); *(mara tatu).*

Ninakushukuru, ee Bwana Mungu wangu kwa sababu haukunifukuze mimi mtenda zambi, lakini ulinistahilisha mimi mwovu, kwa kushariki kusiri zako takatifu za mbingu, lakini, wewe Rabi, rafiki wa wanadamu, uliyekufa na kufufuka kwa ajili yetu na uliyetupa siri za uzima kwa mema na utakaso wa moyo na wa mwili; fanya ili ziponye roho na mwili wangu, zifukuze adui yeyote, yangazie macho na roho yangu, zilete salama moyoni mwangu, kitumaini yasio haya, mapendo ya kweli, hekima kubwa, utii wa amri zako, uzindisho wa neema ya Mungu ndani yangu na upatanisho wa ufalme wako. Nitakumbuka siku zote neema yako uliyeweka katika utakaso wako, halafu sitaishi tena mimi mwenyewe, lakini na wewe Bwana na mkarimu wangu. Nikipoishi katika kitumaini ya uzima wa milele, nitafika halafu katika mapumziko yasiyo mwisho, kutapokuwapo furaha yasio mpaka, ya wao wataostajabu uzuri wa uso wako kukamwa, Kwa sababu uko kweli kweli yeye ambako tunaokwenda kuvuta pumzi na furaha yasio alama ya wao wanaokupenda, ee Kristu Mungu: viumbe vyote vinakuimbia milele na milele. Amina.

**SALA 2 YA MTAKATIFU BAZILE MKUBWA**

Ee Rabi, Kristu Mungu Mfalme wa karini na muumba wa vitu vyote, ninakushukuru kwa wema wako wote uliyenipatia na kwa Komonyo ya siri zako takatifu, ninakuomba, ee Mungu wangu

mwema na mpenda wanadamu, unilinde chini ya kivuli ya mabaya yako: Unifanyizie mpaka siku zangu za mwisho, nistahili kupokea mafumbo yako na ufahamu mwema kwa maondoleo ya zambi na ya uzima wa milele. Kwa sababu uko mkate wa uzima, chemchem takatifu, mgawanya wa mema na tunakutukuza pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

**SALA 3 YA SIMEONI MFASIRI**

Wewe uliyenipa kwa masudi, mwili wako mu chakula, wewe unaokua moto unaonguza waovu usinichome, ee Mwumba wangu; Lakini ingia katika maungu yangu, mu vingo vyangu vyote, mu utumbo wangu na mu roho yangu. Choma miiba ya makosa yangu. Safisha roho yangu, takasa mawazo yangu. Sabitisha viungo na mifupa yangu. Angazia vifungu vyangu tano vya mwili. Unilinde siku zote, unikinge na unilinde ku vitendo vyote ao ku sauti ya mauti juu ya roho yangu, unisafishe na unioshe, unipambe, unitengeneze, unifundishe na uniangaze. Unifanye makao ya roho moja tu, na isiokua makao ya zambi. Na, ninapokua nyumba yako ulipoingia kwa komonyo, roho mubaya na ya tamaa inikimbiye sawa moto, ninaomba usimamizi ya wale wote wanaotakaswa, majeshi ya wasio mauti, Mtangulizi wako, Mitume wako wa arifa, na hata kuliko vyote, Mama wako Mtakatifu na bila doa, Ee Kristu wangu, kubali kupokea na huruma maombi yao, na fanyizia Mwana wako kwa mtumishi wa mwangaza. Kwa sababu uko Mungu mwema Mtakasa wa pekee na mwangazaji wa mioyo zetu na wote tunakukuza namna inayofaa, wewe Mungu wetu na Rabi wetu. Amina.

**SALA 4**

Mwili wako na damu yako, ee Bwana Yesu Kristu, inipe uzima wa milele, na damu yako ya bei iwe nami maondoleo ya zambi. Na ukaristia huo unijalie furaha, afya na heri. Wakati wa ujio wako wa pili wenye hatari, unistahilishe, mimi mkosefu, kukaa kuume kwako kutukufu, kwa maombezi ya Mama wako Mtakatifu kabisa na ya Watakatifu wote. Amina.

**SALA 5 KWA BIKIRA MZAZI-MUNGU.**

Ee Malkia Mtakatifu kamili, Mama wa Mungu, Mwangaza wa moyo wangu uliotiliwa gizani, tumaini langu, tegemeo yangu, kimbilio langu; faraja na heri zangu, ninakushukuru pakunistahilisha mimi mwovu kwa kukumunika mwili takatifu na damu heshimiwa ya Mwana wako. Wewe uliyezaa nuru ya kweli, angazia macho ya kiroho ya moyo wangu. Wewe uliyezaa chemchem ya uzima wa milele, unirudishiye uzima, mimi niliyeuwawa na zambi. Wewe Mama wa Mungu wa huruma moyoni mwangu, unihurumie, huzunisha na sikitisha moyo wangu, unyenyekevu ndani ya mawazo yangu na ufikiri katika akili yangu. Unistahilishe mpaka siku yangu ya mwisho, kwa kupokea bila hukumu utakaso wa siri zako takatifu, kwa uponya wa moyo wangu na wa mwili wangu. Unipe machozi ya majuto na ya ungamo, ili nikuimbie na kukusifu siku zote za uzima wangu, (kwa sababu uko mbarikiwa na mjaliwa na utukufu milele. Amina). *(mara tatu).*

*Padri atasoma wimbo wa Simeoni.*

PADRI: Sasa, ee Rabi, uruhusu mtumishi wako aende kwa utulivu kama ulivyosema, kwa sababu macho yangu yameona wokovu wako ulioweka tayari mbele ya macho ya watu wote; Nuru ya kwangazia mataifa, na kuwa utukufu wa watu wako Israeli (Luka 2, 29).

SHEMASI ao MSOMAJI: Mungu Mutakatifu, Mweza Mutakatifu, Msiye kufa Mtakatifu, utuhurumie *(mara tatu).*

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Utatu Mtakatifu kamili utuhurumie. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Baba yetu uliye mbinguni . . .

## Apolitikion ya Mtakatifu Yoane Krisostomo.

### Sauti ya mnane

Kwa kinywa chako kama taa, neema imechuruzika na ulimwengu uliangaziwa, umevumbua hazina ya uadili, umetuonyesha ukuu wa unyenyekevu. Utafundisha kwa kinywa chako, ewe Baba

wetu Yoane Krisostome, utuombee kwa Bwana, Kristu Mungu, aokoe mioyo yetu. Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

**Kontakion Sauti ya sita**

Utukufu kwa Baba. . .

Kwa mbingu, umepokea neema kimungu, na kwa midomo yako wote tunafunza kumwabudu Mungu moja katika Utatu, ee Yoane Krisostomo, Mtakatifu mwenye heri, tunakusifu kwa ustahilivu, kwani hauishe kutufundisha, unatuangazia vitu takatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Sasa na siku zote. . .

Kwa maombezi ya Watakatifu wote na ya Mzazi-Mungu, ee Bwana, utupe amani yako na utuhurumie, kwani Wewe peke yako mwenye huruma.

Bwana hurumia *(kumi na pili).* Uliye wa thamani. . . Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Kwa jina la Bwana, Padri mtakatifu, bariki.

*Padri atafanya kuaga.*

Utukufu kwako, ee Mungu, matumaini yetu, utukufu kwako.

Uliye umefufuka katika wafu Kristu Mungu wetu wa kweli, kwa maombezi ya Mama wako Mtakatifu asiye na doa wala na lawama kamili. Kwa maombezi ya Yoane Nabii, Mtangulizi, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu, ya Mitume Watakatifu, Watukufu, Washindaji wazuri, ya Wapadri wetu Watawa na wabebaji-Mungu, ya Yoakimu na Anna Mababu-Mungu, Watakatifu, na wenye haki, hata ya Watakatifu wote, utuhurumie, ukatuokoe sawa Mungu Mwema, marahimu na mpenda-wanadamu.

Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

MSOMAJI: Amina.

*Kama hii siku ilifanyika Liturgia ya Mtakatifu Basile, somo la Apolitikion yake ni hii:*

Apolitikion. Sauti ya kwanza

Utume wako umetangaziwa duniani kote, na neno lako, limepokelewa ulimwengu kote. Katika hii ulifundisha ukweli wa umungu, ulifasiri hali ya wanadamu na ulitengeneza mwenendo wa wafu; Ee Baba Mtakatifu Bazile, mkubwa kwa jina la ufalme, mumuombe Kristu Mungu wetu aokoe roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Kontakion. Sauti ya Ine.

Juu ya Kanisa ulionekana kama msingi imara, utafindisha kila mutu Ubwana wenyi kufichwa na ukautia muhuri wa mafundisho Yako, ee Basile Mtukufu, wewe mwenyi kufumbua mbingu.

Sasa na siku zote. . .

Kwa maombezi ya Watakatifu wote na ya Mzazi-Mungu, ee Bwana, utupe amani yako na utuhurumie kwani Wewe peke yako mwenye huruma.

*Kisha soma*:

Kanisa ilionekana kuwa mbingu ya mwangaza mingi na inaangazia waaminifu; kwa hii na sisi tunasimama na tunapaza sauti na kusema; ee Bwana sabitisha hii nyumba.

Imara ya wenye kuamini, ni wewe, Bwana, na sabitisha Eklezya yako, uliyopata kwa damu yako heshimiwa.

Makumbusho milele ya Wenye heri bila kusahabu Wayengaji ya hii Kanisa Takatifu.

Kwa maombezi ya Mapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

# SALA YA KANUNI YA KUSIHI KIDOGOKWA BIKIRA MARIA MZAZI-MUNGU MBARIKIWA KAMILI.

**( Paraklisis Ndogo)**

*Kanuni Kidogo ya Mzazi-Mungu ni Sala ya mapendo ya waaminifu kwa Mzazi Mungu Bikira Maria.*

*Tunaweza kuimba ao kuisoma wakati wa mateso na taabu ya roho na mwili yetu yetu.*

*Kwa hivi, tunaweza kuiimba ao kuisoma saa yote tunapenda.*

PADRI: Abartikiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.
MSOMAJI. Amina.

**Zaburi 142**

Sikia maombi yangu, ee Bwana, usikilize kusihi kwangu; katika uaminifu wako unijibu, katika haki yako. Usihukumu mutumishi wako; maana machoni mwako hakuna mutu aliye hai atahesabiwa haki. Maana adui amefuata nafsi yangu; amepiga uzima wangu chini hata udongo. Amenikalisha katika pahali pa giza, kama wale waliokufa zamani. Kwa hivi roho yangu imezimia ndani yangu; Moyo wangu ndani yangu ni ukiwa. Ninakumbuka siku za kale; ninafikili matendo yako yote; ninawaza kazi ya mikono yako. Ninakunyoshea mikono yangu; nafsi yangu inaona kiu kwa wewe, kama inchi inayochoka. Fanya mbio kwa kunijibu, ee Bwana; roho yangu inazimia; usinifichie uso wako; nisiwe kama wao wanaoshuka shimoni. Unifanye kusikia wema wako asubui; kwa maana ninakutumainia wewe; unijulishe njia nitakayoikwenda; kwa maana ninakunyanyulia nafsi yangu. Uniponyeshe, ee Bwana, na adui zangu, ninakukimbilia unifiche. Unifundishe kufanya mapenzi yako; kwa maana wewe ndiwe Mungu wangu; Roho yako ni mwema; uniongoze katika inchi ya haki. Unipatize uzima, ee Bwana, kwa ajili ya jina lako; kwa haki yako utoe nafsi yangu katika taabu. Na kwa wema wako ukatilie mbali adui zangu, na kuwaharibu wote wanaotesa nafsi yangu; kwa maana mimi ni mutumishi wako.

*Kisha tunaimba mara Ine:*

Bwana ndiwe Mungu naye amefunuliwa kwetu, abarikiwe yeye ajaye kwa jina la Bwana.
Kitwo: Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni Mwema, kwa maana huruma yake ni ya milele.
Bwana ndiwe Mungu. . .
Mataifa yote walinizunguka, kwa jina la Bwana naliwakatilia mbali.
Bwana ndiwe Mungu. . .
Mtendo huu mtendo wa Bwana, nao ni ajabu machoni mwetu.
Bwana ndiwe Mungu. . .

**WIMBO Sauti ya Ine**

Tukimbilie sasa kwa Muzazi-Mungu, sisi wenye zambi na kupondwa na tusujudu, tukiita kwa kutubu toka roho: Bibi Malkia saidia, utuhurumie, fanya mbio tunapotea, kwa wingi wa makosa. Usifukuze watumishi wako kwa mikono mitupu. Kwani tulikupata, wewe peke yako matumaini.
Utukufu kwa Baba. . . Mara ingine hii mwimbo ya yulu.
Sasa na siku zote. . .

Sisi tusiyostahili hatutanyamaza, kusema kamwe uwezo wako ee Muzazi-Mungu. Kama wewe hungepatamisha kwanza, nani angetuokoa toka hatari mingi? Nani angetuchunga huru,

mupaka sasa? Hatutaondoka mbali nawe, ee Bibi Malkia, kwani unaokoa daima watumishi wako toka mateso.

*Tunasoma: Zaburi 50 (51).*

*Kisha hii Zaburi, tunaanza kuimba hii Kanuni:*

## ODE 1 Sauti ya Mnane

Irmosi:

Israeli akipita Baharini, kama inchi kavu, na akikimbia ubaya wa wamisri, aliita: tuimbie. Mukombozi na Mungu wetu.

**WIMBO**

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Nikiushiikwa na majaribu mingi, ninakimbilia kwako, kutafuta wokovu. Ee Mama wa Neno na Bikira, uniokoe toka masumbuko na mateso.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Mashambulio ya mateso yananitikisa, yakijaza nafsi yangu, kwa muchoko mingi. Binti bila doa utulize, na amani ya Mwana na Mungu wako.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Ninakusihi ee Bikira uliyezaa. Mwokozi na Mungu, kusudi unikomboe toka mateso. Kwani sasa nikikukimbilia, ninanyanyua nafsi na mawazo.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Ninapata ugonjwa kwa mwili na roho. Ee Muzazi Mungu peke, unistahilishe nipate, kupona na shuruli yako, kwani uko Muzazi wa Mungu Mwema.

## ODE 3

**Irmosi.**

Ee Bwana Mjengaji, wa anga ya mbinguni, na Mujengazi wa Kanisa, unisimamishe, mapendoni mwako, utimilifu wa tamaa, msaada wa waaminifu, peke yako Mupenda-wanadamu.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Bikira Muzazi-Mungu, ninakuweka mulinzi na kivuli, cha uzima wangu, uniongoze kwa kivuko chako, kwani uko shina ya wema, msaada wa waaminifu, peke yako musifiwa kamili.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Ninakusihi ee Bikira, usambaze mutetemeko wa roho, na kizunguzungu cha muchoko wangu. Bibi arusi ya Mungu, na peke yako bila doa, ulichukua mimba ya Kristu, mukubwa wa utulivu.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Ukizaa mufazili, shina la uzuri tosha utajiri, wa wema kwa wote. Unaweza kutenda yote, kwani ulichukua mimba, ya Kristu Mwenyezi, ewe uliyeitwa heri na Mungu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Unisaidie Bikira, kwani ninajaribiwa, na magonjwa ya nguvu, na mateso ya ugonjwa. Maana ninakujua, ewe bila doa kamili, sawa hazina ya dawa, isiyomalizika.

Ee Muzazi-Mungu okoa, watumishi wako kwa hatari, maana kisha Mungu wote tunakukimbilia, sawa Mulinzi na ukuta usiyobomolewa.

Tazama kwa fazili. Muzazi-Mungu Musifiwa-kamili, katika taabu ya mwili wangu, na ponyesha maumivu ya nafsi yangu.

PADRI: Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba utusikia na ukatuhurumie.

Waimaji: Bwana hurumia *(mara tatu).*

PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Wakristu Waorthodoksi wote.

Waimaji: Bwana hurumia *(mara tatu).*

PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Askofu Mkubwa wetu (jina lake).

Waimaji: Bwana hurumia *(mara tatu).*

PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Mapadri wetu na kwa ndugu wetu wote katika Kristu.

Waimaji: Bwana hurumia *(mara tatu).*

PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya kupata rehema, uzima, amani, afya, wokovu, ulinzi, usamehe na ondoleo ya zambi za watumishi wa Mungu, wadini wetu na Wakristu Waorthodoksi ambao wanakaamo na na wanakutana katika muji huu (Monasteri ao Mission, Parokia) wawakili na wapotani wa Hekalu hii Takatifu na ya watumishi wa Mungu. . .

*Sasa padri anasoma majina ya wahai.*

WAIMBAJI: Bwana hurumia *(mara tatu).*

PADRI: Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu wa huruma na mpenda-wanadamu na kwako tunautoa utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

MSOMAJI: Amina.

**KATHISMA Sauti ya mbili**

Upatanisho wa juhudi na ukuta wa ushindi, chemchem ya rehema, kimbilio ya watu. Bibi-Malkia Muzazi-Mungu, tunakuita daima: Utangulie kutukomboa toka hatari, uliyetunza upesi peke yako.

**ODE 4**

Irmosi.

Nikasikia, ee Bwana, siri ya ikonomia yako, nilifahamu kazi zako, na nilitukuza umungu wako.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Tuliza sikitiko ya tamaa, na mawimbi ya makosa yangu, ewe Bibi-Arusi ya Mungu, uliyezaa Bwana Mwongozi.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Wakati ninapokuita, unipe kilindi cha wema wako, uliyechukua mimba ya Mwokozi, wa wote wanaokuimbia.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Tukipata zawadi yako, ee safi tunaimba wimbo wa ushukuru, sisi tunaokujua, ya kama uko Muzazi-Mungu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Sisi tuliokupokea, Musifiwa-kamili kama matumaini, musaada na ukuta ya wokovu, tunakombolewa toka taabu yote.

## ODE 5

Irmosi.

Utuangaze, kwa amri yako ee Bwana, na kwa mukono yako munyanguliwa, utupe amani yako, ee Mupenda-wanadamu.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Jaza ee Safi, moyo wangu kwa furaha, ukileta shangwe yako bila doa, uliyezaa shina la furaha.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Utukomboe, toka hatari, ee Muzazi-Mungu Safi, uliyezaa Mukombozi wa milele, na Amani inayopita akili zote.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Bibi-Arusi ya Mungu, sambaza kungu ya makosa yangu, kwa mwangaza wa nuru yako, uliyezaa Nuru kimungu, kilichokuwa tangu milele.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Safi ponyesha, ugonjwa wa tamaa yangu, ukinistahilisha kupata tunzo lako, na unipe afya, kwa upatanisho wako.

## ODE 6

Irmosi.

Ninamwanga, mashitaki yangu mbele ya Bwana, ninamwonyesha taabu yangu, maana nafsi yangu ilijazwa na ubaya, na uzima wangu unakaribia Hadeze, na ninakusihi kama Yuna: Mungu wangu, unitoshe toka uharibifu.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu utuokoe.

Bikira, sihi Bwana na Mwana wako, aliyeokoa hali yangu iliyokamatwa, kwa mauti na uharibifu, akijitoa kwa mauti, kusudi aniponyeshe, toka uovu wa adui.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Ninakujua, sawa mulinzi wa uzima, na muchunga wa imara ee Bikira, ukisambaza wingi wa majaribu, na ukifukuza nguvu ya shetani, Na kusihi daima uniponyeshe toka uharibifu wa tamaa yangu.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Tulikupata, kama ukuta wa kimbilio, na wokovu timilifu wa nafsi yetu, na tulizo kwa taabu ee Binti, na tunashangilia kwa nuru yako daima. Bibi Malkia sasa utuokoe, toka mateso na hatari.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Ninalala, sawa mugonjwa kitandani, na hakuna tunzo mwilini mwangu. Lakini ewe ulichukua mimba ya Mungu, na Mwokozi wa dunia na muponya magonjwa. Ninakusihi ewe Mwema, unitoshe toka magonjwa.

Muzazi Mungu okoa, watumishi wako kwa hatari, maana kisha Mungu wote tunakukimbilia, sawa mulinzi na ukuta usiyobomolewa.

Bikira bila uchafu, uliyezaa Neno kwa namna isiyosemwa, katika siku ya mwisho, umusihi, kwani wewe uko na uhodari ya umama.

## KONTAKION Sauti ya Mbili.

Ee Mulinzi usiyepatisha wakristu haya, na mupatanishi wa Muumba usiyeweza kubadilika, usizarau sauti ya kusihi ya wenye-zambi. Lakini fika kama mwema, kwa kutusaidia sisi, tunaokuita na imani: Ujiharikishe kwa upatanisho, na ukimbie kwa kutuomba, ewe Muzazi-Mungu unayelinda, wanaokuheshimu daima.

*Kisha tunaimba Antifonon ya kwanza ya Daraja (Anavathmi)*
Sauti ya Ine

Toka ujana wangu, tamaa mbaya mingi inanigombanisha. Lakini ewe Mwokozi wangu, unilinde na uniokoe *(Mara mbili)*

Enyi muliochukia Sayuni, mupate haya toka Bwana. Kwani kama majani mbele ya moto, mutakuwa wakikauka *(Mara mbili).*

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na Kwa Roho Mutakatifu.
Katika Roho Mutakatifu, kila nafsi inakuwa hai, na kwa usafisho inanyanyuliwa, inaangazwa, katika Utatu Umoja, kwa siri Takatifu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
Katika Roho Mutakatifu, maji ya neema inayotelemuka inatoka, ikinywesha kiumbe kiote, kusudi kiwe na uzima.

**PROKIMENON**

Nitakumbuka jina lako, katika vizazi vyote *(mara tatu).*

Shairi:
Sikiliza, ee Binti, na angalia, na tega sikio lako, sahau vilevile watu wako mwenyewe, na nyumba ya Baba yako, hivi Mufalme atatamani uzuri wako.

## EVANGELIO TAKATIFU

PADRI: Tumusihi Bwana Mungu wetu atustahilishe kusikiliza Evangelio Takatifu

MSOMAJI: Bwana hurumia *(mara tatu).*
PADRI: Hekima. Inukeni, tusikilize Evangelio Takatifu. Amani kwa wote.
MSOMAJI: Na kwa roho yako.
PADRI: Somo la Evangelio Takatifu limeloandikwa na Luka. Tusikilize.
MSOMAJI: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

*Evangelio Takatifu katika Luka, Sura I, mashairi 39-49 na 56).*

Maria akaondoka siku hizi, akakwenda katika inchi ya vilima, kwa haraka hata muji mumoja wa Yudea. Akaingia katika nyumba ya Zakaria, akasalimu Elisabeti. Wakati Elisabeti aliposikia salamu ya Maria, mutoto akaruka ndani ya tumbo lake; Elisabeti akajazwa Roho Mutakatifu, akapaza sauti yake kwa nguvu, akasema: Umebarikiwa wewe katika wanawake, na uzao wa tumbo lako umebarikiwa. Neno hili limetoka wapi, mama ya Bwana wangu anakuja kwangu?

Kwani tazama, sauti ya salamu yako ilipoingia masikio yangu, mutoto aliruka kwa furaha ndani ya tumbo yangu. Heri yeye aliyesadiki kwani maneno haya aliyoyasema Bwana yatatimizwa. Maria akasema: Moyo wangu unasifu Bwana na roho yangu imefurahia Mungu Mwokozi wangu. Maana ametazama unyenyekevu wa mujakazi wake, kwani tazamatangu leo vizazi vyote wataniita heri. Maana Yeye Mwenye nguvu amenitendea matendo makubwa, na jina lake ni takatifu. Maria akakaa naye kadiri ya miezi mitatu, akarudi kwa nyumba yake.

WAIMBAJI: Utukufu kwako, ee Bwana, utukufu kwako.

Sauti ya mbili

WAIMBAJI: Utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Baba. Neno Roho. Utatu katika Umoja, uzime wingi wa maovu wangu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Kwa upatanisho ya Mzazi-Mungu, ee Murehemu, uzime wingi wa maovu wangu.

Shairi: Unirehemu, ee Mungu Murehemu, sawasawa na wema wako, sawasawa na wingi wa rehema zako, uzime makosa yangu.

## PROSOMION: Sauti ya Sita

Usinitumainie nichungwe na mutu, lakini Bibi Malkia, pokea kusihi kwa mutumishi wako. Taabu inanipata, siweze kuvumilia, mishale ya shetani, sina kivuli, wala kimbilio, mimi maskini. Nagombanishwa pande zote, sina mufariji ila wewe, Bibi Malkia wa dunia, matumaini na mulinzi wa waaminifu, usizarau kusihi kwangu, unifanyie vilivyofaa.

Hakuna mutu aliyekimbilia kwako na kutoka mwenyehaya, ee Bikira Muzazi-Mungu. Lakini anaomba neema, na anapata zawadi, kwa ajili ya vilivyo faa alivyoomba.

Geuko ya wenye-taabu, na uponyesho wa wagonjwa, uko Bikira Muzazi-Mungu. Okoe muji na taifa, Amani kwa wapigani, utulivu wa wateswa, peke yako mulinzi wa waminifu.

PADRI. Ee Mungu uwaokoe watu wako ukaubarikie urizi wako. Agua dunia yako kwa huruma na rehema; paza pempe ya wakristu waorthodoksi, ukakunjua juu yetu mafazili yako tele; kwa ajili ya maombezi ya Maria Bibi yetu msiye na doa. Mzazi-Mungu na Bikira daima. Kwa nguvu ya Msalaba mheshimiwa na tukufu. Kwa matunzo ya majeshi yaheshimiwa ya mbinguni yaliyo bila mwili. Kwa maombi ya Yoane Mtangulizi, Mbatizaji, Nabii, Mtukufu na Muheshimiwa. Ya Mitume Watakatifu, Watukufu na Wasifiwa. Ya Wapadri wetu ambao katika Watakatifu na Waaskofu na Walimu Wakubwa, Bazile Mkubwa, Grigori Mutheologo, Yoane Krisostomo, Athanasie na Kirilli, Yoane Mrahimu, wapatriarka wa Aleksandria, Nikola wa Mira, Spirido Askofu Trimithunta wa muujiza, ya Mashahidi Watakatifu watukufu na washindaji wazuri; ya wapadri Watawa na Wabebaji-Mungu; ya Mashahidi Watakatifu watukufu wakubwa, ya Yeorghi Mumebaji ya ushindi (Mtropeoforo), Dimitri mwenye kutosha manukato (Mirovliti), Theodoro Mukubwa wa askari na Theodoro Jemadari (Mstratilati); ya Mababu-Mungu Watakatifu na wenye haki Yoakimu na Anna; ya Mtakatifu *(anataja jina na majina ya kujulisha mtakatifu wa siku ile*) aliye tunakumbuka (tunamukumbuka) leo hata na Watakatifu wako wote pamoja, Tunakusihi, ee Bwana, uliye peke yako na huruma kubwa, usikie sisi watu wenye zambi tukikuomba na ukatuhurumie.

MSOMAJI: Bwana, hurumia *(mara 12).*

PADRI: Kwa kurehemu, na huruma, na upendo-wanadamu wa Mwana wako wa pekee, pamoja naye Uhimidiwa, pamoja na Roho wako Mtakatifu kamili, Mwema, Mpaji-uhai, sasa na siku zote, hata milele na milele.

MSOMAJI: Amina.

## ODE 7

Irmosi.

Watoto toka Yudea, waliofika Babyloni zamani, kwa imani ya Utatu, walishinda moto ya tanuru wakiimba: Mungu wa Mababu wetu, uko Mubarikiwa.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Mwokozi ukitaka, kutegemeza wokovu wetu, ulikaa duniani, tumboni mwa Bikira, ukamufanya kuwa Mulinzi wetu, Mungu wa Mababu wetu, uko mubarikiwa.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Mama Safi umusihi, kwa Mupenda-rehema uliyemuzaa, ili atuponyeshe, toka makosa na uchafu, tunaoita kwa imani: Mungu wa Mababu wetu, uko Mubarikiwa.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.

Ulifanya Muzazi wako, hazina ya wokovu chemchem ya kutokuharibika, mnara wa imara, mulango wa kitubio, kwa sisi tunaokuita: Mungu wa Mababu wetu, uko Mubarikiwa.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Muzazi-Mungu utustahilishe, tunaokaribia kivulini mwako kimungu, kusudi tuponyeshwe toka ugonjwa wa mwili, na wa roho zetu, uliyezaa Mwokozi kwa ajili yetu.

## ODE 8

Irmosi.

Mumwimbie, mufalme wa mbinguni, aliyeimbiwa na Majeshi ya Malaika, na mumutukuze, katika milele yote.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Bikira Binti, usituzarau sisi tunaohitaji, msaada wako tukikuimbia, na tukitukuza katika milele yote.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Ewe Bikira, unaanga dawa mingi kwa sisi, tukikuimbia na kutukuza, kwa imani uzazi wako usiyosemwa.

Tunabarikia Baba. Mwana na Roho Mtakatifu, tunamuimba Bwana.

Ewe Bikira, unaponyesha wagonjwa wa roho zangu, na maumivu ya mwili wangu, ili nikusifu, Mujaliwa na neema.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Ewe Bikira, unafukuza mashambulio wa majaribu, na vita ya tamaa mbaya. Kwa hii tunakuimbia, katika milele yote.

## ODE 9

Irmosi.

Sisi tunakushukuru, Muzazi-Mungu kweli, tuliookolewa kwa njia yako, tukikutukuza pamoja na Malaika.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi Mungu, utuokoe.

Bikira usikatae, mutetemuko wa machozi, ukichukua mimba ya Kristu, aliyepanguza machozi toka kila sura.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Ujaze moyo wangu, kwa furaha ee Bikira, ukipokea utimilifu wafuraha, ukazimisha sikitiko ya zambi.

Mutakatifu kamili, ee Muzazi-Mungu, utuokoe.

Kivuko na Mulinzi, wa wanaokukimbilia, uwe Bikira na ukuta wa imara, makimbilio na kivuli na shangwe.

Utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Bikira utuangaze, kwa nuru yako kwetu, ukisambaza giza ya ujinga, tunaokuheshimu sawa Muzazi-Mungu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Nikizarauliwa, kwa pahali ya mateso, na ugonjwa. Ewe Bikira, uniponyeshe, unigeuze, toka magonjwa kwa afya.

## MATUKUZO (Megalinaria)

Ni wajibu kweli, kukuita, ee Muzazi-Mungu, mwenyi heri daima na usiye na doa tena Mama wa Mungu wetu. Uliye wa damani kuwashinda wa Keruvim, uliye na utukufu, kuwapita bila kiasi wa Serafim, uliye ukimuzaa Mungu Neno, umebaki bila kukuharibu, uliye Muzazi-Mungu kweli, tunakutukuza wewe.

Uliye na urefu kuwashinda na mbinguni, uliye na usafi kupita bila mwangaza, wajua uliye ukitukomboa toka mafingo, unayekuwa Bibi Malkia ya dunia, tunakuheshimu kwa nyimbo.

Kwa sababu ya zambi zangu mingi, mwili na nafsi yangu yanapata ugonjwa. Ninakimbilia kwako, Mujaliwa na neema, unisaidie matumaini, ya wasiotumainia.

Bibi Malkia na Mama wa Mukombozi, pokea maombi, ya watumishi wako wasiostahili, ili upatanishe kwa Muzaliwa kwako, Bibi Malkia wa dunia, uwe mupatanishi.

Kwa nia tayari na kwa furaha, tunakuimbia sasa, ewe Musifiwa kamili, Mzazi-Mungu sihi, pamoja na Mutangulizi, na watakatifu wote, kwa kutuhurumie.

Bubu ni midomo ya watu, wasioheshimu na wasioabudu mufano wako, iliyo muheshimiwa, iliyosemwa Mwongozi, iliyochorua kwa Mutume, Luka Mutakatifu.

Unisamehe mimi muzarauliwa, maana nisijue, makimbilio ingine ila wewe, nimejaliwa na zambi, unihurumie, ewe peke yako matumaini ya wakristu.

TUKUZO KATIKA SIKU YA KWANZA

Kujeni enyi waaminifu wote, tuwasifu nyota mbili, wakubwa nawaangaza, Mikaeli Mukubwa na Gavrieli Kimungu, Wajemadari wawili wa Mungu mwenyezi.

TUKUZO KATIKA SIKU YA PILI

Mutangulizi wa Bwana na Mubatizaji, bakuli mbele ya jua, nyota ya asubui, kwa mwangaza wako, angaza nafsi yangu, nyonge na kipofu kwa tamaa mbaya.

TUKUZO KATIKA SIKU YA TATU NA YA TANO

Naimba usulubisho wako, ee Mwema, naimba mateso yako, na kusujudu maziko yako, tete, misumari, mukuki, sifongo, naisujudu yote, Mwokozi Muvumilivu.

MATUKUZO KATIKA SIKU YA INE

Tunasifu kwa nyimbo Petro, Pavlo, Marko, Luka, Filippo, Matayo, Yoanne, Simona na Tomasi, Andrea Mutukuzwa, pamoja na Yakovo, na Bartolomeo.

Sisi wote tumusifu Mwierarkha, wa maajabu, na Musaidizi asiyeshindwa, katika lazima, Muchungazi Mutakatifu, padri wa Bwana, Nikolao Mukubwa.

TUKUZO KATIKA SIKU YA POSHO

Kwa maombi ya Mitume yako, ya Manabii, ya Mashahidi, ya Waierarkha na ya Watawa, ewe Murehemu na Mwema-Kamili, leta upumuziko kwa nafsi uliopokea.

TUKUZO KATIKA MWISHO

Majeshi yote ya Malaika. Mutangulizi wa Bwana. Mitume Kumi na mbili. Watakatifu wote pamoja na Muzazi-Mungu, mupatanishe kwa ajili, ya wokovu wetu.

MSOMAJI: Mungu Mutakatifu. Mweza Mutakatifu. Musiye kufa Mutakatifu. utuhurumia. *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Utatu Mutakatifu. . . Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . Bwana hurumia *(mara tatu).*

Baba yetu uliye mbinguni. . .

PADRI: Kwa kuwa. . .

**WIMBO Sauti ya mbili**

WAIMBAJI: Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwa kuwa sisi watu wenye zambi, hatuna teto yoyote kukuileta, ila ombi huu tunakutolea kwako, uliye Rabi, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Ee Bwana, utuhurumie, kwa kuwa tunategemea kwako. Usituazibu sana, wala kuzikumbuka zambi zetu. Lakini hata sasa utangalie, kama mwenye huruma, ukatuokoe na maadui wetu. Kwa kuwa wewe u Mungu wetu, tena sisi watu wako. Sisi zote viumbe vya mikono yako; jina lako tunaliita.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Utufungulie mulango wa huruma, ewe Muzazi-Mungu mubarikiwa. Tukikutumaini wewe, tutakuwa bila kuanguka. Kwako tutaziepuka taabu; Kwa kuwa wewe wokovu wa muzao wa wakristu.

PADRI: Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba utusikia na ukatuhurumie.

Waimaji: Bwana hurumia *(mara tatu).*

PADRI: tena tunakuomba kwa ajili kuchunga muji huu (ao Monasteri ao Mission) na muji na migini yote, toka gazabu, njaa, majonjwa ya kuambukiza, tetemeko la inchi, garika, moto, upanga, ushambulio ya watu wageni, magombano, kufa musiba, kwa ajili ya Mungu wetu na mpenda-wanadamu awe Murehemu. Mwema na Mupendwa, kusudi afukuze na asambaze kila gazabu na magonjwa inayokaribia juu yetu, na akomboe sisi toka makanio yake mwenye haki na atuhurumie.

Msaomaji: Bwana hurumia *(mara makumi ine).*

PADRI: Utusikilize, ee Mungu Mwokozi wetu, matumaini ya mwisho wa inchi, na bahari mbali. Na awe murehemu sana kwetu, ee Rabi, kwa ajili ya zambi zote, hata milele na milele.

MSOMAJI: Bwana hurumia *(mara tatu).*

PADRI: Kwa kuwa u Mungu murehemu na mpenda-wanadamu, na kwako tunautoa utukufu kwa Baba na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

MSOMAJI: Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . Bwana hurumia *(mara tatu).* Ee Rabi Mtakatifu, bariki.

PADRI: Kristu Mungu wetu wa kweli, kwa maombezi ya mama yake Mtakatifu asiye na doa wala si la wama kamili, kwa uwezo wa Musalaba Muheshimiwa na muhishaji, kwa kusihi ya Mashahidi watakatifu, Watukufu, Washindaji wazuri, ya Wapadri wetu waaskofu na Walimu Wakubwa, ya Wapadri wetu Matawa na Wabebaji-Mungu, ya Yoakimu na Anna, Mababu-Mungu Watakatifu na wenye haki, ya (*anataja jina la Mutakatifu wa siku ile)*, aliye tunamukumbuka leo, hata na Watakatifu wote, atuhurumie, akatuokoe yu Mungu Mwema, Murahimu na mpenda-wanadamu.

*Tena tunaimba wimbo wa Mwisho na watu wanasujudu Picha ya Muzazi-Mungu.*

**WIMBO WA MWISHO Sauti ya Pili**

Mwema, mukononi mwako mwa nguvu, unachunga wote, wanaokimbilia kwa imani. Hatuna mpatanishi mwingine mbele ya Mungu, katika hatari na sikitiko, sisi wenye-zambi, tunaoinama kwa makosa mingi. Kwa hii, Mama wa Mungu wa juu, tunakusujudu ponyeshe, watumishi wako toka kila shida.

Mama wa Mungu wa juu, uko furaha na mulinzi, wa watenda mabaya, chakula cha wahitaji, mufariji wa wageni, na bakora ya kipofu, mupozi wa wagonjwa, kivuli na muchungaji, ya wenye maumivu, na musaidizi wa mayatima, Bikira tunakusifu ujiharikishe kwa kuponyesha watumishi wako.

Sauti ya mnane.
Bibi Malkia pokea kusihi, na watumishi wako, na utukomboe, toka kila lazima na sikitiko.

Sauti ya mbili.
Ninakuelezea matumaini yangu yote, ee Mama wa Mungu, unilinde chini ya kivuli chako.

Kwa maombezi ya wapadri wetu watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie. Amina.

*TANGAZO: Kwa tarehe 1 mupaka 14 ya Mwezi ya Mnane, tunaimba Wimbo (Exapostilaria) hii, badala ya wimbo ya mwisho.*

Sauti ya tatu.
Mitume mupatane hapa, toka dunia yote, fasini mwa Gesthimani, muzike mwili wangu, nawe Mwana na Mungu wangu, pokea roho yangu.

Ewe furaha ya Malaika, na watu wenye taabu, Mulinzi wa wakristu, Bikira Mama wa Bwana, unilinde na uponyeshe, toka mateso ya milele.

Ninawe mupatanishi, mbele ya Mungu Mufazili, asihesabie matendo yangu, mbele ya Malaika, ninakuomba ewe Bikira, unisaidie upesi.

Ewe mnara wa zahabu, na muji wa kuta kumi na mbili, kiti cha jua mwenye-kungaa, kiti cha ezi cha ufalme, ajabu gani isiyosikilikwa, je unanyonyesha Rabi.

Kwa maombezi ya Mapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe. Amina.

# APODIPNO MUKUBWA

## (YA KWAREZIMA YA PASKA)

*Hii sala ni ya kusoma Mangaribi ya ma siku yifwatayo: kazi moja, Kazi pili, Kazi Tatu, na Kazi ine mu Wakati ya Kwarezima Mkubwa mbele ya paska.*

PADRI: Ahimidiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
Utukufu kwako, ee Mungu, matumaini wetu, utukufu kwako.

Mfalme wa mbinguni, Wewe Mfariji. Roho ya ukweli, uliye pahali popote, na kuvijaza vitu vyote, Wewe hazina ya mambo mema, tena Mpaji wa uhai. Njoo kukaa kwetu na kutusafisha kila doa, hata roho zetu, Mwema we.

MSOMAJI: Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Musiye kufa Mtakatifu, utuhurumie. *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Utatu Mtakatifu Kamili utuhurumie, Bwana utusamehe zambi zetu, Rabi utuondolee makosa yetu, mtakatifu utukaribie na uponye magonjwa yetu, Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni, utupe sisi leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe ndeni zetu kama sisi vilevile tunawasamehe walio na deni zetu, tena usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule mwovu.

PADRI: Kwa kuwa ufalme na uwezo; na utukufu ni wako wa Baba, na wa Mwana, na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele.

Bwana hurumia (Mara 12) Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .
Njooni tumwinamie na tumusujudu Mungu Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumusujudu Kristu aliye Mungu Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie na tumusujudu Yeye Kristu aliye mfalme na Mungu wetu.

**ZABURI 4**

Unijibu wakati ninapoita, ee Mungu wa haki yangu; umenifanyizia nafasi wakati nilipokuwa katika taabu; unirehemu na kusikia maombi yangu. Ee ninyi wana wa watu, hata wakati gani utukufu wangu utageuzwa kuwa zarau? Hata wakati gani mutapenda ubatili na kutafuta uwongo? Lakini mujue ya kuwa Bwana amejiwekea mutawa mbali; Bwana atasikia wakati ninapomwita. Muwe na woga wala musitende zambi; semezaneni na moyo wenu wenyewe juu ya kitanda chenu na kutulia. Toeni zabihu za haki, na wekeeni Bwana tumaini lenu, Wao ni wengi wanaosema: Nani atakayetuonyesha mema? Bwana, utunyanyulie nuru ya uso wako. Umeweka furaha moyoni mwangu, kupita furaha yao wakati wanapozidishwa nafaka na mvinyo. Katika salama nitalala na kupata usingizi, maana wewe Bwana peke yako unanikalisha na salama.

**ZABURI 6**

Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako. Unirehemu, ee Bwana, maana nimekauka; uniponyeshe, ee Bwana, maana mifupa yangu imefazaika. Nafsi yangu imefazaika vilevile; Nawe, ee Bwana, hata wakati gani? Rudi, ee Bwana, uokoe nafsi yangu, uniokoe kwa ajili ya wema wako. Maana katika mauti hapana ukumbusho juu yako, katika Hadeze nani atakayekupa sante? Nimechoka kwa kuungua kwangu; kila usiku ninanyeshea kitanda changu maji; ninatia malalo yangu maji kwa machozi yangu, Jicho langu limeharibika kwa sababu ya huzuni

yangu; na kuchakaa kwa sababu ya watesi wangu wote. Ondokeni kwangu, ninyi wote munaotenda uovu; kwa sababu Bwana amesikia sauti ya kilio changu. Bwana amesikia kusihi kwangu; Bwana atapokea maombi yangu. Adui zangu zote watapata haya na kufazaika sana; watarudi nyuma, watapata haya kwa gafula.

**ZABURI 12 (13)**

Hata wakati gani, ee Bwana, utanisahau hata milele? Hata wakati gani utanifichia uso wako? Hata wakati gani nitafanya shauri katika nafsi yangu? Nikiwa na huzuni moyoni mwangu muchana kutwa? Hata wakati gani adui yangu atatutukuzwa juu yangu? Ee Bwana Mungu wangu, uangalie na kunijibu, tia nuru macho yangu nisilale usingizi wa mauti; adui yangu asiseme: Nimemushinda; adui zangu wasifurahi wakati ninapoondoshwa. Lakini nimeamini rehema yako; Moyo wangu utafurahi ndani ya wokovu wako; nitaimbia Bwana, kwa sababu amenitendea na ukarimu.

Mara ingine:

Ee Bwana Mungu wangu, uangalie na kunijibu, tia nuru macho yangu nisilale usingizi wa mauti; adui yangu asiseme: Nimemushinda.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Aliliya, aliluya, aliluya. Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . .

**ZABURI 24 (25)**

Kwako, ee Bwana, ninanyanyua nafsi yangu. Ee Mungu wangu, nilikuwekea wewe tumaini langu, usiniache kupata haya. Adui zangu wasifurahi kwa kunishinda. Ndiyo, wao wanaokungojea wewe hawatapata haya, hata mumoja; wenye kutenda hila pasipo maana watapata haya. Unionyeshe njia zako, ee Bwana; unifundishe mapito yako. Uniongoze katika kweli yako, na kunifundisha; maana wewe ni Mungu wa wokovu wangu; nitakungojea wewe muchana kutwa. Kumbuka, ee Bwana, huruma zako na wema wako; maana zimekuwa tangu zamani. Usikumbuke zambi za ujana wangu. wala makosa yangu; unikumbuke kwa kadiri ya wema wako. Kwa ajili ya uzuri wako, ee Bwana. Bwana ni mwema na mwenye haki; kwa hivi atafundisha wenye zambi njia. Wapole atawaongoza katika hukumu, na wapole atawafundisha njia yake. Njia zote za Bwana ni wema na kweli, kwao wanaoshika agano lake na shuhuda zake. Kwa ajili ya jina lako, ee Bwana, usamehe uovu wangu, kwa kuwa ni mukubwa. Ni nani anayeogopa Bwana? Atamufundisha katika njia anayoichagua. Nafsi yake itakaa na salama; na wazao wake watariti inchi. Siri ya Bwana ni pamoja nao wanaomwogopa; naye atawaonyesha agano lake. Macho yangu yanatazama kwa upande wa Bwana siku zote; naye atatoa miguu yangu katika wavu. Geuka kwangu, na kunihurumia; kwa sababu mimi ni mukiwa na nimeteswa. Taabu za moyo wangu zimeongezeka; unitoe katika huzuni yangu. Fikili mateso yangu na taabu yangu, na samehe zambi zangu zote. Fikili adui zangu maana wao ni wengi; na wananichukia na machukio makali. Ulinde nafsi yangu na kuniponyesha; usiniache kupata haya, maana nimekuwekea wewe tumaini langu. Ukamilifu na haki zinilinde, kwani ninakungojea wewe. Ukomboe Israeli, ee Mungu, katika taabu zake zote.

**ZABURI 30 (31)**

Nimekukimbilia wewe, ee Bwana, usiniache kupata haya milele: Kwa kila haki yako uniponyeshe. Uniinamia sikio lako, uniponyeshe mbio, uwe mwamba wangu wa nguvu, nyumba yenye boma kuniokoa. Kwa maana wewe ni mwamba wangu na boma langu, na kwa sababu ya jina lako utaniongoza na utanionyesha njia. Unitoe katika wavu walionitegea kwa siri, maana wewe ni boma langu la nguvu. Katika mukono wako ninaweka roho yangu; umenikomboa, ee Bwana, wewe Mungu wa kweli. Nimechukia wenye kuangalia maneno bule ya uwongo, lakini nimeamini Bwana. Nitafurahi na kushangilia kwa rehema yako. Kwa kuwa umeona mateso yangu, unajua roho yangu taabuni. Wala hukunifunga kwa mukono wa adui, umesimamisha miguu yangu kwa pahali pakubwa. Unirehemu. Bwana, kwa sababu niko katika taabu. Jicho langu linaharibika kwa huzuni, roho yangu na mwili wangu kwa maana maisha yangu yamekoma kwa huzuni, na miaka yangu kwa kuugua,

nguvu yangu inapunguka kwa sababu ya uovu wangu, na mifupa yangu imekauka. Nimekuwa shutumu kwa adui zangu zote, lakini zaidi kwa jirani zangu, na woga kwa wenye kunijua, wenye kuniona inje walinikimbia. Nimesahauliwa kama mufu toka mawazo ya watu; nimekuwa kama chombo kilichovunjika. Maana nimesikia masingizio ya watu wengi-Maogopesho pande zote-wakati walipofanya shauri pamoja juu yangu, wafanye hila kuondoa uzima wangu. Lakini nimekutumainia wewe, ee Bwana, nimesema, wewe ni Mungu wangu. Siku zangu ni mikononi mwako; uniponyeshe kwa mukono wa adui zangu na wa wenye kunitesa. Utolee mutumwa wako nuru ya uso wako, uniokoe kwa huruma yako. Ee. Bwana, usiniache kupata haya, kwa kuwa nimekuita; acha waovu kupata haya wanyamaze kwa Hadeze. Midomo ya kusema uwongo iwe bubu, inayosema maneno magumu juu ya wenye haki kwa majivuno na kuzarau. Ee, mukubwa sana ni wema wako uliowekea wenye kukuogopa! Uliofanyia wenye kukutumainia, mbele ya wana wa watu. Utawafunika kwa maficho ya uso wako kwa fitina za mutu. Utawaficha kibandani kwa magomvi ya ndimi. Bwana abarikiwe, kwa sababu amenionyesha rehema yake ya ajabu kwa muji wenye boma. Nami, nilisema kwa haraka: Nimekatika mbele ya macho yako; hata hivi ulisikia sauti ya kilio changu wakati nilipolalamika mbele yako. Pendeni Bwana, ninyi watakatifu wake wote. Bwana anachunga waaminifu na analipa kwa malipo tele mwenye kutenda kwa majivuno. Muwe hodari, moyo wenu upate nguvu, ninyi wote monaongojea Bwana.

**ZABURI 90 (91)**

Yeye anayekaa kwa pahali pa maficho yake aliye juu atakaa chini ya kivuli cha Mwenyezi. Nitasema juu ya Bwana, yeye ni pahali pangu pa kukimbilia na boma la nguvu langu. Mungu wangu ninayemwamini. Kwa maana atakuokoa toka mutego wa muwindaji ndege, na kwa tauni ya uharibifu. Na manyoya yake atakufunika. Na chini ya mabawa yake utakimbilia, kweli yake ni ngabo na kigabo. Hutaogopa kwa woga wa usiku, wala kwa mushale unaoruka muchana; kwa tauni inayotembea katika giza, wala kwa kuharibu kunakoharibu azuhuri, elfu moja wataanguka kando yako, na elfu kumi kwa mukono wako wa kuume; lakini hakutafika karibu nawe. Na macho yako tu utatazama, na kuona zawabu ya waovu. Maana wewe, ee Bwana, ni pahali pangu pa kukimbilia! Umefanya aliye juu kao lako; mabaya hayatakupata wewe wala tauni haitafika na hema yako. Maana ataagiza malaika yake juu yako, wakuchunge katika njia zako zote. Watakuchukua juu mikononi mwao, usivunje muguu wako kwa jiwe. Utakanyaga simba na nyoka mudogo mwenye sumu, utakanyaga mwana-simba na joka. Kwa sababu ametia mapendo yake juu yangu, kwa hivi nitamuponyesha. Nitamuweka juu kwa sababu amejua jina langu. Ataniita na nitamujibu; nitakuwa pamoja naye katika taabu; nitamuponyesha na kumuheshimu. Kwa maisha ndefu nitamushibisha, na kumwonyesha wokovu wangu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Aliluya, aliluya, aliluya, utukufu kwako, ee Mungu. Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Mungu yuko pamoja nasi; yueni, ee ninyi mataifa, na kushindwa.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Tegeni masikio, ninyi yote, mulio mpaka mwisho wa inchi.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Mulio na nguvu sana mutashindwa.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Mukipata nguvu tena, mutashindwa tena.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.
Mukifanya shauri pamoja, litabatilika.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Mukisema neno, halitasimama kwenu.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Wala tutaogopa hofu yenu, wala tutahangaika.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Lakini Bwana Mungu wetu tutakayemutakasa, na yeye atakuwa maogopesho kwetu.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Na kama mimi namutumainia, alinitakasa.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Nami nitamutumainia, naye ataniokola.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Tazama, mimi pamoja na watoto niliopewa na Mungu.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Watu waliotembea katika giza, wameona nuru kubwa.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Tuliikala katika inchi na kivuli cha kifo nuru imeangala yulu yetu.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Maana kwa ajili yetu mutoto amezaliwa, tumepewa mutoto mwanaume.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Kwake utawala wake, yulu ya bega lake.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Na salama yake haina mwisho.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Na jina lake linaitwa: Mujumbe wa shauri kubwa.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Mushauri wa ajabu.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Mungu Mwenyezi, mutawala, Mukubwa wa salama.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Baba ya uzima milele.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Utukufu kwa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

Mungu yuko pamoja nasi, yueni mataifa, na kushindwa.
Maana Mungu yuko pamoja nasi.

**WIMBO**

Kufika mwisho wa siku ya leo, Bwana, nakutukuza, Nakuomba, Mwokozi, unipe mangaribi moja na usiku moja wasipo zambi, na uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . .
Kufika mwisho wa siku ya leo, nakutukuza, Bwana Mkuu, unipe, Mwokozi wangu, mangaribi moja na usiku moja pasipo faraza la anguko, na uniokoe.

Sasa na siku zote. . .
Kufika mwisho ya siku ya leo, nakuimba, Mtakatifu sana, unipe, Mwokozi, mangaribi moja na usiku moja wasipo mitego, na uniokoe.

Sauti ya sita
Hali isiyo na mwili ya wamalaika inakutukuza kwa mimbo isiyo mwisho.

Wenye uzima wa mabawa sita, maserafim, wanakusifu pasipo mapumuziko kwa nyimbo zao.
Na jeshi la wamalaika wanakushangilia kwa wimbo: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu.

Sababu wewe uko mbele ya vitu vyote, Baba, na Mwana wako, wasipo mwanzo.

Pakuonyesha roho ya uzima yenye sifa sawa wewe, unaonyesha umoja wa utatu takatifu.

Bikira Mtakatifu. Mama wa Mungu, na nyinyi shahidi na watumishi wa Neno (Mwana). Kundi lote la Manabii na Mamashahidi, weko na uzima sawa wasiyo kufa, muombe pasipo kuregea kwa ajili ya wote, kwani wote tunapotea.

Tukifunguwa kwa uerevu wa shetani, tutaimba wimbo wa wamalaika: Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana mara tatu Mtakatifu, utuhurumie na utuokoe sisi. Amina.

**FUNDISHO (SIMVOLO) YA IMANI**

Nasadiki Mungu mmoja. Baba mwenyezi, mwumba wa mbingu na wa dunia, hata vyote vilivyoonekana na visivyoonekana, tena Bwana mmoja Yesu Kristu. Mwana wa pekee wa Mungu, aliyezaliwa na Baba mbele ya wakati wote. Nuru toka Nuru, Mungu kweli toka Mungu kweli, aliyazaliwa, si Muumbwa mwenye asili moja (omousion) na Baba, aliye kwake vyote vilifanywa, aliye kwa ajili yetu wanadamu, na ya wokovu wetu alishuka mbinguni, akapata mwili kwa Roho Mtakatifu na kwa Bikira Maria, na akawa mtu. Aliye sulibiwa kwa ajili yetu wakati wa Pontio Pilato. Akateswa, akawekwa kaburini. Na aliyefufuka katika siku ya tatu, kama yanavyo Maandiko. Na akapanda mbinguni ndipo anapokaa kuume kwa Baba. Na atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu walio hai na waliokufa. Ufalme wake utakuwa bila mwisho. Tena Roho Mtakatifu yu Bwana yu Mwumba hai, aliyetoka na Baba, aliyesujudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana, aliyenena kwa midomo ya manabii, kwa Eklezia moja Takatifu. Katholiki na Apostoliki. Naungama kwa ubatizo moja kwa maondoleo ya zambi. Natumaini ufufuo wa wafu hata uzima wa milele utakaokuja. Amin.

Sauti ya sita
Mama Mtakatifu. Mama wa Mungu, utuombee sisi wakosefu, *(mara tatu).*

Nyinyi wote ezi kuu za mbinguni, Malaika na Malaika Watakatifu wakuu, mutuombee sisi wakosefu *(mara mbili).*

Mtakatifu Yoanne. Nabi. Mutangulizi, na Mubatizaji wa Bwana wetu Yesu Kristu, utuombee sisi wakosefu *(mara mbili).*

Watakatifu na Mitume watukufu, Manabii, na Mashahidi na Watakatifu wote, mutuombee sisi wakosefu *(mara mbili).*

Watawa, wababa wetu Wabebaji wa Mungu, wachungaji na Walimu wa dunia muzima, mutuombee sisi wakosefu *(mara mbili).*

Nguvu yenyi kushindiwa ya msalaba takatifu, usituache sisi wakosefu *(mara mbili).*

Mungu uwe mwenyi rehema kwa sisi wakosefu *(mara tatu).*
Bwana hurumia.

*Kisha tunasema Trisayon:*
Mungu Mutakatifu. Mweza Mtakatifu, msiye kufa Mtakatifu, utuhurumie *(mara tatu).*
Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku. . . Utatu Mutakatifu. . . Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . . Baba yetu uliye mbinguni. . .
PADRI: Kwa kuwa. . .

WAIMBAJI: Sauti ya sita
Ee Bwana Mungu wangu, tia nuru macho yangu nisilale usingizi wa mauti, adui yangu asiseme: Nimemushinda.

Utukufu kwa Baba. . .
Saidia roho yangu, ee Mungu, kwa sababu natembea katikati ya mitego mingi, unichunge, na uniokoe, ewe Mwema, Mpenda-wanadamu.

Sasa na siku zote. . . THEOTOKION:
Kwa sababu hatuna na matumaini juu ya zambi zetu nyingi, hurumia huyu aliyezaliwa kwako ee Mzazi-Mungu. Bikira, sababu ombi la mama iko nguvu kwa kupata wema wa Rabi. Usizarau maombi ya wenyi kutenda zambi, ee Mtukufu, kwani yeye ni mwenyi rehema na nguvu ya kuokoa, kwa sababu anachukua mateso yetu mwilini mwake.

*Hii Tropari ni ya siku ya kazi Mbili na kazi Ine.*
Bwana, unajuwa ya kama adui zangu wasioonekana wanakaa kila siku macho wazi, tena unajuwa uzaifu wa mwili wangu, wewe uliniumba, na naweka roho yangu mikononi mwako. Unifunike mu mabawa ya wema wako, kwa sababu nisilale mu mauti. Uangazie macho ya roho yangu kwa raha kubwa ya maneno yako ya umungu. Uniamushe wakati wenye kweneya ili nikukutuze mwema na mpenda-wanadamu.

Angalia upande wangu, unihurumie, juu ya uhaki wako kwa yule anapenda jina lako.
Maamzi yako yenyi kuogoppesha, ee Bwana, wakati malaika watakuwapo, watu watakusanika, vitabu wavi, vitendo vyenyi kufunuliwawangalia, mawazo yenye kuwa wazi.

Maamzi yangu mimi mwenye kuumbwa mu zambi itakuwa je? Nani atanizimia moto? Nani ataniangazia giza? Kama wewe. Bwana haunihurumie, wewe Mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . .
Unipe machozi, ee Mungu, ulivyomutenda zamani nitenda za, bi ili nistahili, kusafisha miguu yako ilionitosha njiani mwa uwongo, na kukutolea manukato ya harufu nzuri na uzima safi,

uliyofanywa katika toba; na nisikie, mimi vilevile, neno pendelevu: Imani yako inakuokoa, wende na amani.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Muzazi-Mungu, nakutumainia wewe. Nikiwa na furaha ya msaada wako, ee Mama mtakatifu, sitaogopa kitu; nikiwa na ulinzi wako, kama silaha, nitafukuza adui zangu na nitawasambaza; kwa kuomba msaada wako wa uwezo na isio na mipaka, nakulalamikia: Ee Mkuu, uniokoe kwa maombezi yako; uniamushe toka usingizi wa giza, kusudi nikutukuze kwa uwezowa huyu alipata mwili kwako, ndiye Mwana wa Mungu.

MSOMAJI: Bwana hurumia (*mara makumi Ine)* . Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Uliye wa thamani kuwa shinda waKeruvi, uliye na utukufu. . . Kwa jina la Bwana, ee Padri bariki.

PADRI: Kwa maombezi ya Mapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

## Sala ya Mtakatifu Bazile Mkubwa

Bwana. Bwana, ulitukomboa toka mukuki wenyi kuruka muchana, utuokoe tena toka tendo lenyi kutembea mu giza. Upokee kuinua kwa mikono yetu sawa sadaka ya mangaribi, tuwe wastahilivu wenyi kupumzika usiku pasipo ugombezi, kwa boma la uovu wowote. Utuokoe koka mashaka na woga shetani alituwekea. Leta rohoni mwetu toba ya zambi, kwa mawazo yetu, kukumbuka hukumu yako ya kweli na ya kyogopesha. Utoboe mwili wetu kwa woga wako, regeza watu wa dunia: Kwa hivi katika mapumziko ya usingizi, tutaangazwa na matezamo ya hukumu zako. Ondosha kwetu wazo lote mbaya, na tamaa yenyi kuzuru. Utuamushe wakati wa sala, tuwe wenyi kujikaza kwa imani, na kutembee katika njia za kawaida, kwa wema na haki ya Mwana wako, ambaye unahimidiwa, pamoja naye, na Roho Mtakatifu mwenyi haki na mwenyi kuleta uhai, sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

Njooni tumwinamie na tumusujudu Mungu Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie Kristu aliye Mfalme wetu.
Njooni tumwinamie yeye Kristu aliye Mfalme na Mungu wetu.

**ZABURI 50 (51).**

Unirehemu, ee Mungu, sawasawa na wema wako; sawasawa na wingi wa rehema zako uzime makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, na kunisafisha na zambi yangu. Maana ninajua makosa yangu, na zambi yangu ni mbele yangu daima. Nimekukosea wewe peke yako, na kufanya yaliyo mabaya machoni mwako; ili ujulikane kuwa mwenye haki wakati unaposema, na kuwa safi wakati unapotoa hukumu. Tazama, niliumbwa katika hali ya uovu; na katika makosa mama yangu alinichukua mimba. Tazama, wewe unataka kweli moyoni, na kwa siri utanijulisha hekima. Unisafishe kwa hisopo na nitakuwa safi; unioshe, na nitakuwa mweupe kupita theluji. Unifanye kusikia furaha na shangwe; ili mifupa uliyovunja ifurahi. Ufiche uso wako usitazame zambi zangu; na uzime maovu yangu yote. Umba moyo safi ndani yangu, ee Mungu, na ufanye upya roho nzuri ndani yangu. Usinitenge na uso wako, wala usiondolee Roho yako mutakatifu. Unirudishie furaha ya wokovu wako; unitegemeze kwa roho ya tayari. Halafu nitafundisha wenye makosa njia zako; na wenye zambi watarudi kwako, Uniponyeshe na damu ya watu, ee Mungu, wewe Mungu wa wokovu wangu; ulimi wangu utaimba na sauti haki yako. Ee Bwana, ufungue midomo yangu, na kinywa changu kitaonyesha sifa zako. Maana hupendezwi na zabihu, ao ningeitoa, hufurahi kwa sadaka ya kuteketezwa. Zabihu za Mungu ni roho ya kuvunjika, moyo uliovunjika na wa toba hutauzarau, ee Mungu. Utendee Sayuni mema kwa mapenzi yako, ujenge kuta za Yerusalema. Halafu utafurahi kwa zabihu za haki, kwa sadaka ya kuteketezwa, na sadaka nzima ya kuteketezwa; halafu watatoa ngombe ndume juu ya masabahu yako.

**ZABURI 101 (102)**

Sikia maombi yangu, ee Bwana, na kilio changu kikufikie. Usinifichie uso wako kwa siku ya taabu yangu: Unitegee sikio lako; kwa siku ninapoita unijibu mbio. Maana siku zangu zinaharibika kama moshi, na mifupa yangu imeteketea kama ukuni unaowaka. Moyo wangu umepigwa kama majani, na umekauka, maana nilisahabu kula chakula changu. Kwa sababu ya sauti ya kuugua kwangu mifupa yangu inafungana na nyama yangu. Mimi ni kama mwari ya jangwa; nimekuwa kama bundi ya pahali pa ukiwa. Ninakesha, na nimekuwa kama zawaradi aliye peke yake juu ya dari ya nyumba. Adui zangu wananilaumu muchana kutwa; wao wanaonikasirikia kama wazimu wanatukana kwa kunitaja mimi. Maana nimekula majivu kama chakula, na kuchanganya kinyweo changu na machozi. Kwa sababu ya gazabu yako na hasira yako: Maana umeninyanyua na kunitupa. Siku zangu ni kama kivuli kinachoshuka; nami nimekauka kama majani. Lakini wewe, ee Bwana, utakaa milele; na ukumbusho wako kizazi hata kizazi; utasimama na kurehemu Sayuni: Kwa maana ni wakati wa kuihurumia, ndiyo, wakati ulioamriwa umefika. Maana watumishi wako wanafurahia mawe yake, na wanahurumia mavumbi yake. Hivi mataifa wataogopa jina la Bwana, na wafalme wote wa inchi utukufu wako: Maana Bwana amejenga Sayuni, ameonekana katika utukufu wake; ameangalia maombi ya masikini, wala hakuzarau maombi yao. Hili litaandikwa kwa kizazi kitakachokuja: Na taifa watakaoumbwa watasifu Bwana. Maana ameangalia toka juu, toka pahali pake patakatifu; toka mbingu Bwana akatazama inchi; ili asikie kuugua kwa mufungwa; kufungua wale waliowekwa kwa mauti; ili watu watangaze jina la Bwana katika Sayuni, na sifa yake katika Yerusalema; wakati mataifa watakapokusanyika pamoja, na falme, ili kutumikia Bwana. Amepunguza nguvu yangu njiani; amefupisha siku zangu. Nilisema: Ee Mungu wangu, usiniondoe katikati ya siku zangu: Miaka yako ni tangu kizazi hata kizazi. Tangu mwanzo uliweka musingi wa inchi; na mbingu na kazi ya mikono yako. Hizi zitaharibika, lakini wewe utadumu: Ndiyo, hizi zote zitachakaa kama nguo; na kama vazi utazibadilisha, nazo zitabadilishwa: Lakini wewe ni sawasawa, na miaka yako haina mwisho. Wana wa watumishi wako watakaa, na wazao wao watasimamishwa mbele yako.

## Sala ya mfalme Manasi

Mwenyezi Mungu, Mungu wa Mababu zetu Abrahamu, Izaaki na Yakobo na wa uzao wao, wewe uliyeumba mbingu na dunia na uzuri wao wote; ulisimamisha bahari kwa sauti ya hukumu yako, wewe uliyefunga shimo kubwa na kulizibia kwa utukufu wa jina lako, ulimwengu nzima inakuogopa na inatetemeka juu ya nguvu yako, sababu hakuna yule ana uwezo wa kuchukua ukuu wa utukufu wako, ao kuchukua ukali wa matisho yako juu ya wakosefu. Lakini neema ya agano lako ni munene na haiwezi kufumbuliwa na mtu hata mumoja; sababu, wewe ni Bwana, ni wewe Mkuu, mwenye huruma, wasipo kisilani na tajiri wa huruma; umesumbushwa kwa vitendo vibaya vya wanadamu, Wewe Bwana, Mungu wa wenyi haki, haukuweka toba juu ya wenyi haki: Abrahamu, Izaaki na Yakobo kwani hawakutenda zambi juu yako, lakini ulitia majuto ju ya mimi mukosefu, kwa sababu nilitenda zambi nyingi sawa muchanga wa bahari; makosa yangu ni mengi, Bwana, sina tena mwema kwa kunyanyua macho mbinguni, sababu ya makosa yangu mengi. Sababu nimefungwa minyororo ya chuma, siwezi kunyanyua kichwa changu sababu ya zambi zangu, sipumzike, kwa sababu nimechokoza hasira yako, tena nilikosa mbele yako, pasipo kutimiza mapendo yako na kuchunga mafundisho yako. Sasa moyoni mwangu, naomba wema wako: Nilikosa, Bwana, nilikosa, najuwa kosa langu; nakuomba, unihurumie, Bwana, unihurumie, nisipotee juu ya makosa yangu, usisirike juu ya vitendo vyangu vibaya, usinitie katika makao ya chini, kwa sababu, Bwana ni wewe Mungu wa toba, Unionyeshe wema wako, kwani, kwa rehema yako kubwa utaniokoa mimi msiyestahili; nitakutukuza katika maisha yangu, kwa sababu ezi kuu zinakutukuza mbinguni utufuku ni wako milele na milele. Amina.

MSOMAJI: Mungu Mutakatifu, Mweza Mutakatifu, Msiye kufa Mutakatifu, utuhurumie *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Utatu Mutakatifu. . . Bwana hurumia *(mara tatu)*. Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . Baba yetu, uliye mbinguni. . .

PADRI: Kwa kuwa ufalme na uwezo, na utukufu ni wako Baba na wa Mwana na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

## WIMBO INGINE Sauti ya sita

Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie; Kwa kuwa sisi watu wenye zambi, hakuna tena yoyote kukutolea, ila ombi hii tunatoa kwako, uliye Rabi, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana. . .

Ee Bwana, utuhurumie kwa kuwa tunatengemea kwako. Utukaribie sana wala kuzikumbuka zambi zetu, lakini hata sasa utwangalie kama mwenye huruma, ukatuokoe na madui zetu, Wewe, u Mungu wetu, tena sisi ni watu wako, sisi wote ni viumbe vya mikono yako na jina lako tunaliita.

Sasa na siku zote. . . THEOTOKION

Utufungulie mlango wa huruma yako, ee Mzazi Mungu Mbarikiwa. Tunayokutumainia wewe, hatutaanguka, Kwako tutaepuka mateso, kwa kuwa wewe ni wokovu wa amini wa wa Kristu.

Bwana hurumia (Mara makumi Ine).

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Uliye wa tamani. . . Kwa jina la Bwana, ee Padri, bariki.

PADRI: Kwa maombezi ya Wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu, Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

PADRI: Mungu, Rabi, Baba Mwenyezi; Mwokozi, Mwana wa pekee, Yesu Kristu na Roho Mtakatifu, umungu moja, nguvu moja, unihurumie; wakati wa mwisho uniokoe mimi mukosefu wako, kwani umetukuzwa milele na milele. Amin.

MSOMAJI: Njooni tumwinamie na tumusujudu Mungu Mfalme wetu.

Njooni tumwinamie na tumusujudu Kristu aliye Mfalme wetu.

Njooni tumwinamie na tumusujudu yeye Kristu aliye Mfalme na Mungu wetu.

**ZABURI 69 (70).**

Ee Mungu, uniokoe; unisaidie mbio, ee Bwana. Wapate haya na kufazaishwa wanaotafuta nafsi yangu; warudishwe nyuma na kuzarauliwa wanaofurahi kwa kuumia kwangu. Warudishwe nyuma kwa ajili ya haya yao wanaosema: Ewe, ewe, Wote wanaokutafuta washangilie na kukufurahia; nao wanaopenda wokovu wako waseme daima: Mungu atukuzwe. Lakini mimi ni masikini na mwenye hitaji unisaidie mbio, ee Mungu; wewe ni musaidia wangu na mwokozi wangu; ee Bwana, usikawie.

**ZABURI 142 (143)**

Sikia maombi yangu, ee Bwana, usikilize kusihi kwangu; katika uaminifu wako unijibu, katika haki yako. Usihukumu mutumishi wako; maana machoni mwako hakuna mutu aliye hai atahesabiwa haki. Maana adui amefuata nafsi yangu; amepiga uzima wangu chini hata udongo. Amenikalisha katika pahali pa giza, kama wale waliokufa zamani. Kwa hivi roho yangu imezimia ndani yangu; Moyo wangu ndani yangu ni ukiwa. Ninakumbuka siku za kale; ninafikili matendo yako yote; ninawaza kazi ya mikono yako. Ninakunyoshea mikono yangu; nafsi yangu inaona kiu kwa wewe, kama inchi inayochoka. Fanya mbio kwa kunijibu, ee Bwana; roho yangu inazimia; usinifichie uso wako; nisiwe kama wao wanaoshuka shimoni. Unifanye kusikia wema wako asubui; kwa maana ninakutumainia wewe; unijulishe njia nitakayoikwenda; kwa maana ninakunyanyulia nafsi yangu. Uniponyeshe, ee Bwana, na adui zangu, ninakukimbilia unifiche. Unifundishe kufanya mapenzi yako; kwa maana wewe ndiwe Mungu wangu; Roho yako ni mwema; uniongoze katika inchi ya haki. Unipatize uzima, ee Bwana, kwa ajili ya jina lako; kwa haki yako utoe nafsi yangu

katika taabu. Na kwa wema wako ukatilie mbali adui zangu, na kuwaharibu wote wanaotesa nafsi yangu; kwa maana mimi ni mutumishi wako.

## DOKSOLOGIA KIDOGO

Utukufu kwa Mungu juu pia, nchini amani urazi kwa wanadamu. Tukusifu, tukuhimidi, tukusujudu, tukutukuza, tukushukuru, maana utukufu wako ni mkuu. Ee Bwana mfalme, Mungu wa juu mbinguni, Baba mwenyezi, ee Bwana Mwana wa pekee Yesu Kristu na wewe Roho Mtakatifu. Ee Bwana, Mungu we, Mwana Kondoo wa Mungu, Mwana wa Baba, unazibeba zambi za dunia utuhurumie, unazibeba zambi za dunia. Upokee ombi letu, uliyeketi kuume kwa Baba na utuhurumie. Kwa kuwa Mtakatifu wa pekee, Bwana wa pekee, Yesu Kristu katika utukufu wa Mungu Baba. Amina. Kila Mangaribi nitakuhimidi, nitalisifu jina lako la milele, hata milele na milele. Ee Bwana wewe ni kimbilio letu, kizazi baada ya kizazi, Mimi nilisema: Ee Bwana, unihurumie, uiponye roho yangu, maana nimekutendea zambi. Ee Bwana, nimekimbilia kwako, unifundishe kutenda mapenzi yako, maana ndiwe Mungu wangu. Maana kwako wewe iko chemchem ya uzima; katika mwangaza wako tutaona mwangaza. Onyesha huruma yako kwao wakujue. Ee Bwana, utujalie usiku huu, kutulinda na zambi. Umehimidiwa, ee Bwana Mungu wa Baba zetu jina lako limesifiwa, na limetukuzwa milele. Amina. Ee Bwana, huruma yako iwe nasi, tumevyokutumaini wewe. Ee Bwana, umehimidiwa, unifundishe zilizo haki zako. Ee Rabi, umehimidiwa, unifahamishe zilizo haki zako. Ee Mtakatifu, umehimidiwa, uniangaze kwa zilizo haki zako. Ee Bwana huruma yako ni ya milele; usiache kutuangalia sisi viumbe vya mikono yako. Sifa zakulaiki, kukuimbia ni kwako, utukufu ni wako, wa Baba na wa Mwana na wa Roho Mtaklatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Trasagion: Mungu Mutakatifu. . . *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Utatu Mutakatifu. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Baba yetu uliye mbinguni. . .

MSOMAJI: Mungu Mutakatifu. Mweza Mutakatifu. Msiye kufa Mutakatifu. utuhurumie *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .

Utatu Mutakatifu. . . Bwana hurumia *(mara tatu).* Utukufu kwa Baba. . Sasa na siku zote. . Baba yetu. uliye mbinguni. . .

PADRI: Kwa kuwa ufalme na uwezo. na utukufu ni wako Baba na wa Mwana na wa Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

*Elezo: Sasa tunaimba Wimbo ifwatayo na tunapiga magoti mara tatu ya kila mwimbo.*

**WAIMBAJI:**

Sauti ya sita

Bwana mwenye ezi, ukae pamoja nasi! Katika sikitiko zetu, ni wewe mwenye kutusaidia, Bwana mwenye ezi, utuhurumie.

Mistarii:

Mumusifu Mungu katika pahali pake takatifu, mumusifu katika anga la uwezo wake.

Mumusifu kwa matendo yake makubwa, mumusifu kwa kadiri ya wingi wa ukubwa wake.
Mumusifu kwa sauti ya baragumu, mumusifu kwa kinubi na tambira.

Mumusifu kwa muchezo na ngoma, mumusifu kwa nzenze na filimbi.

Mumusifu kwa matoazi yanaolia, mumusifu kwa matoazi ya shangwe.

Kila mwenye pumuzi asifu Bwana!

Mumusifu Mungu pahali pake takatifu.

Mumusifu katika anga la uwezo wake.

Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu.

Bwana, kama hatukukuwe na watakatifu sawa waombezi, na wema wako wenye kurehemu, tutasubutu je kukuimba. Mkombozi anayebarikiwa pasipo kupumzika na wamalaika, Wewe unajuwa mioyo, usamehe Roho zetu.

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina. THEOTOKION

Makosa yangu ni mengi, Mama Mzazi Mungu; nakimbilia kwako, wewe safi, naomba usalama. Angalia roho yangu yenyi ugonjwa, umuombe Mwana wako na Mungu wetu anihurumie kwa kosa nililotenda, wewe peke yako mbarikiwa.

Mama Mtakatifu wa Mungu, usiniache katika maisha yangu, usinitoe ku shime ya kinadamu, lakini wewe mwenyewe unilinde na unihurumie.

Naweka kitumaini kwako, Mama Mzazi wa Mungu, unilinde.

Bwana, hurumia (mara makumi Ine).

Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa, na kutukuzwa wakati wote na katika kila saa mbinguni na duniani, uliye mwadilifu, mrahimu tele, mfazili sana unayependa wenye haki, tena kuwahurumia wenye zambi; unayewaita wote kuona wokovu, ukiwaahidi vitu vema vilivyokuja; wewe, ee Bwana, hata katika saa hii uyapokee maombi yetu, na kuyashurutisha maisha yetu njiani pa amri, zako uzitakase roho zetu, uyasafishe miili zetu, uyatengeneze mafikira zetu, usinyoshe nia zetu; ukatuokoe na kila shida, ubaya, na teso, utulindie kwa Malaika wako, ili sisi tukiwa na utunzi na uongozi wao, tufike katika umoja wa imani na kuujulisha utukufu wako usiofifika. Kwa kuwa unahimidiwa milele na milele. Amina.

Bwana hurumia *(mara tatu).*

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Uliye wa thamani. . . Kwa jina la Bwana, ee Padri, bariki.

PADRI: Mungu utufazilie na kutubariki, atuwangazie uso wake na kutuhurumia.

*Kisha tutapiga magoti munene mara tatu na tutasema hii Sala ya Mtakatifu Efrem.*

Bwana, ondosha mbali na mimi nia ya uvivu, ya kupoteza, ya mamlaka na ya masauti bure. (Metania Mkubwa).

Umupe mtumishi wako roho ya kadiri, ya unyenyekevu, ya uvumilivu na ya mapendo (Metania Mkubwa).

Ndiyo, Bwana na Mfalme, unipe nione makosa yangu, nisiamue ndugu yangu, kwani unabarikiwa milele na milele. Amina. (Metania Mkubwa).

Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia, na utusaidie na wokovu sisi Bikira Maria.

## SALA KWA BIKIRA MARIA MZAZI MUNGU MTAKATIFU KAMILI.

MSOMAJI *wa kwanza atasimama mbele ya Picha ya mama Maria kusoma hii Sala:*

Ewe Bibi Malkia; uliye bila doa, bila waa, bila uchafu, safi kamili Bikira Bibi Mungu, uliyemwunganisha Mungu Mwana, na wanadamu kwa uzazi wako wa ajabu, na kuuchanganisha uumba wetu, uliokuwa ondoshwa, nao walio mbinguni, uliye peke yako matumaini ya wakufa moyo, na msaada wa washawishwa, uliye tayari kuwalinda wote wanakukimbilia wewe; wewe makimbilio

ya wa Kristu wote, usinikiri mimi mtu mwenye zambi, mtu wa waa; niliofanya kufaa hata si kitu kwa mafikiri, na maneno, na matendo yangu ya aibu, tena kuwa mtumwa hiari wa anasa kihebu ya maisha kwa uzembe wangu. Lakini kwa kuwa wewe ni Mama wa Mungu Mpenda Wanadamu, unirehemu kwa upendo wanadamu wako mimi mtu mukosaji, na mpotevu, na kuipokea ombi langu linalokutolewa na midomo michafu yangu, na mtoto wako, na Rabi wetu. Na kwa ujasiri wako kama Mama wake unipatanishe, ili kuniikunjua rehema yako ya kupenda wanadamu ya wema wake, na akiyasamehe makosa yangu yasiyohesabiwa, anirudishe katika utubu na kunionyesha mshika mstahiliwa, wa amri yako, uwe daima karibu nami, ewe Mama mrahimu, mwenye upole, na mpenda uwema, katika maisha haya mhifazi na msaidizi wa moto, kuyazuia marukio ya madui, na kuniongoza njiani ya wokovu. Tena katika saa ile ya kufariki duniani, kuitunza roho yangu ya kizilili na kuzifukuza mbali yake zile nyuso za giza za mashetani waovu. Hata katika siku ile ya hukumu iliyokuongofya, kuniokoa na azabu ile ya milele, na kunijalia ku uriti utukufu usiokuelewa wa Mwana wako, na Mungu wetu. Uwe kuniufike, ewe Mzazi Mungu, Mtakatifu kushinda Bibi Malkia wangu, kwa utetezi na hifazi wako, nikiwa na neema, na upenda wanadamu wa Mwana wako wa pekee yeye Bwana, na Mungu, na Mwokozi wetu anaye na haki, utukufu wote, heshima na usujudu, pamoja na Baba wake asiye na mwanzo, pamoja na Roho Mtakatifu Kamili, Mwema, Mwumba hai, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

## SALA KWA BWANA WETU YESU KRISTU

Na utupe, ee Rabi, saa hii tukienda kulala, mapumziko ya mwili, na ya roho tena utulindie na ule usingizi wa giza ya zambi, na ya kila ubaya ungine wa giza, na wa usiku, Zuia mashawishi kuturukia, zimisha mishale ya yule mwovu, yaliyo na moto, yanatupwa kwetu kwa hila. Punguza vitu vibaya vya mwili wetu, ukiangaza kila nia yetu ya nchini na kidunia. Tena kizi yetu, ee Mungu akili ya kukesha, mafikira sawa moyo wangalifu, usingizi wa kisahala, safi na bila mwogofyo wa kishetani. Hata kutuamusha wakati wa kusali tuwe wahodari mu amri zako, na kuyakamata makumbusho ya hukumu yako. Tena utujalie usiku kucha tuwe na sifa yako, ili tulisifu, tulihimidi, tulitukuze jina lako linaloheshimiwa kamili, na kulipaza sana, jina la Baba na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Ee Mzazi Mungu, Mbarikiwa, Bikira daima, Mtukufu kushinda, uipishe sala yetu kwa Mwana wako tena Mungu wetu, na kutuombea aziokoe roho zetu kwa mateteo yako.

Baba ni Matumaini yangu, Mwana ni makimbilio yangu, Roho Mtakatifu ni himaya yangu, Utatu Mtakatifu, utukufu kwako.

Matumaini yangu yote ni kwako, ee Mama wa Mungu, unilinde chini ya himaya yako.

PADRI: Utukufu kwako, ee Kristu Mungu, kitumaini wetu, utukufu kwako.

MSOMAJI: Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mutakatifu. Sasa na siku zote, hata mnilele na milele. Amina. Bwana hurumia *(mara tatu).* Kwa jina la Bwana, bariki, ee Padri.

PADRI: Amani kwa wote. Tuinamishe vichwa vyetu mbele ya Bwana.

Ee Rabi, mtajiri wa huruma, Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, kwa maombezi ya Bikira Takatifu, mama wa Mungu, daima Bikira Maria, kwa nguvu ya utukufu wako na Msalaba wa uhai; kwa ulinzi wa nguvu tukufu za mbingu na za roho, ya mtukufu Nabii Yoane Mbatizaji, Mutangulizi wa sifa yote ya Watakatifu Watukufu na mashahidi wenyi ushindi, ya Wapadri wetu Watawa na Wabebaji wa Mungu, ya Wababu Watakatifu na wenyi haki wa Bwana, Yoakimu na Anna na Watakatifu wote, pokea na uwema uombi letu, utupe rehema ya makosa yetu, utulinde mu mabawa yako, kimbiza mbali nasi adui na mshindaji, leta amani kwa uzima wetu; Bwana, utuhurumie tena hurumia ulimwengu wako na uokoe roho zetu, wewe baba wa Juu, Mpenda-wanadamu.

MSOMAJI: Amina.

*Hii fasi Padri atapiga kidogo magoti, ataangalia mbele waaminifu na atasema na toba:*

Wa ndugu munihurumie

Waaminifu: Mungu akuhurumie wewe Baba mtakatifu na sisi.

MSOMAJI: Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . Bwana hurumia *(mara tatu).* Ee Padri mtakatifu, bariki.

PADRI: Tuombe kwa ajili ya amani ya wote. MSOMAJI: Bwana hurumia (*Kwa kila kitumo).*

Kwa ajili ya Wakubwa wetu na wale wenye kutuongoza.

kwa ajili ya Wakristiani wote, wabudu na wenye kuwaida ya dini.

Kwa ajili ya Askofu wetu (jina lake) na undugu wetu katika Kristu.

Kwa ajili ya Wapadri na ndugu hawapo.

Kwa ajili ya wenye kutusaidia na walitusaidia.

Kwa ajili ya wenye kutuchukia na wenye kutupenda.

Kwa ajili ya wale walituomba ju ya kuwaombea, japo uovu wetu.

Kwa ajili ya ukombozi ya wafungwa.

kwa ajili ya wale weko juu ya bahari.

Kwa ajili ya wagonjwa.

Tuombe tena kwa ajili ya ujazi wa matunda hapa duniani.

Kwa ajili ya wapadri wetu wote na ndugu wenye kuwaida ya dini waliyo kufa mbele yetu; wanaopumzika hapa na dunia nzima.

Kwa ajili ya sisi wenywewe tuseme.

MSOMAJI: Bwana hurumia *(mara tatu).*

*Waimbaji na Waaminifu pamoja wanaimba hii Mimbo ya Mzazi-Mungu na mara moja wanaanza kubusu Mifano ya Watakatifu.*

Sauti ya tatu. Tin Oreotita. Sauti ya tatu.

Kwa huyu aliyelishwa katika Hekalu, katika Patakatifu pa Patakatifu, mwenye kupambwa na hekima na imani na ubikira safi, malaika Mkuu Gabrieli akaleta habari ya mbinguni: «salamu», Bikira Mbarikiwa na Mjalizwa na utukufu, Bwana yupo pamoja nawe.

PADRI: Kwa maombezi ya Wapadri wetu watakatifu, ee Bwana Yesu kristu, Mungu, utuhurumie na utuokoe.

MSOMAJI: Amina.

*Elezo: Hii Sala ifwatayo kila mwaminifu inafaa kuisoma nyumbani mwake, mbele ya musingizi.*

## Sala mbele ya Kulala.

Ee Bwana hurumia wale wanatuchukia na walitutukana; fanya mema kwa wafazili (wenyi mema). Upokee maombi ya ndugu na jirani zetu kwa ajili ya wokovu na uzima wa milele. Tazama wagonjwa, uwape tunzo; ongoza wale weko juu ya bahari, sindikiza wasafiri; uchunge mukubwa wetu mu vita. Kwa wale wanatusaidia na wanatuonyesha mapendo yao, uwape maondoleo ya zambi. Hurumia, kwa ajili ya rehema yako, wale walituomba kuwaombea japo uovu wetu. Ukumbuke, Bwana, mapadri na ndugu zetu waliolala mbele yetu, uwape mapumuziko, kule kunangara nuru ya uso wako. Kumbuka, Bwana, ndugu zetu wafungwa, uwafungue toka mateso yao. Kumbuka, Bwana wale wanaoleta sadaka, na wale wanaotumika mu ma Ekklezia zako Takatifu; Uwapatie rehema ya maombi yao wanakuomba kwa ajili ya uokovu na uzima wa milele, Bwana, utukumbuke tena sisi, wanyenyekevu na wakosefu, watumishi wako waovu, utuangazie roho yetu kwa nuru ya maarifa yako, utuongoze katika njia za kanuni yako, kwa maombezi ya Mama wako Bikira daima na Mzazi-Mungu, na ya Watakatifu wote, kwa sababu umetukuzwa hata milele na milele. Amina.

# SALA YA PASKA

*Kutoka siku ya Paska kufika mu Juma ya Thomas, hii wakati inaitwaa Juma "Diakenisimos". Katika Juma Diakenisimos ku Sala ya Saa na Sala ya Usiku, nikusema Apodipno Kidogo tunasoma hivi.*

PADRI: Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na mileel. Amina.

MSOMAJI: Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya kaburi, aliwapatia uzima. *(mara tatu).*

Tukipokwisha kufikiri ufufuo wa Kristu, tumsujudie Mtakatifu wetu Bwana Yesu aliye peke bila zambi. Ee Kristu, tunausujudu msalaba wako, tunaimbia na kuutukuza ufufuo wako takatifu, kwa sababu wewe ni Mungu wetu, hatumjue tena mwengine ila wewe, jina lako tunalitaja, njooni waaminifu wote tuusujudie Ufufuo Takatifu wa Kristu; na tazama, kwa msalaba wake furaha yanapenya ulimwengu kote, bila ukomo tumutukuze Bwana na tuimbie Ufufuo wake, kwani alipoteswa msalabani kwa ajili yetu amebadilisha mauti kwa kifo chake, *(mara tatu).*

Waliposafirii alfajiri, wakakuta jiwe limekwisha fingirishwa kaburini, Maria na wenzie wakasikia malaika aliyewauliza: Sababu gani munatafuta miongoni mwa wafu Yeye aliye hai katika nuru ya milele? Tazameni utepe: Nendeni mbiyo kuelezea wote ya kwamba Bwana amefufuka akishinda kifo, maana ni Mwana wa Mungu aokoaye wanadamu.

Ulipolala kaburini, ee Bwana Msiyekufa ulivunja nguvu ya gehena na ulifufuka kwa ushindi, ee Kristu Mungu wetu, ukawaamuru wabebaji wa Manemane (Myrofore) kwa kufurahiwa; ukiwaangalia mitume wako ukawapa amani, ewe unayetuokoa na kutupa ufufuo.

Kaburini na Mwili wako, Kuzimu na Roho, kama Mungu, Paradizoni na munyanganyi mwema, unakaa kitini na Baba na Roho, ee Kristu unayekuwapo popote na kuujaza ulimwengu.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho mtakatifu.

Uliye na bei kuliko Paradizo, hakika, mwangavu kuliko makao ya mfalme, ee Kristu uliyetutokea, kaburi yako yaleta uhai: Yaliyo chemchem ya ufufuo wetu.

Sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

Furahiwa, ee makao iliyotakaswa. Hekalu kimungu ya Aliye-Juu sana, Mzazi-Mungu, ni kwa sababu yako ambako tumepewa furaha na tunakulilia ya kwamba: Umebarikiwa katika wanawake, Malkia bila doa.

Bwana hurumia (mara 40). Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku. . .

Uliye wa thamani kuwashinda wakheruvi, uliye na utukufu kuwapita bila kiasi wa Serafi, uliye ukimuzaa Mungu Neno, umebaki bila kukuharibu, uliye Mzazi-Mungu kweli tunakutukuza wewe.

Kwa jina la Bwana, bariki, ee padri.

PADRI: Kwa maombezi ya Mapadri Watakatifu wetu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe Amina. .

*Hii Ibada ile wakati ya Ufufuo wa Bwana Yesu Kristu tunaisoma mangaribi mara tatu pahali pa Sala ya Apodipnon Kidogo. Kisha ile mara tatu Padri anasoma na hii:*

Sala ya Mtakatifu Bazile:

Ewe Rabi Mwenyezi Mubarikiwa, ewe Uliyeangaza muchana na mwangaza ya jua na uliangaza usiku na mwangaza ya nyota, Wewe ulitustahilisha kupita siku nzima na kukaribia usiku. Sikia maombi yetu na ya watu wote na kutuhurumia makosa ya kujuwa ao ya bila kujuwa. Pokea sala zetu za Mangaribi na wingi wa rehema yako na wema wako kwa uriti wako. Malaika wako watakatifu watulinde. Utupe silaha yako ya haki, utuongoze na ukweli wako na nguvu yako. Utuokoe ku kila aibu na ku mutego ya shetani. Utupe mangaribi hii na usiku huu kamilifu, takatifu, amani yasiyo na zambi, yasiyo mnaso, bila mawazo mabaya hata siku zote za maisha yetu, kwa maombezi ya Mzazi-Mungu na ya Watakatifu wote, wale walio kupendeza toka milele. Amin.

MSOMAJI: Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya kaburi, aliwapatia uzima. *(mara tatu).* Kwa jina la Bwana bariki, ee padri.

PADRI: Uliye umefufuka katika wafu Kristu Mungu wetu wa kweli, kwa maombezi ya Mama wako Mtakatifu asiye na doa wala na lawama kamili. Kwa maombezi ya Yoane Nabii, Mtangulizi, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu, ya Mitume Watakatifu, watukufu, washindaji wazuri, ya Wapadri wetu Watawa na wabebaji-Mungu, ya Yoakimu na Anna Mababu-Mungu, Watakatifu, na wenye haki, hata ya Watakatifu wote, utuhurumie, ukatuokoe sawa Mungu Mwema, marahimu na mpenda-wanadamu. Kwa maombezi ya wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe.

PADRI: Kristu alifufuka katika wafu, kwa lufu alishinda mauti, kwa wale waliokuwa ndani ya kaburi, aliwapatia uzima. .

# DOKSOLOGIA UKUBWA YA SIKU KUU YA KITAIFA

SHEMASI: Ee Rabi barikia.
PADRI: Ahimidiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.
WAIMBAJI: Amina.
WAIMBAJI: Kondakion ya Mama Maria

Kwako jemadari kunilinda nina deni
kukushukuru kwa wokovu na kushinda wangu
mimi mji wako, ee Mzazi Mungu.
Tena kwa mamlaka yakosi kushindwa,
na hatari kila namna niepuwe kukuimba,
kwa kelele kuu: Salamu, Bibi Arusi, usiolewa.

## Doksologia ukubwa:

Utukufu kwako uliyeonyesha mwangaza, utukufu kwa Mungu juu pia; amani katika inchi mapendo kwa wanadamu.
Tukusifu, tukuhimidi, tukusujudu, tukutukuza, tukushukuru, maana utukufu wako ni mukubwa.
Ee Bwana Mufalmc Mungu wa yulu na mbinguni, Baba mwenyezi; Ee Bwana Mwana wa pekee Yesu Kristu, na wewe Roho Mutakatifu.
Ee Bwana Mungu we, Mwana Kondoo wa Mungu, Mwana wa Baba, unayezibeba zambi za dunia, utuhurumie, unayezibeba zambi za dunia.
Upokec ombi letu, Unayeketi kuume kwa Baba na kutuhurumia.
Kwa kuwa mutakatifu wa pekee, Bwana wa pekee Yesu Krtistu, katika utukufu wa Mungu Baba, Amina.

Kila siku nitakuhimidi, nitasifu jina 1ako la milele, hata milele na milele.
Ee Bwana, utujalie siku hii kutujilinda na zambi.
Umehimidiwa u, ee Bwana Mungu wa Baba zetu, jina lako Iimesifiwa na limetukuzwa milele. Amina
Ee Bwana, huruma yako iwe nasi, sawa tunakutumainia wewe.
Ee Bwana, umehimidiwa u, unifundishe zilizo haki zako. (mara tatu ).
Ee Bwana wewe U kimbilio letu kizazi baada ya kizazi. Mimi nilisema: ee Bwana unihurumie, uiponye roho yangu, maana nimekutendea zambi.
Kwa sababu kwako iko chemchem ya uzima, katika mwangaza yako tutaona rnwangaza. Onyesha huruma yako kwa wao wakujuwa.
Mungu Mutakatifu, Mweza Mutakatifu, Musiye kufa Mutakatifu, utuhurumie. *(mara tatu).*
Utukufu kwa Baba, na kwa Mwana na kwa Roho Mutakatifu.
Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.
Musiye kufa Mutakatifu, hutuhurumie.
Mungu Mutakatifu, Mweza Mutakatifu, Musiye kufa Mutakatifu, utuhurumie.

SHEMASI ao padri: Utuhurumie, ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba, utusikie na utuhurumie.
WAIMBAJI: Bwana hurumua. *(mara tatu).*
SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili wa wakristu wakristiani waorthodoksi wote.
WAIMBAJI: Bwana uhurumia. *(mara tatu).*
SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiepiskopo na Baba wetu (jina yake) na ya undugu wetu wote katika Kristu.
WAIMBAJI: Bwana hurumia . *(mara tatu).*
SHEMASI: Tena tunakuomba kwa agili ya Mukubwa wa Inchi yetu (jina lake), ya Taifa na waaskari na watu wote.
WAIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*
PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya wandugu wetu wenye walikufa kwa utukufu ya Taifa yetu, wa tangu zamani ao wa sasa, kwa ukumbusho wa pumziko ya heri ya mioyo yao milele na ya ondoleo ya zambi yao ya kusudi na yasiyo kusudi, ya ufahamu na yasiyofahamu.
WAIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*
SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Nyumba hii Takatifu, kila muji na kila Bara zilindiwe ku njaa, tauni, matetemeko ya udongo, garika, moto, silaha, ushambulio ya watu wageni na vita ili itufazilie, mkarimu na wepesi kwa kwinamisha Mungu wetu mwema na mpenda wanadamu, kwa ajili ya kwepusha hasira yoyote yenye kutwelekea na ili tuokolewe ku vitisho adilifu vinavyokuwa juu yetu na atuhurumie.
WAIMBAJI: Bwana hurumia, (mara makumi Ine).
PADRI: Utusikilize, ee Mungu Mwokozi wetu, tumaini wao wanaokaa mpaka za inchi za dunia na ya wao wanao mbali baharini na hewani na utufazilie, ee Rabi, kwa ajili ya zambi zetu na utuhurumie. Kwani wewe ndiwe Mungu wa huruma na rafiki ya wanadamu na tunakutukuza, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, sasa na siku zote hata miolele na milele.
WAIMBAJI: Amina.
SHEMASI: Tumwombe Bwana.
WAIMBAJI: Bwana hurumia.
PADRI: Tunakushukuru, ee Mungu wetu tunapokusanyika mara ingine siku hii mahali hapa mazuri na kwa ajili ya msaada wako tunakutukuza wewe;watawala na watu wote tunakusanyika pamoja nao kwa sababu tendo lako kubwa uliita kwa mkono wako wa kuhume. Sisi yote tunafurahini tunaposema: Utukufu kwako, utufundishe amri zako, ongaza watawala wetu na Taifa lote katika ukweli wako, kwani kandokando letu kuna maadui mengi; na heri ni Taifa letu lilindiwalo nawe.
PADRI: Tena tunakuomba kwa ajili ya mioyo ya ndugu zetu mashahidi.

WAIMBAJI:  Amina.  Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . Bwana hurumia *(mara tatu).*  ee Rabi mtakatifu barikia.
PADRI:  Kristu Mungu wetu wa kweli.  kwa maombezi ya Mama wake asiye na doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa Msalaba uheshimiwa na uhuitaji, kwa matunzo ya majeshi yaheshimiwe ya mbinguni yaliyo bila mwili.  kwa maombezi ya Yoanno Nabii, Mtakatifu, Mheshimiwa na Mtukufu; ya Mitume watakatifu, Watukufu, Wasifiwe kamili . . . (kutaja jina ya Mtakatifu wa Kanisa ile), ya Wapateri, Watakatifu, Watukufu, Washindaji wazuri, ya Wapateri Wabebaji-Mungu, ya Yoakim na Anna, Mababu Mungu, Watakatifu na wenye haki  (Mtakatifu wa hii siku) makumbusho yake leo, hata ya watakatifu wote atuhurumie, akatuokoe, yu Mungu mwema, Mrahimu na Mpenda wanadamu. Kwa maombezi ya wapadri wetu. . .
WAIMBAJI:  Amina.

# IBADA TAKATIFU YA WAFU   (PANNIHIDA)

*Kila mwaka tanafanya hii Ibada mara wa pili, nikusema Mukazi Tano Mangaribi, kisha Esperinos, mbele ya Juma ya Kufunga ( Apokreo) ile wakati ya Triodi na Mukazi Tano, kisha Esperinos, mbele ya Juma ya Pentekostii.  Kila Mwaminifu anaweza kufanya Koliva, nikusema kupika beko ya ngano pamoja na sukari na kuipeleka mu Kanisa ao kupeleka mukate  ao kapompo kwa makubusho na usamehe ya wa ndugu wao walikufa zamani na sasa.*
PADRI:  Abarikiwe Mungu wetu daima, sasa na siku zote, hata milele na milele.

MWIMBAJI:  Amina.
Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Msiye kufa Mtakatifu, utuhurumie  (Mara  tatu).  Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu. Sasa na siku zote, hata milele na milele.  Amina.
Utatu Mtakatifu kamili  utuhurumie, Bwana utusamehe zambi zetu, Rabi utuondolee makosa yetu, Mtakatifu utukaribie na utuponye magonjwa yetu, Bwana hurumia, Bwana hurumia, Bwana hurumia.

Utukufu kwa Baba na kwa Mwana na kwa Roho Mtakatifu.  Sasa na  siku zote, hata milele na milele.  Amina.
Baba yetu Uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje  mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama kule mbinguni.  Utupe sisi  leo chakula chetu cha kila siku, utusamehe ndeni zetu, kama sisi vilevile  tunavyosamehe wadeni wetu.  Na usitutie katika majaribu, lakini utuokoe na yule Mwovu.

PADRI:  Kwa kuwa ufalme, uwezo na utukufu ni wako, wa Baba na wa Mwana  na wa Roho Mtakatifu.  Sasa na siku zote, hata milele na milele.

Mwimbaji atasoma Zaburi 90(91)
Yeye anayekaa kwa pahali pa mafícho yake aliye juu atakaa chini  ya kivuli cha Mwenyezi. Nitasema juu ya Bwana, yeye ni pahali pangu  pa kukimbilia na boma la nguvu langu, Mungu wangu ninayemwamini. Kwa  maana atakuokoa toka mutego wa muwindaji ndege, na kwa tauni ya uharibifu. Na  manyoya yake atakufunika. Na chini ya mabawa yake utakimbilia.  kweli yake ni ngabo na kigabo. Hutaogopa kwa woga wa usiku, wala kwa mushale  unaoruka muchana; kwa tauni inayotembea katika giza, wala kwa kuharibu  kunakoharibu azuhuri, elfu moja wataanguka kando yako, na elfu kumi  kwa mukono wako wa kuume; lakini hakutafika karibu nawe. Na macho yako  tu utatazama, na kuona zawabu ya waovu. Maana wewe, ee Bwana, ni pahali  pangu pa kukimbilia! Umefanya aliye juu kao lako; Mabaya hayatakupata wewe wala tauni haitafika na hema yako. Maana ataagiza malaika yake  juu yako, wakuchunge katika njia zako zote. Watakuchukua juu mikononi mwao, usivunje muguu wako kwa jiwe. Takanyaga simba na nyoka mudogo  mwenye sumu,

utakanyaga mwana-simba na joka. Kwa sababu ametia mapendo yake juu yangu. kwa hivi nitamuponyesha. Nitamuweka juu kwa sababu amejua jina langu. Ataniita na nitamujibu; nitakuwa pamoja naye katika taabu; nitamuponyesha na kumuheshimu. Kwa maisha ndefu nitamushibisha, na kumwonyesha wokovu wangu.

*Kisha Padri na mwimbaji wataimba Alliluya mara kumi na pili, nikusema mara Ine Alliluya mara tatu.*

Mwimbaji atasoma Zaburi 118(119) (Amomos).

Heri wao walio kamilifu kwa njia yao, Wanaotembea katika sheria ya Bwana. Heri wale wanaoshika shuhuda zake, wanaomutafuta kwa moyo wote. Ndiyo, hawatendi uzalimu; wanatembea katika njia zake. Umetuagiza maagizo yako, ili tuyatii sana. Ningependa njia zangu zisimamishwe, nitii amri zako. Halafu sitapata haya, wakati ninapoangalia maagizo yako yote. Nitakushukuru kwa moyo ulio haki, wakati ninapofundishwa hukumu zako zenye haki. Nitatii amri zako: Ee, usiniache kabisa. Kijana atasafisha njia yake na nini; Kwa kutii, akifuata neno lako. Nimekutafuta kwa moyo wangu wote; Usiniache kupotea mbali na maagizo yako. Nimeficha neno lako moyoni mwangu, nisikukosee. Umebarikiwa, Ee Bwana: Unifundishe amri zako. Kwa midomo yangu nimetangaza Hukumu zote za kinywa chako. Nimefurahi kwa njia ya shuhuda zako, sawasawa kwa mali zote. Nitafikili maagizo yako, na kuangalia ngia zako: Sitasahau neno lako. Utendee mutumishi wako kwa ukarimu, ili nipate kuishi; Hivi nitatii neno lako. Ufungue macho yangu, nipate kuona maajabu yanayotoka katika sheria yako. Mimi mugeni katika inchi: Usinifichie maagizo yako. Nafsi yangu inavunjika kwa hamu niliyo nayo kwa hukumu zako wakati wote. Umekemea wenye majivuno wanaolaaniwa, wanaokwenda mbali ba maagizo yako. Uniondolee laumu na zarau; kwa maana nimeshika shuhuda zako. Wakubwa vilevile wakaketi, wakasema juu yangu: Lakini mutumishi wako akafikili amri yako. Shuhuda zako ni furaha yangu, na washauri wangu. Nafsi yangu inaambatana na mavumbi: Unipatize uzima sawasawa na neno lako. Nimesimulia njia zangu, nawe ulinijibu: Unifundishe amri zako. Unifahamishe njia ya maagizo yako: Hivi nitafikili kazi zako za ajabu. Nafsi yangu inayeyuka kwa uzito: Unipatize nguvu sawasawa na neno lako. Uniondolee njia ya uwongo: Unipe sheria yako kwa neema. Nimechagua njia ya uaminifu: Nimeweka hukumu zako mbele yangu. Ninaambatana na shuhuda zako: Ee Bwana, usinihayarishe. Nitakwenda mbio katika njia ya maagizo yako, wakatyi utakaponiongezea moyo wangu. Unifundishe, ee Bwana, njia ya amri zako: Nami nitaishikia hata mwisho. Unipe ufahamu, nami nitashika sheria yako; Ndiyo, nitaitii, kwa moyo wangu wote. Unitembeze katika njia ya maagizo yako; Kwa maana ninapendezwa nayo. Unielekee moyo wangu na shuhuda zako, wala si na tamaa. Ugeuze macho yangu mbali na kutazama ubatili, na unipatize uzima katika njia zako. Usimamishe neno lako kwa mutumishi wako, anayekuogopa. Uniondolee laumu ninaloogopa; Maana hukumu zako ni njema. Tazama, nimekuwa na hamu sana kwa maagiko yako: Unipatize uzima katika haki yako. Rehema zako zije kwangu, ee Bwana, hata wokovu wako, sawasawa na neno lako. Hivi nitaweza kumujibu yeye anayenilaumu; kwa maana ninatumainia neno lako. Wala usiondoe neno la kweli kinywani mwangu kabisa; Maana nimetarajia hukumu zako. Hivi nitashika sheria yako daima, milele na milele. Na nitatembea huru kwa kuwa nimetafuta maagiko yako. Nitasema juu ya shuhuda zako vilevile mbele ya wafalme, wala sitakuwa na haya. Nitajifurahisha sana kwa maagiko yako niliyoyapenda. Ninanyanyua mikono yangu vilevile kwa maagizo yako niliyoyapenda; Na nitafikili amri zako. Kumbuka neno ulilomwambia mutumishi wako, kwa sababu umenitumainisha. Hii ni taraja yangu katika taabu yangu: Ya kwamba neno lako limenipatiza uzima. Wenye majivuno wamenizihaki sana: Hata hivi sikugeuka mbali na sheria yako. Nimekumbuka hukumu zako za kale, ee Bwana, na nilijifariji. Hasira yenye moto imenishika, kwa ajili ya waovu wanaoacha sheria yako. Amri zako zimekuwa nyimbo zangu katika nyumba ya kusafiri kwangu. Nimekumbuka jina lako, ee Bwana, wakati wa usiku, na nimetii sheria yako. Maneno haya nilikuwa nayo, kwa sababu nimeshika amri zako. Bwana ni sehemu yangu: Nimesema ya kuwa nitatii maneno yako. Nimeomba upendeleo wako kwa moyo wangu wote: Nilifikili njia zangu, nikageuza miguu yangu kwa shuhuda zako. Nikafanya mbio, wala

sikukawia, kutii maagizo yako. Kamba za waovu zimenizunguka; Lakini sikusahau sheria yako. Katikati ya usiku nitasimama kukushukuru kwa sababu ya hukumu zako za haki. Mimi ni mwenzao wa watu wote wanakuogopa, na wao wanaotii mafundisho yako. Dunia, ee Bwana, inajaa rehema yako: Unifundishe amri zako. Umetendea mema mutumishi wako, ee Bwana, sawasawa na neno lako. Unifundishe hukumu njema na hekima; Maana nimeamini maagizo yako. Wakati sijateswa bado, nikapotea; Lakini sasa ninatii neno lako. Wewe ni mwema, nawe unatenda mema; unifundishe amri zako. Wenye majivuno wamefanya uwongo juu yangu; na moyo wangu wote nitashika mafundisho yako. Moyo wao umenipa kama mafuta; Lakini mimi ninafurahia sheria yako. Ilikuwa vema kwangu kuteshwa; Ili nijifundishe amri zako. Sheria ya kinywa chako ni njema kwangu kuliko elfu za zahabu na feza. Mikono yako imenifanya na kunitengeneza: Unipe ufahamu, ili nijifundishe maagizo yako. Wao wanaokuogopa wataniona na kufurahi; Kwa sababu nimetarajia neno lako. Ninajua, ee Bwana, ya kuwa hukumu zako ni za haki, na kwa uaminifu wako umenitesa. Wema wako, ninakuomba, uwe faraja yangu, sawasawa na neno lako kwa mutumishi wako. Rehema zako zije kwangu, ili nipate kuishi: Maana sheria yako ni furaha yangu. Wenye majivuno wahayarishwe, maana wameniangusha kwa uwongo: Wale wanaokuogopa wageuke kwangu, nao watajua shuhuda zako. Moyo wangu uwe mukamilifu katika amri zako: Nisipate haya. Nafsi yangu inalegea kwa kutamani wokovu wako: Ninatarajia neno lako. Macho yangu yanapunguka kwa kutamani neno lako, wakati ninaposema: Wakati gani utanifariji? Maana nimekuwa kama chupa katika moshi; Hata hivi sisahau amri zako. Siku za mutumishi wako na ngapi? Wenya majivuno wamenichimbia mashimo, wasiofuata sheria yako. Maagizo yako yote ni maaminifu, wananitesa bule; unisaidie. Walikuwa karibu na kuniharibu katika inchi; Lakini sikuacha mafundisho yako. Unipatize uzima kwa wema wako; Hivi nitatii ushuhuda wa kinwa chako. Kwa milele, e Bwana, neno lako ni imara mbinguni. Uaminifu wako ni kwa vizazi vyote; Umeweka inchi, nayo inakaa. Kwa hukumu zako vimekaa hata leo; Maana vitu vyote ni watumishi wako. Kama sheria yako isigalikuwa furaha yangu, kama ningalipotea katika taabu yangu. Sitasahau mafundisho yako kamwe; maana umenipatiza uzima nayo.

*Padri anaimba ile mustari ya mwisho:* Sitasahau mafundisho yako kamwe; maana umenipatiza uzima nayo.
Na Padri ingine ao Mwimbaji ataimba hii mustari ya mwisho mara ya pili.

PADRI ao SHEMASI: Utuhurumie, ee Mungu, kwa huruma yako kubwa, tunakuomba sikiliza na hurumia.
MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*
PADRI ao SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya wakristu, watawa na waorthodoksi wote.
MWIMBAJI: Bwana hurumia *(mara tatu).*
PADRI ao SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Mwarkiepiskopo wetu (jina lake).
MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*
PADRI ao SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Raisi Mukubwa yetu (jina lake), ya watawala, Taifa, waaskari na watu wote.
MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*
PADRI ai SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya wandugu wanaogombana vita kwa utukufu wa Taifa letu, wa tangu zamani ao wa sasa kwa ukumbusho wa pumziko ya heri ya mioyo yao milele na ya ondoleo ya zambi yao ya kusudi na yasiyo kusudi, ya hufahamu na yasiyofahamu.
MWIMBAJI: Bwana hurumia . *(mara tatu).*
PADRI ao SHEMASI: Tena tunakuomba mapumziko ya moyo wa watumishi wa Mungu tangu mwanzo ya dunia mupaka sasa na uwasamehe makosa yao yote ya kupenda na yasiyo kupenda.
MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*
SHEMASI: Tumwombe Bwana.
MWIMBAJI: Bwana hurumia.

PADRI: Ee Mungu wa roho na wa mwili, uliyeshinda lufu na kumuharibu shetani, wewe uliyeleta uzima duniani, leta, ee Bwana, mapumuziko kwa roho ya watumishi wako pahali pa mwangaza, pa majani mazuri, pa mapumziko, kule kunakimbia maumivu, sikitiko na masumbuko. Uwasamehe zambi zao zote walitenda kwa sauti, kwa matendo na kwa mawazo, kwa sababu Wewe ni Mungu Mwema na Mpenda-wanadamu; kwani hakuna mutu hata moja, anakaa mu uzima huu pasipo kufanya zambi; kwa sababu wewe peke yako msiye zambi; haki yako, ni
haki ya milele, na amri yako na ya kweli.
SHEMASI: Tumwombe Bwana:
MWIMBAJI: Bwana hurumia.
PADRI: Kwa kuwa wewe ni Ufufuo, uzima na mapumziko ya milele ua watumishi wako wamelala, Kristu Mungu wetu, na kwako tunatoa utukufu, pamoja na Baba yako wasipo mwanzo, na Roho Mtakatifu wako kamili, Mwema, Mpaaji wa uzima, sasa na siku zote, hata milele na milele.
MWIMBAJI: Amina.

*Msomaji anaendelea kusoma ingina kipande ya Amomos (Zaburi 118(119)*

Mimi ni yako, uniokoe; kwa maana nimetafuta mafundishi yako. Waovu wameningojea ili waniharibu; lakini agizo lako ni pana sana. Ee ninapenda sana sheria yako! Ni mawazo yangu muchana kutwa. Maagizo yako yananitia hekima kuliko adui zangu; maana ni pamoja nami siku zote. Nina ufahamu kupita walimu wangu wote; Maana shuhuda zako ninazifikili. Ninafahamu kupita wazee, kwa sababu nimetii mafundisho yako. Nimezuiza miguu yangu na kila njia mbaya, ili nitii neno lako. Sikugeuka mbali na hukumu zako; Maana wewe mwenyewe umenifundisha. Maneno yako ni matamu sana kwangu! Kupita asali kwa kinywa changu. Kwa njia ya mafundisho yako ninapata ufahamu: Kwa hivi ninachukia kila njia ya uwongo. Neno lako ni taa kwa miguu yangu, na nuru kwa njia yangu. Nimeapa na kahakikisha, ya kuwa nitashika hukumu zako za haki. Nimeteswa sana: Unipatize uzima, ee Bwana, sawasawa na neno lako. Upokee, ninakuomba, sadaka za moyo za kinywa changu, ee Bwana, na unifundishe hukumu zako. Nafsi yangu ni mukononi mwangu daima; Hata hivi sisahau sheria yako. Waovu wameniwekea mutego; Hata hivi sikuopotea mbali na mafundisho yako. Nimefanya shuhuda zako kuwa uriti wangu daima; Maana ni furaha ya moyo wangu. Nimeelekeza moyo wangu kutenda amri zako, daima hata mwisho ninachukia wenye nia mbili; lakini ninapenda sheria yako. Wewe ni maficho yangu na ngabo yangu: Ninatarajia neno lako. Muniondokee, ninyi watenda mabaya; Ili nishike maagizo ya Mungu wangu. Unitegemeze sawasawa na neno lako, ili nipate kuishi; wala usiniache kuhayarishwa kwa sababu ya taraja yangu. Unitegemeze, nami nitakuwa na salama, na nitaangalia amri zako daima. Umefanya si kitu wote wanaopotea mbali na amri zako; Kwa maana hila yao ni mwongo. Unaondosha waovu wote wa inchi kama takataka;kwa hivi ninapenda shuhuda zako. Mwili wangu unatetemeka kwa kukuogopa; na ninaogopa hukumu zako. Nimefanya hukumu na haki: Usiniache kwa watesi wangu. Uwe zamana kwa mutumishi wako apate mema: Wenye majivuno wasinitese. Macho yangu yanalegea kwa wokovu wako, nakwa neno lako lenye haki. Utendee mutumishi wako sawasawa na rehema yako, na unifundishe amri zako. Mimi ni mutumishi wako, unipe ufahamu; ili nijue shuhuda zako. Ni wakati kwa Bwana kutenda kazi; Kwa kuwa wamefanya sheria yako bule. Kwa hivi ninapenda maagizo yako kupita zahabu, ndiyo, kupita zahabu iliyo safi. Kwa hivi ninaona mafundisho yako yote kywa na haki; Na ninachukia kila njia ya uwongo. Shuhuda zako ni za ajabu: Kwa hivi nafsi yangu inazishika. Kufunua kwa maneno yako kunaleta nuru; kunamupa mujinga ufahamu. Nikafungua kinywa changu wazi, ninakokota roho; maana nilitamani maagizo yako. Ugeuke kwangu na unirehemie, kama ulivyofanyaga nao wanaopenda jina lako. Agiza hatua zangu katika neno lako; Wala uovu wo wote usinitawale. Unikomboe na mateso ya mutu: Hivi nitashika mafundisho yako yote. Uangazie mutumishi wako uso wako;na unifundishe amri zako. Mito ya maji inetelemuka toka macho yangu, kwa sababu hawatii sheria yako. Wewe ni mwenye haki, ee Bwana, na hukumu zako ni za haki. Umeagiza shuhuda zako kwa haki na kwa uaminifu mwingi. Bidii yangu imenimaliza, kwa sababu watesi wangu wamesahau maneno yako. Neno lako ni safi kabisa; kwa hivi sisahau mafundisho yako. Haki yako ni haki ya milele, na sheria yako ni kweli. Taabu na uchungu

zimenishika: Hata hivi maagizo yako ni furaha yangu. Shuhuda zako ni za haki kwa milele: Unipe ufahamu na nitaishi. Nimeita kwa moyo wangu wote; unijibu, e Bwana: Nitashika amri zako. Nimekuita; uniokoe, na nitatii shuhuda zako. Nimetangulia mapambazuko ya asubui, nikalia: Nilitarajia maneno yako. Macho yangu yalitangulia makesha ya usiku, ili nipate kufikili neno lako. Usikie sauti yangu sawasawa na wema wako: Unipatize uzima, ee Bwana, sawasawa na hukumu zako. Wanakaribia wanaofuata uovu; Wao ni mbali na sheria yako. Wewe ni karibu, ee Bwana; Na maagizo yako yote ni kweli. Tangu zamani nilijua toka shuhuda zako, ya kuwa umeziweka kwa milele. Fikili mateso yangu na uniokoe; maana sisahau sheria yako. Uniombee na kuniokoa; Unipatize uzima sawasawa na neno lako. Wokovu ni mbali nawaovu; Maana hawatafuti amri zako. Rehema zako ni kubwa, ee Bwana: Unipatize uzima sawasawa ma hukumu zako. Wenye kunifuata na watesi wangu ni wengi; Hata hivi sikwenda mbali na shuhuda zako. Nikaona wadanganyifu, nikawachukia; kwa sababu hawatii neno lako. Uangalie namna ninavyopenda mafundisho yako: Unipatize uzima, ee Bwana, sawasawa na wema wako. Jumla ya neno lako ni kweli; Na kila moja ya hukumu zako zenye haki ni ya milele. Wakubwa wamenitesa bule; Lakini moyo wangu unaogopa maneno yako. Ninafurahia neno lako, kama mwenye kupata mateka mengi. Ninachukia na kuchukizwa sana na uwongo; Lakini ninapenda sheria yako. Mara saba kila siku ninakusifu, kwa sababu ya hukumu zako za haki. Salama kubwa ni yao wanaopenda sheria yako; nao hawana njia ya kukwaa. Nimetarajia wokovu wako, ee Bwana, na nimefanya maagizo yako. Nafsi yangu imetii shuhuda zako; Na ninazipenda sana. Nimetii mafundisho yako na shuhuda zako;maana njia zangu zote ni mbele yako. Kilio changu kikukaribie, ee Bwana: Unipe ufahamu sawasawa na neno lako. Kusihi kwangu kuje mbele yako: Uniponyeshe sawasawa na neno lako. Midomo yangu itoe sifa; Kwa kuwa unanifundisha amri zako. Ulimi wangu uimbe juu ya neno lako; Maana maagizo yako yote ni haki. Mukono wako uwe tayari kunisaidia; maana nimechagua mafundisho yako. Nimetamani sana wokovu wako, ee Bwana; Na sheria yako ni furaha yangu. Nafsi yangu iishi, na itakusifu; Na hukumu zako zinisaidie. Nimepotea kama kondoo mupotevu; utafute mutumishi wako; Kwa maana sisahau maagizo yako.

*Padri anaimba ile mistari wa pili ya mwisho:* "Nafsi yangu iishi. . . " na kisha ataiimba mara moya na padri ingine ao mwimbaji.

## MAHIMIDI YA WAFU (EVLOGITARIA)

Ee Bwana, umehimidiwa U. unifundishe zilizo haki zako.

Kundi la Watakatifu, lilipata chemchem ya uzima na mulango wa Paradizo; na mimi nitapata njia kwa kutubu; mimi ni kondoo mupotevu; uniite tena, ee Mwokozi, na uniokoe.

Ee Bwana, umehimidiwa U. . .

We wa zamani, uliniumba toka si kitu, na ulinisifu kwa sura yako takatifu, lakini juu ya kuvunja amri, ulinirudisha tena ku udongo kule ulinitosha; kwa mufano wako sasa unirudisha; na ufanye mara ingine uzuri wangu wa kwanza.

Ee Bwana, umehimidiwa U. . .

Mimi ni sura, ya utukufu wako usiyonewa, hata niko na alama ya zambi;ee Rabi unirehemu kiumbe chako, na unisafishe kwa wema wako, tena unipatie inchi ninayotamania, unifanye mara ingine mwana inchi wa Paradizo.

Ee Bwana umehimidiwa U. . .

Ee Mungu, pumzisha mtumishi (Wa) wako, na u(uwa)mupangishe katika Paradizo, fasi ya kundi la watakatifu, ee Bwana, na wenyi haki watangaa sawa nyota za mwangaza; u(uwa)mupumzishe mu(wa)tumishi wako huyu (hawa) anayelala(wanao), umusamehe (uwa) zambi zake (zao) zote.

Utukufu kwa Baba na kwa Bwana na kwa Roho Mtakatifu

Tuimbe na kupaza sauti; kwa uaminifu mianga tatu ya umungu moja; ewe Mtakatifu, Baba wasiyo mwanzo, Mwana aliye na baba bila mwanzo na Roho Mtakatifu;angaza sisi tuliokuabudu kwa imani, na utuopoe ku moto ya milele.

Sasa na siku zote hata milele na milele. Amina.

Salamu Muheshimiwa, uliyemzaa Mungu mwilini, juu ya wokovu wa wote, kwa ajili yako kabila la wanadamu ilipara wokovu; katika yako tutapata Paradizo, Mzazi-Mungu, safi mbarikiwa.

Alliluia, Alliluia, Alliluia, utukufu kwako, ee Mungu. *(mara tatu).*

SHEMASI: Utuhurumie, ee Mungu, kwa huruma yako kubwa, tunakuomba sikiliza na hurumia.

MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*

SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya wakristu , watawa na waorthodoksi wote.

MWIMBAJI: Bwana hurumia . *(mara tatu).*

SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Askofu Mukubwa yetu (jina lake).

MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*

SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya Mukubwa ya Inchi yetu (jina lake), ya Taifa, waaskari na watu wote.

MWIMBAJI: Bwana hurumia. *(mara tatu).*

SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya wandungu wanaogombana nvita kwa utukufu na uhuru wa Taifa letu, wa tangu zamani ao wa sasa kwa ukumbusho wa pumziko ya heri ya mioyo yao milele na ya ondoleo ya zamani yao ya kusudi na yasiyo kusudi, ya hufahamu na yasiyofahamu.

MWIMBAJI: Bwnana hurumia *(mara tatu)*..

SHEMASI: Tena tunakuomba mapumziko ya moyo wa mu(wa)tumishi wa Mungu, na u(uwa)musamehe makosa yake(yao) yote ya kupenda na yasiyo kupenda.

MWIMBAJI: Bwana hurumia *(mara tatu)*..

PADRI: Ili, Bwana Mungu, aweke moyo pahali wenyi haki wanapumzika, tunaomba rehema ya Mungu, ufalme wa mbinguni, na maondoleo ya zambi zake (zao), kwa Kristu Mfalme msiye kufa na Mungu wetu.

MWIMBAJI: Amina.

SHEMASI: Tumwombe Bwana.

MWIMBAJI: Bwana hurumia.

PADRI: Ee Mungu wa roho na wa mwili, uliyeshinda lufu. . . . *(angalia yulu).*

PADRI: Tumwombe Bwana.

MWIMBAJI: Bwana hurumia.

PADRI: Kwa kuwa Wewe ni ufufuo, uzima na mapumziko. . . *(angalia yulu).*

MWIMBAJI: Amina.

MSOMAJI *anasoma Zaburi 50(51).*

# KANUNI YA WAFU

## Wimbo ya kwanza.

Kwa maombezi ya Mashahidi Wako, ee Bwana, umpumzishe roho ya watumishi wako.

Ee Kristu, Mashahidi Watakatifu wanakuomba daima katika uwanja ya mbinguni kwa ajili wa waamini waliofariki ili uwape sehemu ya uriti wa mema ya milele.

Roho zao zipumzike mahali pa wema

Wakati ulitengeneza kiumbe, ukaniweka ku panda-njia ya ulimwengu, ukamuumba mtu kwa udongo toka si kitu na akawa wa milele: Ee Mwokozi, pumzisha roho wa waaminifu watumishi wako.

Utukufu kwa Baba. . .

Ku mwanzo uliniweka kuwa raia na mchungaji wa Paradizo tena ukanifukuzamo wakati nilivunja amri yako: Ee Bwana, pumzisha roho za waaminifu Wako.

Sasa na siku zote. . .

Huyu zamani kwa ubavu moja aliumba Eva babu wetu, alizaliwa tumboni mwako takatifu mwenyi kuchukua mwili wetu, na kwa hii ee Bikira Mtakatifu Kamili, aliharibu nguvu ya mauti.

## Wimbo ya tatu.

Kwa maombezi. . .

Ee Chemchem ya uzima, Mashahidi wako walishindana vema na walipokea Kwako taji ya washindaji; roho za marehemu waaminifu zipate katika wao ukombozi wa milele.

Roho zao. . .

Ya kwanza, uliponifundisha kwa miujiza ya nuru, ku mwisho ukajishusha katika huruma yako kubwa, na mimi kondoo mwenye kupokea ambaye uliyetafuta uliponipata, ukanipa uzima.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Bwana, wale waliopita karibu nawe na uzaifu wa hii uzima uwape wakae na furaha katika makao ya milele: Uwahakikishe kwa imani na mapendo.

Sasa na siku zote. . .

Hakuna hata mmoja aliye safi kuliko Wewe, ee Mtakatifu Mzazi-Mungu, kwani peke yako ulipata safi ya Mungu wa milele, mkubwa na wa ukweli aliyeharibu nguvu ya mauti.

SHEMASI: Tena na tena ku amani tumwombe, Bwana.
MWIMBAJI: Bwana hurumia.
SHEMASI: Tena tunakuomba kwa ajili ya wakristu, watawa na waorthodoksi wote.
MWIMBAJI: Bwana hurumia.
SHEMASI: *( Angalia yulu Ekteni kiloko).*
PADRI: Kwa kuwa Wewe ni Ufufuo, Uzima na mapumziko ya watumishi wako. . . . .
WAIMBAJI: KATHISMA Sauti ya Sita
Kweli iko ulimwengu ya bure na maisha yetu kivuli na ndoto. Basi kila mwanainchi anaogopa kwa bure, sawa ilituonesha Madiko; wakati dunia tutaiala, mara moja ku kaburi tutaingia, pahali weko pamoja wafalme na masikini;kwa ivi, ee Kristu Mungu, kama mpenda wanadamu aliyelala pumuzisha kwa milele.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa niku zote. THEOTOKION.
Mtakatifu Kamili, ee Mzazi-Mungu, usiniache katika maisha yangu, usinitoe ku shime ya kinadamu, lakini wewe mwenyewe unilinde na unihurumie.

## Wimbo ya ine.

Kwa maombezi. . .

Ee Bwana, ulipowaonyesha alama za hekima ya kabisa na ya wema wako wenyi ukarimu wa zawadi, ukewaweka Mashahidi Watakatifu ku hesabu ya Malaika katika mbinguni.

Roho zao. . .

Ee Kristu, uwape utukufu wako usiyokadirika wale waliopita karibu nawe na wanakaa katika makao ya heri kule kunasikilika daima wimbo wa furaha.

Utukufu. . .

Ee Mungu wa mapendo, wale ulioomba kwa udongo uwape waimbie ufalme wako kimungu milele: Ukiwatakasa ku zambi yote, uwagewuze kuwa wana wa nuru.

Sasa na siku zote. . .

Wewe ni kikombe safi kamili tena hekalu takatifu, safina ya agano takatifu, mahali ya utakatifu wote, utukufu na ubikira wa Yakobo, Wewe ni mteule wa Bwana Mungu wetu.

## Wimbo ya tano.

Kwa maombezi. . .

Kama sadaka takatifu na malimbuko ya wanadamu, Mashahidi Watakatifu walitolewa kwa Mungu aliyewatukuza; sasa na daima wanatupatia neema ya wokovu.

Roho zao. . .

Ee Bwana, uwape waaminifu watumishi wako waliolala mbele yetu maondoleo ya zambi; makao ya mbinguni na sehemu ya zawadi zako.

Utukufu kwa Baba. . .

Kwa desturi, peke yako ni mwenyi kuleta uzima ku ulimwengu; bahari ya wema isiyoweza kufumbuliwa, Mungu wa mapendo, peke Yako msiyekufa, ee Bwana, uwape marehemu watumishi wako ufalme wa mbinguni.

Sasa na siku zote. . .

Ee Malkia wa ulimwengu, huyu aliyezaliwa Kwako amekuwa nguvu, wokovu na sifa ya roho zenye kupotea alizookoa toka milango ya Hadeze sababu ya kutukuza jina lako katika imani.

## Wimbo ya sita.

Kwa maombezi. . .

Ee Bwana, maandamano ya Mashahidi waliokufwata katika mateso Yako wakati uliposulubiwa msalabani uliyakusanya karibu yako:  Ee Mungu wa wema, tunakuomba, uwape marehemu mapumziko ya milele.

Roho zao. . .

Ee Mwokozi, ku ile siku ya ajabu wakati utakapokuja katika utukufu juu ya mawingu mbinguni sababu ya kuhukumu dunia yote, uwape waaminifu watumishi wako kwa kukutana pamoja nawe katika nuru ya milele.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Bwana, Wewe ni Chemchem ya uzima na kwa nguvu yako ya umungu uliondoa wafungwa ku Hadeze:  Ndiyo maana tunakuomba uwape watumishi waliokupata katika imani makao ya heri na malimbuko ya Paradizo.

Sasa na siku zote. . .

Zamani, tulipovunja amri takatifu ya Bwana, tukarudi ku udongo, lakini katika Wewe, ee Bikira, tunapanda mara ingine mbinguni toka dunia kisha kukunguta uvumbi ya kaburi.

*Ekteni kiloko sawa ilifanyikwa kisha Wimbo wa Tatu.*

## KONDAKION

*Tunaimba hii sauti ya Mnane*

Pamoja na watakatifu, pumzisha, ee Kristu, roho ya watumishi wako, mu fasi pasipo umivu, bila sikitiko, bila muchoko lakini uzima wa milele.

## IKOS

Paka Wewe wa pekee uko musiyekufa, uliyeumba mutu;Sisi wote toka inchi tuliumbwa na kwa hii inchi tutarudia, sawa vile Wewe uliniumba na uliniambia; ya kama inchi uwe na kwa inchi utakwenda;pahali fasi sisi watu wa inchi tutakwenda na tutaimba mwimbo ya kaburi, Alliluia.

## Wimbo ya saba.

Kwa maombezi. . .

Kwa damu yako Mashahidi waliokombolewa ku uhalifu wa kwanza na kusafishwa kwa damu yao walioonyesha waziwazi sadaka yako takatifu: ee Bwana Mungu wa baba zetu, umetukuzwa.

Roho zao. . .

Ulipoangusha mauti, ee Neno Chemchem ya uzima, pokea sasa karibu Yako wale waliolala katika imani; wanaimbia utukufu wako wakisema: Ee Bwana Mungu wa baba zetu, umetukuzwa.

Utukufu kwa Baba. . .

Kwa pumzi Yako ya umungu ulifufua wanadamu; ee Mungu mkuu na Mwokozi, pokea marehemu ufalme wako ili wakuimbie: Ee Bwana Mungu wa Baba zetu, umetukuzwa.

Sasa na siku zote. . .

Ncha ya viumbe, ee Bikira Safi kamili, ulipata mimba ya Mungu mshindaji wa mauti aliyevunja milango ya Hadeze, sisi waaminifu tunakuimbia, ee Mtakatifu kamili, kama Mzazi-Mungu.

## Wimbo ya mnane.

Kwa maombezi. . .

Enyi washindaji wahodari. wa Kristu, muliposhindana kwa moyo mkuu, mulipokea taji ya washindaji mukiimba: Ee Kristu, tunakutukuza milele.

Roho zao. . .

Ee Bwana kwa waaminifu waliacha hii uzima na waliopata karibu Yako, kwa neema Yako uwapumzisha ili wakutukuze milele.

Utukufu kwa Baba. . .

Ee Mwokozi, pokea mu uwanja wako marehemu wenye haki wa dunia; uwahakikisha kwa ajili ya imani waliokutumainia, ili wakutukuze milele.

Sasa na siku zote. . .

Ee Bikira mtukufu, tunakuita mwenye heri wewe uliyezaa kwa ajili yetu mwilini Neno la mbinguni tena mwenyi heri ambaye tunatukuza milele.

## Wimbo ya tisa.

*Tunaimba hii Wimbo sauti ya sita*

Kwa maombezi. . .

Ee Bwana, Matumaini kimungu ilisabitisha makundi ya Mashahidi, na kivukutu yake yote kama juu ya mabawa ikawachukua mpaka ku mapendo Yako, wakatangulia kuonyesha mapumziko imara ya Siku zijao ambayo utakaowapa marehemu kwa wema wako.

Roho zao. . .

Ee Kristu, wema Wako uwape marehemu waaminifu kupata nuru yako ya umungu yenyi kuangaa! Uwape mapumziko katika kifua cha Abrahamu wewe peke Yako mwenye huruma, na uwastahilisha, ee Bwana, wapate heri ya milele.

Utukufu kwa Baba. . .

Tangu mwanzo Wewe ni wema na rehema, wewe mwenye kupenda wema. Bahari ya huruma ya milele: Kwa wale uliyoondoa kwa hii fasi ya upotevu na ku kivuli cha mauti, uwape nuru yako ya milele.

Sasa na siku zote. . .
Ee Bikira Safi, wewe na Safina ya agano, hema takatifu, meza ambako inaandikwa Amri ta mapendo; kwa ajili yako maondoleo ya zambi inapewa kwa waaminifu wenye kuhakikisha kwa damu ya huyu aliyejifanya mutu tumboni mwako, ee Bikira Mtakatifu.

*Kisha Trisagio*: Mungu Mutakatifu. . . . Utatu Mtakatifu. . . Baba yetu. . .

*Kisha tunaimba Hii wimbo sauti ya Ine*
(Meta pnevmaton dikeon)

Pamoja na roho za wenyi haki kamilifu, ee Mwokozi, pumzisha roho ya watumishi wako na uichunge hii mu uzima wa heri uliyo karibu nawe, ewe rafiki ya wanadamu.

(Is tin katapafsin su)

Pa fasi ya ukimya, ee Bwana, kule watakatifu wote wanapumzika, pumzisha na roho ya watumishi wako, kwa sababu wewe ni msiye kufa.

Utukufu kwa Baba. . .
(Si i o Theos imon)

Wewe Mungu wetu, ulishuka kuzimu na kufungua maumivu ya wafungwa, Ewe mpumzisha na roho ya watumishi wako, Mwokozi.

Sasa na siku zote (I moni Agni)

Wewe peke safi na asiye doa Bikira, uliyemzaa Mungu msiye kufa wa kusemwa, umuombe aokoe roho ya watumishi wake.

SHEMASI: Utuhurumie, ee Mungu, kwa huruma kubwa, tunakuomba sikiliza na hurumia.
*Vile ataendelea Shemasi yote sala yake sawa yulu.*
*Padri atasoma hii sala ya yulu:* Ee Mungu wa roho na wa mwili, uliyeshinda lufu. . . . .
PADRI: Kwa kuwa wewe ni ufufuo. . .
MWIMBAJI: Amina. Utukufu kwa Baba . . . sasa na siku zote. . . Bwana hurumua *(mara tatu).* ee Rabi Mutakatifu barikia:

PADRI: Kristu Mungu ukweli wetu kwa wafu na wazima na aliyefufuka katika wafu, kwa maombezi ya Mama wake asiye doa wala si lawama kamili, kwa uwezo wa msalaba uheshimiwa na uhuitaji. kwa matunzo ya majeshi yaheshimiwe ya mbinguni yaliyo bila mwili. kwa maombezi ya Yoanno Nabii, Mtakatifu, Mbatizaji, Mheshimiwa na Mtukufu; ya Mitume Watakatifu, watukufu. wasifiwe kamili. . (kutaja jina la Mtakatifu wa Kanisa ile), ya wapadri Watakatifu wetu na Waekumeniki Wakubwa, walimu na Waierarka, ya Washahidi, Watakatifu, watukufu, Washindaji Wazuri, ya Wapadri Wabebaji-Mungu, ya Yoakim na Anna, Mababu ya Mungu, Watakatifu na wenye haki (mtakatifu wa ile siku), makubusho yake leo, hata ya watakatifu wote atuhurumie, akatuokoe, Yu Mungu mwema, Mrahimu na Mpenda wanadamu.

PADRI anaimba: Makubusho milele, makumbusho milele, makubusho milele yao.
MWIMBAJI: Makubusho milele. *(mara tatu).*

PADRI: Makubusho milele. *(mara tatu).*
PADRI: Kwa maombezi ya wapadri wetu Watakatifu, ee Bwana Yesu Kristu Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe. .
MWIMBAJI: Amina.

## WAKATI GANI NA NAMNA GANI INAPASWA KUFUNGA CHAKULA

Uzima ya Ukristu ni ya mateso na mashindano ya kupata uhuru juu ya kutoka katika minyororo ya zambi na ufalme wa mateso yetu; ni mashindano kwa kufikiamneema ya Bwana Yesu kwa utakaso na uzima kimungu. Kwa kutimiza hii mashindano kitu cha kwanza ni Kufunga (Kwarezima). Kugunga na amri ya Mungu ni desturi ya tangu zamani kat6ika kanisa yetu, ni bunduki kweli ya hii uzima ya Kikristu. Kama tunafunga, matunda tutavuna ni haya:

1. Kuzuia mashindano ya Shetani.
2. Kuzuia tamaa mbaya za mwili.
3. TUtakasa roho yetu toka tabia mbalimbali mbaya.
4. Kuepuka mawazo mbaya ya mwili.

Kusali vizuri.

Kupata msaada wa kupokea fazila za Kristu. Kwani kufunga iwe faida kubwa sana kwa uzima wa roho yetu, kanisa yetu iliweka vizuri nyakati gani sisi waorthodoksi tunapaswa kufunga. Hapa tutaonyesha nyakati zote kartika mwaka zile tunaweza kufunga.

1. Mu kazi tatu na mu Kazi tano.

Tangu wakati wa Mitume, katika siku hizi mbili tunakumbuka mateso takatifu ya Bwana Yesu. Tunakumbuka ya siku hizi mbili ni kula chakula bila mafuta. Kama siku hizi mbili ni Siku Kuu kubwa, tutakula chakula yote. Kama ni makumbusho ya Mtakatifu Mkubwa tutakula na mafuta. Kama ni shangilio ya Siku Kuu ya Mzazi-Mungu ao ya Mtakatgifu Yoane Mbatizaji tunaweza kula mafuta na samaki.

Lakini kwa siku zingine za juma tunaweza kula chakula chake tunataka, nikusema kama hakuna kifungo ya Kanisa.

Mu Posho na mu Juma hakuna kufunga ya nguvu, nikusema yasipo mafuta. Katika mwaka mzima paka mu Posho moja inakatazwa kula mafuta, ni mu Posho Mkubwa, siku moja mbele ya Ufufuo wa Bwana Yesu Kristu.

2. Kwarezima Mkubwa, mbele ya Ufufuo wa Kristu

Hii ni Kwarezima mkubwa tena ya nguvu kuliko ingine yote. Inaanza mu Kazi moja Safi, maana kisha siku ya yenye ya Jivini (Tirofagi) na inaisha siku ya yenye ya paska. Mari ya Kanisa yetu ni kuacha kula mafuita siku zote za muda wa hii Kwarezima, ila tu mu Posho na siku ya yenye ya kila juma. Lakini, mu Kazi moja, kazi mbili na mu Kazi ine watu wengine wanakula chakula na mafuta. Hii inawezekana kwa wale weko wagonjwa, hawana nguvu mwilini mwao. Hii inafanyika paka na baraka ya padri wa roho.

Kwa hii wakati wa Kwarezima Mkubwa tunakula:

Samaki siku Kuu ya Habari Njema ya Mzazi-Mungu (25 Mwezi ya tatu) na siku ya Matawi.

Mafuta siku Kuu ya Mashahidi Watakatifu Wakumi ine ( 9 Mwezi ya tatu) na siku Kuu ya Baraza ya malaika Gabrieli (26 Mwezi ya tatu).

3. Kwarezima ya Kuzaliwa Kwake Bwana yesu Kristu.

Kwarezima ingine mkubwa ni ile ya kuzaliwa kwake Bwana Yesu Kristu. Inaanza tarehe 15 Oktoba mpaka 24 Desemba, katika hii Kwarezima tunakula samaki kila siku, paka mu kazi tatu na mu kazi tano hapana, tangu tarehe 21 Novemba mpaka tarehe 17 Desemba.

Tena tunakula samaki Siku Kuu ya Kuingia Kwake Bikira Maria Hekaluni tarehe 21 Novemba na siku zifwatayo. Tena tangu tarehe 18 Desemba mpaka 24 ta hii mwezi yunaweza kula mafuta na vinyo, hapana mu kazi tatu na mu kazi tano ya kila juma ambako tunakula paka chakula bila mafuta.

Tena tunafunga kabisa siku ya kwanza ya hii Kwarezima, maana tarehe 15 Novemba na tarehe 24 Desemba.

4. Kwarezima ya Mitume Watakatifu.

Hii Kwarezima inaanza mu Kazi moja kisha Juma ya watakatifu wote na inaisha tarehe 28 Yuni siku moja mbele ya Siku Kuu ya Mitume Wakubwa Petro na Paulo. Namna ya kuchunga hii Kwarezima ni sawasawa na Kwarezima ya Kuzaliwa kwake Bwana Yesu. Nikusema hatukule nyama, mayayi, maziwa na ingine, lakini tunakula samaki siku zote, paka mu Kazi tatu na mu Kazi tano ambako tunakula chakula bila mafuta.

tena hatukule mafuta siku moja mbele ya siku Kuu ya Mitume, lakini kama ni mu Posho ao siku ya yenye tunakula chakula na mafuta.

Tena tunakula samaki kila siku kisha siku Kuu ya Kuzaliwa kwake Mtakatifu Yoane Mtangulizi tarehe 24 Juni.

Kam siku Kuu ya Mitume Petro na Paulo inafikia  mu kazi tatu ao mu kazi tano tutakula paka mafuta na samaki.

Mafuta na vinyo inatembea pamoja, nikusema kama tunakula chakula na mafuta tunaweza kunywa na vinyo.

5. Kwarezima ya Mzazi-Mungu (Mwezi ya mnane).

Hii Kwarezima tunamusifu Mzazi-Mungu, inaanza ku mwanzo wa mwezi wa Augusti na inaisha tarehe 14 ya hii mwezi. Ni Kwarezima mkubwa sana sawa ile ya Ufufuo wa Kristu. Ikiwezekana, hatutakula mafuta siku zote, paka mu Posho na siku ya Bwana tutakula mafuta. Vilevile tunaweza kula samaki Siku Kuu ya kugeuza kwake Sura Yesu Kristu Mwokozi wetu na kila siku ya hii Mashangilio. Kama siku Kuu ya Mzazi-Mungu (15 Augusti) inafikia mu Kazi Tatu na mu Kazi Tano, tutakula paka samaki, hapana nyama. Lakini kama inafikia Siku zingine tutakula nyama na chakula ingine yote.

Siku ya kufunga katika Mwaka.

1)Tarehe 5 Januari siku moja mbele ya Epifania ya Bwana Yesu tutakula chakula bila mafuta.
.  2)Tarehe 14 Septemba ni makumbusho ya kupazwa kwa Msalaba Takatifu. Tunakula chakula bila mafuita. Kwa mufano, kama tunashangilia hii Siku Kuu usiku nzima (Agripnia), tutakula chakula na mafuta sababu ya muchoko ya sala ya usiku. Hii ni desturi ya Monasteri yetu,

3. Tarehe 29 Augusti ni Makumbusho ya Kukatwa Kichwa cha Yoane Nabii na Mtangulizi. Tunakula chakula bila mafuta.

*Maelezo:  Kama siku Kuu hizi zinafikia mu Posho ao siku ya Bwana tunakula chakula na mafuta.*

*Nyakati tunakula vyakula vyote.*

1. Wakati wa siku Kuu ni mbili.

Ni tangu Siku Kuu ya kuzaliwa kwake Bwana Yesu Kristu tarehe 25 Desemba mpaka tarehe 6 Januari. Tunakula vyakula vyote, paka siku moja mbele ya Epifania ya kristu tunafunga sana.

2. Juma ya Diakenisimos. Ni Juma kisha Ufufuo wa Bwana Yesu;  inaanza siku ya Ufufuo wa Kristu mpaka siku ya Bwana ya Mtume Thomas.

3. Tangu siku ya Bwana ya Pentikosti mpaka siku ya Bwana ya Watakatifu wote.

4. Juma tatu za wakati wa Triode:  Juma ya kwanza ni makumbusho ya Mtoza-Kodi na Mfarisayo;  tunakula vyakula vyote kila siku. Juma ya mbili ni makumbusho ya Mwana Mpotevu; tunakula vyakula vyote. Mu Kazi Tatu na mu Kazi Tano tunafunga, hatukule mafuta.

Juma ya Tatu ni makumbusho ya Jivini (Tirofagi);  tunakula yote, lakini hapana nyama. Tumekuisha kula nyama mpaka JUma ya Apokreo. Tokea hii Juma mpaka Juma ya Jivini hatukule nyama, lakini tunakula chakula ingine yote.

Kama tulivyosema, kifingo cha mu Kazi tatu na mu kazi tano ni cha mwaka mzima, nikusema haipaswe kula chakula na mafuta. Lakini kama tuko na shangilio kubwa mu hii masiku tutakula ao samaki, ao paka mafuta na vinyo.

Tunakula samaki wakati wa siku Kuu za mashangilio ya Mzazi-Mungu na ya Yoane Nabii Mtangulizi na Mbatizaji. Makumbusho ya Watakatifu wengine tunashangilia na mafuta na vinyo.

Tena tunakula samaki mu Kazi Tatu kwa Siku Kuu katikati ya Pentikosti, na mu Kazi Tatu ya Sindikizo ya Ufufuo wa Bwana Yesu Kristu, siku moja mbele ya Siku Kuu ya kupenda kwake Bwana Yesu Kristu mbinguni.

Kisha  tutaonyesha vizuri kila mwezi siku gani tutafunga na chakula gani tutakula.

**MWEZI YA JANUARI.**

Tarehe 6:  Ni Epifania ya Kristu.  Tunakula yote.

Tarehe 7:  Baraza ya Yoane Mtangulizi. Tunakula samaki.

11 Makumbusho ya Mt. Theodosios. Tunakula mafuta na vinyo.

16. Usujudu ya monyororo ya Mtume Petro. Tunakula mafuta na vinyo.

17. Ya Mtakatifu Antonios. Tunakula mafuta na vinyo.

18. Ya Watakatifu Athanasios na Kirillos.  Mafuta na vinyo.

20. Ya Mtakatifu Efthimios mukubwa. Mafuta na vinyo.

22 Ya Mutume Timotheos na Mushahindi Anastasios ya Persia. Mafuta na vinyo.

25 Ya Mtakatifu Askofu Grigorie mutheologo.  Mafuta na vinyo.

27. Kuhamisha Mifupa ya Mt. Yoane Krisostomo.  Mafuta na vinyo.

30. Makumbusho ya Maaskofu  Wakubwa  tatu. Basile Mkuu, Grigorie na Yoane Krisostome. Mafuta na vinyo.

**MWEZI YA  FEBRUARI**

2. Mapokeleo ya Bwana Yesu Kristu  mikononi  mwa Mt. Simeoni. Tunakula samaki.

8. Mtakatifu Mshahidi askari Mkubwa Theodoros. Mafuta na vinyo.

10. Mt. Haralambos Askofu na Shahindi. Mafuta na vinyo.

11. Mtakatifu Askofu Vlasios.  Mafuta na vinyo.

17. Mt. shahindi Theodoros wa Tironi. Mafuta na vinyo.

24. Kupata Kichwa cha Mt. Yoane Mutangulizi.  Mafuta na vinyo.

**MWEZI WA MARSI.**

9. Mashahindi  makumi Ine.  Mafuta na vinyo.

25. Habari Njema ya  Maria Mzazi-Mungu. Samaki.

26. Baraza ya Malaika Mtakatifu  Gabrieli. Mafuta na vinyo.

**MWEZI  WA APRILI**

23. Mtakatifu  Georgie Shahidi. Mafuta na vinyo.

25. Mutume na Mwevangelizaji  Marko. Mafuta na vinyo.

30. Mutume Yakovo. Mafuta na vinyo.

**MWEZI WA MAI.**

2. Mapokeo ya Mifupa ya Mt. Athanasios.  Mafuta na vinyo.

8.  Mutume na Mwevangelizaji Yoane mutheologo. Mafuta na vinyo.

15. Mt. Pahomi mkubwa na askofu Akilios wa mji Larisa. Mafuta na vinyo.

21. Watakatifu Konstantinos na Heleni. Mafuta na vinyo.

25. Kupata mara ya tatu Kichwa cha Mt. Yoane Mtangulizi. Mafuta na vinyo.

**MWEZI WA JUNI**
8. Kutosha Mifupa ya Mt. Theodoros askari mkubwa. Mafuta na vinyo.
11. Mitume Watakatifu Bartholomeo na Barnava. Mafuta na vinyo.
24. Kuzaliwa kwake Mt. Yoane Mutangulizi. Tunakula samaki.
29. Mitume Petro na Paulo. Samaki.
30. Mitume Kumi na mbili. Mafuta na vinyo.

**MWEZI WA JULI.**
1. Watakatifu Kosmas na Damianos. Mafuta na vinyo.
2. Kuweka Kanzu ya Mzazi-Mungu Hekaluni. Mafuta na vinyo.
17. Mtakatifu shahidi Mwanamuke Marina. Mafuta na vinyo.
20. Nabii Elia wa Thesvitis. Mafuta na vinyo.
22. Maria Magdalena. Mafuta na vinyo.
25. Kulala kwake Mtakatifu Anna. Mafuta na vinyo.
26. Mtakatifu Shahidi Paraskevi. Mafuta na vinyo.
27. Mt. Shahidi Panteleimon Mafuta na vinyo.

**MWEZI WA AUGUSTI**
6. Kugeuza kwake Sura ya Bwana Yesu. Tunakula samaki.
15. Kulala kwake Mzazi-Mungu. Samaki.
29. Kukatwa kwake Kichwa ya Mt. Yoanne Mutangulizi. Chakula bila mafuta.
31. Kuweka Mushipi ya Mzazi-Mungu Hekaluni. Mafuta na vinyo.

MWEZI WA SEPTEMBA.
1. Mwanzo wa mwaka ya Kanisa. Simeoni Mustilitis. Mafuta na vinyo.
6. Muujiza ya Malaika Mkuu Mikaeli. Mafuta na vinyo.
8. Kuzaliwa kwake Mzazi-Mungu. Samaki.
9. Yoakimu na Anna. Mafuta na vinyo.
13. Kufungua Kanisa ya Ufufuo ya Bwana Yesu. Mafuta na vinyo.
14. Kupazwa kwa Msalaba wa Bwana Yesu. Chakula bila mafuta.
20. Shahidi Efstathios askari mkubwa. Mafuta na vinyo.
23. Kutunga mimba ya Yoane Nabii na Mubatizaji. Mafuta na vinyo.
26. Mt. Yoane Mutheologo na mwevangelizaji. Mafuta na vinyo.

**MWEZI WA OKTOBA**
6. Makumbusho ya Mtume Thomas. Mafuta na vinyo.
18. Mutume na Mwevangelizaji Luka. Mafuta na vinyo.
23. Yakovo, nduguu ya Mungu. Mafuta na vinyo.
26. Mt. Shahindi Dimitrios. Mafuta na vinyo.

**MWEZI WA NOVEMBA.**
1. Mashahidi Watakatifu Kosma na Damiano. Mafuta na vinyo.
8. Baraza ya Malaika wakuu. Mafuta na vinyo.
12. Mtakatifu Mrehemu Yoane. Mafuta na vinyo.
13. Mt. Yoane Krisostomo. Mafuta na vinyo.
14. Mtume Filipo. Samaki.
16. Mtume na Mwevangelizaji Mattheo. Mafuta na vinyo.
21. Kuingia kwake Mzazi-Mungu Hekaluni. Samaki.
25. Mt. Shahindi Mwanamuke Ekaterini. Mafuta na vinyo.
30. Mtume Andrea. Mafuta na vinyo.

**MWEZI WA DESEMBA**

4. Mt. Yoane Damaskinos na Mt. Varvara. Mafuta na vinyo.
5. Mt. Mutawa Savvas mwenye kutakaswa. Mafuta na vinyo.
6. Mt. Askofu Nikolao. Mafuta na vinyo.
9. Kutunga kwake mimba Mt. Anna. mama ya Mzazi-Mungu. Mafuta na vinyo.
12. Mt. Askofu Spiridon. Mafuta na vinyo.
15. Mt. Askofu Eleftherios. Mafuta na vinyo.
17. Nabii Danieli na Mt. Dionisios askofu ya Egina. Mafuta na vinyo.
20. Mt. Ignatios askofu ya Antiokia. Mafuta na vinyo.
25. Kuzaliwa kwake Bwana Yesu Kristu. tunakula vyakula vyote.

## YALIYOMO

**SALA KATI YA USIKU (MESONIKTIKO)..............................................................1**

**IBADA YA MESONIKTIKO YA KILA SIKU...........................................................2**

**MESONIKTIKON YA KILA MUPOSHO................................................................5**

**MESONIKTIKON YA SIKU YA MUNGU.............................................................9**

**IBADA YA ASUBUI (ORTHROS)..............................................................10**

**SALA YA SAA...........................................................................................27**
**SAA YA TATU.........................................................................................30**
**SAA YA SITA...........................................................................................33**
**SAA YA TISA...........................................................................................36**
**ALA YA MANGARIBI...............................................................................42**
**APODIPNO KIDOGO.................................................................................50**

**NYIMBO ZA UTATU MTAKATIFU NA WIMBO WA MWANGAZA**

**(FOTAGOGIKA)...................................................................................55**

**KANUNI AKATHISTE YA MZAZI-MUNGU..........................................................58**

**K A T A V A S I E S ...................................................................................68**
**SALA YA CHAKULA...................................................................................82**
**APOLITIKIA NA THEOTOKIA ZA UFUFUO WA BWANA YESU**
**KRISTU...................................................................................................83**
**APOLITIKIA YA WATAKATIFU.......................................................................86**
**APOLITIKIA NA KONTAKIA ZA SIKU KUU ZA BWANA WETU YESU**
**KRISTU...................................................................................................88**
**APOLITIKIA NA KONDAKIA ZA SIKU KUU ZA MZAZI-**
**MUNGU..................................................................................................90**
**APOLITIKIA NA KONTAKIA YA JUMA.......................................................91**

**SALA YA KOMONYO TAKATIFU.......................................................................93**

**SALA YA KANUNI YA KUSIHI KIDOGO....................................................104APODIPNO**

**MUKUBWA..................................................................................114**

**SALA YA PASAKA............................................................................................127**
**DOKSOLOGIA UKUBWA YA SIKU KUU YA KITAIFA............................128**
**IBADA TAKATIFU YA WAFU (PANNIHIDA)..............................................130**
**WAKATI GANI NA NAMNA GANI INAPASWA KUFUNGA CHAKULA.....140**

**YALIYOMO...........................................................................................................144**

**UTUKUFU KWA UTATU MUTAKATIFU.**
**MONASTERI YA MTAKATIFU GRIGORIO**
**KILIMA TAKATIFU**
**KINGIRIKI-UYUNANI**
**2005**